**5 APRILI, 2023**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

**Kikao cha Pili – Tarehe 5 Aprili, 2023**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Katibu!

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

## HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI):**

Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya

Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko huo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**MHE. DKT. CHRISTINE C. MNZAVA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA AFYA NA MASUALA YA UKIMWI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu (Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania *TACAIDS*) kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**MHE. FURAHA N. MATONDO K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu) kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**SPIKA:** Ahsante sana. Katibu!

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge maswali. Tutaanza na Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, Mbunge wa Rorya sasa aulize swali lake.

Na. 16

### Ujenzi wa zahanati kwa vijiji vilivyokamilisha maboma nchini

**MHE. JAFARI W. CHEGE** aliuliza: -

Je, nini mpango wa Serikali kumaliza ujenzi wa zahanati kwa vijiji vilivyokamilisha ujenzi wa maboma?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Dugange Majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba wa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, Mbunge wa Rorya kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutoa fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma ya zahanati yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi ambapo katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2017/2018 hadi 2021/2022 kiasi cha shilingi bilioni 71.95 zimetolewa kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma 1,214 ya zahanati nchini kote. Aidha, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 15 kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma ya zahanati 300, hadi kufikia Februari, 2023 kiasi cha shilingi bilioni 14.6 zimekwishatolewa.

Mheshimiwa Spika, Jumla ya zahanati 762 kati ya 1,514 ujenzi umekamilika na zimeanza kutoa huduma. Aidha, Ujenzi wa maboma 752 ya zahanati upo katika hatua mbalimbali za ukamilishaji.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutenga bajeti kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma ya zahanati yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jafari Wambura Chege swali la nyongeza.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nataka kujua kwa kuwa kasi ya utoaji wa fedha hailingani na uhitaji wa maboma yanayohitajika kwa zahanati kwa vijiji vyote. Je, Serikali haioni sasa kuna umuhimu kwa mwaka huu wa bajeti kutenga fedha kukamilisha maboma yote ambayo yanahitajika kwenye vijiji vilivyohitaji ujenzi wa zahanati?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, kwa kuwa Serikali imekuwa ikitenga fedha shilingi milioni 500 mpaka shilingi milioni 700 kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya kwenye kata 26 kwenye jimbo moja. Je, Serikali haioni sasa badala ya kupeleka fedha hizi kwenye umaliziaji wa kituo cha afya kimoja, fedha hii iende kukamilisha maboma yote yaliyojengwa na nguvu za wananchi kwenye eneo hilo hilo la jimbo ambao wanaweza wakakamilisha maboma 14 badala ya kituo cha afya kimoja kwenye eneo moja la wilaya moja?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA- (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya

nyongeza ya Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, Mbunge wa Jimbo la Rorya kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kasi ya ukamilishaji wa maboma ya zahanati nchini kote kwa kweli ni kubwa na Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ameweka kipaumbele cha hali ya juu sana katika sekta ya afya na ndiyo maana katika kipindi cha miaka hii miwili zaidi ya maboma 1,600 ya zahanati yamekamilishwa na zahanati hizo zimeanza kutoa huduma. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kasi hii ya Serikali itaendelea ili kuhakikisha kwamba maboma hayo ambayo bado hayajakamilishwa yanakamilishwa na kuanza kutoa huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, pili kuhusiana na kuacha kujenga vituo vya afya na kuweka kipaumbele kwenye zahanati, mfumo wa huduma za afya una utaratibu wa rufaa kwa ngazi. Ngazi za zahanati zina umuhimu wake katika ngazi ya vijiji lakini ngazi ya vituo vya afya ni rufaa ya zahanati na tunafahamu zahanati hazifanyi upasuaji na hazilazi kwa hiyo lazima tuendelee na nguvu za kujenga vituo vya afya sambamba na ujenzi wa zahanati.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, niwakumbushe maswali yawe mafupi na majibu mafupi. Mheshimiwa George Mwenisongole.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Nilitaka kujua ni vigezo vipi vinatumika katika kugawa hizo fedha za umaliziaji wa maboma ya zahanati kwani Jimbo la Mbozi tuna maboma zaidi ya 20 lakini kiasi kinachokuja ni kidogo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa George Mwenisongole, Mbunge wa Jimbo la Mbozi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, vigezo ambavyo vinatumika kupeleka fedha ni idadi ya watu, umbali wa kijiji hicho kwenda kwenye kijiji chenye zahanati cha jirani zaidi. Lakini katika Jimbo la Mbozi pia Serikali imeendelea kupeleka fedha na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tutaendelea kupeleka fedha pia.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro, swali la nyongeza.

**MHE. GEORGE N. RUHORO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Jimbo la Ngara bado lina kata nyingi hazina vituo vya afya, je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha tunapata vituo vya afya kwenye kata hizo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA- (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ndaisaba George, Mbunge wa Jimbo la Ngara kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeshafanya tathmini na kuainisha maeneo ya kimkakati ya kujenga vituo vya afya ikiwemo katika Kata za Jimbo la Ngara.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mohamed Monni swali la nyongeza.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, boma la zahanati ya Isusumya limekuwa la muda mrefu sana na tulileta maombi maalum. Nataka kujua sasa mpaka leo hatujajua nini kinaendelea, nini mpango wa Serikali wa kuhakikisha kwamba zahanati hiyo imekamilika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mohamed Monni, Mbunge wa Jimbo la Chemba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimuelekeze Mkurugenzi wa Halmashauri ya Chemba kutenga fedha za ukamilishaji wa Boma shilingi milioni 50 kwenye mwaka wa fedha ujao ili kukamilisha boma hili ambalo halmashauri imeona ni kipaumbele na tayari imeshaleta maombi maalum kwa ajili ya ukamilishaji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ester Bulaya swali la nyongeza.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Serikali imekuwa ikitoa kiwango cha fedha kinachofanana katika umaliziaji wa maboma yote bila kuangalia hali halisi ya gharama za ujenzi.

Je, hamuoni kuna haja ya kufanya tathmini ili kutoa fedha kulingana na gharama ya ujenzi na maeneo husika ili maboma yaweze kukamilika kwa wakati?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):**

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ester Bulaya, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba tumekuwa tukitoa fedha kwa kiwango kinachofanana kwa maeneo tofauti na hivi sasa Serikali inafanya tathmini ya kutoa bei au *BOQ* kulingana na maeneo kijiografia, umbali lakini pia na gharama kutokana na maeneo hayo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Justin Nyamoga swali la nyongeza.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, Kituo cha Afya cha Kata ya Ukumbi pamoja na Zahanati ya Kijiji cha Ilutila ni miaka 16 sasa ni maboma. Je, ni lini Serikali itamalizia kituo hicho cha afya pamoja na hiyo zahanati?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Justin Nyamoga, Mbunge wa Jimbo la Kilolo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ilishaweka utaratibu na tulishawaelekeza Wakurugenzi wa halmashauri kuleta vipaumbele vya maboma hasa ya vituo vya afya lakini pia na zahanati ambazo zinauhitaji mkubwa katika maeneo hayo. Kwa hiyo, nimwelekeze Mkurugenzi wa Halmashauri ya Kilolo kuwasilisha rasmi Ofisi ya Rais, TAMISEMI maombi ya vituo hivi ili Serikali iweze kuona namna ambavyo Serikali itatafuta fedha lakini pia na mapato ya ndani yatachangia kukamilisha vituo hivyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jackson Kiswaga swali la nyongeza.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kijiji cha Ndihuli kilichopo Kata ya Magulilwa kilijenga boma zaidi ya miaka saba. Je, ni lini sasa Serikali itatuonea huruma ipeleke fedha hapo tuweze kumalizia?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Jackson Kiswaga, Mbunge wa Jimbo la Kalenga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimuombe Mheshimiwa Mbunge awasilishe maombi hayo kupitia kwa Mkurugenzi ili tuweze kuona namna ambavyo tutatenga fedha kwenye bajeti za miaka ijayo kwa ajili ya kukamilisha boma hili kwa ajili ya zahanati.

**SPIKA:** Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate swali la nyongeza.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Spika, ahsante, Jimbo la Tunduru Kusini lina maboma saba yako katika hatua mbalimbali katika Vijiji vya Mkapunda, Chuwala, Ukandu, Nazya pamoja na Lupanji; je, Serikali ina mpango gani sasa wa kupeleka fedha kumalizia maboma hayo ya zahanati?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Iddi Mpakate, Mbunge wa Jimbo la Tunduru Kusini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tumekwisha elekeza na nirudie kuwakumbusha Wakurugenzi wa halmashauri kuhakikisha wanaweka vipaumbele vya ujenzi na ukamilishaji wa maboma ya zahanati katika maeneo yenye uhitaji mkubwa. Kwa hiyo, maboma haya saba ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyataja, Ofisi ya Rais TAMISEMI tutachukua lakini tutafanya mawasiliano na Wakurugenzi ili tuone yapi tuanze nayo kwa awamu lakini tutaendelea kutenga fedha kwa kadiri ya upatikanaji wa fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga swali la nyongeza.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kuna boma la Mji mwema, Mkalanga pamoja na Kata ya Kivavi, ni lini Serikali itamalizia maboma ambayo wananchi wameshayajenga?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, Mbunge wa Jimbo la Makambako kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, boma hili la Mji mwema lakini na Mkalanga ni maboma ambayo tayari tulishayaingiza kwenye bajeti ya mwaka ujao wa fedha. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutakwenda kutekeleza ukamilishaji wa maboma hayo mwaka ujao wa fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Furaha Matondo swali la nyongeza.

**MHE. FURAHA N. MATONDO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Wananchi wa Kata ya Nyasaka Mtaa wa Kiloleli B wamenunua kiwanja kwa ajili ya

kujenga zahanati. Je, ni lini Serikali itawajengea zahanati katika kiwanja hicho?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Furaha, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, niwapongeze Kijiji hiki kwa kununua eneo kwa ajili ya ujenzi wa zahanati lakini nimwelekeze Mkurugenzi kuanza kutenga fedha kwa awamu kwa ajili ya ujenzi wa zahanati hii.

**SPIKA:** Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mbunge wa Mpanda Vijijini sasa aulilze swali lake.

Na. 17

**Mfumo wa utawala wa Serikali za Mitaa katika Kambi ya Wakimbizi Mishamo**

**MHE. MOSHI S. KAKOSO** aliuliza:-

Je, ni lini mfumo wa utawala wa Serikali za Mitaa utaanza kufanya kazi katika Kambi za Wakimbizi Mishamo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Moshi

Selemani Kakoso, Mbunge wa Jimbo la Mpanda Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Makazi ya Wakimbizi ya Mishamo yaliyopo Mkoa wa Katavi, Wilaya ya Tanganyika yalisajiliwa rasmi mwaka 1979. Baada ya usajili, Shirika la Dini la *Tanganyika Christian Refugee Services* lilipewa jukumu la kusimamia Makazi hayo na kutoa huduma za kijamii ikiwa ni pamoja na kufanya mpango wa kugawanya mitaa. Kupitia Mpango huo ilipatikana mitaa 21 iliyotambuliwa kwa namba kutoka mtaa namba 1 hadi 21.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa mitaa hiyo inatambulika kama vijiji baada ya wakazi hao kutumia majina badala ya namba zilizosajiliwa awali. Aidha, kuanzia Mwaka 1980 Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la *UNHCR* imekuwa ikitoa huduma za kijamii ikiwemo ujenzi wa shule, zahanati na barabara katika Makazi ya Wakimbizi Mishamo.

Mheshimiwa Spika, Maeneo haya yanaendelea kutambulika kupitia Gazeti la Serikali namba 537 la tarehe 19/07/2019. Aidha, Maeneo hayo bado yapo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na mara yatakapokabidhiwa Ofisi ya Rais TAMISEMI mfumo wa Utawala wa Serikali za Mitaa utaanza kufanya kazi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso swali la nyongeza.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, nishukuru kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa kumekuwa na mkanganyiko wa kutoa huduma za kijamii kwenye eneo ambalo lina utawala wa aina mbili, Ofisi ya Mambo ya Ndani na Ofisi ya TAMISEMI na wanaotoa fedha ni TAMISEMI. Je, mkanganyiko huu ni lini Serikali itakwenda kuuondoa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa Umoja wa Mataifa ulijitoa kuhudumia kambi za wakimbizi na kukabidhi Serikali na Serikali ikatoa uraia. Tunavyozungumza leo hii eneo la utawala kata tayari kuna madiwani ambao wanafanya shughuli za kiutawala lakini eneo la Serikali za vijiji hakuna utawala wa aina yoyote. Ni lini mtakaa na Wizara ya Mambo ya Ndani ili muondoe sintofahamu ambayo ipo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mbunge wa Jimbo la Mpanda Vijijini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, mkanganyiko ambao umetokana na vijiji hivi kuwa chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Ofisi ya Rais TAMISEMI kimsingi tunaendelea kuiweka sawa; na ndiyo maana siku za nyuma hatukuwa na madiwani katika zile kata nne lakini mwaka 2020 madiwani walichaguliwa. Pia kuna watendaji wa vijiji ambao siku za nyuma hawakuwepo; na linaloendelea sasa ni utaratibu tu wa ndani ya Serikali kuongea kati ya Ofisi ya Rais TAMISEMI na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ili tuweze kukubaliana mfumo mzuri zaidi wa kuendesha vijiji hivyo.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutakaa na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kuondoa changamoto ambayo ipo kwa sasa, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Rehema Migilla swali fupi.

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Mfumo wa Tawala za Serikali za Mitaa ni pamoja na kutoa haki kwa wananchi kupiga kura na kuchaguliwa. Lakini katika makazi ya wakimbizi wa Ulyankulu

wananchi hawa wana haki ya kumchagua Rais na Wabunge lakini hawana haki ya kumchagua diwani, wenyeviti wa Serikali za Mitaa na Vitongoji.

**SPIKA:** Swali lako.

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini sasa wananchi hawa watapa haki ya kuchagua diwani, wenyeviti wa vitongoji na vijiji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri sijui kama hili la haki ya kuchagua diwani liko katika Wizara yako kama halipo katika wizara yako wewe nijulishe ili nilipeleke kwenye wizara inayohusika.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, haliko kwenye Wizara yangu.

**SPIKA:** Haliko kwenye Wizara yako, sawa. Mheshimiwa Rehema Migila peleka swali la msingi ili ujibiwe na Wizara inayohusika. Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Ofisi ya Rais Utumishi na Utawala Bora Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji Mbunge wa Mwera sasa aulize swali lake.

Na. 18

**Kuchukua hatua dhidi ya viongozi wanaowanyima haki wananchi kunufaika na *TASAF***

**MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI** aliuliza: -

Je, Serikali inachukua hatua gani kwa viongozi wanaowanyima wananchi kwa makusudi haki yao ya kuwa wanufaika wa *TASAF?*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali namba 18 lililoulizwa na Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji naomba kutumia nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuniamini. Nataka nimwakikishie yeye na watanzania wote kwamba tutaendelea kufanya kazi na kazi itaendelea.

Mheshimiwa Spika, Sasa, kwa niaba ya Waziri wa Nchi ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na utawala Bora, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji Mbunge wa Mwera kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, zoezi la utambuzi wa wanufaika wa *TASAF* ni zoezi shirikishi na hujumuisha Wataalam kutoka Halmashauri, Maafisa wa *TASAF*, Wananchi wa maeneo husika yanayosimamiwa na viongozi wa vijiji/mitaa/shehia.

Mheshimiwa Spika, inapotokea kiongozi au viongozi wamewanyima haki wananchi kwa makusudi bila sababu yoyote ile hatua zifuatazo huchukuliwa dhidi yao:

(a) Endapo uongozi wa vijiji/mitaa/shehia utashinikiza kuondoa majina ya kaya kwenye orodha ya utambuzi bila kuafikiwa na jamii, zoezi la utambuzi husitishwa na taarifa hupelekwa kwa Mkurugenzi wa Halmashauri/Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais (Zanzibar) na nakala hupelekwa kwa Mkurugenzi wa *TASAF*.

(b) Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri/Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais (Zanzibar) huchunguza

tuhuma hizo na ikithibitisha tuhuma hizo mhusika husitishwa kujihusisha na shughuli zozote za Mpango wa *TASAF*. Aidha, baada ya kusimamishwa, mhusika huchukuliwa hatua za kinidhamu ikiwa ni pamoja na kupewa karipio au kuondolewa kwenye nafasi yake.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji swali la nyongeza.

**MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba niishukuru Serikali kwa majibu yake mazuri, lakini naomba niulize maswali mawili ya nyongeza; la kwanza, je, Serikali inatambua kwamba tabia hii inafanyika katika jimbo langu?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Je, Serikali sasa iko tayari kulifanyia kazi hii ili kuondokana na tatizo hili kwa wananchi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Serikali inatambua juu ya tabia za baadhi ya viongozi au wananchi wanaoshiriki katika kuhakikisha kwamba wanawanyima watu haki zao. Nataka nimwakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba kwa kutambua hilo Serikali imejidhatiti kuhakikishi kwamba inachukua hatua zote husika na pale inapotokea wananchi wanashindwa kwenda kushtaki basi na sisi pia kama wawakilishi wa wananchi tunaruhusiwa kufikisha vilio katika ofisi hizo mbili ikiwemo mkurugenzi na ofisi ya makamu wa pili wa Rais kama nilivyoeleza.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali

itaendelea kuhakikisha kwamba haki za watu wote wanaostahiki kuingia katika mfuko wa *TASAF* zinapatikana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Miraji Mtaturu, swali la nyongeza.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, zoezi la *TASAF,* kwa maana ya kukwamua familia maskini ni zoezi zuri. Huko nyuma lilikuwa liko kwenye *package* ya kuwalipa tu kwa ajili ya kuwasaidia kwenye mambo mbalimbali; sasa kumeongezwa *package* ya kuwapa hadhi halafu wanalipwa. Lakini maeneo mengi tumeanza kuona wazee wetu…

**SPIKA:** Swali lako Mheshimiwa Mtaturu.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Spika, tumekuwa wazee wetu wakitumikishwa wanafanya zaidi ya miaka 60 kitu ambacho sio kizuri katika maeneo yetu; je, Serikali inasemaje kuhusu jambo hili?

**SPIKA:** Ngoja kabla sijaiambia Serikali nataka nikuelewe wewe kwa hiyo ni jambo bayo kufanya kazi na kulipwa? Yaani uliza swali lako vizuri ili Serikali ijue inakujibuje, ni jambo bayo wale maskini kuambiwa wafanye kazi halafu walipwe?

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Spika, si maskini watu wazee zaidi ya miaka 70 wanafanya kazi ya kuchimba mitaro, kutengeneza barabara, ambayo *package* hiyo ilikuwa inalenga kwa ajili ya vijana ambao wanatoka kwenye familia maskini swali langu ndio hilo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge Mtaturu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba katika baadhi ya maeneo malalamiko haya yamekuwepo. Sisi kama Serikali tumekwishatoa mwongozo na huo ndio mwongozo unaoongoza shughuli za *TASAF;* kwamba wazee wote walio juu ya miaka 60 na akina mama wajawazito pamoja na watoto wadogo hawaruhusiwi kufanya kazi katika mazingira hayo ambayo yeye anayasema. Isipokuwa Serikali, na sheria vinaelekeza kwamba vijana wenye nguvu watafanya kazi kwa niaba ya wazee hao. Na kama itatokea kwamba mzee amelazimishwa basi sheria itafuata mkondo wake katika kuchukua hatua za msingi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sasa hayo maelezo ni ya jumla najaribu kuwaza mzee kama anao uwezo wa kufanya hiyo kazi halafu anyimwe; nadhani pengine huo mwongozo wa Serikali utazame. Kuna wazee kweli hawawezi kufanya kazi lakini wapo wazee wanaweza kufanya kazi na kama ameenda yeye kuomba hiyo kazi hoja ya kulazimisha ndiyo shida. Kama yeye ndio alienda kuomba kazi ni kwamba hiyo kazi angeweza kuifanya sehemu nyingine. Na hata humo ndani kuna wazee ambao wanaweza ubunge, wako wazee wanapewa mikataba hata Serikalini, sasa tukiweka kwa jumla namna hiyo Mheshimiwa Naibu Waziri hii inakaaje?

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Serikali naomba nitoe maelezo mafupi juu ya jambo hili.

Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Serikali unataka wazee walio juu ya umri wa miaka 60 wasipewe kazi hizo kwa sababu ya ugumu wake; lakini inapotokea kwamba mazingira hayo yapo mwongozo unawaongoza kwamba

wachukuliwe vijana ambao ndani ya kaya ile anayetoka huyo mzee ili wafanye kazi kwa niaba ya yule mzee. Sasa kumekuwa na *incidence* ambazo vijana wanakataa kwenda kufanya kazi au wakati mwingine wanawakatalia wazee wao kufanya kazi, kwa hiyo mzee kwa kutambua kwamba kuna hela ataikosa anaamua mwenyewe aende kufanya kazi hiyo. Sasa haya ni mazingira yaliyopo, lakini sisi kama Serikali tumeweka sheria na miongozo ambayo iko *very strict,* kwamba mzee aliyezidi miaka 60, mama mjamzito, mtoto chini ya miaka 18 hawaruhusiwi kufanya kazi.

**SPIKA:** Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga Mbunge wa Kilombero sasa aulize swali lake.

Na. 19

**Kuzisaidia Taasisi za Wenza wa Viongozi Wakuu wa Nchi kibajeti**

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuzisaidia Kibajeti Taasisi za Wenza wa Viongozi Wakuu wa nchi ili ziweze kujiendesha na kupata ufadhili?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejiment ta Utumishi wa Umma na Utawala Bora naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abubakar Damian Asenga Mbunge wa Kilombero kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa sheria za nchi, taasisi za wenza wa viongozi wakuu wa nchi zinasajiliwa na

kuendeshwa kwa taratibu zinazotumika kusajili na kuendesha taasisi nyingine binafsi na zisizo za Kiserikali. Hadi sasa Serikali haina mwongozo wa kisheria au kikanuni unaoielekeza kutoa usaidizi wa kibajeti kwa taasisi za wenza wa viongozi wakuu wa nchi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga swali la nyongeza.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Spika, swali langu linataka kufahamu kimsingi kwamba taasisi kubwa za nchi yetu, kwa maana ya Mahakama, Bunge na *executive* ya *president,* wale viongozi wakuu na wenza wao wanapokuwa madarakani wanaanzisha taasisi ambazo zinafanya makubwa katika nchi yetu. Taasisi hizo zinaaminika duniani zinapata fedha nyingi katika nchi yetu. Wanavyoondoka madarakani hakuna mfumo mzuri wa kiserikali wa kuziendeleza taasisi hizi. Kwa mfano *Mkapa Foundation, WAMA, Tulia Trust* leo inafanya makubwa lakini ukiondoka inapotea, Mama Magufuli alikuwa na taasisi ya wazee hatumwoni Mama Magufuli akiendeleza taasisi ya wazee.

Mheshimiwa Spika, swali langu kwa Serikali viongozi hawa wanapotoka madarakani kuna utaratibu gani wa kuendelea kusaidia taasisi hizi kubwa kama nchi zilizoendelea, tunavyoona Jimmy Carter leo inaweza kuwa January Makamba. Ahsante.

**SPIKA:** Sikuwa najijua kama mimi ni mwenza wa kiongozi mkubwa wa nchi hii mpaka muda huu aliposema Mheshimiwa Abubakar. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, swali alilouliza Mheshimiwa Abubakari Asenga Mbunge ni swali zuri; lakini kwa kuwa hadi hapa tunapozungumza sasa hakuna

sheria wala mwongozo wowote unaotutaka sisi kufanya kazi au kupeleka kibajeti juu ya hizo taasisi za wenza wa viongozi naweza kusema kwa namna moja au nyingine kwamba hatuna la kufanya kwa sasa hivi. Hata hivyo, kama mawazo yako yatakuwa mazuri tutaangalia, lakini kuchukua fedha za umma kupeleka kwenye taasisi za watu binafsi hili jambo halijakaa sawa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda Mbunge wa Newala Vijijini swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Yahya Ally Mhata.

Na. 20

**Upatikanaji wa vitabu vya kufundishia na kujifunzia**

**MHE. YAHYA A. MHATA K.n.y. MHE. MAIMUNA S. MTANDA** aliuliza:-

Je, hali ya upatikanaji wa vitabu vya kufundishia na kujifunza katika shule za msingi na sekondari ipoje?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Juma Kipanga, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda, Mbunge Wa Newala Vijijini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha uandishi, uchapaji na usambazaji wa vitabu vya kiada na viongozi vya mwalimu kwa masomo yote ya elimu ya awali na msingi darasa la I – VII. Vitabu hivyo ni pamoja na vitabu vya kiada vilivyotafsiriwa kwa ajili ya shule zinazotumia Kiingereza kama lugha ya kufundishia. Vitabu vya kiada vya wanafunzi walio nje ya mfumo rasmi (Mpango wa Elimu ya Msingi kwa Waliokosa – MEMKWA), vitabu vya kiada vya breli kwa wanafunzi wasioona na vitabu vilivyokuzwa maandishi kwa ajili ya wanafunzi wenye uoni hafifu. Aidha, imekamilisha kuandika, kuchapa na kusambaza jumla ya vitabu vya kiada vya masomo 171 kati ya 183 ya sekondari ikiwemo vitabu vya masomo ya sayansi, hisabati, sanaa, lugha, biashara, kilimo, michezo, muziki na vitabu vya ufundi ambavyo vipo hatua ya uchapaji. Vitabu 12 vilivyobaki ni vya masomo chaguzi (*optional subjects*) ikiwemo Kichina ambavyo vinatarajiwa kukamilika mwezi Juni 2023.

Mheshimiwa Spika, kutokana na jitihada hizo, hali ya upatikanaji wa vitabu, kwa shule za msingi na sekondari imefikia uwiano wa kitabu kimoja kwa wanafunzi watatu.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Yahya Ally Mhata swali la nyongeza.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nichukue nafasi hii kuishukuru Serikali kwa majibu mazuri nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, ukisoma ripoti ya *CAG* ya mwaka 2021/2022 utaona kwamba kuna upungufu mkubwa wa upatikanaji wa vitabu mashuleni licha ya kwamba Serikali imepeleka fedha katika wizara husika. Kwa mfano ukiangalia Halmashauri Biharamulo ilikuwa na upungufu wa asilimia 45 katika ripoti ya *CAG*. Ukiangalia Halmashauri ya Bunda takriban vitabu 194,000 havikuwasilishwa mashuleni pamoja

na kwamba Serikali imetoa fedha. Sasa je, Serikali haioni kuna haja ya kuzipatia fedha hizi shule husika ili wao wakagiza moja kwa moja kwa wazabuni badala ya utaratibu uliopo sasa hivi fedha hizi kwenda kwenye wizara ambao umekuwa na mlolongo mkubwa sana?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; uwiano kati ya kitabu na mwanafunzi sasa hivi ni kati ya kitabu kimoja wanafunzi watano tofauti kabisa na malengo ya Serikali moja kwa moja. Je, Serikali ina mpango gani wa dharura hasa katika zile halmashauri za pembezoni kuondokana kadhia hiyo katika hoja ya vitabu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mheshimiwa Juma Kipanga majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Yahya Ally Mhata Mbunge wa Nanyumbu kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza kwenye majibu yangu ya swali la msingi, kwamba Serikali hainunui vitabu badala yake Serikali kupitia *TET* inaratibu zoezi zima. Kwanza inatunga, inachapa na baadaye kusambaza. Gharama zinazotumika ni zile za kuhakikisha kwamba vitabu vinatungwa, vinachapwa na baadaye kusambazwa kwenye maeneo mbalimbali. Kwa hiyo naomba nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kuwa zoezi hili kupitia mamlaka yetu ya elimu *TET* tutaendelea kuliafanya kwa uaminifu na uadilifu mkubwa kwa sababu ni jukumu letu la msingi kuhakikisha kwamba vitabu vinafika shuleni kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, katika swali lake la pili amezunguzia suala la uwiano wa vitabu ni kweli uwiano wa vitabu bado hatujafikia katika ile *ratio* ya moja kwa moja lakini naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunaendelea na

zoezi hili na hivi sasa Serikali imefanya uwekezaji mkubwa pale Mamlaka ya Elimu Tanzania kwa kununua mitambo ambayo yenye uwezo wa kuzalisha vitabu vingi kwa siku ambao utatuhakikishia sasa maene yote ambayo yenye upungufu wa vitabu tunaenda kuwafikia ili kuweza kufikia ile *ratio* ya moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo sasa hivi tumeanzisha maktaba mtandao ambayo katika yale maeneo ambayo mtandao upo au TEHAMA ipo vitabu hivi vinaweza kuwa *accessed* na wanafunzi pamoja na walimu kwa urahisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Vincent Paul Mbogo Mbunge wa Nkasi Kusini sasa aulize swali lake.

Na. 21

**Hitaji la Kituo cha Polisi Kata ya Kala – Nkasi**

**MHE. VINCENT P. MBOGO** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itajenga kituo cha Polisi katika kata ya Kala Wilayani Nkasi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi Mheshimiwa Jumanne Sagini majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Vincent Paul Mbogo, Mbunge wa Nkasi Kusini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali imetoa kiasi cha shilingi 115,809,000 kwa ajili ya kujenga Kituo cha Polisi Daraja C katika Kata ya Kala Tarafa ya Wampembe Wilaya ya Nkasi. Taratibu za ujenzi wa kituo tayari umeanza mwezi Machi, 2023. Kituo hiki kinajengwa eneo la Mpasa na kitahudumia vijiji vya Mpasa, Kala, Mlambo, Tundu, King'ombe na kilambo cha Mkolechi**.**

**SPIKA:** Mheshimiwa Vincent Mbogo swali la nyongeza.

**MHE. VINCENT P. MBOGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwanza niishukuru Serikali kwa sababu niliomba fedha kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Polisi Kala Kijiji cha Mpasa ambapo kuna biashara kubwa sana ya Samaki inafanyika. Ukanda wa Ziwa Tanganyika kuna uhalifu wa mara kwa mara hasa Kata ya Kizumbi;

Je, ni lini Serikali itajenga kituo cha polisi Kata ya Kizumbi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI**: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Vincent Paul Mbogo Mbunge wa Nkasi Kusini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, tunashukuru kwamba Mheshimiwa Mbogo amekuwa akitoa ushirikiano kwa Wizara yetu na wakati mwingine kupitia halmashauri yake amekuwa akitenga maeneo kwa ajili ya ujenzi wa kituo hiki. Nimuahidi tu, baada ya kumaliza kituo hiki kadri hali ya fedha itakavyoruhusu maeneo tete kama ya Kizumbi tutaweza pia kuyajengea kituo cha polisi ngazi ya kata. Nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Kilimo Mheshimiwa Emmnuel Peter Cherehani Mbunge wa Ushetu sasa aulize swali lake.

Na. 22

**Kampuni za Tumbaku kuruhusiwa kwenye *AMCOS***

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itaruhusu kampuni zinazonunua tumbaku kwenda kwenye *AMCOS* kujinadi ili kuongeza ushindani?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani, Mbunge wa Jimbo la Ushetu kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Hapo awali Serikali iliruhusu kampuni za ununuzi wa tumbaku kujinadi kwa wakulima na kuingia mikataba kwa misimu mitatu ya kilimo. Kilimo cha mikataba kwa misimu mitatu kiliathiri bei ya Tumbaku kwa mkulima kutokana na ongezeko la gharama za uendeshaji kampuni na uzalishaji. Jambo hilo lilisababisha Serikali kubadili mfumo huo na kwenda mfumo wa msimu mmoja ili kuongeza ushindani na ufanisi.

Mheshimiwa Spika, Kilimo cha mkataba kwa msimu ni mbadala mzuri kwa wakulima na kampuni kwasababu kinapunguza gharama zinazotokana na kampuni kujinadi. Vilevile, kilimo hicho kinatoa fursa kwa pande zote mbili kujitathmini kabla ya kuingia mkataba kwa msimu unaofuata.

Mheshimiwa Emmanuel Cherehani, swali la nyongeza.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa vile utaratibu unaotumika sasa ni wa mkataba wa mwaka mmoja mmoja. Swali la kwanza; je, Serikali ina mkakati gani sasa ya kuwafanya wakulima hawa waweze kutambua ni kampuni ipi nzuri ili waweze kuingia nayo mkataba?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; kwa kuwa Bodi ya Tumbaku na ndiyo msimamizi mzuri wa zao hili, lakini haina fedha kabisa haina magari hata ya kwenda kwenye masoko, je, Serikali ina mkakati gani sasa wa kuweza kuiopatia fedha Bodi ya Tumbaku ili iweze kusimamia vizuri masoko ya tumbaku hapa nchini? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza kwa sababu Bodi ya Tumbaku ina ofisi katika mikoa yote ya tumbaku na Bodi ndiyo *custodian* wa taarifa zote za makampuni ya ununuzi wa tumbaku tumekuwa tukitumia nafasi hiyo kuendelea kuwapa taarifa sahihi wakulima kupitia ofisi zetu hizo ili watambue mnunuzi mzuri wa kuingia naye kwenye mkataba. Sambamba na hilo, pia tunayo taarifa za wanunuzi wote katika tovuti ya Bodi.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili la bajeti kilifanyika kikao cha wadau wote wakakubaliana kwamba ili kuijengea Bodi uwezo kuanzia msimu unaokuja tutaanza kuchaja shilingi thelathini katika kila tumbaku mbichi kwa ajili ya kuiboresha Bodi yetu ya Tumbaku ili iweze kufanya ufatiliaji na kuendeleza zao hili la tumbaku.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Dkt. Florence George Samizi, Mbunge wa Muhambwe, sasa aulize swali lake.

Na. 23

**Kujenga Madaraja Mto Lumpungu – Muhambwe**

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itajenga Daraja la Mto Lumpungu katika Jimbo la Muhambwe?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Florence George Samizi, Mbunge wa Muhambwe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mto Lumpungu unatenganisha nchi ya Burundi na Tanzania katika Wilaya ya Kibondo Mkoa wa Kigoma kwenye Kijiji cha Kibuye, Kata ya Kumsenga. Kwa kuwa ujenzi wa daraja hili utahusisha nchi mbili Burundi na Tanzania, Serikali itaanzisha mazungumzo na nchi ya Burundi ili ziweze kukubaliana kuhusu ujenzi wa daraja hili, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Florence Samizi swali la nyongeza.

**MHE: DKT. FLORENCE G. SAMIZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi niweze kuuliza maswali la nyongeza. Swali la kwanza; je, ni lini Serikali itaanzisha mchakato huo ili kuwasaidia kuchochea biashara ya ujirani mwema inayofanyika katika Kijiji hiki cha Kibuye katika Kata ya Kumsenga? *(Makofi)*

Mheshimiswa Spika, swali la pili; kwa kuwa Mto huo unatenganisha takribani vijiji sita vya Jimbo hili la Muhambwe na wananchi wanapita mipaka holela, je, Serikali haioni iko sababu ya kuharakisha mchakato huu wa daraja ili kuwe na mahali maalum pa kupita hili kudhibiti vitendo vya uhalifu katika Jimbo hili? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Florence George Samizi, Mbunge wa Muhambwe, kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, daraja hili halipo na linaunganisha nchi mbili, kwa hiyo ni daraja ambalo litahusisha wadau wengine si tu Burundi na Wizara ya Ujenzi, pia itahusisha Taasisi nyingine kama Ulinzi na Usalama, TAMISEMI, Ardhi, Wizara ya Fedha na Mambo ya Nje. Kwa hiyo, wadau wote hawa watakapokuwa wameona kuna haja thabiti ya kujenga na kuona inakidhi vigezo na sisi tukajiridhisha kama nchi, ndiyo tutaanza sasa kuwasiliana na wenzetu wa Burundi. Kwa hiyo sisi tumeshaanzisha huo mchakato kwa upande wetu kuona vigezo vyote vinakidhi, halafu tuweze kuwahusisha wenzetu wa Burundi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Silyvestry Francis Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Muharami Mkenge.

Na. 24

**Ujenzi wa Barabara ya Njia Nane Kibaha - Chalinze - Morogoro**

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE K.n.y. MHE. SILVESTRY F. KOKA** aliuliza:-

Je, ujenzi wa barabara ya njia nane kutoka Kibaha – Chalinze hadi Morogoro umefikia hatua gani?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Silvestry Francis Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS),* imekamilisha upembuzi yakinifu wa awali kutathimini uwezekano wa kujenga barabara ya Kibaha – Chalinze – Morogoro yenye urefu wa kilomita 205 kwa utaratibu wa ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi. Matokeo ya utafiti huo yalionesha mradi kuwa na manufaa makubwa ya kiuchumi na kifedha iwapo itajengwa barabara ya njia nne ya kulipia katika ushoroba mwingine *(new corridor).* Barabara ya sasa inayotumika itaendelea kutumika na watumiaji ambao hawatakuwa tayari kupita katika barabara ya kulipia.

Mheshimiwa Spika, Mtaalam Elekezi ameanza kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa awali ili kumpata mwekezaji wa kufanya ujenzi wa barabara ya kiwango cha *expressway* yenye njia nne ambapo sehemu ya Kibaha – Mlandizi – Chalinze kilometa 78.9 imekamilika na kuidhinishwa na Wizara

ya Fedha na Mipango tarehe 7/3/2023. Tangazo la kuwataka wazabuni kuonesha nia ya kuwekeza katika mradi huu limetolewa tarehe 14/3/2023 na mwisho ni tarehe 18/4/2023.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya Chalinze hadi Morogoro kilomita126.1, upembuzi na usanifu wa awali unaendelea na unatarajiwa kukamilika mwezi Agosti, 2024, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Muharami Mkenge, swali la nyongeza.

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza kwa niaba ya muuliza swali.

Swali la kwanza; je, ni lini Serikali itakamilisha Barabara ya zamani kutoka Picha ya Ndege mpaka Mlandizi ili kupunguza foleni katika Barabara ya Morogoro?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Barabara ya Makofia - Mlandizi ni barabara ambayo ipo katika Ilani ya Chama kwa miaka mingi Je, ni lini Serikali itaanza kulipa fidia kwa wananchi wanaoishi katika maeneo haya kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi wa hiyo barabara? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mpango ni kuiboresha na kuipanua barabara mpya ambayo tunayo, kwa sasa tutaanza kufanya hiyo kazi ya kujenga barabara hizo nne badala ya kuanza na ile barabara ya zamani aliyotaja Mheshimiwa Mbunge. Nadhani kwa kufanya hivyo tutakuwa

tumepunguza msongamano ambao upo na ndiyo lengo kubwa kuijenga ile barabara kwa njia nne zinazokwenda, zinazorudi lakini pia na zile zilizopo zitaendelea kuwepo.

Mheshimiwa Spika, suala la pili la Barabara ya Makofia – Mlandizi, Serikali sasa hivi inatafuta fidia ili kuwafidia wale wananchi ambao walishatathminiwa ambapo tuta-*review* tathmini na kuanza kuijenga hiyo barabara kwa kiwango cha lami, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Deo Mwanyika, swali la nyongeza.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona. Barabara ya Makambo – Songea barabara kubwa ya kiuchumi ni lini ujenzi wa barabara hiyo utaanza?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu swali la nyongeza na Mheshimiwa Deo Mwanyika, Mbunge wa Njombe Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara hii tayari imeshapata fedha kutoka *World Bank* ambapo tutaanzia mbele ya Njombe kuelekea Songea na kipande cha Njombe kuja Makambako Serikali inaendelea kutafuta fedha. Kwa hiyo sasa hivi tuko kwenye maandalizi ya kuanza kuitangaza ili ianze kujengwa kwa maana ya kukarabatiwa upya *total rehabilitations*, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Mifugo na Uvuvi Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake. *(Makofi)*

Na. 25

**Ufugaji wa vizimba vya Samaki Ziwa Nyasa**

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI** aliuliza:-

Je, ni kwa nini Serikali haijagawa fedha kwa ajili ya ufugaji wa vizimba vya samaki katika Ziwa Nyasa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa David Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Ruvuma, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ili kufuga samaki kwa vizimba inabidi kuainisha maeneo yanayofaa ziwani kwa kuzingatia vigezo vya kisheria na kitaalam. Katika awamu ya kwanza Serikali ilitoa fedha katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa Victoria ambayo ilishakidhi vigezo vya kisheria na kitaalam baada ya kufanyiwa tathmini katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 na 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Serikali kupitia Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi *(TAFIRI)* imepanga kufanya tathmini ya kimkakati ya mazingira *(Strategic Environmental Assessment)* katika Ziwa Nyasa ili kuanisha maeneo yanayofaa kwa ufugaji wa samaki kwa vizimba kwa kuzingatia vigezo vya kisheria na kitaalam. Pia *(TAFIRI)* itaanza

ufugaji samaki kwa majaribio kwa kushirikiana na wananchi kufanya uzalishaji wa vifaranga vya samaki aina ya magege *(Oreochromis karongae*) na ufugaji wake kwa vizimba. Hatua hii inalenga kuwajengea uwezo wananchi ili waweze kuendelea na ufugaji pindi taratibu zitakapokamilika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jacqueline Msongozi, swali la nyongeza.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, sasa naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa nini Serikali inadhoofisha ustawi wa Ziwa Nyasa katika Mkoa wa Ruvuma ikiwa pamoja na kuwadhoofisha wananchi wa Mkoa wa Ruvuma hususani Wilaya ya Nyasa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Mheshimiwa Rais ametenga shilingi bilioni 20 kwa ajili ya kuendeleza Maziwa, lakini bilioni 20 hizi zote zinapelekwa katika Ziwa Victoria, je, kwa nini Serikali haiweki uwiano sahihi katika Maziwa yote haya matatu ikiwemo Ziwa Victoria, Ziwa Nyasa na Ziwa Tanganyika? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

Subiri kwanza naona Mheshimiwa Waziri kasimama. Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa fursa hii ya kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Jacqueline Msongozi.

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali hili kwa ruhusa yako sekunde moja, naomba nitumie fursa hii ndani ya Bunge hili Tukufu, kumshukuru Mwenyezi Mungu na pili kumshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa imani yake kwangu na kunikabidhi kazi hii ya kuongoza Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Naomba pia niendelee pia kuomba

ushirikiano kwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu wakati wote wa kutekeleza majukumu haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maswali ya Mheshimiwa Msongozi la kwanza juu ya kudhohofisha Ziwa. Nataka nimhakikishie yakwamba Serikali haina mpango wa kudhoofisha Ziwa Nyasa na katika bajeti hii ya 2022/2023 na hata katika bajeti ya 2021/2022 Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan inayo mambo iliyofanya katika Ziwa Nyasa ikiwemo ujenzi wa Soko katika Jimbo la Nyasa linaloongozwa na Mheshimiwa Mbunge *Engineer* Stella Manyanya. Hivi sasa tupo katika hatua ya mwisho ya kukamilisha hatua za ujenzi wa soko lile ilimradi tuweze kuliruhusu liweze kutumika, lakini kama haitoshi kuhusiana na…

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, tusaidie kufupisha hayo majibu tafadhali.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jibu la pili, uwiano, katika jibu la msingi alilolitoa Mheshimiwa Naibu Waziri ambaye nampongeza kwa majibu yale mazuri, ni kwamba hatua ya mwaka huu ni hatua ya Ziwa Nyasa. Naomba Mheshimiwa Mbunge Msongozi na Wabunge wa Mkoa wa Ruvuma, lakini pia vilevile na Wabunge wa Mkoa wa Kigoma wawe na uhakika kwamba sasa zamu yao na wao inafikiwa baada ya hatua hizi za msingi kuwa zimetekelezwa ikiwa ni pamoja na Ziwa Rukwa pia vilevile litafikiwa, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Profesa Patrick Alois Ndakidemi, Mbunge wa Moshi Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 26

**Kuboresha barabara zinazopeleka watalii Mlima Kilimanjaro**

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha barabara zinazowapeleka Watalii Mlima Kilimanjaro?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Mary Masanja, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Profesa Patrick Alois Ndakidemi, Mbunge wa Moshi Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuweka kipaumbele na jitihada katika ukarabati wa barabara zinazotumika kupeleka watalii katika Hifadhi ya Taifa Kilimanjaro kwa kushirikiana na wadau na mamlaka zinazohusika na utengenezaji na ukarabati wa barabara hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa jitihada hizo zilizofanyika ni pamoja na ujenzi wa barabara za Machame, Mweka na Marangu kwa kiwango cha lami na ukarabati wa mara kwa mara wa barabara za changarawe zinazoelekea lango la Rongai, Lemosho, Kilema, Londorosi na Umbwe. Aidha, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 Serikali itafanya

ukarabati kwa kiwango cha changarawe kwa barabara inayoelekea kwenye lango la Umbwe.

**SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Ndakidemi, swali la nyongeza.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa. Swali la kwanza; je, Serikali ina mpango gani wa kufungua *VIP route* ya Kibia ambayo hupeleka watu maalum kupanga Mlima Kilimanjaro ili tuweze kupata fedha za kigeni kama ambavyo tume-*plan*.

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili mti mrefu kuliko yote Barani Afrika wenye mita 81.5 upo katika msitu wa Mlima Kilimanjaro katika Kijiji cha Pema, miundombinu ya kufika katika eneo hili na mazingira ya eneo hili ni mabaya. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuboresha eneo hili ili tuweze kupata fedha za kigeni? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Profesa Patrick Alois Ndakidemi, Mbunge wa Moshi Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba tu nimtaarifu Mheshimiwa Profesa Patrick pamoja na wananchi wa Moshi kwamba kwa sasa hivi tayari Wizara imeshaanza ukarabati wa lango hili la *VIP route* ambapo lipo takribani asilimia sabini na kwa sasa tunatafuta Wawekezaji kwa ajili ya kujenga huduma za malazi na chakula. Pia kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, tutajenga lango kuu linalopitia katika hiyo *VIP route* ambayo itawasaidia wageni kuingia katika Hifadhi ya *KINAPA*.

Mheshimiwa Spika, kwenye suala hili lingine mti mrefu zaidi hapa Afrika tumeshaanza kutenga kutenga fedha kwa

ajili ya kuweka miundombinu sahihi katika eneo hilo ili Wataliii waweze kufika kwa urahisi. Kwa hiyo, kwa bajeti hii ambayo itapitishwa na Bunge lako hili tunatarajia kwamba zoezi hili litaanza kwa mwaka wa fedha unaokuja, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Subira Khamisi Mgalu, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 27

**Fedha kwa ajili ya uendeshaji Mabaraza ya Uwezeshaji Wanawake**

**MHE. SUBIRA K. MGALU** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatenga fedha kwa ajili ya uendeshaji wa Mabaraza ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Exaud Kigahe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, nakushukuru na kwa niaba ya Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikiendesha Majukwaa ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi tangu mwaka 2017. Lengo kuu la majukwaa hayo ni kuwakutanisha wanawake ili waweze kujadili fursa za kiuchumi na

changamoto mbalimbali wanazokutana nazo wakati wa utekelezaji wa shughuli za kiuchumi nchini.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwaka 2021/2022, mikoa yote 26 imezindua majukwaa ya wanawake katika halmashauri 140 kati ya halmashuri 184 na kata 1,149 kati ya kata 2,404. Lakini pia mitaa na vijiji 1,776 kati ya mitaa na vijiji 7,613.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Serikali ilitenga fedha zaidi ya milioni 72 na katika mwaka wa fedha unaokuja 2023/2024, Serikali imetenga shilingi milioni 200 kwa ajili ya uendeshaji wa majukwaa hayo.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Subira Mgalu, swali la nyongeza.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza naishukuru Serikali kwa majibu mazuri ambayo imeonesha kwa mara ya kwanza Serikali yetu imetenga pesa kwa ajili ya kuwezesha majukwaa haya.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mkoa wa Pwani unaongoza nchi nzima wa kusajili majukwaa 1,723 na kuyasajili 945 ambayo yamepelekea kuanzisha kampuni ya *Go Mama Public Company Limited*. Je, Serikali ipo tayari kutumia Milioni 200 zinazotengwa mwaka huu wa Fedha kwa ajili ya kuwezesha Mkoa wa Pwani kwa kuwa umeonesha dira umeanzisha kampuni ambayo inayo matarajio ya kujenga kiwanda cha vifungashio?

Swali la pili, kwa kuwa Serikali ina Mifuko mingi ya Uwezeshaji zaidi ya 72 ambayo ipo katika Wizara tofauti tofauti. Je, Serikali haioni ipo haja ya Mifuko hii kuwa chini ya chombo kimoja ili iwe fursa kwa majukwaa haya ya

uwezeshaji badala ya majukwaa haya kutegemea asilimia 10 ya mikopo ya mapato ya ndani ya Halmashauri. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshiiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru na naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Subira kwa kazi kubwa anayoifanya katika Mkoa wa Pwani kama ambavyo wamesema wameanzisha hiyo kampuni ya *Go* Mama ambayo wanasema ina nia ya kuanzisha kiwanda cha vifungashio ambayo italeta pato kubwa sana katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema Serikali imeendelea na itaendelea kusaidia na kuwawezesha wanawake kiuchumi kupitia fursa mbalimbali ikiwemo Mifuko hii ya kuwezesha wananchi kiuchumi. Kwa hiyo, kwa kazi hiyo wanayoifanya naamini tutaangalia katika bajeti hii ili tuone namna gani mahsusi kusaidia kampuni hii ambayo inaenda kusaidia kujenga viwanda katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili tayari Serikali tumeshaanza utaratibu wa kuunganisha Mifuko hii ambayo mingi ipo ndani ya Serikali katika Wizara mbalimbali, pia mingine kutoka sekta binafsi, kwa hiyo tunaifanyia kazi, naamini katika mwaka wa fedha ujao tutafanya hivyo ili kuhakikisha Mifuko hii inakuwa na tija kwa ajili ya kuwasaidia wanawake kiuchumi. Nashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Asya Sharif Omar, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 28

**Hitaji la Viwanda vya Kusindika Ngozi**

**MHE. ASYA SHARIF OMAR** aliuliza:-

Je, kuna mkakati gani wa kuongeza viwanda vya kusindika ngozi za mbuzi na ng'ombe?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Uwekezaji Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Asya Sharif Omar, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuhakikisha kuwa uwekezaji katika sekta ya ngozi unaongezeka. Mikakati hiyo ni pamoja na kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji ili kuvutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi lakini Vilevile, Serikali katika kuhakikisha inavutia na kuhamasisha uwekezaji katika sekta ya ngozi, imehakikisha viwanda vya ngozi vya ndani vinapata malighafi za kutosha hapa nchini kwa kuongeza ushuru kwa ngozi zinazouzwa nje ya nchi. Mfano, asilimia 80 kwa ngozi ghafi na asilimia 10 kwa ngozi iliyoongezwa thamani hadi kufikia kuwa ya "*wet blue*". Aidha, Serikali imekuwa ikitoa vivutio mbalimbali ikiwa ni sehemu ya kuvutia uwekezaji kama vile kusamehe kodi kwa mitambo inayoingizwa kutoka nje ya nchi kwa lengo la kusindika na kuzalisha ngozi na bidhaa za ngozi hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mikakati hiyo, Serikali inaendelea kuhamasisha uwekezaji katika sekta ya ngozi kwa

kuweka mazingira bora ya ufanyaji biashara nchini kupitia MKUMBI. Ninakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Asya naona umekaa, huna swali?

**MHE. ASYA SHARIF OMAR:** Ninalo Mheshimiwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Asya Omar, swali la nyongeza.

**MHE. ASYA SHARIF OMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza ninaishukuru Serikali kwa majibu yake mazuri.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa bado mahitaji ni makubwa ya wananchi hao wajasiriamali ambao wanajishughulisha na biashara ya ngozi ya mbuzi na ng'ombe, hasa tukizingatia kwamba wananchi wengi wana mahitaji makubwa lakini tunanunua nje. Kwa mfano, mikoba ya kike ambayo ni *hand bag*, viatu pia mikanda ya akina Baba.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuongeza nguvu ya viwanda ili vifaa hivi sasa viwe vina ubora katika nchi yetu?

Swali la pili, pamoja na kuwa umesema mnatafuta uwekezaji labda mtuambie Serikali viwanda vingapi ambavyo kwa sasa vipo, katika nchi yetu vinavyojishughulisha na usindikaji wa ngozi ya mbuzi na ng'ombe?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Asya Sharif, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli mahitaji ya ngozi ambazo zipo katika hatua ya mwisho kwa maana *finished leather* kwa ajili ya bidhaa za ngozi ikiwemo mikoba na viatu bado ni changamoto katika viwanda vyetu vya ndani. Moja ya mikakati tuliyonayo ni kuhakikisha tunawahamasisha kwanza wafugaji kuzalisha ngozi zinazokidhi mahitahji, ikiwa ni pamoja na kuchunga mifugo yetu katika hali nzuri, ikiwa ni pamoja na kutokupiga chapa kuharibu ngozi, pia kupiga fimbo au viboko, mbuzi na kondoo.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili tunahamasisha uwekezaji katika viwanda hivi ambavyo vitatumia malighafi yetu kuzalisha bidhaa za ngozi kwa maana ya ngozi hadi mwisho *(finished leather)* kwa hiyo ni moja ya mikakati ambayo Seriakli inaendelea kufanya, katika kuhakikisha tunakuwa na ngozi nzuri.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na takwimu, tutamletea takwimu sahihi ya viwanda kwa sababu bado tunaendelea kuhamasisha na kuna viwanda vingi vidogo ambavyo vinaendelea kuzalisha bidhaa za ngozi katika nchi yetu, vikitumia ngozi kutoka ndani ya nchi lakini nyingine kutoka nje ya nchi. Ninakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako, kwa maswali ya Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka, Mbunge wa Liwale, sasa aulize swali lake.

Na. 29

**Mradi wa kupeleka maji Liwale Mjini**

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA** aliuliza:-

Je, ni lini mradi wa visima vitatu katika Kijiji cha Turuki utakamilika kwa ajili ya kupeleka maji Liwale Mjini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zuberi Mohamedi Kuchauka, Mbunge wa Liwale kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha huduma ya maji katika Mji wa Liwale katika mwaka wa fedha wa 2022/2023 Serikali imechimba visima vitatu katika Kijiji cha Turuki. Visima hivyo kwa pamoja vina uwezo wa kuzalisha lita 1,008,000 kwa siku na vitaongeza uzalishaji wa maji kutoka lita 1,200,000 kwa siku hadi kufikia lita 2,208,000 kwa siku.

Mheshimiwa Spika, usanifu kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya usambazaji maji hayo ulikamilika mwezi Machi, 2023 na ujenzi umepangwa kutekelezwa na kukamilika katika mwaka wa fedha 2023/2024. Kazi zitakazofanyika ni pamoja na ulazaji wa mtandao wa bomba umbali wa kilomita 78 na ujenzi wa matanki mawili (2) yenye ujanzo wa lita 1,300,000.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, swali la nyongeza.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza napenda kutoa shukrani za dhati kwa majibu mazuri ya Serikali yanayotia matumaini, lakini hata hivyo namshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanznaia, Mama yetu Mama Samia Suluhu Hassan, tumepata fedha zile za UVIKO, tumejenga chujio na sasa hivi tunapata maji safi ka Mji wetu wa Liwale. Nina swali moja tu la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, vipo Vijiji vya Ngongowele, Makata, Mtatawa, Kihangala, Kipelele, Nguta, Mpengele, Ndapaka, Mlembwe na Nangano. Vijiji hivi bado havijapata maji safi na salama. Naomba kupata *comfort* kutoka Serikalini, ni lini wananchi wa vijiji hivi wataweza kufikiwa na mradi wa maji ili kutimiza ile azma ya kumtua Mama ndoo kichwani iweze kukamilika? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Kuchauka Zuberi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, napenda kupokea shukrani zake na vile vile tumuombee Mheshimiwa Rais, kwa ababu adhma ya kumtua Mama ndoo kichwani hakika inatekelezwa maeneo yote.

Mheshimiwa Spika, vijiji alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge tayari *RUWASA* Mkoa inafanyiakazi na mwaka ujao wa fedha tutavifikia kwa kila kijiji, kila tunapopata fedha kuhakikisha maeneo yote ya Liwale yanakwenda kupata maji safi na salama.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya afya, Mheshimiwa Mariam Madalu Nyoka, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 30

**Changamoto ya usafiri Hospitali ya Mkoa wa Ruvuma**

**MHE. MARIAM M. NYOKA** aliuliza: -

Je, Serikali haioni umuhimu wa kununua gari la utawala na gari la Mganga Mfawidhi katika Hospitali ya Mkoa wa Ruvuma?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Mheshimiwa Godwin Mollel majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Madalu Nyoka, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mhehsimiwa Spika, Serikali imenunua magari 727 kwa ajili ya kubebea wagonjwa na magari 146 kwa shughuli za kiutawala. Hadi sasa magari 20 yamepokelewa na magari 117 yapo njiani kutoka kwa mtengenezaji.

Mheshimiwa Spika, magari yote yanatarajiwa kuwasili nchini na kukabidhiwa katika vituo vya kutolea huduma kabla ya mwezi Juni 2023. Aidha, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Ruvuma ni miongoni mwa Hospitali zitakazopata mgao wa magari hayo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mariam Nyoka, Swali la nyongeza.

**MHE. MARIAM M. NYOKA:** Mheshimia Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi nyingine.

Mheshimiwa Spika, hospitali za Wilaya za Mkoa wa Ruvuma pamoja na vituo vyake vya afya vina changamoto kubwa ya magari ya kubebea wagonjwa, kutoka kwenye vituo vya afya kwenda kwenye hospitali za Wilaya au kwenda hospitali ya Rufaa ya Mkoa. Serikali ina mpango gani wa kupeleka magari ya kubebea wagonjwa katika vituo hivi

vya afya au hospitali zake za Wilaya Mkoa wa Ruvuma? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mhehsimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwamba anafuatilia vizuri sana masuala yanayoendelea kwenye Wilaya zao kwa kushirikiana na Wabunge.

Mheshimiwa Spika, unaona kwamba kuna magari ya kubebea wagonjwa zaidi ya 727 maana yake ni kwamba hakuna Wilaya ambayo itakosa gari. Tutashirikiana na wenzetu wa TAMISEMI kuyatizama yale maeneo *specific* yenye uhitaji maalum ambayo yanahitaji kupewa magari zaidi ya moja na nadhani eneo lake la Mkoa wa Rukwa ni mojawapo ya hiyo mikoa Lindi, Mtwara, Kigoma na sehemu zingine ili tuone ni namna gani tunatatua hilo tatizo kwa wakati ambao tumeusema hapa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, sina matangazo mpaka sasa hapa mbele, japo nawaona wageni hapo juu. Matangazo ya wageni yatakaponifikia nitawatangaza wageni tulio nao Bungeni. Sasa nimuite Katibu ili tuendelee na ratiba yetu. Katibu.

**5 APRILI, 2023**

**NDG. NENELWA J. MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa Fedha 2023/2024

**SPIKA:** Sasa nitumie fursa hii kumuita Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa kwa ajili ya kuwasilisha makadilio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Mheshimiwa Waziri Mkuu, karibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimia Spika, nashukuru sana. Naomba kutoa hoja kwamba kutokana na taarifa zilizowasilishwa leo ndani ya Bunge lako tukufu na Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge za Utawala, Katiba na Sheria; Afya na Masuala ya UKIMWI; Ustawi na Maendeleo ya Jamii; na Bajeti zilizochambua Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Mfuko wa Bunge, sasa naliomba Bunge lako lipokee na kujadili Taarifa ya Mapitio ya Utekelezaji wa Kazi za Serikali kwa mwaka 2022/2023 na Mwelekeo wa Kazi zake kwa mwaka 2023/2024. Aidha, naomba Bunge lako tukufu likubali kupitisha makadirio ya mapato na matumizi ya fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu na taasisi zilizo chini yake pamoja na Ofisi ya Bunge kwa mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ninamshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa fadhila zake ambazo zimetuwezesha kukutana hapa leo kwa ajili ya kujadili taarifa ya mapitio ya utekelezaji wa kazi za serikali kwa mwaka 2022/2023 na mwelekeo wake kwa mwaka 2023/2024 tukiwa wenye afya njema.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kuwa huu ni Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge la Kumi na Mbili ambao ni mahsusi kwa ajili ya mjadala wa Bajeti, niwaombe

Waheshimiwa Wabunge wenzangu, tuitumie vyema fursa hii kutoa maoni na ushauri ili kuisaidia Serikali kuimarisha utekelezaji wa vipaumbele vilivyoainishwa kwenye Mpango na Bajeti ya mwaka 2023/2024. Napenda kuwahakikishia kuwa Serikali itapokea maoni na ushauri wenu na kuyafanyia kazi kwa maslahi mapana ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, ninatoa salamu za pole kwa nchi yetu kwa nyakati tofauti imekumbwa na maafa na matukio mbalimbali yaliyosababisha athari mbalimbali zikiwemo vifo, majeruhi na uharibifu wa mali na mazingira. Nitumie fursa hii kuwapa pole Watanzania wote waliopoteza ndugu, jamaa na mali zao katika maafa. Aidha, ninamwomba Mwenyezi Mungu awajalie majeruhi wote uponyaji wa haraka na aendelee kuwapumzisha kwa amani wale waliopoteza maisha

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii vilevile kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kutuongoza vyema na kupata maendeleo na mafanikio makubwa katika kipindi kifupi cha miaka miwili ya uongozi wake. Mafanikio hayo ni pamoja na uboreshaji wa miundombinu na huduma za afya, maji, elimu, umeme na uchukuzi, kuboresha hali ya chakula na lishe na kuimarisha hali ya kisiasa nchini na mahusiano ya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kutokana na uongozi wake makini na jitihada zao katika kuhakikisha Taifa letu linapata maendeleo.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amefanya teuzi na mabadiliko ya baadhi ya Watendaji

Wakuu wa Taasisi na viongozi wa Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Mabadiliko hayo, yamelenga kuimarisha utendaji kazi Serikalini ikiwa ni pamoja na utoaji huduma bora na kushughulikia kero mbalimbali za wananchi.

Mheshimiwa Spika, ninawapongeza sana viongozi na watendaji wote walioteuliwa na Mheshimiwa Rais wetu mpendwa kushika nyadhifa mbalimbali. Kipekee, niwapongeze Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama Mbunge wa Peramiho na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu; Mheshimiwa George Boniface Simbachawene Mbunge wa Kibakwe na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; na Mheshimiwa Abdallah Hamis Ulega Mbunge wa Mkuranga na Waziri wa Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Spika, vilevile, nimpongeze Mheshimiwa Hamis Mohamed Mwinjuma almaarufu Mwana FA, Mbunge wa Jimbo la Muheza kwa kuteuliwa kushika nafasi ya Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo. Ninawatakia kila la kheri Viongozi wote walioteuliwa katika utekelezaji wa majukumu yao mapya.

Mheshimiwa Spika, vilevile, nitumie fursa hii kuwasisitiza wateuliwa wote kuzingatia maelekezo mbalimbali ya Mheshimiwa Rais yakiwemo aliyatoa kwenye semina ya uongozi iliyofanyika hivi karibuni, Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2022 pamoja na mipango ya kitaifa na kimataifa katika utekelezaji wa majukumu yao. Aidha, natoa rai kwa viongozi hao kuhakikisha wanatanguliza mbele maslahi ya Taifa na kuwahudumia wananchi ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kukupongeza wewe binafsi kwa kuliongoza Bunge hili kwa hekima na umahiri mkubwa. Nampongeza pia Mheshimiwa Naibu Spika kwa

namna ambavyo ameendelea kusimamia shughuli za Bunge kwa uwezo mkubwa.

Waheshimiwa Wabunge wenzangu, hakika mtakubaliana nami kuwa viongozi hawa ni makini sana na wameonesha ukomavu mkubwa sana wa kisiasa wakati wote wakiendesha vikao vya Bunge hili. Nitoe wito kwetu sote tuendelee kuwapa ushirikiano ili waendelee kuliongoza vema Bunge letu na kulifanya liendelee kuheshimika ndani na nje ya mipaka ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii pia, kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mbunge wa Madaba na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria; Mheshimiwa Stansilaus Nyongo, Mbunge wa Jimbo la Maswa Mashariki na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI; Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, Mbunge wa Viti Maalumu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii; Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Mbunge wa Babati Vijijini na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti; na Wajumbe wote wa Kamati hizo kwa michango yao iliyosaidia kuboresha Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Mfuko wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, natambua ulifanya mabadiliko ya Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati za Kudumu za Bunge. Nitumie nafasi hii kuwapongeza sana wote walioteuliwa na kuwatakia kila la heri katika utekelezaji wa majukumu yao. Vilevile, nawashukuru sana Wajumbe wa Kamati zote za Kudumu za Bunge kwa ushauri walioutoa wakati wa kupitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara, Mikoa, Wakala, Idara za Serikali zinazojitegemea na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Maoni na ushauri wao utazingatiwa vilivyo wakati wa utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako tukufu lilifanya Uchaguzi wa Wenyeviti wa Bunge ambao watakusaidia kuongoza vikao vya Bunge. Nawapongeza Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge wa Viti Maaalum na Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii na Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Mbunge wa Babati Vijijini na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, pamoja na Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile, Mbunge wa Mufindi Kusini; na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kwa kuchaguliwa kuwa Wenyeviti wa Bunge. Nawapongeza sana na kuwatakia majukumu mema ya kuliongoza Bunge letu.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu Kiongozi, Wakuu wa Mikoa, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Makatibu Wakuu, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Naibu Makatibu Wakuu na Wakuu wa Wilaya, Idara, Mashirika, Wakala na Taasisi zote za Serikali kwa ushirikiano mkubwa mnaonipa katika kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Kipekee, niwapongeze na kuwashukuru wafanyakazi wote wa Serikali na taasisi zake kwa kufanya kazi kwa weledi, utaalamu na umahiri mkubwa na hivyo, kuwezesha Serikali kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, nawashukuru Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, Mbunge wa Peramiho na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), pia Mheshimiwa Profesa Joyce Lazaro Ndalichako, Mbunge wa Kasulu Mjini na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu. Pia, Mheshimiwa Paschal Patrobas Katambi, Mbunge wa Shinyanga Mjini na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), pamoja na Mheshimiwa Ummy Hamis Nderiananga, Mbunge wa Viti Maalumu na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera,

Bunge na Uratibu) kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu.

Mheshimiwa Spika, vilevile nitumie nafasi hii kuwashukuru sana Dkt. Jim James Yonazi, Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Profesa Jamal Adam Katundu, Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Wakurugenzi na Wakuu wa Vitengo, Wakuu wa taasisi zilizopo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu na wafanyakazi wote kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa wakati nikitekeleza majukumu yangu.

Mheshimiwa Spika, aidha, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitamshukuru Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, Mbunge wa Kibakwe na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; pia, Dkt. John Antony Kiang'u Jingu, Katibu Mkuu, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu na Bwana Kaspar Kaspar Mmuya, Katibu Mkuu, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa ushirikiano walionipa wakati wakiwa Waziri wa Nchi, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu mtawalia katika Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu). Ahsante sana na hongereni sana kwa kupata nafasi nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuzishukuru sekta binafsi, nchi rafiki, washirika wa maendeleo, taasisi na mashirika ya kimataifa na madhehebu ya dini kwa kuendelea kuunga mkono juhudi za Serikali za kuleta maendeleo. Serikali inatambua na kuthamini michango yenu, hususan katika utekelezaji wa afua muhimu kwa kutoa misaada, mikopo nafuu na wakati mwingine utaalamu, kitendo ambacho kimekuwa chachu ya kuharakisha maendeleo ya yetu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo, naomba kuwasilisha makadirio ya bajeti ambayo ni sehemu ya

utekelezaji wa vipaumbele vilivyobainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi mwaka 2020 na maelekezo ya nyaraka za kisera na za kitaifa, kikanda na kimataifa, ikiwemo Dira ya Maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki 2050, Ajenda 2063 ya Maendeleo ya Afrika, Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030, Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano, na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2023/2024. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nielezee kidogo Utekelezaji wa Miradi ya Kipaumbele kwa mwaka 2022/2023. Serikali imeendelea kutekeleza miradi ya maendeleo itakayoimarisha uchumi wa nchi na maendeleo ya watu. Hadi kufikia Januari, 2023 zimetolewa takribani shilingi trilioni 8.64 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya miundombinu ya reli, barabara, viwanja vya ndege, huduma za jamii na nishati. Utekelezaji wa miradi hiyo upo katika hatua mbalimbali kama ifuatavyo:-

Mosi, Ujenzi wa Reli ya Kati kwa Kiwango cha Kimataifa *(SGR)*. Serikali imetoa jumla ya shilingi bilioni 762.99 kutekeleza mradi huo ambapo kipande cha Dar es Salaam – Morogoro chenye urefu wa kilometa 300 utekelezaji wake umefikia asilimia 97.91. Kipande cha Morogoro – Makutupora chenye urefu wa kilometa 422 kimefikia asilimia 92.23 na kipande cha Mwanza – Isaka kilometa 341 kimefikia asilimia 25.75. Kipande cha Makutupora – Tabora kilometa 371 kimefikia hatua ya asilimia 4.59 na kuanza kwa ujenzi wa kipande cha Tabora - Isaka kilometa 165 na Tabora – Kigoma kilometa 105 maandalizi yake yanaendelea.

Pili, Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere utakaotoa megawati 2,115. Serikali imetoa takribani shilingi bilioni 869.93 kwa ajili utekelezaji wa mradi huu ambao umefikia asilimia 83. Zoezi la ujazaji maji katika bwawa lilizinduliwa rasmi na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 22

Desemba, 2022. Hadi Februari, 2023 kiwango cha maji kimefikia mita 134.39 kutoka usawa wa bahari ikilinganishwa na kiwango cha mita 163 kinachohitajika ili kuanza uzalishaji. *(Makofi)*

Tatu, Uboreshaji wa Shirika la Ndege Tanzania. Utekelezaji wa mradi huu umegharimu takribani shilingi bilioni 20.52. Shughuli zilizofanyika ni pamoja na kulipa sehemu ya gharama za ununuzi wa ndege tano ambapo kati ya hizo, ndege moja ni aina ya Boeing 767-300F ya mizigo, ndege mbili aina ya Boeing 737-9, ndege moja aina ya Boeing 787-8 *Dreamliner* na ndege moja aina ya *De Havilland Dash 8-Q400*. Ndege nne kati ya 13 hizo zinatarajiwa kuwasili nchini kabla ya Novemba, 2023 na ndege moja ya mizigo inatazamiwa kuwasili nchini hivi karibuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuwasili kwa ndege hizo kutasaidia Shirika la Ndege Tanzania *(ATCL)* kutanua mtandao wa safari za ndani na nje ya nchi na hivyo kuchochea ukuaji wa sekta nyingine za uchumi kama utalii, biashara na kilimo. *(Makofi)*

Nne, Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi kutoka Hoima, Uganda hadi Tanga, Tanzania lenye urefu wa kilometa 1,443. Takribani shilingi bilioni 30.39 zimetolewa ili kulipa fidia wananchi 7,486 kati ya 9,122 wanaopisha eneo la mkuza wa bomba na Serikali imeendelea kulipa hisa za umiliki katika Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki hadi kufikia dola za Marekani milioni 131. Aidha, tayari kibali cha kuanza ujenzi wa Bomba la Mafuta kimetolewa Januari, 2023. Vilevile, ujenzi wa karakana ya kuweka mfumo wa kupasha joto mabomba katika Kijiji cha Sojo, Nzega Tabora umefikia asilimia 49.

Tano, Mradi wa Kiwanda cha Sukari Mkulazi. Takribani shilingi bilioni 39.84 zimetolewa ili kuendelea na ujenzi wa kiwanda ambao umefikia asilimia 75. Aidha, hekta 219 zimepandwa miwa na kufanya ukubwa wa eneo lililopandwa

miwa kufikia hekta 2,974 sawa na asilimia 83 ya lengo la kupanda hekta 3,600. Kiwanda hicho kinatarajiwa kuongeza uzalishaji wa tani 50,000 za sukari kwa mwaka pindi kitakapoanza uzalishaji na hivyo kupunguza mahitaji ya kuagiza sukari kutoka nje ya nchi.

Sita, Mradi wa Daraja la Kigongo – Busisi, Mwanza. Takribani shilingi bilioni 93.09 zimetolewa kuendelea na ujenzi wa daraja hili ambao umefikia asilimia 63. Kukamilika kwa Daraja hili kutapunguza muda wa wananchi kuvuka eneo la Kigongo – Busisi kutoka takribani masaa mawili mpaka dakika nne kwa kutumia usafiri wa gari na dakika 10 kwa watembea kwa miguu. Aidha, daraja hili litakuwa na uwezo wa kupitisha magari ya aina yote wakati wote na kubeba uzito hadi tani 160. *(Makofi)*

Saba, Miradi ya Ujenzi na Ukarabati wa Viwanja vya Ndege. Serikali ilitoa takribani bilioni 77.23 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato ambapo utekelezaji umeshafikia asilimia 10.2. Kazi nyingine ni kukamilika kwa upanuzi wa njia ya kutua na kuruka ndege na kufungwa kwa mfumo wa kuongozea ndege katika Kiwanja cha Ndege cha Dodoma, kukamilika kwa ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Geita na kuendelea na ujenzi na ukarabati wa Viwanja vya Ndege vya Songea kwa asilimia 98, Iringa asilimia 42 na Musoma asilimia 43.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kuhusu hali ya uchumi nchini. Kwa kipindi cha takribani mwaka mmoja sasa, dunia imekumbwa na msukosuko wa kiuchumi kutokana na vita inayoendelea baina ya nchi za Ukraine na Urusi. Vita hiyo ilianza wakati uchumi wa dunia ukiwa bado haujatengemaa kutoka kwenye madhara ya janga la UVIKO–19. Kwa msingi huo, tumeshuhudia uchumi wa mataifa makubwa hususan katika Bara la Ulaya ukiyumba na gharama za maisha kuongezeka kutokana na mfumuko wa bei za nishati na chakula duniani.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa ya Shirika la Fedha Duniani ya Januari, 2023, kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia imepungua kutoka asilimia 6.2 mwaka 2021 hadi asilimia 3.4 mwaka 2022. Aidha, kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia inatarajia kupungua na kufikia asilimia 2.9 mwaka 2023. Vilevile kasi ya ukuaji wa uchumi wa nchi zilizoendelea imepungua na kufikia asilimia 2.7 mwaka 2023 kutoka asilimia 5.4 mwaka 2021 na inatarajiwa kupungua na kufikia asilimia 1.2 mwaka 2023.

Mheshimiwa Spika, uchumi wa nchi zinazoendelea na zinazoibuka kiuchumi ulipungua na kufikia asilimia 3.9 mwaka 2022 ikilinganishwa na asilimia 6.7 mwaka 2021. Aidha, ukuaji wa uchumi katika nchi zinazoendelea na zinazoibuka kiuchumi Barani Asia, ikijumuisha China na India ulipungua na kufikia asilimia 4.3 mwaka 2022 ikilinganishwa na asilimia 7.4 mwaka 2021. Kwa upande wa Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara, ukuaji wa uchumi ulipungua na kufikia wastani wa asilimia 3.8 mwaka 2022 ikilinganishwa na asilimia 4.7 mwaka 2021.

Mheshimiwa Spika, kiwango cha wastani wa ukuaji wa Pato la Taifa kwa kipindi cha mwaka 2022 kwa nchi nyingi za ukanda wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika ni asilimia 4.0 ikilinganishwa na wastani wa ukuaji wa asilimia 4.2 mwaka 2021. Aidha, wastani wa ukuaji wa uchumi kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ulikuwa ni asilimia 5.6 mwaka 2022 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 5.7 mwaka 2021.

Mheshimiwa Spika, hali hii imesababishwa na kupungua kwa uzalishaji na shughuli za kiuchumi katika nchi husika kwa mwaka 2020 kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo, utekelezaji wa masharti yaliyowekwa kuzuia maambukizi ya UVIKO-19 kama kufunga mipaka, kusitisha safari za ndege za kimataifa, kusitisha baadhi ya shughuli za kiuchumi

zinazohusisha mikusanyiko na kuzuia watu kutoka sehemu moja na kwenda nchi nyingine.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kusuasua kwa ukuaji wa uchumi wa dunia na Mataifa ya Afrika hususan nchi za ukanda wa Jangwa la Sahara, Jumuiya za *SADC* na Afrika Mashariki, hali ya ukuaji wa uchumi kwa nchi yetu kwa kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka ya kwanza hadi ya tatu ya mwaka 2022 imeimairika ikilinganishwa na mwaka 2021.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Januari hadi Septemba, 2022, uchumi wa Taifa ulikua kwa wastani wa asilimia 5.2 ikilinganishwa na asilimia 4.9 katika kipindi kama hicho mwaka 2021. Ukuaji chanya wa uchumi ulichangiwa na hatua zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ikiwemo, uwekezaji wa kimkakati katika miundombinu ya nishati, maji, afya, elimu, barabara, reli na viwanja vya ndege, lakini pia kuongezeka kwa uzalishaji wa madini, hususan dhahabu na makaa ya mawe, kuongezeka kwa mikopo katika sekta binafsi ambayo imechochea shughuli za kiuchumi na kuongezeka kwa shughuli za utalii.

Mheshimiwa Spika, ukuaji wa uchumi wa Tanzania kwa mwaka 2022 unatarajiwa kupungua hadi kufikia wastani wa asilimia 4.7 kutoka ukuaji wa asilimia 4.9 mwaka 2021 na kuongezeka hadi kufikia asilimia 5.3 mwaka 2023. Maoteo ya ukuaji wa uchumi wa Tanzania yamezingatia hatua zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali katika kukabiliana na athari zitokanazo na vita kati ya Ukraine na Urusi, ikiwemo kuchochea uzalishaji katika sekta za kilimo, mifugo, uvuvi na madini, uimarishaji wa miundombinu ya barabara mijini na vijijini, nishati na maji, uboreshaji wa huduma za jamii, kuendelea na utekelezaji wa miradi inayochachua shughuli za kiuchumi ikiwemo reli, upanuzi wa bandari, usambazaji umeme vijijini na uboreshaji wa mazingira ya biashara na uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kulingana na utabiri wa hali ya hewa ambao umebainisha uwezekano wa kuwa na mvua chini ya wastani, hali hiyo inaweza kuathiri uzalishaji katika sekta ya kilimo, upatikanaji wa nishati ya umeme, na maji na hivyo kuathiri ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Spika, madhara ya vita vya Urusi na Ukraine yamesababisha kuongezeka kwa kasi ya kupanda bei ya bidhaa kama mafuta duniani na hivyo kuchangia kuongezeka kwa gharama za uzalishaji na usafirishaji na kupanda kwa bei za bidhaa mbalimbali. Mfumuko wa bei nchini kwa mwaka 2022 ulifikia wastani wa asilimia 4.3 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 3.7 mwaka 2021. Hata hivyo, kiwango hiki kipo ndani ya malengo ya kati ya asilimia ya asilimia 3.0 hadi 5.0 na vigezo vya mtangamano wa kiuchumi wa kikanda wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika.

Mheshimiwa Spika, sababu zilizochangia kuongezeka kwa mfumuko wa bei katika kipindi husika ni pamoja na kupanda kwa bei za bidhaa ikiwemo mafuta ya kula, mbolea na petroli kufuatia kuvurugika kwa mnyororo wa uzalishaji na usambazaji wa bidhaa na huduma katika Soko la Dunia uliotokana na athari za vita kati ya nchi za Urusi na Ukraine na kupungua kwa upatikanaji wa mazao ya chakula nchini na nchi jirani kulikosababishwa na mabadiliko ya tabianchi hususan maeneo yanayotegemea mvua za vuli.

Mheshimiwa Spika, mfumuko wa bei nchini unatarajiwa kuendelea kuwa tulivu na kubaki katika wigo wa tarakimu moja na ndani ya vigezo vya mtangamano wa kiuchumi vya kikanda kutokana na hatua zilizochukuliwa na zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali, ikiwemo kuongeza bajeti katika sekta za kilimo, mifugo, uvuvi na nishati ili kuchochea uzalishaji wa ndani na kupunguza nakisi ya urari wa biashara, usimamizi madhubuti wa sera za fedha na bajeti, utulivu wa thamani ya shilingi na kuimarika upatikanaji wa umeme hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali inayolenga kuimarisha uwekezaji hapa nchini. Katika mwaka 2022/2023, Serikali kupitia Bunge lako Tukufu imetunga Sheria ya Uwekezaji Tanzania Namba 10 ya Mwaka 2022 ambayo pamoja na mambo mengine, inalenga kuweka mazingira bora ya uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali imeendelea kuratibu mradi wa maandalizi ya Kongani ya Viwanda ya Kwala yenye ukubwa wa ekari 2,500 ambapo kiasi cha dola za Kimarekani bilioni tatu zinatarajiwa kuwekezwa. Mradi huu unatarajiwa kuzalisha jumla ya ajira za moja kwa moja 100,000, ajira zisizokuwa za moja kwa moja 300,000 na bidhaa za takriban dola za Marekani bilioni sita kwa mwaka. Vilevile, Serikali inaendelea kuratibu maandalizi ya kongani na maeneo mengine ya kiuchumi ikiwemo, Kongani ya Magu na Misungwi pamoja na Eneo Maalumu la Kiuchumi la pale Nala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, Serikali inaendelea kuratibu maandalizi ya kongani na maeneo mengine ya kiuchumi ikiwemo, Kongani ya Magu na Misungwi pamoja na eneo Maalum la Kiuchumi Nala.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutekeleza programu zinazolenga kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara na uwekezaji nchini. Programu hizi zinajumuisha kuboresha mazingira ya uondoshaji wa shehena bandarini ambapo Serikali inajenga Mfumo wa Pamoja wa Kielektroniki wa Uondoshwaji wa Shehena 22 Bandarini. Aidha, Serikali imekamilisha mkakati wa uendeshaji wa mfumo huo na Mfumo wa Utoaji wa Vibali na Leseni za Mazao utakaounganishwa na Mfumo wa pamoja wa Kielektroniki wa Uondoshwaji wa Shehena Bandarini kwa ajili ya kurahisisha utoaji wa vibali na leseni za mazao.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/2024 Serikali itaendelea kuhamasisha Sekta Binafsi kushiriki katika miradi na programu za maendeleo ili kuongeza mchango wa sekta hiyo katika kukuza uchumi. Aidha, Serikali itaendelea kufanya mapitio ya Sera, Sheria, Kanuni na miongozo mbalimbali inayohusu uwekezaji kwa lengo la kuweka mazingira bora ya uwekezaji nchini ili pamoja na kukuza ushiriki wa Watanzania katika miradi ya kimkakati ya uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, hali ya siasa na kuimarika kwa demokrasia nchini; kwa ujumla hali ya siasa nchini ni tulivu na Vyama vya Siasa vinaendelea kutekeleza majukumu yao ikiwemo kufanya mikutano ya hadhara katika maeneo mbalimbali nchini. Aidha, Serikali imeendelea kuratibu vikao vya maridhiano ya kisiasa na Vyama vya Siasa nchini ili kuleta umoja, amani na utulivu katika nchi yetu ambao umekuwa ni utamaduni wetu tangu Uhuru.

Mheshimiwa Spika, kipekee naomba nimpongeze Mheshimiwa Daktari Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye amekuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha kunakuwepo na mtangamano wa kisiasa na unaojumuisha siasa safi, za kiustaarabu na zinazoheshimu mawazo ya kila mmoja wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kukuza na kuimarisha demokrasia ya vyama vingi nchini, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa imeratibu shughuli za Vyama vya Siasa kwa kuhakikisha kunakuwepo na fursa sawa katika shughuli za siasa hapa nchini. Katika mwaka 2022/2023 Serikali imetoa ruzuku jumla ya shilingi bilioni 17.5 kwa Vyama vya Siasa sita vyenye sifa ya kupata ruzuku. Vyama hivyo ni NCCR-Mageuzi, CCM, CHADEMA, DP, CUF na ACT-Wazalendo. Hatua hii, imesaidia kuendeleza na kuimarisha uendeshaji wa shughuli za Vyama vya Siasa na demokrasia nchini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2022/2023, chaguzi ndogo za ubunge ziliendeshwa katika jimbo la Amani Zanzibar na Udiwani katika kata 12 Tanzania Bara. Chaguzi hizo zimefanyika kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo vifo na baadhi ya Waheshimiwa Madiwani kukosa sifa za kuendelea na nyadhifa hizo.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuvishukuru vyama vyote vilivyoshiriki chaguzi hizo kwani vimeonesha ukomavu mkubwa wa kisiasa. Kipekee nikipongeze Chama cha Mapinduzi kwa ushindi wa Jimbo la Amani pamoja na viti 12 vya udiwani katika chaguzi hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/2024 shughuli za maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 pamoja na Uchaguzi wa Serikali za Mitaa utakaofanyika mwaka 2024 zitaendelea. Kazi zitakazofanyika ni pamoja na kulifanyia maboresho Daftari la Kudumu la Wapiga Kura; kuboresha mifumo ya menejimenti ya uchaguzi; kuendelea na mchakato wa marekebisho ya sheria za uchaguzi; kuandaa Kanuni za Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani; na kutoa elimu ya Mpiga kura kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuwaomba Viongozi wa Vyama vya Siasa kuhamasisha Wanachama na Watanzania wote wenye sifa kujiandikisha kwenye Daftari 25 hilo na kupata kitambulisho halali cha mpiga kura pale zoezi hilo litakapoanza rasmi.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie Bunge letu; katika mwaka 2022/2023 Ofisi ya Bunge imeendesha Mikutano Mitatu ya Bunge na Mikutano mitatu ya Kamati za Kudumu za Bunge. Katika kipindi hicho, jumla ya Maswali ya Msingi 460 pamoja na ya nyongeza 1,426 yaliulizwa Bungeni na kujibiwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, Bunge pia lilijadili na kupitisha Miswada saba na maazimio mawili ya Kimataifa yanayotokana na Kamati za Kudumu za Bunge na hatimaye kuwasilishwa Serikalini kwa utekelezaji. Vilevile Kamati za Kudumu za Bunge zilifanya uchambuzi wa Miswada ya Sheria, Sheria ndogo, Taarifa za Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali, Taarifa za Utendaji wa Wizara na Taasisi za Serikali na ufuatiliaji wa utekelezaji wa afua za UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/2024 Ofisi ya Bunge itaendelea kusimamia shughuli za mikutano minne ya Bunge na mikutano minne ya Kamati za Kudumu za Bunge. Kuratibu ushiriki wa Wabunge katika Mikutano ya Kimataifa ikiwemo Bunge la Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika, Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki, Bunge la Umoja wa Afrika na Mabunge ya Jumuiya ya Madola. Aidha, Ukumbi wa Bunge utaendelea kuimarishwa pamoja na kukarabati Jengo la kumbi za Bunge na majengo ya Ofisi.

Mheshimiwa Spika, sekta ya Mahakama; ni azma ya Serikali ya Awamu ya Sita kuhakikisha haki inapatikana kwa wananchi wote bila kujali hadhi ya mtu, uchumi wala kabila. Katika kutekeleza azma hiyo, Serikali imeendelea kufanya maboresho mbalimbali ya kiutendaji pamoja na ujenzi wa miundombinu muhimu ya mahakama kwa lengo la kuongeza ufanisi wa utendaji wa mahakama na kuimarisha mifumo ya utoaji haki.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2022/2023 Serikali imekamilisha miradi ya ujenzi wa Mahakama tatu za hakimu mkazi katika Mikoa ya Lindi, Songwe na Katavi. Aidha, ujenzi wa Mahakama za Wilaya 28 katika Wilaya za Same, Mwanga, Tandahimba, Nanyumbu, Namtumbo, Mvomero, Gairo, Ngara, Kilombero, Mkinga, Kakonko, Buhigwe, Uvinza, Butiama, Rorya, Itilima, Busega, Mbogwe, Nyang'hwale,

Kyerwa, Misenyi, Tanganyika, Kaliua, Manyoni, Bunda, Kilindi, Rungwe na Sikonge umekamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile ujenzi wa mahakama ya mwanzo katika Wilaya ya Kilindi eneo la Kimbe na ukarabati wa Mahakama Kuu ya Tabora pamoja na Mahakama ya Hakimu Mkazi Moshi umekamilika.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Serikali inaendelea na ujenzi wa Mahakama nne za Wilaya za Ulanga, Ubungo, Liwale na Kwimba pamoja na Mahakama za Mwanzo saba za Kinesi, Mahenge, Luilo, Newala, Usevya, Nyakibimbili na Kabanga. Kwa upande mwingine, inaendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa jengo la makao makuu Jijini Dodoma, nyumba za majaji na ukarabati wa jengo la zamani la makao makuu Dodoma na jengo la mahakama Wilaya ya Maswa.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha mifumo ya utoaji haki, Serikali imeongeza majaji wa mahakama ya rufaa kutoka 16 hadi 24 na wa mahakama kuu kutoka 78 hadi 98. Vilevile, idadi ya mahakimu iliongezeka kutoka mahakimu 245 hadi 293.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2022/2023 Mahakama imesikiliza na kukamilisha mashauri 134,989. Ufanisi huu umechangiwa na ongezeko la watendaji katika mahakama, kuendesha mashauri na mikutano kwa njia ya mtandao na kukamilika kwa miundombinu muhimu ya Mahakama.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/2024 Serikali itaendelea kutekeleza miradi ya ujenzi wa miundombinu kwa lengo la kusogeza huduma za Mahakama karibu na wananchi ili huduma hizo zipatikane kwa wakati na gharama nafuu.

Mheshimiwa Spika, sekta ya uzalishaji; nianze na kilimo, Serikali imeendelea kutoa kipaumbele katika sekta ya kilimo ili

kuinua Pato la Taifa na la mtu mmoja mmoja. Aidha, hatua mbalimbali zenye lengo la kuongeza tija na uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara zimeendelea kuchukuliwa. Hatua hizo ni pamoja na; kuwezesha wakulima kupata mbegu bora zinazoendana na hali ya hewa nchini; kutoa ruzuku ya pembejeo hususan mbolea na mbegu; kuwezesha upatikanaji wa teknolojia mpya na zana za 29 kisasa; kuimarisha huduma za ugani; kuongeza eneo la umwagiliaji kwa kuanzisha skimu mpya na kukarabati skimu za umwagiliaji zilizopo; na upatikanaji wa masoko ya mazao ndani na nje ya nchi ili kuhakikisha wakulima wananufaika na mauzo ya mazao.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2022/2023 Serikali imesaini Mikataba 31 yenye thamani ya jumla ya shilingi bilioni 284.14 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa skimu za umwagiliaji. Mikataba hiyo inahusu ujenzi wa mabwawa nane, skimu mpya 13 na ukarabati wa skimu za umwagiliaji 17. Ujenzi na ukarabati wa skimu hizo utaongeza eneo la umwagiliaji kwa hekta 50,930 na hivyo kufanya eneo la umwagiliaji kufikia hekta 778,210.6 kutoka hekta 727,280 mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto za hali ya hewa, hali ya upatikanaji wa chakula cha kutosha katika maeneo yote nchini imeendelea kuimarika. Katika msimu wa kilimo wa mwaka 2022/2023, uzalishaji wa mazao ya chakula kitaifa ulikuwa tani milioni 17.4 ikilinganishwa na mahitaji halisi ya tani milioni 15.1. Uzalishaji huo umeihakikishia nchi utoshelevu wa chakula kwa asilimia 115 kwa msimu wa kilimo wa mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uwepo wa ziada ya mazao ya chakula. Nitoe wito kwa Watanzania kuhifadhi mazao ya nafaka kwani utengamano wa hali ya chakula nchini umeendelea kuwepo kutokana na ziada inayotokana na mazao yasiyo ya nafaka.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kuhakikisha hali ya chakula inaendelea kuimarika. Hadi Januari, 2023, tani 29,084.21 za mahindi zilisambazwa katika Halmashauri 59 zilizopata changamoto ya upungufu wa chakula kwa mwaka 2022/2023. Mahindi hayo yaliuzwa kwa bei ya chini ya soko ili kuimarisha upatikanaji wa chakula katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hatua hizo, Serikali imeendelea kuratibu upatikanaji wa mbolea, mbegu bora na viuatilifu kwa wakati ili kuongeza uzalishaji na tija katika kilimo. Hadi Februari, 2023, upatikanaji wa mbolea umefikia tani 407,333 sawa na asilimia 58.33 ya mahitaji ya tani 698,260. Upatikanaji huo umechangiwa na tani 28,672 zilizozalishwa ndani, tani 251,697 zilizoingizwa kutoka nje ya nchi na tani 126,963 ambazo ni bakaa ya msimu wa 2022/2023. Serikali inaendelea kuhakikisha mbolea iliyobaki inapatikana na kusambazwa kwa wakulima kwa wakati ili kukidhi mahitaji ya kila mkoa na kupunguza makali ya bei.

Mheshimiwa Spika, Serikali katika kukabiliana na changamoto ya uzalishaji wa ndani wa mafuta kula, imetoa tani 591.1 za mbegu za alizeti kwa wakulima wa Mikoa ya Singida, Dodoma, Kagera, Mbeya na Mwanza kwa utaratibu wa ruzuku. Hatua hiyo, itasaidia sana kuongeza uzalishaji wa mafuta ya kula na kupunguza matumizi ya fedha za kigeni kuagiza kutoka nje ya nchi. Vilevile imegawa lita 63,606 za viuatilifu katika mikoa 15 nchini ili kuthibiti viwavijeshi, nzi wa matunda na ndege waharibifu aina ya kwelea kwelea. Hatua hiyo imesaidia kuokoa ekari 159,015 za mazao mbalimbali yakiwemo mahindi na mpunga.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kasi ya kutoa huduma kwa wakulima inaongezeka, Serikali imeendelea kuimarisha huduma za ugani kwa kutoa mafunzo na vitendea kazi kwa maafisa ugani. Licha ya hayo, imeanzisha Kituo Cha Huduma kwa Wateja. Kituo hicho kimeshatoa huduma ya

ushauri na taarifa za kilimo kwa wakulima na wadau wapatao 12,248. Aidha, kwa kupitia Mfumo wa M-Kilimo, wakulima 7,269,101 na Maafisa Ugani 9,985 wamesajiliwa kwa ajili ya huduma za ushauri wa kitaalamu. Teknolojia hii itawawezesha wakulima, wafugaji na wavuvi kuyafikia masoko ya mazao kwa njia ya simu.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kuimarisha ushirika nchini. Hatua hizo ni pamoja na kutoa mafunzo kwa watendaji, kuimarisha udhibiti na usimamizi wa Vyama vya Ushirika; kuhamasisha Wananchi kujiunga au kuanzisha Vyama vya Ushirika; kuimarisha upatikanaji wa masoko ya ndani na nje ya Nchi; kukuza matumizi ya TEHAMA na kufanya kaguzi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hatua hizo, mauzo kuipitia vyama vya ushirika yameongezeka ambapo hadi Januari 2023, zimeuzwa jumla ya tani milioni 1.83 zenye thamani ya shilingi trilioni 1.7 ikilinganishwa na tani 597,298 zenye thamani ya shilingi trilioni 1.5 mwaka 2021/2022 kutoka kwenye mazao ya tumbaku, korosho, pamba, kahawa, ufuta, kakao, mkonge, chai, mbaazi, soya, zabibu, miwa na maharage.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa uwezeshaji, Benki ya Maendeleo ya Kilimo imefanikiwa kutoa mikopo ya moja kwa moja yenye thamani ya shilingi bilioni 78.54 kwa wakulima 119,797 wanaojishughulisha na kilimo, mifugo na uvuvi. Aidha, kupitia Mfuko wa Dhamana kwa Wakulima Wadogo imetoa dhamana ya mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 12.95 na kunufaisha wananchi 961 katika Mikoa 20 katika shughuli za kilimo, mifugo na uvuvi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/2024 Serikali itaendelea kuongeza uzalishaji na tija; kuimarisha miundombinu ya umwagiliaji, na upatikanaji wa pembejeo. Vilevile, itaendelea kuimarisha huduma za ugani na

upatikanaji wa masoko ya mazao ya kilimo na kuwajengea uwezo wakulima wadogo.

Mheshimiwa Spika, kuimarika kwa huduma za ugani ikiwemo utoaji elimu kwa umma kuhusu ufugaji bora wa ng'ombe wa maziwa wa kibiashara umesababisha kuongezeka kwa uzalishaji wa maziwa kufikia lita bilioni 3.62 katika mwaka 2022/2023 ikilinganishwa na lita bilioni 3.4 mwaka 2021/2022. Aidha, uzalishaji wa zao la nyama umeongezeka kwa asilimia 4.3 kutoka tani 769,966.66 mwaka 2021/2022 hadi tani 803,264.32 mwaka 2022/2023. Vilevile, jumla ya vipande milioni 14.19 vya ngozi vyenye thamani ya shilingi bilioni 31.11 vilizalishwa ikilinganishwa na vipande milioni 13.56 vyenye thamani ya shilingi bilioni 28.5 vilivyozalishwa mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2022/2023, Serikali imenunua pikipiki 1,200 na magari 13 ili kurahisisha utoaji wa huduma za ugani katika ngazi ya Kata na Vijiji. Vilevile Serikali imewezesha mafunzo rejea kwa Maafisa Ugani 487 na Wataalam Wawakilishi 28 kutoka Sekta Binafsi katika kanda nane. Mafunzo hayo yalihusu Mpango wa Mabadiliko wa Sekta ya Mifugo, Ufugaji bora na wa Kibiashara, Fursa za Uwekezaji katika Sekta ya Mifugo, Matumizi ya Mifumo ya TEHAMA katika utoaji wa huduma za Ugani, Uboreshaji wa Kosaafu za Mifugo, Udhibiti wa Magonjwa ya Mifugo, Uendelezaji wa malisho na upatikanaji wa maji.

Mheshimiwa Spika, vifo vya mifugo vinavyotokana na magonjwa yanayoenezwa na kupe vimepungua kwa takriban asilimia 60. Mafanikio hayo yametokana na hatua ya Serikali kuimarisha huduma za mifugo pamoja 35 na ujenzi wa miundombinu muhimu ikiwemo majosho ya kuogesha mifugo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/2024 Serikali itaendelea kuimarisha sekta ya mifugo kwa kuhakikisha upatikanaji wa mbegu bora za mifugo, malisho, maji na

vyakula vya mifugo. Halikadhalika, Serikali itaboresha huduma za utafiti na mafunzo ya taaluma za mifugo pamoja na kuanzisha na kuendeleza vituo atamizi vya uwekezaji vya vijana.

Mheshimiwa Spika, Kwa Sekta ya Uvuvi, Serikali imeendelea kuinua kipato cha wananchi wake, kuimarisha upatikaji wa samaki na uendelevu kupitia ukuzaji wa viumbe maji. Katika mwaka 2022/2023, tani 28,856.87 za samaki zilivuliwa kutoka katika ukuzaji viumbe maji ikiwemo ufugaji kwenye mabwawa na vizimba. Kiasi hicho cha samaki kiliwezesha mauzo ya nje ya nchi yenye thamani ya shilingi bilioni 238.49. Vilevile tani za mwani 4,134.6 zenye thamani ya shilingi bilioni 4.34 zilizalishwa na kuuzwa nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2022/2023 Serikali imeendelea kuboresha hali ya masoko ya samaki nchini kupitia ujenzi wa masoko mbalimbali ya samaki. Masoko yaliyoboreshwa ni pamoja na Zingibari (Halmashauri ya Mkinga), Kipumbwi (Pangani), Ng'ombo (Nyasa), Manda (Ludewa), Maporomoko (Tunduma), Kyamkwikwi (Muleba), Nyamikoma kule Busega pamoja na Mialo ya kupokelea samaki katika Halmashauri za Momba (Masuche), Nkasi (Karungu) na Chato *(Chato beach)*.

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2023/2024 Serikali itendelea kuimarisha upatikanaji wa mbegu bora za mifugo, marisho, vyakula vya mifugo na maji. Vilevile itatoa kipaumbele katika kuimarisha afya ya mifugo, kuboresha huduma za ugani, kuanzisha na kuendeleza vituo atamizi vya uwekezaji vya vijana, kuimarisha huduma za utafiti na mafunzo ya taaluma za mifugo vilevile.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Serikali itaendelea kuimarisha Shirika la Uvuvi Tanzania, usimamizi na udhibiti wa ubora, usalama na viwango vya samaki na mazao ya uvuvi pamoja na kuimarisha huduma za utafiti, mafunzo na ugani. Aidha, Serikali itaimarisha miundombinu ya masoko ya samaki, vituo

vya kuendeleza ukuzaji wa viumbe maji na kuanza ujenzi wa meli za uvuvi katika bahari kuu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maliasili na utalii; Serikali imeendelea kuimarisha sekta za maliasili na utalii kupitia utekelezaji wa programu mbalimbali ili kukuza utalii, hasa kuitangaza nchi yetu na vivutio vyake kitaifa na kimataifa pamoja na kuimarisha mchango wa sekta hizo kwenye Pato la Taifa. Katika mwaka 2022/2023, programu mbalimbali zimeendelea kutekelezwa ikiwemo Programu ya *Tanzania - The Royal Tour* na utangazaji wa vivutio vya utalii kupitia matukio mbalimbali na vyombo vya habari ikiwemo *Tanzania Safari Channel.*

Mheshimiwa Spika, kutokana na jitihada hizo, idadi ya watalii wa kimataifa imeongezeka kutoka watalii 922,692 katika mwaka 2021 hadi kufikia watalii takribani milioni 1.4 kwa mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 57.7. Vilevile idadi ya watalii wa ndani imeongezeka kutoka watalii 788,933 mwaka 2021 hadi watalii milioni 2.4 kwa mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 199.5. Aidha, Hifadhi ya Taifa ya Serengeti imeendelea kuwa hifadhi bora duniani ambapo kwa miaka minne mfululizo kuanzia mwaka 2019 hadi mwaka 2022 imepata tuzo ya dhahabu ya utoaji wa huduma bora iliyotolewa na *European Society for Quality Research.*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Hifadhi ya Taifa ya Ngorongoro, kumekuwa na changamoto ya ongezeko la watu, mifugo, makazi holela na shughuli za kibinadamu, hivyo kukosekana kwa uwiano baina ya uhifadhi, ukuzaji wa utalii na maendeleo ya jamii. Hali hiyo imekuwa ikitishia uendelevu wa hifadhi na ustawi wa maisha ya watu wetu wanaoishi katika hifadhi hiyo kutokana na sheria za uhifadhi kutoruhusu shughuli nyingine za kiuchumi na kimaendeleo katika eneo hilo. Ili kutatua changamoto hiyo, Serikali iliendesha zoezi la hiari la kuondoa makazi na shughuli za kibinadamu ndani ya Hifadhi kwa kuhamisha wenyeji waliokuwa tayari kuhama

kwenda kwenye maeneo yaliyotengwa katika Kijiji cha Msomera katika Halmashauri za Wilaya za Handeni na Kilindi Mkoani Tanga.

Mheshimiwa Spika, zoezi hilo limefanyika kwa umakini mkubwa na kwa kuzingatia haki za wanaohama. Hadi kufikia Januari, 2023 jumla ya kaya 1,524 zenye watu 8,715 na mifugo 32,842 zilikuwa zimekwisha andikishwa kwa ajili ya kuhama kwa hiari kwenda Kijiji cha Msomera. Kati ya kaya hizo, kaya 551 zenye watu 3,010 na mifugo 15,521 tayari zimehamishwa kwa hiari kwenda Msomera.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/2024 Serikali itaendelea kuibua na kuendeleza mazao ya utalii ya kimkakati ikiwemo utalii wa fukwe, mikutano na matukio mbalimbali, meli, michezo na utamaduni. Vievile, itaendelea kuimarisha miundombinu katika maeneo ya hifadhi, kukarabati majenzi ya kale na kuyatangaza kidijitali pamoja na kutekeleza mikakati ya kuongeza thamani ya mazao ya misitu.

Mheshimiwa Spika, sekta ya madini; Serikali imeendelea kuipa kipaumbele sekta ya madini ili kuhakikisha inanufaisha wananchi na kuongeza mchango wa sekta hiyo kwenye Pato la Taifa. Katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali ilianzisha vituo 26 vya ununuzi wa madini na kutoa jumla ya leseni tano za uchenjuaji wa madini. Aidha, jumla ya shilingi bilioni 409.66 sawa na asilimia 85.43 ya lengo la shilingi bilioni 479.55 zilikusanywa kutokana na mrabaha, ada ya ukaguzi, mauzo ya madini kwenye masoko na vituo na ada ya leseni za uchimbaji.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/2024 Serikali itaendelea kuhamasisha biashara na uwekezaji katika sekta ya madini, kuwaendeleza wachimbaji wadogo, kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini, kusimamia mifumo ya

ukaguzi wa shughuli za migodi na kuzijengea uwezo taasisi zinazosimamia sekta hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa sekta ya nishati Serikali imeendelea kutekeleza azma yake ya kuimarisha shughuli za kiuchumi na kijamii kwa kuhakikisha wananchi wake wanapata nishati ya umeme, mafuta na gesi kwa uhakika na bei nafuu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2022/2023, Serikali imeendelea kutekeleza miradi ya kusambaza umeme vijijini awamu ya tatu mzunguko wa pili. Hadi Machi, 2023 asilimia 76.7 ya vijiji vya Tanzania Bara vimeunganishwa na huduma ya umeme. Utekelezaji wa miradi hiyo ikiwa ni pamoja na mkakati wa kuboresha upatikanaji wa nishati bora na safi ya kupikia kwa wananchi wanaoishi vijijini inaendelea vizuri na ipo katika hatua mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2022/2023, Serikali imekamilisha ufungaji wa mitambo mitatu yenye uwezo wa kuzalisha megawati 135 katika mradi wa *Kinyerezi I Extension*. Kufungwa kwa mitambo hiyo kumeongeza uwezo wa mitambo kufua umeme katika gridi ya Taifa kwa asilimia 7.52. Aidha, uboreshaji wa mtandao wa miundombinu ya kusafirisha na kusambaza umeme nchini umesaidia kuboresha maisha ya watu kwa kutoa fursa za kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mafuta na gesi; katika kutimiza azma ya kuhakikisha kuwa asilimia 80 ya Watanzania wanatumia nishati safi kupikia ifikapo mwaka 2033 kimeundwa kikosi kazi cha Taifa kuchakata na kutoa suluhu ya afua ya nishati safi ya kupikia ambacho kinasimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu. Hii ni kufuatia maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu matumizi ya nishati safi ya kupikia. Kazi zinazoendelea ni pamoja na kuandaa rasimu ya Dira ya Taifa

ya Miaka 10 ya Kuhamia katika matumizi ya nishati safi ya kupikia pamoja na Rasimu ya Mpango Mkakati.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa gesi, Serikali inaendelea kufanya tafiti katika vitalu vya mafuta na gesi katika vitalu vya kimkakati ikiwa ni pamoja na kuimarisha Mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia na Mkakati wa Matumizi ya Nishati Jadidifu na Tungamotaka.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/2024 Serikali itaendelea kukamilisha utekelezaji wa miradi ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa nishati ya umeme, mafuta na gesi. Aidha, Serikali itaendelea kutekeleza Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu na kusambaza umeme katika vitongoji 36,336 vya Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, sekta ya ardhi imeendelea kuwa kiungo wezeshi kwa shughuli za sekta nyingine za uzalishaji ikiwemo viwanda, kilimo, mifugo, maliasili, utalii, madini na miundombinu. Katika mwaka 2022/2023, Serikali imeandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji 110 katika halmashauri za wilaya 16 na Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Wilaya tatu za Kigoma, Nsimbo na Ngorongoro. Idadi hii inafanya kuwa na jumla ya vijiji 2,673 vyenye mipango ya matumizi ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/2024, Serikali itaendelea kuwezesha na kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijijini, wilaya na kanda, utatuzi wa migogoro ya ardhi, kuboresha Mfumo wa Taarifa za Matumizi ya Ardhi Nchini, na kupanga, kurasimisha na kumilikisha ardhi kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Usafiri na usafirishaji; Miundombinu ya usafiri na usafirishaji ni msingi wa uchumi wa Taifa na inatoa huduma muhimu kwa wananchi wetu. Usimamizi thabiti wa miundombinu hiyo unaipa fursa Serikali

kuongeza thamani ya huduma na rasilimali fedha zinazoonekana moja kwa moja kwa manufaa ya jamii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara na madaraja; katika mwaka 2022/2023 Serikali imejenga jumla ya kilomita 317.65 za barabara kwa kiwango cha lami ambazo zimehusisha barabara kuu, barabara za mikoa na wilaya. Ujenzi huo umesaidia kurahisisha utoaji wa huduma ya usafiri na usafirishaji katika maeneo tofauti nchini na umezingatia uendelevu kwa watumiaji wa sasa na wa baadaye.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kupunguza msongamano wa magari katika majiji na miji ili kuongeza ufanisi katika utendaji na utekelezaji wa majukumu ya wananchi na ukuaji wa uchumi wa Taifa. Katika hatua za kuhakikisha kuwa huduma za uchukuzi zinaboreshwa, Serikali inaendelea na awamu ya pili, tatu, nne na tano ya ujenzi wa barabara na miundombinu ya mabasi yaendayo haraka Mkoani Dar es Salaam na ujenzi wa barabara za mchepuo *(bypass)* katika Mkoa wa Dodoma na Wilaya ya Maswa.

Mheshimiwa Spika, Awamu ya Pili *(BRT II)* ya ujenzi huo inayohusisha barabara ya Kilwa kutoka katikati ya Jiji la Dar es Salaam kuelekea Mbagala na barabara ya Kawawa kutoka makutano ya Magomeni kupitia Chang'ombe hadi makutano ya barabara ya Kilwa umefikia asilimia 82. Mradi huu una barabara zenye urefu wa kilomita 20.3, vituo vya mabasi 29, barabara za juu mbili, majengo mawili ya *Terminal, Depot* moja na *Feeder station* nne. Aidha, awamu ya tatu *(BRT III)* inayohusisha barabara ya Nyerere kutoka katikati ya Jiji la Dar es Salaam hadi Gongolamboto yenye urefu wa kilometa 23.6 imekamilika kwa asilimia tano na ujenzi unaendelea.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Jiji la Dodoma, ujenzi wa barabara ya Mchepuko ya Dodoma imelenga kupunguza foleni ya magari katikati ya Jiji kutokana na

magari yanayosafiri katika Ushoroba wa kati na Ushoroba wa Barabara Kuu ya *Trans-Africa 4* inayoanzia Cape Town (Afrika Kusini) hadi Cairo, Misri. Mradi huu wenye barabara yenye urefu wa jumla ya kilometa 112.3 umefikia kwa asilimia 17 katika sehemu ya kwanza na sehemu ya pili imefikia asilimia 22. Aidha, ujenzi wa barabara ya mchepuo Maswa *(Maswa Bypass)* yenye urefu wa kilometa 11.3 kwa kiwango cha lami umefikia asilimia 72.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa vivuko; Serikali imeendelea kujenga vivuko vipya na kukarabati vivuko vilivyochakaa nchini ili kuwaondolea kero ya usafiri wananchi wanaotegemea vivuko ili kuharakisha na kurahisisha shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2022/2023 Serikali imeendelea na ujenzi wa vivuko vipya vya Kisorya – Rugezi, Ijinga – Kahangala, Bwiro – Bukondo na Nyakarilo – Kome. Vilevile, ujenzi wa vivuko vya Buyagu – Mbalika na Magogoni – Kigamboni ambao upo kwenye hatua za ununuzi. Aidha, ukarabati wa vivuko vya MV Musoma, MV Kazi, MV TEMESA na MV Tanga umekamilika kwa asilimia 100 na ukarabati wa vivuko vya MV Misungwi, MV Nyerere, MV Kilombero, MV Mara, MV Ujenzi, MV Kitunda, MV Ruhuhu, MV Old Ruvuvu na MV Magogoni unaendelea.

Mheshimiwa Spika, Viwanja vya Ndege na Usafiri wa Anga; Usafiri wa anga ni kiungo muhimu katika kuchangia ukuaji wa pato la mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla. Usafiri huu umeendelea kutengeneza fursa za ajira zilizo rasmi na zisizokuwa rasmi, kuimarisha upatikanaji wa huduma za usafiri wa uhakika, na hivyo kutoa mchango muhimu katika maendeleo ya kiuchumi. Kwa kutambua umuhimu huo, Serikali imeendelea kutoa kipaumbele katika uimarishaji na uboreshaji wa huduma za usafiri wa anga nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali katika mwaka 2022/2023 imeendelea na awamu ya kwanza ya ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato. Kukamilika kwa ujenzi wa kiwanja hiki kutarahisisha usafirishaji wa watu na bidhaa kutoka na kuingia katika Jiji la Dodoma, kati ya Tanzania na nchi mbalimbali, kukuza utalii na uchumi na kuongeza fursa za ajira. Aidha, ujenzi huo utakapokamilika pamoja na kuimarisha usafiri anga kwa kuruhusu ndege kubwa na za kimataifa kutua, utasaidia kufanya Jiji la Dodoma kuwa Jiji la kisasa na la kimataifa.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha usafiri wa anga, mashirika ya ndege ya nchi maarufu, kama vile Shirika la Ndege la *KLM, Eurowing Airline, Edelweiss airline* na Saudia *Airline* yameanza kutoa huduma za usafiri wa anga kuanzia Tanzania. Hatua hizi zitaendelea kuimarisha sekta ya utalii na hivyo kuongeza mchango wa sekta hiyo kwenye mapato na ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuzungumzia sekta ya Reli. Katika mwaka 2022/2023 Serikali imefanya ununuzi wa vifaa vya uendeshaji wa Reli ya *SGR* ambapo utengenezaji wa mabehewa 59 ya abiria umefikia asilimia 92. Kati ya mabehewa hayo, 14 yaliwasili nchini Novemba, 2022 na 45 yaliyobaki yanatarajiwa kuwasili Mei, 2023. Aidha, utengenezaji wa vichwa vya treni 17 vya umeme na seti 10 za treni *(Electric Multiple Unit - EMU)* kwa ajili ya treni ya abiria umefikia asilimia 31.6 na seti moja ya treni hizo inatarajiwa kuwasili Juni, 2023. Aidha, utengenezaji wa mabehewa 1,430 ya mizigo umefikia asilimia 35. Upatikanaji wa vifaa hivyo utaboresha na kuongeza kiwango cha ubebaji mizigo na kupunguza gharama za usafiri na usafirishaji, na hivyo kupunguza gharama za maisha.

Mheshimiwa Spika Aidha, katika mwaka wa fedha 2022/2023, pamoja na uendelezaji wa ujenzi wa reli ya *SGR,* Serikali imeendelea na ukarabati wa njia ya reli ya kati kutoka

Dar es Salaam hadi Mwanza, Kigoma na Mpanda. Mkataba wa ukarabati wa njia ya reli ya Kaliua-Mpanda ulishasainiwa Novemba, 2022.

Mheshimiwa Spika, Usafiri katika Maziwa Makuu; katika kuimarisha huduma za usafiri na usafirishaji katika maziwa makuu, Februari, 2023, meli ya MV Mwanza (Hapa Kazi Tu) iliyo katika Ziwa Victoria ilishushwa majini kwa ajili ya ukamilishaji. Meli hiyo inatarajiwa kuanza kutoa huduma katika mwaka 2023/2024. Aidha, ukarabati wa meli ya *MV* Umoja katika Ziwa Victoria na MT Sangara katika Ziwa Tanganyika unaendelea. Kukamilika kwa meli hizo kutaboresha huduma za usafiri wa abiria na mizigo kwa njia ya meli, kufungua masoko mapya ndani na nje ya nchi, kurahisisha shughuli za kibiashara, uzalishaji wa mazao, uvuvi, madini na kuchochea utalii katika maeneo ya maziwa makuu utakuwa umeimarika.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa bandari; Serikali imeendelea kutekeleza Mradi wa Bandari Kavu ya Kwala, ambapo ujenzi wa barabara ya zege yenye urefu wa kilometa 15.5 kutoka Vigwaza umefikia asilimia 98 na ujenzi wa Bandari umefikia asilimia 87. Kukamilika kwa bandari hiyo na kuanza kutumika kutapunguza msongamano wa mizigo na magari katika Bandari ya Dar es Salaam, kuongezea nafasi ya kuhifadhi mizigo na kupunguza muda wa magari kusafirisha mizigo nao tumeanza kushuhudia kasi hiyo inaendelea. Hali hiyo itaiwezesha Bandari ya Dar es Salaam kufanya kazi kwa ufanisi zaidi na hivyo kuongeza mapato kwa bandari na wafanyabiashara.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/2024 sekta ya usafiri na usafirishaji itaendelea kukamilisha ujenzi wa miundombinu na uboreshaji wa huduma za usafiri kwa njia reli, anga, barabara na majini. Aidha, Serikali imeamua kwa dhati kuanza ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo kwa kuhamisha wananchi waliolipwa fidia, wanaotakiwa kupisha ujenzi wa

bandari na kuanza maandalizi ya ujenzi wa miundombinu wezeshi kwa ajili ya bandari ya Bagamoyo ikiwemo barabara, reli na umeme.

Mheshimiwa Spika, naomba kuzungumzia maeneo ya Mawasiliano na teknolojia ya Habari. Serikali imeendelea kuimarisha miundombinu ya mawasiliano na teknolojia ya habari nchini kwa lengo la kuongeza chachu ya maendeleo ya jamii, siasa, usalama na uchumi kwa kuzingatia mabadiliko ya teknolojia ulimwenguni.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2022/2023 Serikali imeendelea kutekeleza Mfumo wa Anwani za Makazi kwa kuzingatia maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyatoa tarehe 08 Februari 2022 wakati wa uzinduzi wa Operesheni Anwani za Makazi. Utekelezaji wa Mfumo huo umefanyika nchi nzima ambapo hadi Februari 2023 jumla ya taarifa milioni 12.66 za anuani za makazi zikijumuisha majengo na viwanja zimekusanywa. Utekelezaji wa Mfumo wa anuani za makazi umewezesha utambuzi wa mtu, kitu au jengo lilipo na hivyo kuimarisha usalama na kurahisisha utoaji wa huduma na ufikishaji wa bidhaa mahali stahiki. Aidha, Serikali inaendelea na uhakiki wa taarifa za anwani za makazi zilizokusanywa ili kuboresha taarifa hizo.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Serikali imekamilisha ujenzi wa minara 1,201 katika kata 1,087 zenye vijiji 3,378. Kwa upande wa Zanzibar ujenzi wa minara 42 umekamilika na kufanya eneo lote la Zanzibar kuwa na mawasiliano ya simu. Aidha, Serikali imesaini mikataba ya ujenzi wa minara katika kata 1,242 zenye vijiji 3,684 Tanzania Bara. Kukamilika kwa miradi hiyo kutafanya Taifa kuongeza usikivu katika mawasiliano ya njia ya simu na usafirishaji wa taarifa kwa kasi na kiwango kinachokusudiwa. Nitoe wito kwa Watanzania wote kuendelea kuchangamkia fursa zinazotokana na matumizi ya teknolojia ya mawasiliano katika kujenga uchumi wa kidijitali.

Mheshimiwa Spika, Uchumi wa Kidijitali; ni ukweli usiopingika kuwa fursa za kidijitali na uchumi zimekuwa zikiongezeka ulimwenguni. Fursa hizo zimewezesha ushiriki wa watu wengi na kurahisisha upatikanaji wa huduma za kimtandao. Vilevile, maendeleo ya kidijitali yamerahisisha mawasiliano ya kijamii, kisiasa na kiuchumi kwa kupunguza gharama, kuokoa rasilimali muda na upatikanaji wa taarifa na fursa mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu huo, Serikali katika mwaka 2023/2024, itaendelea na maandalizi ya Mkakati wa Taifa wa Uchumi wa Kidijitali ili kuhakikisha nchi yetu haibaki nyuma katika ulimwengu wa kidijitali na kuwa wananchi wananufaika na fursa zitokanazo na uchumi huo. Kwa upande mwingine itaendelea kujenga misingi ya matumizi ya TEHAMA ikiwa ni pamoja na kuendeleza na kuboresha Mfumo wa Kidijitali wa Mfumo wa Anwani za Makazi.

Mheshimiwa Spika, Huduma za Jamii; nianze na Elimu, tangu awali Serikali ya Awamu ya Sita imejipambanua katika kuinua viwango vya elimu kwa kuweka mazingira bora ya kufundishia na kujifunzia. Hii ni pamoja na kuhakikisha kila mtoto wa Tanzania anapata fursa ya kusoma na kumaliza mzunguko wa elimu kama inavyotakiwa. Ili kutekeleza azma hiyo, Serikali imeendelea kujenga, kukarabati na kukamilisha miundombinu ya kutolea elimu katika ngazi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2022/2023, Serikali imeendelea na ujenzi wa shule mpya 231 za sekondari, upanuzi wa shule kongwe 11 za sekondari, ujenzi wa shule mpya sita za msingi, ujenzi wa vyumba vya madarasa 1,072 katika shule kongwe za msingi na ujenzi wa nyumba za Walimu 809 ambapo kati ya nyumba hizo, 298 ni za Walimu wa shule za msingi na 511 za Walimu wa shule za sekondari. Aidha, imeendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa shule za wasichana za bweni kidato cha tano na sita katika mikoa

yote Tanzania bara ambapo ujenzi wa shule 10 kati ya 26 umekamilika.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea pia kutoa mikopo na kuongeza wigo wa upatikanaji wa Mikopo ya Elimu ya Juu sambamba na kuboresha miundombinu ya vyuo vya elimu ya juu nchini. Katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, kiasi cha shilingi bilioni 654 zilitengwa kwa ajili ya mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu ikilinganishwa na shilingi bilioni 570 zilizotengwa mwaka 2021/2022. Aidha, idadi ya wanufaika imeongezeka kutoka 177,605 mwaka 2021/2022 hadi 202,877 mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia imeongeza kiwango cha posho ya kujikimu ya wanafunzi wa elimu ya juu kutoka shilingi 8,500 hadi shilingi 10,000 kwa siku. Mafanikio haya ni kielelezo tosha cha umakini, uzalendo, maono na mapenzi makubwa ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuboresha ustawi wa maisha ya wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu. Kwa upande mwingine, kupitia Samia *Scholarship,* Serikali imetoa ufadhili kwa wanafunzi 244 wa kike wenye ufaulu wa juu ili kusoma katika vyuo vikuu mbalimbali katika fani za Utabibu, Uhandisi, Sayansi, Teknolojia na Hisabati. Ama kwa hakika mama anajali! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/2024, Serikali itaendelea kuhuisha Mitaala ya Elimu na kuongeza fursa za upatikanaji wa elimu na mafunzo ya ufundi stadi na elimu ya juu.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Maji; Serikali imeendelea kuimarisha usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji ikiwa ni pamoja na kuhifadhi na kulinda vyanzo vya maji, kujenga mabwawa makubwa, ya kati na madogo katika maeneo mbalimbali nchini kwa lengo la kuongeza uwezo wa nchi

kuhifadhi maji na kuboresha huduma ya upatikanaji wa maji safi na salama katika maeneo ya miji na vijiji.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutekeleza dhamira yake ya kuhakikisha upatikanaji wa huduma ya maji mijini na vijijini inafikia asilimia 95 na 85 mtawalia mwaka 2025. Hadi kufikia Februari, 2023, hali ya upatikanaji wa huduma za maji mijini imeongezeka kutoka asilimia 86 mwaka 2022 hadi kufikia asilimia 88 na vijijini imeongezeka kutoka asilimia 72.3 mwaka 2022 hadi kufikia asilimia 77.

Mheshimiwa Spika, ongezeko la hali ya upatikanaji wa huduma ya maji mijini na vijijini limetokana na kukamilika kwa miradi 36 ya maji mijini na miradi 382 ya maji vijijini inayonufaisha wananchi zaidi ya milioni mbili. Aidha, miradi mingine 139 mijini na 647 vijijini ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/2024, Serikali itaendelea kutekeleza miradi ya maji vijijini na mijini ikiwemo miradi ya miji 28; ujenzi wa Bwawa la Kidunda; kuanza ujenzi wa Bwawa la Farkwa hapa Dodoma; kujenga mabwawa ya ukubwa wa kati; kuanza ujenzi wa miradi ya uondoshaji wa majitaka; na kuimarisha usimamizi na uhifadhi wa rasilimali za maji ili kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabia ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Afya; ni azma ya Serikali ya Awamu ya Sita kuhakikisha Watanzania wote wanapata huduma bora za afya. Kwa msingi huo, Serikali imeendelea kutoa kipaumbele katika sekta ya afya kwa kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuimarisha utoaji wa huduma hizo. Mikakati hiyo ni pamoja na ujenzi wa vituo vya kutolea huduma za afya pamoja na kuimarisha upatikanaji wa dawa na vifaa tiba.

Mheshimiwa Spika, Serikali katika kutekeleza azma yake kusogeza huduma za afya karibu na wananchi, imekamilisha

awamu ya kwanza ya ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Kanda kule Mtwara; na Hospitali za Rufaa za Mikoa ya Mara, Songwe, Shinyanga, Geita na Katavi. Aidha, imekamilisha ujenzi wa hospitali 59 za halmashauri, ukarabati wa hospitali kongwe 19 za halmashauri na ujenzi wa maboma ya zahanati 300. Tayari vituo hivyo vimeanza kutoa huduma.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha utoaji wa huduma za afya za dharura, Serikali imejenga majengo ya huduma za dharura katika hospitali za kanda na kufikisha hospitali 36 zenye huduma hiyo kutoka hospitali saba za mwaka 2022. Mafanikio haya yamepatikana kutokana na jitihada za makusudi za Mheshimiwa Rais wetu mpendwa kwani kwa mara ya kwanza tangu uhuru, nchi yetu imeweka historia ya kuwa na mfumo wa huduma za dharura kuanzia ngazi ya Wilaya hadi Taifa. Awali huduma hizo zilikuwa zinapatikana katika ngazi ya Kanda na Taifa pekee. Uwepo wa huduma za dharura katika hospitali zetu utapunguza sana vifo kwa asilimia 40.

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu inatambua kuwa, ujenzi wa miundombinu ya vituo vya kutolea huduma za afya hauwezi kuwa na tija pasipokuwa na watumishi wenye weledi, vifaa, vifaatiba na vitendanishi. Kutokana na ukweli huo, hadi kufikia Februari, 2023, Serikali imesambaza vifaa vyenye thamani ya shilingi bilioni 44.3 pamoja na kuajiri watumishi wa kutoa huduma katika vituo vya kutolea huduma za afya. Aidha, kupitia Programu ya Mfuko wa Pamoja wa Afya, jumla ya shilingi bilioni 48.35 zimetolewa kwa ajili ya uboreshaji wa huduma za afya.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Serikali yetu itaendelea kuimarisha miundombinu ya kutolea huduma za afya, kuimarisha upatikanaji wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi, kuimarisha utoaji wa huduma za kibingwa na ubingwa bobezi, kuimarisha huduma za afya ya uzazi na kudhibiti magonjwa ya mlipuko. Vilevile, itaendelea kutoa

mafunzo kwa wataalam wa sekta ya afya katika ngazi za ubingwa na ubingwa bobezi.

Mheshimiwa Spika, Huduma kwa Makundi Maalum, Watu Wenye Ulemavu; Serikali imeendelea kuboresha huduma kwa Watu Wenye Ulemavu ambapo mwaka 2022/2023, ilitenga jumla ya shilingi bilioni 3.46 kwa ajili ya kukamilisha ukarabati wa vyuo vya Watu Wenye Ulemavu vya Mtapika kule (Masasi – Mtwara), Luanzari (Tabora), Sabasaba (Singida) na Yombo ( Jijini Dar es Salaam). Ukarabati huu umewezesha Chuo cha Luanzari kuanza kutoa mafunzo kwa kudahili wanafunzi 400 baada kufungwa kwa zaidi ya miaka kumi.

Mheshimiwa Spika, ili kuongeza ufanisi wa upatikanaji, utunzaji, uchakataji na utumiaji wa taarifa za Watu wenye Ulemavu, Serikali imetengeneza Mfumo wa Kielektroniki wa Watu Wenye Ulemavu. Mfumo huo utawezesha kumsajili na kumtambua mtu mmoja mmoja mwenye ulemavu, mahali alipo, shughuli anayoifanya na mahitaji yake. Vilevile, utawawezesha kuunganishwa na huduma mbalimbali zikiwemo kupata cheti za kuzaliwa, matibabu, kuandikishwa shule ya awali na msingi, mikopo ya asilimia mbili inayotokana na mapato ya ndani ya halmashauri na vifaa saidizi.

Mheshimiwa Spika, vilevile Serikali imeandaa Mwongozo wa Utekelezaji, Ujumuishwaji na Uimarishaji wa Huduma kwa Watu Wenye Ulemavu wa Mwaka 2022. Mwongozo huo utasaidia kuhakikisha masuala ya usawa, haki, fursa na huduma kwa Watu Wenye Ulemavu yanaimarishwa katika nyanja zote za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Serikali katika mwaka 2023/2024, imepanga kuwawezesha Watu Wenye Ulemavu kujiajiri na kuajiriwa kwa kuongeza fursa za mafunzo ya ufundi stadi na marekebisho kutoka watu 460 hadi 1,200.

Mheshimiwa Spika, Huduma kwa Wazee; Serikali imeendelea kuwatambua na kutoa huduma za msingi za chakula, malazi, mavazi na matibabu kwa wazee wasiojiweza 268 wanaoishi katika makazi 14 ya wazee kule Kibirizi, Njoro, Kolandoto, Bukumbi, Ipuli, Fungafunga, Mwanzange, Misufini, Nunge, Nyabange, Kilima, Sukamahela, Magugu pamoja na Nandanga. Natoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu na wananchi kwa ujumla kuendelea kuunga mkono juhudi za Serikali katika kuwahudumia wazee na hii ni namna bora ya kutambua umuhimu na michango waliyotoa katika ujenzi wa Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, Ulinzi na Usalama; hali ya ulinzi na usalama wa mipaka ya nchi yetu imeendelea kuwa shwari bila uwepo wa matukio hatarishi. Katika kuhakikisha hali ya usalama nchini inaendelea kuimarishwa, vyombo vyetu vya ulinzi na usalama vimeendelea kulinda mipaka ya nchi; kudumisha amani, usalama wa raia, mali zao na kufundisha wananchi ulinzi wa umma.

Mheshimiwa Spika, Jeshi letu limeendelea kushirikiana na Umoja wa Mataifa, Umoja wa Afrika na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika katika operesheni mbalimbali za ulinzi wa amani. Katika mwaka 2022/2023, vikosi vyetu vilipeleka waangalizi wa kijeshi, wanadhimu na makamanda kwenye nchi zenye migogoro za Lebanon, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Jamhuri ya Afrika ya Kati na Msumbiji. Ushiriki huo ni muhimu kwa kuwa unalitambulisha Taifa kimataifa, kuwaweka askari wetu tayari kila wakati, kujifunza teknolojia mpya na kushirikisha vijana katika kuleta amani.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutambua, kusajili na kutoa vitambulisho vya Taifa ili kuwezesha upatikanaji wa huduma mbalimbali za kijamii, kiuchumi na kiusalama. Aidha, hivi karibuni Serikali imefanya marekebisho ya Kanuni za Usajili na Utambuzi wa Watu za Mwaka 2023 ili

kuwawezesha Watanzania kuendelea kutumia Vitambulisho vya Taifa bila kuwa na ukomo wa matumizi. Hatua hii inapunguza usumbufu na gharama kwa wananchi na Serikali kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kutoa wito kwa watoa huduma wote zikiwemo Ofisi za Balozi mbalimbali hapa nchini kuendelea kutambua na kutoa huduma stahiki kwa wananchi wenye vitambulisho vya Taifa bila kujali tarehe za ukomo zilizo kwenye vitambulisho hivyo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali itaendelea kuviimarisha na kuviongezea uwezo vyombo vya ulinzi na usalama kwa kuvipatia vifaa na zana bora za kisasa. Vilevile, Jeshi litaendelea kuwajengea vijana wa Kitanzania ukakamavu, uzalendo na uwezo wa kujitegemea.

Mheshimiwa Spika, naomba kuzungumzia Masuala ya Kazi na Wafanyakazi. Serikali imeendelea kuboresha mazingira ya kazi na wafanyakazi kwa kusimamia viwango vya kazi pamoja na masuala ya afya na usalama mahali pa kazi. Katika mwaka 2022/2023, jumla ya kaguzi 3,327 za viwango vya kazi zilifanyika sawa na asilimia 69.31 ya kaguzi 4,800 zilizopangwa kufanyika. Vilevile, kaguzi 96,693 zinazohusu afya na usalama mahali pa kazi zilifanyika ambapo kumekuwa na ongezeko la upimaji wa afya kutoka wafanyakazi 125,616 mwaka 2021/2022 hadi wafanyakazi 169,735 mwaka 2022/2023. Kufuatia kaguzi hizo, waajiri 173 waliokiuka sheria za kazi walichukuliwa hatua.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine, Serikali imeimarisha Mfumo wa Kielektroniki wa Kushughulikia Maombi ya Vibali vya Kazi. Uimarishaji wa mfumo huo, pamoja na mambo mengine umechangia kwa kiasi kikubwa kuongeza ufanisi katika utoaji wa vibali vya kazi nchini. Mathalani, hadi kufikia Februari, 2023 jumla ya vibali vya kazi 8,576 vilitolewa

sawa na asilimia 92.14 ya maombi ya vibali 9,307 yaliyopokelewa.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Serikali itaendelea kuimarisha usimamizi na utekelezaji wa Sheria za kazi, uratibu wa ajira za wageni na masuala yote yanayohusu usalama na afya mahali pa kazi. Aidha, Serikali itaendelea, kutoa elimu na ushauri kwa wafanyakazi, waajiri na vyama vyao ili kuwa na rasilimali watu imara na yenye tija kwa maendeleo endelevu ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuzungumzia Hifadhi ya Jamii. Sekta ya Hifadhi ya Jamii imekuwa na mchango mkubwa kwenye uchumi pamoja na ustawi kwa wananchi. Aidha, hadi Februari, 2023, deni la shilingi trilioni 2.17 limelipwa katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma *(PSSSF)*. Fedha hizo ni stahili ya mafao kwa wanachama waliorithiwa kutoka uliokuwa Mfuko wa *PSPF* mwaka 1999.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Mfuko wa *PSSSF* umelipa mafao kwa wastaafu, wategemezi na wanufaika wengine wapatao 41,939 yenye thamani ya shilingi trilioni 1.074 na pensheni ya kila mwezi ya shilingi bilioni 507.28 sawa na wastani wa shilingi bilioni 63.41 kila mwezi kwa wastaafu 158,351. Aidha, Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii *(NSSF)* umelipa mafao ya shilingi bilioni 438.32 kwa wastaafu, wategemezi na wanufaika wengine wapatao 66,628. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 72.3 zililipwa kama pensheni ya kila mwezi kwa wastaafu 27,570 ikiwa ni wastani wa shilingi bilioni 9.04 kwa kila mwezi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mapenzi makubwa aliyonayo kiongozi wetu kwa wananchi wake, alielekeza kurejesha michango ya watumishi walioondolewa kazini kwa kughushi vyeti. Utekelezaji wa maelekezo hayo umeanza ambapo hadi sasa jumla ya watumishi 11,896 wamerejeshewa michango yao yenye thamani ya shilingi

bilioni 35.02 kupitia *PSSSF* na *NSSF*. Mifuko hiyo inaendelea kuwalipa watumishi hao kadri inavyopokea taarifa kutoka kwa waajiri.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kujenga mazingira wezeshi kwa waajiri, kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara na uwekezaji na kupunguza gharama za uendeshaji ili kukuza uchumi wa nchi na kulinda rasilimali watu. Hatua hizo ni pamoja na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi kupunguza kiwango cha uchangiaji kwa Waajiri wa Sekta Binafsi kutoka asilimia 0.6 hadi asilimia 0.5.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Serikali itaendelea kuimarisha Sekta ya Hifadhi ya Jamii kwa kuhakikisha wananchi wengi wanajumuishwa katika mpango wa Hifadhi ya Jamii wa uchangiaji.

Mheshimiwa Spika, natoa wito kwa sekta isiyo rasmi ikiwemo mama na baba lishe, machinga, bodaboda, wakulima, wavuvi, wafugaji, na wengineo kujiunga na Mifuko hiyo ya *NSSF* kwa manufaa yao ya baadae.

Mheshimiwa Spika, ukuzaji wa fursa za ajira na ujuzi; Serikali imeendelea kuratibu masuala ya uzalishaji wa fursa za ajira nchini kupitia utekelezaji wa miradi ya kielelezo, kujenga mazingira wezeshi kwa wawekezaji na kuimarisha ushirikiano baina ya Serikali na sekta binafsi. Katika mwaka 2022/2023, jumla ya fursa za ajira 547,031 zilizalishwa. Kati ya hizo, ajira 321,363 zilizalishwa kupitia Serikali na utekelezaji wa miradi ya maendeleo 225,668 kupitia sekta binafsi

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuchukua hatua ili kuhakikisha wahitimu wa mafunzo ya ujuzi wanaunganishwa na fursa za kujiajiri. Utaratibu huo utamwezesha mhitimu wa mafunzo ya ujuzi kupata sehemu ya uzalishaji yenye viwango vinavyohitajika nchini na

usimamizi wa watalaam wenye uzoefu katika fani husika kwa kipindi maalum cha miezi 6 hadi 12 kutegemeana na aina ya fani.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/2024 Serikali itaendelea kuwezesha na kuratibu masuala ya ukuzaji wa fursa za ajira na kazi za staha kwa kuboresha na kutekeleza Sera, Mikakati na Mipango mbalimbali ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa ili kuhakikisha nguvu kazi ya Taifa inapata fursa za kujiajiri na kuajiriwa ili kuchangia katika maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuzungumzia Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi; Serikali imeendelea kutekeleza shughuli mbalimbali zinazolenga kuwawezesha wajasiriamali kukuza mitaji yao na kufikia masoko makubwa kupitia Vituo vya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Katika mwaka 2022/2023 jumla ya shilingi bilioni 326.6 zilitolewa kwa wajasiriamali 903,763. Kati yao wanawake ni 478,994 sawa na asilimia 53 na wanaume 424,769 sawa na asilimia 47. Upatikanaji wa fedha hizo umewawezesha wajasiriamali kuanzisha na kukuza biashara zao. Aidha, kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake *(Women Development Fund)*, mikopo yenye thamani ya Shilingi Milioni 663.4 ilitolewa kwa wanawake 96 ili kuwawezesha kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/2024 Serikali itaendelea kuimarisha utendaji wa mifuko na programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi na kuwaunganisha na wajasiriamali na fursa za kiuchumi. Aidha, Serikali itaendelea kuimarisha vituo vya uwezeshaji ili kuchochea shughuli za kiuchumi kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, maendeleo ya vijana; Serikali imeendelea kuwawezesha vijana ili kujiajiri, kushiriki kwenye shughuli za maendeleo na kuchangia katika Pato la Taifa. Katika mwaka wa fedha unaoendelea 2022/2023 Mfuko wa Maendeleo ya Vijana umetoa mikopo yenye thamani ya

shilingi bilioni 1.88 kwa ajili ya kuwezesha miradi 85 ya vijana katika sekta za kilimo, viwanda na biashara kwenye Halmashauri 28.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali imetoa mafunzo ya ujasiriamali, usimamizi, kurasimisha na kuendeleza biashara kwa vijana 2,497 walio katika Mikoa ya Kagera, Dodoma, Katavi, Shinyanga na Lindi. Vilevile, kazi ya kuboresha Mwongozo wa Utoaji mikopo kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana imekamilika na Mfuko unatoa mikopo kwa vijana walio katika vikundi, mtu mmoja mmoja na makampuni.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine, Serikali imeendelea kutekeleza Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili kupitia Mpango wa Jenga Kesho Iliyo Bora. Mpango huo unalenga kuongeza ushiriki wa vijana katika sekta ya kilimo kwa kuwapatia mafunzo, mashamba, mahitaji na kuwaunganisha na fursa za masoko. Awamu ya kwanza ya utekelezaji wa Mpango huo imeanza Mkoani Dodoma katika Shamba la Chinangali II lenye ukubwa wa ekari 400. Aidha, zaidi ya hekta 47,000 zimeshapatikana katika Mikoa mbalimbali nchini na upimaji udongo unaendelea.

Mheshimiwa Spika, kupitia Programu ya Taifa ya Kukuza Ujuzi, Serikali imetoa fursa za mafunzo ya ujuzi wa kujiajiri au kuajiri kwa vijana 14,542 katika fani mbalimbali kupitia mafunzo ya uanagenzi, uzoefu wa kazi, ufugaji wa samaki na viumbe maji na kilimo cha kisasa kwa njia ya vizimba.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2023/2024, Serikali itaendelea kuimarisha uwezo wa Mfuko wa Maendeleo ya Vijana katika kutoa mikopo na mafunzo ya ujasiriamali kwa vijana wengi ili kuwawezesha kujiajiri na kuchangia uchumi wa Taifa. Vilevile, itaanzisha kampeni ya kuwashawishi vijana kushiriki katika kilimo.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie masuala mtambuka; Sensa ya Watu na Makazi 2022. Nchi yetu ilitekeleza zoezi la Sensa ya Watu na Makazi Tarehe 23 Mwezi wa Nane, 2022. Zoezi hilo lililojumuisha sensa ya watu na makazi, anwani za makazi na majengo lilifanyika kwa mafanikio makubwa na wananchi kuonesha ushirikiano wa hali ya juu. Matokeo ya awali ya Sensa ya Watu na Makazi yalizinduliwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Tarehe 30 Oktoba, 2022. Matokeo hayo ya awali yamechangia kwa kiasi kikubwa katika maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali ya mwaka 2023/2024. Aidha, Serikali imeshakamilisha ripoti Nane ambazo zimejikita kwenye mgawanyo wa idadi ya watu kwa umri na jinsi. Ripoti hizi zitasaidia kuongeza wigo wa matumizi ya takwimu.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa wito kwa viongozi wenzangu na wananchi kuwa tuendelee kuhamasisha matumizi ya matokeo ya sensa ya watu na makazi, majengo na anwani za makazi katika biashara, shughuli za kijamii na mipango ya maendeleo ya nchi. Aidha, nitumie fursa hii kulishukuru Bunge lako Tukufu kwa ushirikiano mkubwa kabisa ambao Waheshimiwa Wabunge waliuonesha wakati wa utekelezaji wa zoezi la Sensa. Nawashukuru Wenyeviti wa Kamati ya Sensa katika ngazi mbalimbali kwa uongozi wao mahiri, Makamisaa wa Sensa na wadau mbalimbali kutoka sekta ya umma na binafsi na wananchi wote katika kuunga mkono juhudi za Serikali katika kufanikisha Sensa ya Watu na Makazi, Majengo na Anwani za Makazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ni Mapambano Dhidi ya Rushwa; katika mwaka 2022/2023, Serikali imeendelea kupambana na vitendo vya rushwa na ufisadi ambapo nguvu kubwa ilielekezwa kwenye uzuiaji wa vitendo hivyo. Hadi kufikia Februari, 2023, kesi za rushwa zipatazo 696 zikiwemo kesi mpya 203 ziliendeshwa Mahakamani. Kati ya

kesi hizo, kesi 248 ziliamuliwa Mahakamani na watuhumiwa 142 walikutwa na hatia.

Mheshimiwa Spika, vilevile, ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi ya Maendeleo 810 yenye thamani ya shilingi trilioni 6.89 umefanyika. Kutokana na ufuatiliaji huo, miradi 119 yenye thamani ya shilingi billioni 46.04 ilionekana kuwa na kasoro mbalimbali katika utekelezaji na inaendelea kufanyiwa uchunguzi ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha ujao wa mwaka 2023/2024 Serikali itaendeleza mapambano haya ya rushwa na ufisadi kwa kuweka kipaumbele katika kuzuia vitendo vya rushwa. Serikali pia itatoa elimu kwa umma kuhusu madhara ya vitendo vya rushwa kupitia programu ambazo tunazo chini ya mfumo unaoitwa TAKUKURU- RAFIKI.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie mapambano dhidi ya UKIMWI. Sote tunafahamu UKIMWI umeendelea kuwa miongoni mwa majanga makubwa duniani kwa miongo kadhaa. Serikali kwa kutambua ukweli huo, imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za mapambano dhidi ya ugonjwa huo. Jitihada hizo ni pamoja na kuandaa mikakati na kutekeleza afua mbalimbali za kupunguza maambukizi, unyanyapaa pamoja na vifo vitokanavyo na janga hilo imeendelea kuimarishwa.

Mheshimiwa Spika, kama mtakumbuka katika maadhimisho ya siku ya UKIMWI Duniani ya Mwaka 2022 yaliyofanyika Mkoani Lindi, Mheshimiwa Dokta Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alizindua Mkakati wa Tano wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI wa Mwaka 2021/2022 – 2025/2026. Mkakati huo umelenga kuhakikisha kuwa malengo ya sifuri tatu yatafikiwa ifikapo mwaka 2030. Malengo hayo ni kudhibiti maambukizi mapya ya VVU, kukomesha unyanyapaa na kutokomeza vifo vitokanavyo na UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, kutokana na jitihada zilizofanyika ikiwemo matumizi ya dawa za *ARV*, afua za kinga zinazotekelezwa na wadau mbalimbali nchini na afua za mabadiliko ya tabia, tohara ya kitabibu kwa wanaume na kuzuia maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto, maambukizi mapya ya VVU kwa watu wazima (miaka 15 na zaidi) yameshuka kutoka 110,000 mwaka 2010 hadi 54,000 mwaka 2022. Wakati huo huo, vifo vinavyotokana na UKIMWI vimepungua kwa asilimia 55 kutoka vifo 65,000 mwaka 2010 hadi 29,000 mwaka 2022. Vilevile, maambukizi mapya kutoka kwa Mama kwenda kwa Mtoto yameshuka kutoka asilimia 18 mwaka 2010 hadi asilimia Saba mwaka 2022.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya dawa za kufubaza Virusi vya UKIMWI kwa WAVIU wanaojua hali zao za maambukizi yameongezeka kutoka asilimia 95 mwaka 2016 hadi asilimia 98 mwaka 2022. Hadi kufikia Desemba 2022 WAVIU zaidi ya Milioni 1.5 walikuwa kwenye huduma za tiba na matunzo. Aidha, WAVIU wanaofahamu hali zao za maambukizi na wapo kwenye matibabu ni asilimia 99 na WAVIU waliopo kwenye matibabu na wamefubaza VVU ni asilimia 98. Mafanikio haya ni makubwa ikilinganishwa na malengo yetu ya Kimataifa lakini pia na ya Kitaifa ya kufikia 95-95-95.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio makubwa yaliyopatikana, bado tuna mambo mengi yanayohitaji kufanyiwa kazi ili kufikia azma yetu ya kumaliza kabisa janga la UKIMWI. Kwa kutambua hilo, Serikali itaendelea kutenga rasilimali za kutosha kwa ajili ya Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti UKIMWI na kutoa elimu kwa umma kuhusu athari za UKIMWI pamoja na afua nyingine mahsusi za kudhibiti janga hilo. Kwa upande mwingine, Serikali itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali katika kutekeleza afua za mapambano dhidi ya UKIMWI. Nitumie fursa hii kushukuru sana asasi za kiraia na wadau wa maendeleo kwa michango

yao katika kuungana na Serikali yetu kwenye mapambano ya kutokomeza UKIMWI nchini.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni Mapambano Dhidi ya Dawa za Kulevya. Serikali yetu kwa kutambua madhara ya dawa za kulevya kwa nguvu kazi hapa nchini, imeendelea kushirikiana na wadau mbalimbali katika mapambano dhidi ya dawa hizo. Katika mwaka 2022/2023 imeendesha oparesheni za kuwakamata wanaojihusisha na biashara hiyo pamoja na kuzuia mianya ya kusafirisha na kusambaza dawa hizo. Katika oparesheni hizo watuhumiwa 7,113 pamoja na kilogramu 20,450.30 za dawa za kulevya zilikamatwa. Dawa hizo ni *heroin* kilogramu 53.01, *cocaine* gramu 843.55, bangi kilogramu 12,869.39, mirungi kilogramu 7,525.53, na aina nyingine ya dawa za kulevya *methamphetamine* na *mescaline* gramu 1,024.7. Aidha, iliteketeza ekari 69 za bangi katika maeneo mbalimbali nchini na kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu madhara ya matumizi ya dawa za kulevya.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeimarisha huduma za matibabu kwa watumiaji wa dawa za kulevya kwa kuongeza idadi ya kliniki zinazotoa huduma kwa waathirika wa dawa za kulevya kutoka tisa mwaka 2020/2021 hadi kliniki 15 zinazohudumia waathirika zaidi ya 14,500 mwaka 2022/2023. Licha ya hayo, Serikali kupitia Programu ya Kukuza Ujuzi imewezesha Waraibu wa Dawa za Kulevya waliopata nafuu wapatao 245,000 kupata mafunzo ya ujuzi kupitia vyuo vya *VETA*, Don Bosco na *SIDO*.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kusimamia na kuratibu uendeshwaji wa nyumba za upataji nafuu 44 nchini *(Sober House)* kuzijengea uwezo asasi za kiraia 65 ambazo zinatoa elimu kuhusu madhara ya dawa za kulevya kwa jamii, kuandaa Mwongozo wa Utoaji Elimu kuhusu Tatizo la Dawa za Kulevya Nchini ambao umezinduliwa tarehe 02 Julai, 2022 kwa lengo la kuwapatia elimu na mbinu sahihi kulingana na mahitaji ya makundi mbalimbali ya kijamii. Nitoe wito kwa

wadau wote mkiwemo Waheshimiwa Wabunge wenzangu, asasi za kiraia, viongozi wa dini, vyombo vya habari na jamii nzima kushirikiana na Serikali katika kutoa elimu kuhusu madhara ya dawa za kulevya ili kuokoa kizazi cha sasa na kizazi kijacho.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie uratibu wa maafa; Serikali imeendelea kuhakikisha nchi inakuwa stahimilivu dhidi ya majanga kwa kuweka utaratibu mzuri kabisa wa kushughulikia masuala ya maafa hapa nchini. Ili kuweka utaratibu huo, Serikali imetunga Sheria ya Usimamizi wa Maafa Na. 6 ya mwaka 2022, pia tuna Mkakati wa Taifa wa Usimamizi wa Maafa wa mwaka 2022-2027, vilevile tuna Mpango wa Taifa wa Kujiandaa na Kukabiliana na Maafa wa mwaka 2022 ukiwemo pia na Mkakati wa Taifa wa Afya Moja wa mwaka 2022-2027 na Mwongozo wa Taifa wa Kupambana na Vitendo vya Kihalifu katika Bahari na Maziwa Makuu wa mwaka 2022. Kama mtakumbuka, nyaraka hizo nilizizindua tarehe 9 Februari, 2023 kwa ajili ya utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, nyaraka hizo zimeweka utaratibu wa kuhakikisha kuwa Wizara, Idara, Taasisi za Umma na zisizo za umma pamoja na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa zinashiriki kikamilifu katika kutekeleza shughuli za kuzuia na kupunguza madhara ya majanga. Aidha, zimeweka pia utaratibu wa kujiandaa, kukabiliana na kurejesha hali iliyotoweka pindi maafa yanapotokea. Nitoe wito kwa taasisi husika kuandaa mipango kazi na taratibu za usimamizi wa maafa pamoja na ushughulikiaji wa dharura hizo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023 jumla ya Wajumbe 555 wa Kamati za Usimamizi wa Maafa na Waratibu wa Maafa walipata mafunzo ya kuimarisha uwezo wa utendaji katika Mikoa ya Arusha, Morogoro, Kilimanjaro, Lindi, Mtwara na Singida. Aidha, jumla ya wavuvi 344 katika mwambao wa Ziwa Victoria na vijana 40 wa kujitolea katika Mikoa ya Dodoma, Iringa, Songwe na Tabora walipata

mafunzo ya uokoaji, yaliyowaongezea uwezo wa kukabiliana na maafa kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, katika kuendeleza ushirikiano na nchi nyingine katika kushughulikia masuala ya maafa ikiwemo nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika, Tanzania imekuwa nchi ya kwanza kusaini mkataba wa kuanzisha Kituo cha Huduma za Binadamu na Operesheni za Dharura cha Kanda ya *SADC*. Hapa lengo la kuanzisha kituo hicho ili kusimamia utoaji wa huduma na misaada ya kibinadamu kwa nchi wanachama. Hii ni kutokana na ukweli kwamba, masuala ya majanga hayana mipaka na hayana muda na yanahitaji jitihada za pamoja katika kuyashughulikia.

Mheshimiwa Spika, mtakumbuka, katika kuendeleza uhusiano na nchi nyingine, hivi karibuni nchi yetu imeungana na mataifa mengine duniani kutoa misaada ya kibinadamu kwa nchi zilizopatwa na maafa makubwa yaliyosababisha vifo na majeruhi pia uharibifu wa mali na mazingira. Nchi hizo ni pamoja na Malawi iliyokumbwa na mafuriko yaliyosababishwa na Kimbunga Freddy kilichotokea tarehe 13 Machi 2023 na nchi ya Uturuki iliyokumbwa na tetemeko la ardhi mwezi Februari mwaka huu. Misaada iliyotolewa kwa nchi ya Malawi ni pamoja na mahindi tani 1,000, mablanketi 6,000, mahema 50, fedha taslimu shilingi milioni 705, dawa za binadamu na helkopta mbili kwa ajili ya kusaidia uokoaji. Aidha, fedha taslimu dola za Marekani milioni moja zilitolewa kwa nchi ya Uturuki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali itaendelea na ujenzi wa Kituo cha Taifa cha Usimamizi wa Maafa Jijini Dodoma, kuimarisha maghala ya vifaa vya misaada ya kibinadamu kwa kuongeza vifaa na kuendelea kutoa misaada kwa waathirika wa maafa.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kila Wizara na Taasisi kulingana na majukumu yao watalazimika pia kuandaa vifaa vya maafa kutegemeana na maafa yanayoweza kujitokeza kwenye Wizara zao.

Mheshimiwa Spika, naomba kuzungumzia uratibu wa masuala ya lishe. Katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali imeendelea kutekeleza afua mbalimbali za lishe ili kuimarisha afya na hivyo kuwezesha wananchi kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo. Kutokana na umuhimu wa masuala ya lishe, tarehe 30 Septemba, 2022 Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, alisaini mikataba na Wakuu wa Mikoa yote Tanzania Bara kwa lengo la kuhakikisha kipaumbele kinatolewa kwenye masuala ya lishe ikiwa ni pamoja na kuhakikisha Halmashauri zinatenga shilingi 1,000 kwa kila mtoto wa chini ya miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, vilevile alielekeza fedha zinazopangwa kutekeleza afua za lishe kutolewa kwa wakati na kutumika kwa malengo yaliyokusudiwa, ikiwa ni pamoja na kuimarisha uhamasishaji wa utekelezaji wa afua za lishe bora na kuweka mikakati ya kuhakikisha kwamba vyakula vinavyohitajika kukamilisha lishe vinapatikana katika ngazi zote.

Mheshimiwa Spika, maelekezo hayo ya Mheshimiwa Rais yaliongeza chachu ya utekelezaji wa masuala ya lishe sambamba na malengo yaliyoainishwa kwenye Mpango Jumuishi wa Kimataifa wa Masuala ya Lishe wa Mwaka 2021/2022 - 2025/2026. Aidha, katika Mkutano wa Nane wa Wadau wa Lishe Kitaifa, uliofanyika Desemba, 2022 Mkoani Mara, Mkakati wa Sekta Binafsi unaoainisha mikakati ya sekta hiyo kuiunga mkono Serikali kuimarisha hali ya lishe nchini ulizinduliwa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na jitihada mbalimbali za Serikali na wadau, yapo baadhi ya mafanikio yaliyopatikana

ambayo ni pamoja na kupungua kwa udumavu kutoka asilimia 34.4 mwaka 2015/2016 hadi asilimia 30 mwaka 2022 na kupungua kwa kiwango cha ukondefu kutoka asilimia 4.5 hadi 3.3 katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali itaendelea kutoa kipaumbele katika utekelezaji wa Mpango Jumuishi wa Pili wa Kitaifa wa Masuala ya Lishe wa Mwaka 2021/2022 - 2025/2026. Nitoe wito kwa wananchi kuzingatia ulaji sahihi wa vyakula mchanganyiko kama tunavyoelekezwa na wataalamu wetu wa masuala ya Lishe. Vilevile, niwaombe Wadau wa Maendeleo na Sekta Binafsi kuendelea kuunga mkono juhudi za Serikali katika kuimarisha hali ya lishe nchini.

Mheshimiwa Spika, suala la mazingira, Serikali ya Awamu ya Sita katika kuweka msisitizo wa uhifadhi wa mazingira, imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali pamoja na maboresho ya sera na sheria ili ziwiane na mahitaji ya sasa ya kitaifa, na sio kitaifa tu, ni pamoja na kikanda na kimataifa. Katika kutelekeza azma hiyo, Serikali imeandaa Mpango Kabambe wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (2022 - 2032) kwa lengo la kutoa mwongozo wa hatua za kuchukua ili kutatua changamoto za mazingira nchini kwa kuzingatia sehemu husika na hatua mahsusi zinazopaswa kuchukuliwa.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Serikali imeandaa Kanuni za Biashara ya Kaboni za mwaka 2022 na kutangazwa katika Gazeti la Serikali kupitia *GN* 636 kwa lugha ya Kiingereza na *GN* 637 kwa lugha ya Kiswahili. Aidha, Serikali imeandaa Mwongozo kwa ajili ya kutoa maelekezo mbalimbali kuhusu ushiriki wa wadau katika biashara hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine Serikali imeratibu ushiriki wa nchi katika mikutano ya kimataifa. Mikutano hiyo imekuwa na mafanikio na munafaa kwa Taifa letu ambapo kupitia Mkutano wa 27 wa Nchi Wanachama

wa Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi, Tanzania imepata miradi ya nishati jadidifu ambayo inafadhiliwa na Benki ya Dunia, Taasisi ya Afrika 50 na Shirika la Nishati la Afrika kwa kushirikiana na kampuni ya *China Renewable Energies*.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/2024 Serikali itaendelea kusimamia utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira na kuchukua hatua za kupunguza uharibifu wa mazingira hapa nchini. Aidha, itaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu hifadhi na usimamizi wa mazingira, mabadiliko ya tabianchi na fursa ya biashara ya kaboni. Vilevile, itaratibu utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021 na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191 pamoja na kutoa elimu kwa umma kuhusu mabadiliko ya Sheria na Sera ya Mazingira.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na kuhamasisha wananchi juu ya kuibua fursa zilizo kwenye Uchumi wa Bluu kupitia matumizi endelevu ya rasilimali maji kwa kuzingatia uhifadhi wa mazingira na ushirikishwaji wa jamii. Hatua zinazochukuliwa ni pamoja na kuendelea kukamilisha Sera ya Taifa ya Uchumi wa Bluu pamoja na Mkakati wa Utekelezaji. Sera hiyo italenga kukuza uwekezaji katika rasilimali za Uchumi wa Bluu, kuongeza fursa za ajira na kazi za staha kupitia shughuli za Uchumi wa Bluu, na kuwa na usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za Uchumi wa Bluu unaozingatia misingi ya utawala bora.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie kidogo kuhusu Utawala Bora. Serikali imeendelea kujenga uelewa wa pamoja kwa wadau wote hususan wananchi kuhusu masuala ya kisheria, upatikanaji wa haki zao, kuongeza uwazi na kupunguza gharama. Vilevile Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ikiwemo kukamilisha rasimu ya awali ya ufasiri wa Sheria Kuu 219 na Sheria Ndogo 148 kwa lugha ya Kiswahili. Zoezi la ufasiri wa Sheria Kuu na Sheria Ndogo zote kutoka lugha ya Kiingereza kwenda lugha ya Kiswahili ili

kupanua wigo wa matumizi ya lugha ya Kiswahili kama lugha ya Sheria katika vyombo vya utoaji haki ikiwemo Mahakama, Mabaraza na vyombo vingine vyenye jukumu la kutoa haki linaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/2024 Serikali itaendelea kutekeleza kampeni ya msaada wa kisheria ya Mama Samia, kuimarisha mifumo ya utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala na kuendelea kutafsiri sheria kutoka lugha ya Kiingereza kuwa lugha ya Kiswahili ili kuwawezesha wananchi kuelewa mwenendo wa mashauri yanayowahusu na hivyo kuweza kupata haki zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuimarisha matumizi ya Mfumo wake wa TEHAMA wa kubadilishana taarifa ambapo hadi sasa jumla ya mifumo 60 ya Taasisi 55 imeunganishwa na inabadilishana taarifa. Utekelezaji huo pia ni maelekezo ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuwa na mifumo michache inayobadilishana taarifa. Uunganishaji wa mifumo hiyo umeongeza tija na ufanisi katika kuwahudumia wadau hususan wananchi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/2024 Serikali itaendelea kurahisisha utendaji kazi kwa kutumia Mifumo ya TEHAMA, kupunguza gharama za kutoa huduma ili kutoa unafuu kwa wafunzi pamoja na kuimarisha mifumo inayobadilishana taarifa.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutekeleza afua mbalimbali za kupinga ukatili dhidi ya watoto shuleni na nje ya shule. Katika mwaka 2022/2023 hatua zilizochukuliwa ili kupinga ukatili huo ni pamoja na kuunda madawati 1,393 ya ulinzi na usalama wa mtoto katika shule za msingi na sekondari kwenye Mikoa ya Rukwa, Arusha, Tanga, Dar es Saalam, Pwani, Shinyanga, Dodoma na Geita. Vilevile Mabaraza ya Watoto 560 yameundwa kwa lengo la kutoa fursa kwa watoto kutoa maoni yao kwa uhuru na

kuwajengea uwezo wa kujiamini, kujieleza na kujifunza masuala mbalimbali yanayohusu haki na ustawi wa watoto.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Serikali imeendelea kuhamasisha jamii kushiriki katika ulinzi na usalama wa mtoto ili kutokomeza ukatili dhidi ya watoto. Aidha, kupitia jitihada mbalimbali ikiwemo utekelezaji wa Programu Jumuishi ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto (2021/2022 - 2024/2025), wananchi wameendelea kuhamasishwa kujitolea kwa hiari kupambana na vitendo vya ukatili ikiwa ni pamoja na kutambua wajibu wao juu ya ulinzi wa mtoto kuanzia ngazi ya familia.

Mheshimiwa Spika, nitoe rai kwa Mamlaka zinazohusika chini ya uratibu wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu kuimarisha mfumo wa ushughulikiaji wa matukio ya ukatili dhidi ya watoto ndani na nje ya shule unaowajumuisha wasimamizi wa shule, wazazi, walezi na jamii na kuandaa Mfumo jumuishi wa kukusanya taarifa na takwimu za vitendo vya ukatili dhidi ya watoto.

Mheshimiwa Spika, naomba kukumbusha wito uliotolewa na Mke wa Rais wa Awamu ya Nne, Mama Salma Kikwete usemao, “Mtoto wa mwenzio ni wako.” Ni muhimu.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zimeendelea kushughulikia changamoto mbalimbali zinazojitokeza kwa lengo la kuulinda, kuuenzi na kuudumisha Muungano wetu. Katika mwaka wa fedha 2022/2023, jumla ya hoja nne kati ya nane zilipatiwa ufumbuzi na kuondolewa katika orodha ya hoja za Muungano.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Serikali iliandaa kitabu kinachoitwa “Muungano wa Tanganyika na Zanzibar: Chimbuko, Misingi na Maendeleo.” Kitabu hiki kimepatiwa ithibati tayari kwa ajili ya kutumika kama kitabu cha ziada

kwa shule za sekondari nchini ili kuendelea kukuza uelewa wa vijana wetu kuhusu Muungano.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha ujao wa 2023/2024, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar zitaendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kuendelea kutatua changamoto zilizosalia kwa lengo la kuulinda, kuuenzi na kuudumisha Muungano wetu lakini pia kuendelea kuelimisha umuhimu wa Muungano ndani ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie ushirikiano wa kikanda na kimataifa. Sote tumeshuhudia kuimarika kwa mahusiano yetu na nchi nyingine duniani, jumuiya za kikanda na mashirika ya kimataifa chini ya Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Kuimarika kwa ushirikiano huo kumetokana na Serikali kuendelea kutekeleza Sera ya Mambo ya Nje inayoweka msisitizo katika kutekeleza diplomasia ya kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha mahusiano na mataifa mengine duniani, Viongozi wetu Wakuu wakiongozwa na Rais wetu wameshiriki katika ziara mbalimbali ambazo zimeiletea manufaa makubwa nchi yetu. Mathalan, Mwezi Novemba 2022, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu aliitembelea nchi ya China kufuatia mwaliko uliotolewa na Mheshimiwa Xi Jinping, Rais wa Jamhuri ya Watu wa China. Vilevile, Viongozi wetu Wakuu wameshiriki katika ziara mbalimbali za kikazi katika nchi za Marekani, Qatar, Ethiopia, Kenya, Misri, Oman, Afrika Kusini, Rwanda, na Burundi.

Mheshimiwa Spika, kufuatia ziara hizo, nchi yetu imenufaika katika uboreshaji wa miundombinu, huduma za jamii, biashara, uwekezaji, uchumi wa kidijitali, maendeleo ya kijani, uchumi wa bluu, uvuvi, fedha, utalii, afya na kilimo.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza diplomasia ya kiuchumi, Serikali imeratibu majadiliano ya awamu ya pili ya kuanzisha Eneo Huru la Biashara la Bara la Afrika kwa upande wa Afrika Mashariki. Ushiriki wa nchi yetu katika eneo huru la biashara utachochea sana ukuaji wa uchumi na biashara, kukuza ushiriki wetu katika biashara ya dunia na kujenga uwezo wa kuongeza thamani ya bidhaa kupitia sera bora za kukuza teknolojia, ubunifu na ushindani.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka ujao wa fedha wa 2023/2024, Serikali itaendelea kufungua nchi kiuchumi kwa kuvutia uwekezaji na kutangaza vivutio mbalimbali tulivyonavyo nchini vikiwemo vya utalii vilivyoko hapa nchini, kuimarisha mahusiano ya kikanda na kimataifa na kutangaza fursa za utalii na uwekezaji katika sekta mbalimbali za maeneo ya kipaumbele hususan uchumi wa Bluu na kidijitali.

Mheshimiwa Spika, naomba nielezee hali iliyoko katika Serikali kuhamia Dodoma. Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kutekeleza kwa vitendo zoezi la Serikali kuhamia Dodoma kwa lengo la kurahisisha utoaji wa huduma za Serikali kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2022/2023, Serikali imeendelea na Awamu ya Pili ya ujenzi wa majengo ya Ofisi za Wizara na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika Mji wa Serikali pale Mtumba *(Magufuli City)*. Ujenzi huo umefikia wastani wa asilimia 60. Aidha, kazi nyingine zinazoendelea ni pamoja na ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato kitakachogharimu Shilingi bilioni 165 na ujenzi wa barabara ya mzunguko ya nje yenye urefu wa kilomita 112.3 kwa gharama ya Shilingi bilioni 221. Kwa upande wa Balozi na Jumuiya za Kimataifa, Balozi za nchi za Ujerumani, Ufaransa, China na Umoja wa Mataifa zimefungua Ofisi ndogo Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2023/2024, Serikali itaendelea kukamilisha awamu ya pili ya ujenzi wa majengo ya Ofisi za Wizara, Ofisi za Taasisi na miundombinu ya kudumu kwenye Mji wa Serikali pamoja na kuendelea kuratibu uhamiaji wa Taasisi.

Mheshimiwa Spika, sanaa, utamaduni na michezo. Serikali kwa kutambua umuhimu wa kukuza utamaduni, sanaa na michezo, imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuimarisha sekta hiyo kwa kuzingatia kuwa sekta hii ni chachu ya kuendeleza utamaduni wa Kitanzania, utambulisho wa Taifa, chanzo kikubwa cha ajira, kuimarisha afya pamoja na kuchangia katika pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, ili kukuza na kuendeleza lugha ya Kiswahili ndani na nje ya nchi, Serikali imechukua hatua mbalimbali ikiwemo kusajili vituo 30 vya kufundisha Kiswahili. Kati ya hivyo, vituo 10 vipo katika Balozi za nchi yetu nchini Korea Kusini, Ufaransa, Italia, Mauritius, Nigeria, Sudan, Zimbabwe, Uholanzi, Cuba na Umoja wa Falme za Kiarabu; na vituo vinne nje ya Balozi zetu katika nchi za Afrika Kusini, Italia, Ujerumani na Ethiopia. Pia tuna vituo 16 vya kufundisha lugha hiyo vimeanzishwa nchini. Aidha, kwa upande mwingine Tanzania imesaini makubaliano na nchi ya Afrika Kusini kuiwezesha nchi hiyo kutumia Kiswahili kuwa Lugha ya kujifunza na kufundishia katika elimu ya msingi.

Mheshimiwa Spika, vilevile Serikali imeendelea kuimarisha Mfuko wa Utamaduni na Sanaa ili kuwawezesha wasanii kuendeleza kazi zao kwa kuwapa mikopo na elimu ya ujasiriamali. Hadi kufikia Februari, 2023 tayari imeshatoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 1.07 kwa wanufaika 45 ambao ni wasanii na wadau wa sanaa. Mikopo hiyo imewawezesha wasanii na wadau wa sanaa kuandaa kazi bora na zenye uwezo wa kuhimili ushindani katika soko la sanaa.

Mheshimiwa Spika, kwa nafasi hii, nimpongeze sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa motisha kwa vilabu vya ndani vinavyoshiriki mashindano ya kimataifa kupitia Goli la Mama ambapo amekuwa akitoa shilingi milioni tano kwa kila goli linalofungwa. Sote tumeshuhudia *Simba Sports Club* almaarufu Wekundu wa Msimbazi wakijitwalia kitita cha shilingi milioni 50 wakati huo huo *Young Africans Sports Club* almaarufu Timu ya Wananchi wakijitwalia shilingi milioni 45. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninavipongeza sana vilabu vya Yanga na Simba kwa kufikia hatua ya robo fainali katika michuano ya Klabu Bingwa Afrika na Kombe la Shirikisho Barani Afrika. Ni matumaini yetu sote kuwa vilabu hivyo na vingine vitakavyoshiriki mashindano hayo ya kimataifa vitaendelea kujituma na kupambana ili vikombe vya ushindi vije nyumbani. Mungu ibariki Simba, Mungu ibariki Yanga kwa mashindano hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2023/2024 Serikali itaendelea kuratibu Programu ya ukarabati wa viwanja vya michezo katika shule 56 katika mikoa yote Tanzania Bara; kuratibu Programu ya Sanaa na michezo ya kuanzia ngazi ya Mtaa kwa Mtaa kuelekea ngazi za juu ikiwemo "*Taifa Cup*"; kutenga maeneo ya michezo kwa lengo la kujenga miundombinu ya mchezo na kuimarisha michezo katika ngazi za mikoa na wilaya; kuhakikisha kazi za sanaa na utamaduni zinazoandaliwa zinazingatia maadili ya jamii na Taifa kwa ujumla; na kuendelea kutambua maeneo ya urithi wa utamaduni na ukombozi katika mikoa na Halmashauri za Wilaya kwa lengo la kulinda, kuhifadhi na kuendeleza maeneo hayo ili kuinua utalii wa kiutamaduni na kiukombozi nchini.

Mheshimiwa Spika, mwisho, katika mwaka 2023/2024 Ofisi ya Waziri Mkuu itaendelea kuratibu utekelezaji wa Sera

na shughuli za Serikali ili kuendelea kutoa huduma bora kwa wananchi, kuratibu shughuli za maafa nchini, kuratibu Shughuli za Serikali Bungeni, kushughulikia kero na malalamiko mbalimbali ya wananchi, kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utendaji wa Serikali, na kuratibu masuala yanayohusu Kazi, Maendeleo ya Vijana, Ajira, Hifadhi ya Jamii na Huduma za Watu Wenye Ulemavu.

Mheshimiwa Spika, nimeeleza kwa muhtasari baadhi ya shughuli ambazo Serikali imetekeleza kwa kipindi kilichopita na mwelekeo wa kazi zitakazofanyika kwa mwaka 2023/2024. Kwa kuhitimisha, napenda kusisitiza mambo muhimu yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuhitimisha napenda kusisitiza mambo muhimu yafuatayo;

(i) Wizara, Taasisi za Serikali, Tawala za Mikoa na Halmashauri ziimarishe ukusanyaji wa mapato na usimamizi wa nidhamu ya matumizi ya fedha za umma pamoja na utekelezaji wa vipaumbele vilivyoainishwa katika Mpango na Bajeti ya Mwaka 2023/2024 hususan miradi ya Kitaifa ya Kimkakati;

(ii) Wadau wote pamoja na Serikali kwa ujumla waendelee kutumia matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 katika shughuli mbalimbali kama vile uwekezaji, biashara, tafiti na mipango mbalimbali ya maendeleo. Serikali itaendelea kusimamia utekelezaji wa Mpango Kazi wa Mwongozo wa Kitaifa wa Matumizi ya Matokeo ya Sensa ili kuongeza uelewa, uwazi na kupanua wigo wa matumizi ya matokeo ya sensa kwa Serikali pia wananchi na wadau wote;

(iii) Viongozi wote wa Serikali, dini, mila na Vyama vya Siasa tuendelee kukemea kwa nguvu zote ushiriki

wa sehemu yoyote ya jamii katika matendo yasiyoendana na mila, tamaduni na desturi za Watanzania. Hii ni pamoja na wazazi na walezi wote kushiriki kikamilifu katika makuzi na malezi bora ya watoto wetu yatakayoweza kuwasaidia kuwaepusha na vitendo viovu;

(iv) Serikali na Taasisi ziendelee kuhakikisha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini yanaendelea kuimarishwa ili kuvutia uwekezaji wa ndani na nje ya nchi;

(v) Wizara na Taasisi ziendelee kutenga fedha kwa ajili ya shughuli za ufuatiliaji na tathmini katika maeneo yao ikiwa ni pamoja na kuwajengea uwezo wataalam wanaotekeleza jukumu hilo. Lengo ni kuwezesha utendaji wenye matokeo na kufanikisha utoaji wa huduma bora kwa wananchi; na

(vi) Viongozi wa siasa, dini na wadau wengine wahamasishe wananchi kushiriki kikamilifu katika maandalizi na uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa Mwaka ujao 2024.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nitoe Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha za Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge Kwa Mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2023/2024 Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zilizo chini yake inaliomba sana Bunge lako tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 173,733,110,000; kati ya fedha hizo, shilingi 121,364,753,320 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 52,368,356,680 ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile naliomba sana, sana, sana Bunge lako tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 165,627,897,000

kwa ajili ya Mfuko wa Bunge. Kati ya fedha hizo, shilingi 160,458,877,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 5,169,020,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**HOTUBA YA MHESHIMIWA KASSIM MAJALIWA MAJALIWA (MB.), WAZIRI MKUU WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, KUHUSU MAPITIO NA MWELEKEO WA KAZI ZA SERIKALI NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA ZA OFISI YA WAZIRI MKUU NA OFISI YA BUNGE KWA MWAKA 2023/2024 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**UTANGULIZI**

**Shukrani**

***1. Mheshimiwa Spika***, naomba kutoa hoja kwamba kutokana na taarifa zilizowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge za Utawala, Katiba na Sheria; Afya na Masuala ya UKIMWI; Ustawi na Maendeleo ya Jamii; na Bajeti zilizochambua Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Mfuko wa Bunge, sasa naliomba Bunge lako lipokee na kujadili Taarifa ya Mapitio ya Utekelezaji wa Kazi za Serikali kwa mwaka 2022/2023 na Mwelekeo wa Kazi zake kwa mwaka 2023/2024. Aidha, naomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha makadirio ya mapato na matumizi ya fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu na taasisi zilizo chini yake pamoja na Ofisi ya Bunge kwa mwaka 2023/2024.

**2. *Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote, ninamshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa fadhila zake ambazo zimetuwezesha kukutana hapa leo kwa ajili ya kujadili Taarifa ya Mapitio ya Utekelezaji wa Kazi za Serikali kwa Mwaka 2022/2023 na mwelekeo wake kwa mwaka 2023/2024 tukiwa wenye afya njema.

***3. Mheshimiwa Spika***, itakumbukwa kuwa huu ni Mkutano wa 11 wa Bunge la 12 ambao ni mahsusi kwa ajili ya mjadala wa bajeti. Niwaombe Waheshimiwa Wabunge wenzangu, tuitumie vyema fursa hii kutoa maoni na ushauri ili kuisaidia Serikali kuimarisha utekelezaji wa vipaumbele vilivyoainishwa kwenye Mpango na Bajeti ya Mwaka 2023/2024. Napenda kuwahakikishia kuwa Serikali itapokea maoni na ushauri wenu na kuyafanyia kazi kwa maslahi mapana ya wananchi.

**Salamu za Pole**

***4. Mheshimiwa Spika,*** nchi yetu kwa nyakati tofauti imekumbwa na maafa na matukio mbalimbali yaliyosababisha athari mbalimbali zikiwemo vifo, majeruhi, na uharibifu wa mali na mazingira. Nitumie fursa hii kuwapa pole Watanzania wote waliopoteza ndugu, jamaa na mali zao katika maafa. Aidha, ninamwomba Mwenyezi Mungu awajalie majeruhi wote uponyaji wa haraka na aendelee kuwapumzisha kwa amani wale waliopoteza maisha.

**Salamu za Pongezi**

***5. Mheshimiwa Spika***, nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kutuongoza vyema na kupata maendeleo na mafanikio makubwa katika kipindi kifupi cha miaka miwili ya uongozi wake. Mafanikio hayo ni pamoja na uboreshaji wa miundombinu na huduma za afya, maji, elimu, umeme na uchukuzi, kuboresha hali ya chakula na lishe na kuimarisha hali ya kisiasa nchini na mahusiano ya kimataifa.

***6. Mheshimiwa Spika***, napenda pia kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kutokana na uongozi wao makini na jitihada zao katika kuhakikisha Taifa letu linapata maendeleo.

***7.*** ***Mheshimiwa Spika***, hivi karibuni, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amefanya teuzi na mabadiliko ya baadhi ya watendaji wakuu wa taasisi na viongozi wa Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Mabadiliko hayo, yamelenga kuimarisha utendaji kazi Serikalini ikiwa ni pamoja na utoaji huduma bora na kushughulikia kero mbalimbali za wananchi.

***8.*** ***Mheshimiwa Spika***, ninawapongeza viongozi na watendaji wote walioteuliwa na Mheshimiwa Rais wetu mpendwa kushika nyadhifa mbalimbali. Kipekee, niwapongeze Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama Mbunge wa Peramiho na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu; Mheshimiwa George Boniface Simbachawene Mbunge wa Kibakwe na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; na Mheshimiwa Abdallah Hamis Ulega Mbunge wa Mkuranga na Waziri wa Mifugo na Uvuvi. Vilevile, nimpongeze Mheshimiwa Hamis Mohamed Mwinjuma almaarufu Mwana FA, Mbunge wa Jimbo la Muheza kwa kuteuliwa kushika nafasi ya Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo. Ninawatakia kila la kheri viongozi wote walioteuliwa katika utekelezaji wa majukumu yao mapya.

***9.*** ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, nitumie fursa hii kuwasisitiza wateuliwa wote kuzingatia maelekezo mbalimbali ya Mheshimiwa Rais yakiwemo aliyatoa kwenye semina ya viongozi iliyofanyika hivi karibuni, Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 pamoja na mipango ya kitaifa na kimataifa katika utekelezaji wa majukumu yao. Aidha, natoa rai kwa viongozi hao kuhakikisha wanatanguliza mbele maslahi ya Taifa na kuwahudumia wananchi ipasavyo.

***10.*** ***Mheshimiwa Spika***, nitumie fursa hii kukupongeza wewe binafsi kwa kuliongoza Bunge hili kwa hekima na umahiri mkubwa. Nimpongeze pia Mheshimiwa Naibu Spika kwa namna ambavyo ameendelea kusimamia shughuli za Bunge

kwa uwezo mkubwa. Waheshimiwa Wabunge wenzangu hakika mtakubaliana nami kuwa Viongozi hawa ni makini sana na wameonesha ukomavu mkubwa wa kisiasa wakati wote wakiendesha vikao vya Bunge hili. Nitoe wito kwetu sote tuendelee kuwapa ushirikiano ili waendelee kuliongoza vema Bunge letu na kulifanya liendelee kuheshimika ndani na nje ya mipaka ya nchi yetu.

***11. Mheshimiwa Spika,*** nitumie nafasi hii, kumshukuru Mheshimiwa *Dkt.* Joseph Kizito Mhagama, Mbunge wa Madaba na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria; Mheshimiwa Stansilaus Nyongo, Mbunge wa Jimbo la Maswa Mashariki na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI; Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, Mbunge wa Viti Maalumu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii; Mheshimiwa Sillo Daniel Baran, Mbunge wa Babati Vijijini na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti na wajumbe wote wa kamati hizo kwa michango yao iliyosaidia kuboresha Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Mfuko wa Bunge.

***12. Mheshimiwa Spika,*** ninatambua ulifanya mabadiliko ya Wenyeviti na Wajumbe wa kamati za kudumu za Bunge. Nitumie fursa hii kuwapongeza sana wote walioteuliwa na kuwatakia kila la kheri katika utekelezaji wa majukumu yao. Vilevile, ninawashukuru sana Wajumbe wa Kamati zote za Kudumu za Bunge lako tukufu kwa ushauri walioutoa wakati wa kupitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara, Mikoa, Wakala, Idara za Serikali zinazojitegemea na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Maoni na ushauri wao utazingatiwa vilivyo wakati wa utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2023/2024.

***13. Mheshimiwa Spika,*** Bunge lako Tukufu lilifanya uchaguzi wa wenyeviti wa Bunge ambao watakusaidia kuongoza vikao vya Bunge. Niwapongeze Mheshimiwa Najma Murtaza Giga

Mbunge wa Viti Maaalum na Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii na Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Mbunge wa Babati Vijijini na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, na Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile Mbunge wa Mufindi Kusini na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kwa kuchaguliwa kuwa wenyeviti wa Bunge. Nawapongeza sana na kuwatakia majukumu mema ya kuliongoza Bunge.

***14. Mheshimiwa Spika,*** ninawashukuru Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri; Katibu Mkuu Kiongozi; Wakuu wa Mikoa; Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Makatibu Wakuu; Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Naibu Makatibu Wakuu; na Wakuu wa Wilaya, Idara, Mashirika, Wakala na Taasisi zote za Serikali kwa ushirikiano mkubwa mnaonipa katika kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Kipekee, niwapongeze na kuwashukuru wafanyakazi wote wa Serikali na taasisi zake kwa kufanya kazi kwa weledi, utaalamu na umahiri mkubwa na hivyo, kuwezesha Serikali kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

***15. Mheshimiwa Spika***, kwa namna ya pekee, nawashukuru Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, Mbunge wa Peramiho na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu); Mheshimiwa Profesa Joyce Lazaro Ndalichako, Mbunge wa Kasulu Mjini na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu); Mheshimiwa Paschal Patrobas Katambi, Mbunge wa Shinyanga Mjini na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu) na Mheshimiwa Ummy Hamis Nderiananga, Mbunge wa Viti Maalumu na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu.

***16. Mheshimiwa Spika***, vilevile, nawashukuru sana Dkt. Jim James Yonazi, Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na

Uratibu); Prof. Jamal Adam Katundu, Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu); Wakurugenzi na Wakuu wa Vitengo; Wakuu wa taasisi zilizopo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu; Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu na wafanyakazi wote kwa ushirikiano mkubwa wanaonipatia wakati nikitekeleza majukumu yangu. Aidha, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitamshukuru Mheshimiwa George Boniface Simbachawene Mbunge wa Kibakwe na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Dkt. John Antony Kiang'u Jingu, Katibu Mkuu, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu na Bwana Kaspar Kaspar Mmuya, Katibu Mkuu, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa ushirikiano walionipa wakati wakiwa Waziri wa Nchi, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu mtawalia katika Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu). Ahsanteni na Hongereni Sana!

***17. Mheshimiwa Spika***, ninapenda pia kuzishukuru sekta binafsi, nchi rafiki, washirika wa maendeleo, taasisi na mashirika ya kimataifa na madhehebu ya dini kwa kuendelea kuunga mkono juhudi za Serikali za kuleta maendeleo. Serikali inatambua na kuthamini michango yenu hususan katika utekelezaji wa afua muhimu kwa kutoa misaada, mikopo nafuu na wakati mwingine utaalamu, kitendo ambacho kimekuwa chachu ya kuharakisha maendeleo ya nchi yetu.

***18. Mheshimiwa Spika,*** baada ya utangulizi huo, naomba kuwasilisha makadirio ya bajeti ambayo ni sehemu ya utekelezaji wa vipaumbele vilivyobainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2020; maelekezo ya nyaraka za kisera za kitaifa, kikanda na kimataifa ikiwemo Dira ya Maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki 2050, Ajenda 2063 ya Maendeleo ya Afrika, Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030, Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano, na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2023/2024.

**UTEKELEZAJI WA MIRADI YA KIPAUMBELE KWA MWAKA 2022/2023**

***19. Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kutekeleza miradi ya maendeleo itakayoimarisha uchumi wa nchi na maendeleo ya watu. Hadi kufikia Januari, 2023 zimetolewa takribani Shilingi trilioni 8.64 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya miundombinu ya reli, barabara, viwanja vya ndege, huduma za jamii na nishati. Utekelezaji wa miradi hiyo upo katika hatua mbalimbali kama ifuatavyo:

**Mosi: Ujenzi wa Reli ya Kati kwa Kiwango cha Kimataifa (SGR)**
Serikali imetoa jumla ya Shilingi bilioni 762.99 kutekeleza mradi huo ambapo kipande cha Dar es Salaam – Morogoro (km 300) utekelezaji umefikia asilimia 97.91; kipande cha Morogoro – Makutupora (km 422) asilimia 92.23; kipande cha Mwanza - Isaka (km 341) asilimia 25.75; kipande cha Makutupora - Tabora (km 371) asilimia 4.59; na kuanza kwa ujenzi wa kipande cha Tabora - Isaka (km 165) na Tabora – Kigoma (Km 506).

**Pili: Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere (MW 2,115)**
Serikali imetoa takribani Shilingi bilioni 869.93 kwa ajili utekelezaji wa mradi huu ambao umefikia asilimia 83. Zoezi la ujazaji maji katika bwawa lilizinduliwa rasmi na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 22 Desemba 2022. Hadi Februari, 2023 kiwango cha maji kimefikia mita 134.39 kutoka usawa wa Bahari ikilinganishwa na kiwango cha mita 163 kinachohitajika ili kuanza uzalishaji.

**Tatu: Uboreshaji wa Shirika la Ndege Tanzania**
Utekelezaji wa mradi huu umegharimu takribani Shilingi bilioni 20.52. Shughuli zilizofanyika ni pamoja na kulipa sehemu ya gharama za ununuzi wa ndege tano ambapo kati ya hizo, ndege moja ni aina ya Boeing 767-300F ya mizigo, ndege mbili aina ya Boeing 737-9, ndege moja aina ya Boeing 787-8 Dreamliner na ndege moja aina ya De Havilland Dash 8-Q400.

Ndege nne kati ya hizo zinatarajiwa kuwasili nchini kabla ya Novemba, 2023 na ndege moja ya mizigo inatazamiwa kuwasili nchini hivi karibuni. Kuwasili kwa ndege hizo kutasaidia Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) kutanua mtandao wa safari za ndani na nje ya nchi na hivyo kuchochea ukuaji wa sekta nyingine za uchumi kama utalii, biashara na kilimo.

**Nne: Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania) lenye urefu wa km 1,443**
Takribani shilingi bilioni 30.39 zimetolewa ili kulipa fidia wananchi 7,486 kati ya 9,122 wanaopisha eneo la mkuza wa bomba; na Serikali imeendelea kulipa hisa za umiliki katika Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki hadi kufikia dola za Marekani milioni 131.0. Aidha, tayari kibali cha kuanza ujenzi wa Bomba la Mafuta kimetolewa Januari, 2023. Vilevile, ujenzi wa karakana ya kuweka mfumo wa kupasha joto mabomba katika kijiji cha Sojo, Nzega Tabora umefikia asilimia 49.

**Tano: Mradi wa Kiwanda cha Sukari Mkulazi**
Takribani shilingi bilioni 39.84 zimetolewa ili kuendelea na ujenzi wa kiwanda ambao umefikia asilimia 75. Aidha, hekta 219 zimepandwa miwa na kufanya ukubwa wa eneo lililopandwa miwa kufikia hekta 2,974 sawa na asilimia 83 ya lengo la kupanda hekta 3,600. Kiwanda hicho kinatarajiwa kuongeza uzalishaji wa tani 50,000 za sukari kwa mwaka pindi kitakapoanza uzalishaji na hivyo kupunguza mahitaji ya kuagiza sukari nje ya nchi.

**Sita: Mradi wa Daraja la Kigongo – Busisi (Mwanza)**
Takribani shilingi bilioni 93.09 zimetolewa kuendelea na ujenzi wa daraja hili ambao umefikia asilimia 63. Kukamilika kwa Daraja hili kutapunguza muda wa Wananchi kuvuka eneo la Kigongo – Busisi kutoka takribani masaa 2 mpaka dakika 4 kwa kutumia usafiri wa gari na dakika 10 kwa watembea kwa miguu. Aidha, daraja hili litakuwa na uwezo wa kupitisha magari ya aina yote wakati wote na kubeba uzito wa hadi tani 160.

**Saba: Miradi ya Ujenzi na Ukarabati wa Viwanja vya Ndege**
Serikali ilitoa takribani shilingi bilioni 77.23 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato ambapo utekelezaji umefikia asilimia 10.2. Kazi nyingine ni kukamilika kwa upanuzi wa njia ya kutua na kuruka ndege na kufungwa kwa mfumo wa kuongozea ndege katika Kiwanja cha Ndege cha Dodoma; kukamilika kwa ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Geita; na kuendelea na ujenzi na ukarabati wa Viwanja vya Ndege vya Songea kwa asilimia 98, Iringa asilimia 42 na Musoma asilimia 43.

**HALI YA UCHUMI**

***20. Mheshimiwa Spika***, kwa kipindi cha takribani mwaka mmoja sasa, Dunia imekumbwa na msukosuko wa kiuchumi kutokana na vita inayoendelea baina ya nchi za Ukraine na Urusi. Vita hiyo ilianza wakati uchumi wa dunia ukiwa bado haujatengemaa kutoka kwenye madhara ya janga la UVIKO – 19. Kwa msingi huo, tumeshuhudia uchumi wa mataifa makubwa hususan katika bara la Ulaya ukiyumba na gharama za maisha kuongezeka kutokana na mfumuko wa bei za nishati na chakula duniani.

***21. Mheshimiwa Spika***, kwa mujibu wa taarifa ya Shirika la Fedha la Duniani ya Januari, 2023, kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia imepungua kutoka asilimia 6.2 mwaka 2021 hadi asilimia 3.4 mwaka 2022. Aidha, kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia inatarajia kupungua na kufikia asilimia 2.9 mwaka 2023. Vilevile, kasi ya ukuaji wa uchumi wa nchi zilizoendelea imepungua na kufikia asilimia 2.7 mwaka 2022 kutoka asilimia 5.4 mwaka 2021 na inatarajiwa kupungua na kufikia asilimia 1.2 mwaka 2023.

***22. Mheshimiwa Spika***, uchumi wa nchi zinazoendelea na zinazoibuka kiuchumi ulipungua na kufikia asilimia 3.9 mwaka 2022 ikilinganishwa na asilimia 6.7 mwaka 2021. Aidha, ukuaji wa uchumi katika nchi zinazoendelea na zinazoibuka kiuchumi barani Asia, ikijumuisha China na India ulipungua na kufikia

asilimia 4.3 mwaka 2022 ikilinganishwa na asilimia 7.4 mwaka 2021. Kwa upande wa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara, ukuaji wa uchumi ulipungua na kufikia wastani wa asilimia 3.8 mwaka 2022 ikilinganishwa na asilimia 4.7 mwaka 2021.

***23.*** ***Mheshimiwa Spika***, kiwango cha wastani wa ukuaji wa Pato la Taifa kwa kipindi cha mwaka 2022 kwa nchi nyingi za ukanda wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika ni asilimia 4.0 ikilinganishwa na wastani wa ukuaji wa asilimia 4.2 mwaka 2021. Aidha, wastani wa ukuaji wa uchumi kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ulikuwa ni asilimia 5.6 mwaka 2022 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 5.7 mwaka 2021. Hali hii imesababishwa na kupungua kwa uzalishaji na shughuli za kiuchumi katika nchi husika kwa mwaka 2020 kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo: utekelezaji wa masharti yaliyowekwa kuzuia maambukizi ya UVIKO-19 kama kufunga mipaka, kusitisha safari za ndege za kimataifa, kusitisha baadhi ya shughuli za kiuchumi zinazohusisha mikusanyiko na kuzuia watu kutoka nje.

***24.*** ***Mheshimiwa Spika***, pamoja na kusuasua kwa ukuaji wa uchumi wa dunia na mataifa ya Afrika hususan nchi za ukanda wa Jangwa la Sahara, Jumuiya za SADC na Afrika Mashariki, hali ya ukuaji wa uchumi kwa nchi yetu kwa kipindi cha robo ya kwanza hadi ya tatu ya mwaka 2022 imeimairika ikilinganishwa na mwaka 2021. Katika kipindi cha Januari hadi Septemba 2022, uchumi wa taifa ulikua kwa wastani wa asilimia 5.2 ikilinganishwa na asilimia 4.9 katika kipindi kama hicho mwaka 2021. Ukuaji chanya wa uchumi ulichangiwa na hatua zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ikiwemo uwekezaji wa kimkakati katika miundombinu ya nishati, maji, afya, elimu, barabara, reli na viwanja vya ndege; kuongezeka kwa uzalishaji wa madini, hususan dhahabu na makaa ya mawe, kuongezeka kwa mikopo katika sekta binafsi ambayo imechochea shughuli za kiuchumi na kuongezeka kwa shughuli za utalii.

***25.*** ***Mheshimiwa Spika,*** ukuaji wa uchumi wa Tanzania kwa mwaka 2022 unatarajiwa kupungua hadi kufikia wastani wa asilimia 4.7 kutoka ukuaji wa asilimia 4.9 mwaka 2021 na kuongezeka hadi kufikia asilimia 5.3 mwaka 2023. Maoteo ya ukuaji wa uchumi wa Tanzania yamezingatia hatua zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali katika kukabiliana na athari zitokanazo na vita kati ya Ukraine na Urusi ikiwemo: kuchochea uzalishaji katika sekta za kilimo, mifugo, uvuvi na madini; uimarishaji wa miundombinu ya barabara mijini na vijijini, nishati na maji; uboreshaji wa huduma za jamii; kuendelea na utekelezaji wa miradi inayochachua shughuli za kiuchumi ikiwemo reli, upanuzi wa bandari, usambazaji umeme vijijini; na uboreshaji wa mazingira ya biashara na uwekezaji. Hata hivyo, kulingana na utabiri wa hali ya hewa ambao umebainisha uwezekano wa kuwa na mvua chini ya wastani, hali hiyo inaweza kuathiri uzalishaji katika sekta ya kilimo, upatikanaji wa nishati ya umeme, na maji na hivyo kuathiri ukuaji wa uchumi.

**Mfumuko wa Bei**

***26.*** ***Mheshimiwa Spika***, madhara ya vita vya Urusi na Ukraine yamesababisha kuongezeka kwa kasi ya kupanda bei ya mafuta duniani na hivyo kuchangia kuongezeka kwa gharama za uzalishaji na usafirishaji na kupanda kwa bei za bidhaa mbalimbali.

***27.*** ***Mheshimiwa Spika***, mfumuko wa bei nchini kwa mwaka 2022 ulifikia wastani wa asilimia 4.3 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 3.7 mwaka 2021. Hata hivyo, kiwango hiki kipo ndani ya malengo ya kati ya asilimia 3.0 hadi 5.0 na vigezo vya mtangamano wa kiuchumi wa kikanda wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika. Sababu zilizochangia kuongezeka kwa mfumuko wa bei katika kipindi husika ni pamoja na: kupanda kwa bei za bidhaa ikiwemo mafuta ya kula, mbolea na petroli kufuatia kuvurugika kwa mnyororo wa uzalishaji na usambazaji wa bidhaa na huduma katika soko la dunia uliotokana na athari za vita kati ya nchi za

Urusi na Ukraine; na kupungua kwa upatikanaji wa mazao ya chakula nchini na nchi jirani kulikosababishwa na mabadiliko ya tabianchi hususan maeneo yanayotegemea mvua za vuli.

***28.*** ***Mheshimiwa Spika***, mfumuko wa bei nchini unatarajiwa kuendelea kuwa tulivu na kubaki katika wigo wa tarakimu moja na ndani ya vigezo vya mtangamano wa kiuchumi vya kikanda kutokana na hatua zilizochukuliwa na zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali ikiwemo: kuongeza bajeti katika sekta za kilimo, mifugo, uvuvi na nishati ili kuchochea uzalishaji wa ndani na kupunguza nakisi ya urari wa biashara; usimamizi madhubuti wa sera za fedha na bajeti; utulivu wa thamani ya shilingi na kuimarisha upatikanaji wa umeme nchini.

**UWEKEZAJI**

***29.*** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali inayolenga kuimarisha uwekezaji hapa nchini. Katika mwaka 2022/2023, Serikali kupitia Bunge lako tukufu imetunga Sheria ya Uwekezaji Tanzania Namba 10 ya Mwaka 2022 ambayo pamoja na mambo mengine inalenga kuweka mazingira bora ya uwekezaji. Aidha, Serikali imeendelea kuratibu mradi wa maandalizi ya Kongani ya Viwanda ya Kwala yenye ukubwa wa ekari 2,500 ambapo kiasi cha Dola za Kimarekani bilioni tatu zinatarajiwa kuwekezwa. Mradi huu unatarajiwa kuzalisha jumla ya ajira za moja kwa moja 100,000, ajira zisizo za moja kwa moja 300,000 na bidhaa za takriban Dola za Marekani bilioni 6 kwa mwaka. Vilevile, Serikali inaendelea kuratibu maandalizi ya kongani na maeneo mengine ya kiuchumi ikiwemo, Kongani ya Magu na Misungwi pamoja na Eneo Maalumu la Kiuchumi Nala.

***30.*** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kutekeleza programu zinazolenga kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara na uwekezaji nchini. Programu hizi zinajumuisha

kuboresha mazingira ya uondoshaji wa shehena bandarini ambapo Serikali inajenga Mfumo wa Pamoja wa Kielektroniki wa Uondoshwaji wa Shehena Bandarini. Aidha, Serikali imekamilisha mkakati wa uendeshaji wa mfumo huo na Mfumo wa Utoaji wa Vibali na Leseni za Mazao utakaounganishwa na Mfumo wa Pamoja wa Kielektroniki wa Uondoshwaji wa Shehena Bandarini kwa ajili ya kurahisisha utoaji wa vibali na leseni za mazao.

***31. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Serikali itaendelea kuhamasisha sekta binafsi kushiriki katika miradi na programu za maendeleo ili kuongeza mchango wa sekta hiyo katika kukuza uchumi. Aidha, Serikali itaendelea kufanya mapitio ya sera, sheria, kanuni na miongozo mbalimbali inayohusu uwekezaji kwa lengo la kuweka mazingira bora ya uwekezaji nchini ikiwa ni pamoja na kukuza ushiriki wa Watanzania katika miradi ya kimkakati ya uwekezaji.

**SIASA**

**Hali ya Siasa na Kuimarika kwa Demokrasia Nchini**

***32. Mheshimiwa Spika,*** kwa ujumla hali ya siasa nchini ni tulivu na Vyama vya Siasa vinaendelea kutekeleza majukumu yao ikiwemo kufanya mikutano ya hadhara katika maeneo mbalimbali nchini. Aidha, Serikali imeendelea kuratibu vikao vya maridhiano ya kisiasa na Vyama vya Siasa nchini ili kuleta umoja, amani na utulivu katika nchi yetu ambao umekuwa ni utamaduni wetu tangu tupate uhuru. Kipekee naomba nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye amekuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha kunakuwepo na mtangamano wa kisiasa nchini unaojumuisha siasa safi, za kiustaarabu na zinazoheshimu mawazo ya kila mmoja wetu.

***33. Mheshimiwa Spika,*** katika jitihada za kukuza na kuimarisha demokrasia ya vyama vingi nchini, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa imeratibu shughuli za Vyama vya Siasa kwa

kuhakikisha kunakuwepo na fursa sawa katika shughuli za siasa nchini. Katika mwaka 2022/2023, Serikali imetoa ruzuku jumla ya shilingi bilioni 17.5 kwa vyama vya siasa sita vyenye sifa ya kupata ruzuku. Vyama hivyo ni NCCR-Mageuzi, CCM, CHADEMA, DP, CUF na ACT-Wazalendo. Hatua hii, imesaidia kuendeleza na kuimarisha uendeshaji wa shughuli za vyama vya siasa na demokrasia nchini.

***34.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, chaguzi ndogo za ubunge ziliendeshwa katika jimbo la Amani, Zanzibar na udiwani katika kata 12 Tanzania Bara. Chaguzi hizo zimefanyika kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo vifo na baadhi ya Waheshimiwa Madiwani kukosa sifa za kuendelea na nyadhifa hizo. Nitumie fursa hii kuvishukuru vyama vyote vilivyoshiriki chaguzi hizo kwani vimeonesha ukomavu mkubwa wa kisiasa. Kipekee nikipongeze Chama cha Mapinduzi kwa ushindi wa Jimbo la Amani pamoja na viti 12 vya udiwani katika chaguzi hizo.

***35.*** ***Mheshimiwa Spika**,* katika mwaka 2023/2024, shughuli za maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 pamoja na Uchaguzi wa Serikali za Mitaa utakaofanyika mwaka 2024 zitaendelea. Kazi zitakazofanyika ni pamoja na kulifanyia maboresho Daftari la Kudumu la Wapiga Kura; kuboresha mifumo ya menejimenti ya uchaguzi; kuendelea na mchakato wa marekebisho ya sheria za uchaguzi; kuandaa kanuni za uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani; na kutoa elimu ya mpiga kura kwa wananchi. Nitumie fursa hii kuwaomba viongozi wa vyama vya siasa kuhamasisha Wanachama na Watanzania wote wenye sifa kujiandikisha kwenye daftari hilo na kupata kitambulisho halali cha mpiga kura pale zoezi hilo litakapoanza rasmi.

**BUNGE**

***36.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Ofisi ya Bunge imeendesha mikutano mitatu ya Bunge na mikutano

mitatu ya Kamati za Kudumu za Bunge. Katika kipindi hicho, jumla ya maswali ya msingi 460 pamoja na ya nyongeza 1,426 yaliulizwa Bungeni na kujibiwa na Serikali.

***37. Mheshimiwa* Spika,** Bunge pia lilijadili na kupitisha miswada saba na maazimio mawili ya Kimataifa yanayotokana na Kamati za Kudumu za Bunge na hatimaye kuwasilishwa Serikalini kwa utekelezaji. Vilevile, Kamati za Kudumu za Bunge zilifanya uchambuzi wa Miswada ya Sheria, Sheria ndogo, Taarifa za Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali, Taarifa za Utendaji wa Wizara na Taasisi za Serikali na ufuatiliaji wa utekelezaji wa afua za UKIMWI.

***38. Mheshimiwa* Spika,** katika mwaka 2023/2024, Ofisi ya Bunge itaendelea kusimamia shughuli za mikutano minne ya Bunge na mikutano minne ya Kamati za Kudumu za Bunge. Kuratibu ushiriki wa Wabunge katika mikutano ya kimataifa ikiwemo Bunge la Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika, Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki, Bunge la Umoja wa Afrika na Mabunge ya Jumuiya ya Madola. Aidha, Ukumbi wa Bunge utaendelea kuimarishwa pamoja na kukarabati jengo la kumbi za Bunge na majengo ya ofisi.

**MAHAKAMA**

***39. Mheshimiwa Spika,*** ni azma ya Serikali ya awamu ya sita kuhakikisha haki inapatikana kwa wananchi wote bila kujali hadhi ya mtu, uchumi wala kabila. Katika kutekeleza azma hiyo, Serikali imeendelea kufanya maboresho mbalimbali ya kiutendaji pamoja na ujenzi wa miundombinu muhimu ya mahakama kwa lengo la kuongeza ufanisi wa utendaji wa mahakama na kuimarisha mifumo ya utoaji haki.

***40. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023, Serikali imekamilisha miradi ya ujenzi wa Mahakama tatu za hakimu mkazi katika Mikoa ya Lindi, Songwe na Katavi. Aidha, ujenzi wa Mahakama za Wilaya 28 katika Wilaya za Same, Mwanga,

Tandahimba, Nanyumbu, Namtumbo, Mvomero, Gairo, Ngara, Kilombero, Mkinga, Kakonko, Buhigwe, Uvinza, Butiama, Rorya, Itilima, Busega, Mbogwe, Nyang'hwale, Kyerwa, Misenyi, Tanganyika, Kaliua, Manyoni, Bunda, Kilindi, Rungwe na Sikonge umekamilika. Vilevile, ujenzi wa mahakama ya mwanzo katika Wilaya ya Kilindi eneo la Kimbe na ukarabati wa Mahakama Kuu ya Tabora pamoja na Mahakama ya Hakimu Mkazi Moshi umekamilika.

***41. Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Serikali inaendelea na ujenzi wa Mahakama nne za Wilaya za Ulanga, Ubungo, Liwale na Kwimba pamoja na Mahakama za Mwanzo saba za Kinesi, Mahenge, Luilo, Newala, Usevya, Nyakibimbili na Kabanga. Kwa upande mwingine, inaendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa jengo la makao makuu Jijini Dodoma, nyumba za majaji na ukarabati wa jengo la zamani la makao makuu Dodoma na jengo la mahakama Wilaya ya Maswa.

***42. Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha mifumo ya utoaji haki, Serikali imeongeza majaji wa mahakama ya rufaa kutoka 16 hadi 24 na wa mahakama kuu kutoka 78 hadi 98. Vilevile, idadi ya mahakimu iliongezeka kutoka mahakimu 245 hadi 293.

***43. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023 Mahakama imesikiliza na kukamilisha mashauri 134,989. Ufanisi huu umechangiwa na ongezeko la watendaji katika mahakama, kuendesha mashauri na mikutano kwa njia ya mtandao na kukamilika kwa miundombinu muhimu ya mahakama.

***44. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Serikali itaendelea kutekeleza miradi ya ujenzi wa miundombinu kwa lengo la kusogeza huduma za Mahakama karibu na wananchi ili huduma hizo zipatikane kwa wakati na gharama nafuu.

## SEKTA ZA UZALISHAJI

### Kilimo

***45. Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kutoa kipaumbele katika sekta ya kilimo ili kuinua Pato la Taifa na la mtu mmoja mmoja. Aidha, hatua mbalimbali zenye lengo la kuongeza tija na uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara zimeendelea kuchukuliwa. Hatua hizo ni pamoja na: kuwezesha wakulima kupata mbegu bora zinazoendana na hali ya hewa nchini; kutoa ruzuku ya pembejeo hususan mbolea na mbegu; kuwezesha upatikanaji wa teknolojia mpya na zana za kisasa; kuimarisha huduma za ugani; kuongeza eneo la umwagiliaji kwa kuanzisha skimu mpya na kukarabati skimu za umwagiliaji zilizopo; na upatikanaji wa masoko ya mazao ndani na nje ya nchi ili kuhakikisha wakulima wananufaika na mauzo ya mazao.

***46. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Serikali imesaini mikataba 31 yenye thamani ya jumla ya shilingi bilioni 284.14 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa skimu za umwagiliaji. Mikataba hiyo inahusu ujenzi wa mabwawa nane, skimu mpya 13 na ukarabati wa skimu za umwagiliaji 17. Ujenzi na ukarabati wa skimu hizo utaongeza eneo la umwagiliaji kwa hekta 50,930 na hivyo kufanya eneo la umwagiliaji kufikia hekta 778,210.6 kutoka hekta 727,280 mwaka 2021/2022.

***47. Mheshimiwa Spika,*** pamoja na changamoto za hali ya hewa, hali ya upatikanaji wa chakula cha kutosha katika maeneo yote nchini imeendelea kuimarika. Katika msimu wa kilimo wa mwaka 2022/2023, uzalishaji wa mazao ya chakula kitaifa ulikuwa tani milioni 17.4 ikilinganishwa na mahitaji halisi ya tani milioni 15.1. Uzalishaji huo umeihakikishia nchi utoshelevu wa chakula kwa asilimia 115 kwa msimu wa kilimo wa mwaka 2023/2024.

***48. Mheshimiwa Spika,*** pamoja na uwepo wa ziada ya mazao ya chakula. Nitoe wito kwa Watanzania kuhifadhi mazao ya nafaka kwani utengamano wa hali ya chakula nchini

umeendelea kuwepo kutokana na ziada inayotokana na mazao yasiyo ya nafaka.

***49.*** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kuhakikisha hali ya chakula inaendelea kuimarika. Hadi Januari, 2023, tani 29,084.21 za mahindi zilisambazwa katika Halmashauri 59 zilizopata changamoto ya upungufu wa chakula kwa mwaka 2022/2023. Mahindi hayo yaliuzwa kwa bei ya chini ya soko ili kuimarisha upatikanaji wa chakula katika maeneo hayo.

***50.*** ***Mheshimiwa Spika***, sambamba na hatua hizo, Serikali imeendelea kuratibu upatikanaji wa mbolea, mbegu bora na viuatilifu kwa wakati ili kuongeza uzalishaji na tija katika kilimo. Hadi Februari, 2023 upatikanaji wa mbolea umefikia tani 407,333 sawa na asilimia 58.33 ya mahitaji ya tani 698,260. Upatikanaji huo umechangiwa na tani 28,672 zilizozalishwa ndani, tani 251,697 zilizoingizwa kutoka nje ya nchi na tani 126,963 ambazo ni bakaa ya msimu wa 2022/2023. Serikali inaendelea kuhakikisha mbolea iliyobaki inapatikana na kusambazwa kwa wakulima kwa wakati ili kukidhi mahitaji ya kila mkoa na kupunguza makali ya bei.

***51.*** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali katika kukabiliana na changamoto ya uzalishaji wa ndani wa mafuta kula, imetoa tani 591.1 za mbegu za alizeti kwa wakulima wa mikoa ya Singida, Dodoma, Kagera, Mbeya na Mwanza kwa utaratibu wa ruzuku. Hatua hiyo, itasaidia kuongeza uzalishaji wa mafuta ya kula na kupunguza matumizi ya fedha za kigeni kuagiza kutoka nje ya nchi. Vilevile, imegawa lita 63,606 za viuatilifu katika mikoa 15 nchini ili kuthibiti viwavijeshi, nzi wa matunda na ndege waharibifu aina ya *Quelea Quelea*. Hatua hiyo imesaidia kuokoa ekari 159,015 za mazao mbalimbali yakiwemo mahindi na mpunga.

***52.*** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha kasi ya kutoa huduma kwa wakulima inaongezeka, Serikali imeendelea

kuimarisha huduma za ugani kwa kutoa mafunzo na vitendea kazi kwa maafisa ugani. Licha ya hayo, imeanzisha Kituo Cha Huduma kwa Wateja. Kituo hicho kimeshatoa huduma ya ushauri na taarifa za kilimo kwa wakulima na wadau wapatao 12,248. Aidha, kwa kupitia mfumo wa *M-Kilimo*, wakulima 7,269,101 na Maafisa Ugani 9,985 wamesajiliwa kwa ajili ya huduma za ushauri wa kitaalamu. Teknolojia hii itawawezesha wakulima, wafugaji na wavuvi kuyafikia masoko ya mazao kwa njia ya simu.

**Kuimarisha Ushirika**

***53.*** ***Mheshimiwa* Spika,** Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kuimarisha ushirika nchini. Hatua hizo ni pamoja na kutoa mafunzo kwa watendaji, kuimarisha udhibiti na usimamizi wa vyama vya ushirika; kuhamasisha Wananchi kujiunga au kuanzisha vyama vya ushirika; kuimarisha upatikanaji wa masoko ya ndani na nje ya nchi; kukuza matumizi ya TEHAMA na kufanya kaguzi.

***54.*** ***Mheshimiwa* Spika,** kutokana na hatua hizo, mauzo kuipitia Vyama vya ushirika yameongezeka ambapo hadi Januari 2023, zimeuzwa jumla ya tani milioni 1.83 zenye thamani ya shilingi trilioni 1.7 ikilinganishwa na tani 597,298 zenye thamani ya shilingi trilioni 1.5 mwaka 2021/2022 kutoka kwenye mazao ya tumbaku, korosho, pamba, kahawa, ufuta, kakao, mkonge, chai, mbaazi, soya, zabibu, miwa na maharage.

**Benki ya Maendeleo ya Kilimo**

***55.*** ***Mheshimiwa* Spika,** kwa upande wa uwezeshaji, Benki ya Maendeleo ya Kilimo imefanikiwa kutoa mikopo ya moja kwa moja yenye thamani ya shilingi bilioni 78.54 kwa wakulima 119,797 wanaojishughulisha na kilimo, mifugo na uvuvi. Aidha, kupitia Mfuko wa Dhamana kwa Wakulima Wadogo imetoa dhamana ya mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 12.95 na kunufaisha wananchi 961 katika mikoa 20 katika shughuli za kilimo, mifugo na uvuvi.

***56.*** ***Mheshimiwa* Spika,** katika mwaka 2023/2024, Serikali itaendelea kuongeza uzalishaji na tija; kuimarisha miundombinu ya umwagiliaji, na upatikanaji wa pembejeo. Vilevile, itaendelea kuimarisha huduma za ugani na upatikanaji wa masoko ya mazao ya kilimo na kuwajengea uwezo wakulima wadogo.

**Mifugo**

***57.*** ***Mheshimiwa Spika,*** kuimarika kwa huduma za ugani ikiwemo utoaji elimu kwa umma kuhusu ufugaji bora wa ng'ombe wa maziwa wa kibiashara umesababisha kuongezeka kwa uzalishaji wa maziwa kufikia lita bilioni 3.62 katika mwaka 2022/2023 ikilinganishwa na lita bilioni 3.4 mwaka 2021/2022. Aidha, uzalishaji wa zao la nyama umeongezeka kwa asilimia 4.3 kutoka tani 769,966.66 mwaka 2021/2022 hadi tani 803,264.32 mwaka 2022/2023. Vilevile, jumla ya vipande milioni 14.19 vya ngozi vyenye thamani ya shilingi bilioni 31.11 vilizalishwa ikilinganishwa na vipande milioni 13.56 vyenye thamani ya shilingi bilioni 28.5 vilivyozalishwa mwaka 2021/2022.

***58.*** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023, Serikali imenunua pikipiki 1,200 na magari 13 ili kurahisisha utoaji wa huduma za ugani katika ngazi ya Kata na Vijiji. Vilevile, Serikali imewezesha mafunzo rejea kwa Maafisa Ugani 487 na wataalam wawakilishi 28 kutoka sekta binafsi katika kanda nane. Mafunzo hayo yalihusu Mpango wa Mabadiliko wa Sekta ya Mifugo, Ufugaji bora na wa Kibiashara, Fursa za Uwekezaji katika sekta ya mifugo, matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika utoaji wa huduma za ugani, uboreshaji wa kosaafu za mifugo, udhibiti wa magonjwa ya mifugo, uendelezaji wa malisho na upatikanaji wa maji.

***59.*** ***Mheshimiwa Spika,*** vifo vya mifugo vinavyotokana na magonjwa yanayoenezwa na kupe vimepungua kwa takriban asilimia 60. Mafanikio hayo yametokana na hatua ya Serikali kuimarisha huduma za mifugo pamoja na ujenzi wa miundombinu muhimu ikiwemo majosho ya kuogesha mifugo.

***60. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Serikali itaendelea kuimarisha sekta ya mifugo kwa kuhakikisha upatikanaji wa mbegu bora za mifugo, malisho, maji na vyakula vya mifugo. Hali kadhalika, Serikali itaboresha huduma za utafiti na mafunzo ya taaluma za mifugo pamoja na kuanzisha na kuendeleza vituo atamizi vya uwekezaji vya vijana.

**Uvuvi**

***61. Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuinua kipato cha wananchi wake, kuimarisha upatikaji wa samaki na uendelevu kupitia ukuzaji wa viumbe maji. Katika mwaka 2022/2023, tani 28,856.87 za samaki zilivuliwa kutoka katika ukuzaji viumbe maji ikiwemo ufugaji kwenye mabwawa na vizimba. Kiasi hicho cha samaki kiliwezesha mauzo ya nje ya nchi yenye thamani ya shilingi bilioni 238.49. Vilevile, tani za mwani 4,134.6 zenye thamani ya shilingi bilioni 4.34 zilizalishwa na kuuzwa nje ya nchi.

***62. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Serikali imeendelea kuboresha hali ya masoko ya samaki nchini kupitia ujenzi wa masoko mbalimbali ya samaki. Masoko yaliyoboreshwa ni pamoja na Zingibari (Halmashauri ya Mkinga), Kipumbwi (Pangani), Ng'ombo (Nyasa), Manda (Ludewa), Maporomoko (Tunduma), Kyamkwikwi (Muleba), Nyamikoma (Busega) pamoja na mialo ya kupokelea samaki katika Halmashauri za Momba (Masuche), Nkasi (Karungu) na Chato (Chato beach).

***63. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Serikali itaendelea kuimarisha upatikanaji wa mbegu bora za mifugo, malisho, vyakula vya mifugo na maji. Vilevile, itatoa kipaumbele katika kuimarisha afya ya mifugo, kuboresha huduma za ugani, kuanzisha na kuendeleza vituo atamizi vya uwekezaji vya vijana, kuimarisha huduma za utafiti na mafunzo ya taaluma za mifugo.

***64. Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Serikali itaendelea kuimarisha Shirika la Uvuvi Tanzania, usimamizi na udhibiti wa ubora, usalama na viwango vya samaki na mazao ya uvuvi pamoja na kuimarisha huduma za utafiti, mafunzo na ugani. Aidha, Serikali itaimarisha miundombinu ya masoko ya samaki, vituo vya kuendeleza ukuzaji wa viumbe maji na kuanza ujenzi wa meli za uvuvi katika bahari kuu.

**MALIASILI NA UTALII**

***65. Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuimarisha sekta za maliasili na utalii kupitia utekelezaji wa programu mbalimbali ili kukuza utalii, kuitangaza nchi yetu na vivutio vyake kitaifa na kimataifa pamoja na kuimarisha mchango wa sekta hizo kwenye pato la Taifa. Katika mwaka 2022/2023, programu mbalimbali zimeendelea kutekelezwa ikiwemo Programu ya Tanzania - *The Royal Tour na* utangazaji wa vivutio vya utalii kupitia matukio mbalimbali na vyombo vya habari ikiwemo *Tanzania Safari Channel*.

***66. Mheshimiwa Spika,*** kutokana na jitihada hizo, idadi ya watalii wa kimataifa imeongezeka kutoka watalii 922,692 katika mwaka 2021 hadi kufikia watalii takriban milioni 1.4 mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 57.7. Vilevile, idadi ya watalii wa ndani imeongezeka kutoka watalii 788,933 mwaka 2021 hadi watalii milioni 2.4 mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 199.5. Aidha, Hifadhi ya Taifa ya Serengeti imeendelea kuwa hifadhi bora duniani ambapo kwa miaka minne mfululizo kuanzia mwaka 2019 hadi 2022 imepata tuzo ya dhahabu ya utoaji wa huduma bora iliyotolewa na *European Society for Quality Research*.

***67. Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa Hifadhi ya Taifa ya Ngorongoro, kumekuwa na changamoto ya ongezeko la watu, mifugo, makazi holela na shughuli za kibinadamu hivyo kukosekana kwa uwiano baina ya uhifadhi, ukuzaji wa utalii na maendeleo ya jamii. Hali hiyo imekuwa ikitishia uendelevu wa

hifadhi na ustawi wa maisha ya watu wanaoishi katika hifadhi hiyo kutokana na sheria za uhifadhi kutoruhusu shughuli nyingi za kiuchumi na kimaendeleo katika eneo hilo. Ili kutatua changamoto hiyo, Serikali iliendesha zoezi la hiari la kuondoa makazi na shughuli za kibinadamu ndani ya Hifadhi kwa kuhamisha wenyeji waliokuwa tayari kuhama kwenda kwenye maeneo yaliyotengwa katika Kijiji cha Msomera katika Halmashauri za Wilaya za Handeni na Kilindi mkoani Tanga.

***68.*** ***Mheshimiwa Spika,*** zoezi hilo limefanyika kwa umakini mkubwa na kwa kuzingatia haki za wanaohama. Hadi kufikia Januari, 2023 jumla ya kaya 1,524 zenye watu 8,715 na mifugo 32,842 zilikuwa zimejiandikisha kwa ajili ya kuhama kwa hiari kwenda Kijiji cha Msomera. Kati ya kaya hizo, kaya 551 zenye watu 3,010 na mifugo 15,521 tayari zimehamishwa kwa hiari kwenda Msomera.

***69.*** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024 Serikali itaendelea kuibua na kuendeleza mazao ya utalii ya kimkakati ikiwemo utalii wa fukwe, mikutano na matukio, meli, michezo na utamaduni. Vievile, itaendelea kuimarisha miundombinu katika maeneo ya hifadhi, kukarabati majenzi ya kale na kuyatangaza kidijitali pamoja na kutekeleza mikakati ya kuongeza thamani ya mazao ya misitu.

**MADINI**

***70.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuipa kipaumbele sekta ya madini ili kuhakikisha inanufaisha wananchi na kuongeza mchango wa sekta hiyo kwenye Pato la Taifa. Katika mwaka 2022/2023, Serikali ilianzisha vituo 26 vya ununuzi wa madini na kutoa jumla ya leseni tano za uchenjuaji wa madini. Aidha, jumla ya shilingi bilioni 409.66 sawa na asilimia 85.43 ya lengo la shilingi bilioni 479.51 zilikusanywa kutokana na mrabaha, ada ya ukaguzi, mauzo ya madini kwenye masoko na vituo na ada ya leseni za uchimbaji.

***71. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Serikali itaendelea kuhamasisha biashara na uwekezaji katika sekta ya madini; kuwaendeleza wachimbaji wadogo; kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini; kusimamia mifumo ya ukaguzi wa shughuli za migodi; na kuzijengea uwezo taasisi zinazosimamia sekta hiyo.

**NISHATI**

***72. Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kutekeleza azma yake ya kuimarisha shughuli za kiuchumi na kijamii kwa kuhakikisha wananchi wake wanapata nishati ya umeme, mafuta na gesi kwa uhakika na bei nafuu.

**Umeme**

***73. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023, Serikali imeendelea kutekeleza miradi ya kusambaza umeme vijijini awamu ya tatu mzunguko wa pili. Hadi Machi, 2023 asilimia 76.7 ya Vijiji vya Tanzania Bara vimeunganishwa na huduma ya umeme. Utekelezaji wa miradi hiyo ikiwa ni pamoja na mkakati wa kuboresha upatikanaji wa nishati bora na safi ya kupikia kwa wananchi wanaoishi vijijini inaendelea vizuri na ipo katika hatua mbalimbali.

***74. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Serikali imekamilisha ufungaji wa mitambo mitatu yenye uwezo wa kuzalisha megawati 135 katika mradi wa Kinyerezi I *Extension*. Kufungwa kwa mitambo hiyo kumeongeza uwezo wa mitambo kufua umeme katika gridi ya Taifa kwa asilimia 7.52. Aidha, uboreshaji wa mtandao wa miundombinu ya kusafirisha na kusambaza umeme nchini umesaidia kuboresha maisha ya watu kwa kutoa fursa za kiuchumi na kijamii.

**Mafuta na Gesi**

***75. Mheshimiwa Spika,*** katika kutimiza azma ya kuhakikisha kuwa asilimia 80 ya Watanzania wanatumia nishati safi kupikia ifikapo mwaka 2033, kimeundwa kikosi kazi cha Taifa kuchakata na kutoa suluhu ya afua ya nishati safi ya kupikia ambacho

nakisimamia mimi mwenyewe. Hii ni kufuatia maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu matumizi ya nishati safi ya kupikia. Kazi zinazoendelea ni pamoja na kuandaa rasimu ya Dira ya Taifa ya miaka 10 ya kuhamia katika matumizi ya nishati safi ya kupikia pamoja na Rasimu ya Mpango Mkakati.

***76.*** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa gesi, Serikali inaendelea kufanya tafiti katika vitalu vya mafuta na gesi asilia katika vitalu vya kimkakati ikiwa ni pamoja na kuimarisha Mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia na Mkakati wa matumizi ya nishati jadidifu na tungamotaka.

***77.*** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024, Serikali itaendelea kukamilisha utekelezaji wa miradi ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa nishati ya umeme, mafuta na gesi. Aidha, Serikali itaendelea kutekeleza Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu na kusambaza umeme katika vitongoji 36,336 vya Tanzania Bara.

**ARDHI**

***78.*** ***Mheshimiwa Spika,*** sekta ya ardhi imeendelea kuwa kiungo wezeshi kwa shughuli za sekta nyingine za uzalishaji ikiwemo viwanda, kilimo, mifugo, maliasili, utalii, madini na miundombinu. Katika, mwaka 2022/2023, Serikali imeandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji 110 katika Halmashauri za Wilaya 16 na Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Wilaya tatu za Kigoma, Nsimbo na Ngorongoro. Idadi hii inafanya kuwa na jumla ya vijiji 2,673 vyenye Mipango ya Matumizi ya Ardhi.

***79.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Serikali itaendelea kuwezesha na kuandaa Mipango ya Matumizi ya ardhi ya Vijiji, Wilaya na Kanda; utatuzi wa migogoro ya ardhi; kuboresha Mfumo wa Taarifa za Matumizi ya Ardhi nchini; na kupanga, kurasimisha na kumilikisha ardhi kwa wananchi.

## USAFIRI NA USAFIRISHAJI

***80.*** ***Mheshimiwa Spika,*** miundombinu ya usafiri na usafirishaji ni msingi wa uchumi wa Taifa na inatoa huduma muhimu kwa wananchi wetu. Usimamizi thabiti wa miundombinu hiyo unaipa fursa Serikali kuongeza thamani ya huduma na rasilimali fedha zinazoonekana moja kwa moja kwa manufaa ya jamii.

### Barabara na Madaraja

***81.*** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023, Serikali imejenga jumla ya kilomita 317.65 za barabara kwa kiwango cha lami ambazo zimehusisha barabara kuu, barabara za mikoa na wilaya. Ujenzi huo umesaidia kurahisisha utoaji wa huduma ya usafiri na usafirishaji katika maeneo tofauti nchini na umezingatia uendelevu kwa watumiaji wa sasa na wa baadaye.

***82.*** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali inatambua umuhimu wa kupunguza msongamano wa magari katika majiji na miji ili kuongeza ufanisi katika utendaji na utekelezaji wa majukumu ya wananchi na ukuaji wa uchumi wa Taifa. Katika hatua za kuhakikisha kuwa huduma za uchukuzi zinaboreshwa, Serikali inaendelea na Awamu ya Pili, Tatu, Nne na Tano ya ujenzi wa barabara na Miundombinu ya Mabasi yaendayo Haraka Mkoani Dar es Salaam na ujenzi wa barabara za mchepuo (bypass) katika Mkoa wa Dodoma na Wilaya ya Maswa.

***83.*** ***Mheshimiwa Spika***, Awamu ya Pili (BRT II) ya ujenzi huo inayohusisha barabara ya Kilwa kutoka katikati ya Jiji la Dar es Salaam kuelekea Mbagala na barabara ya Kawawa kutoka makutano ya Magomeni kupitia Chang'ombe hadi makutano ya barabara ya Kilwa umefikia asilimia 82. Mradi huu una barabara zenye urefu wa kilomita 20.3; vituo vya mabasi 29; barabara za juu mbili; majengo mawili ya *Terminal*; *Depot* moja na *Feeder station* nne.

Aidha, Awamu ya Tatu (BRT III) inayohusisha Barabara ya Nyerere kutoka katikati ya Jiji la Dar es Salaam hadi

Gongolamboto yenye urefu wa kilomita 23.6 imekamilika kwa asilimia 5.

***84.*** ***Mheshimiwa Spika***, kwa upande wa Jiji la Dodoma, ujenzi wa barabara ya mchepuko ya Dodoma umelenga kupunguza foleni ya magari katikati ya Jiji kutokana na magari yanayosafiri katika ushoroba wa kati na ushoroba wa Barabara Kuu ya *Trans-Africa 4* inayoanzia Cape Town, Afrika Kusini hadi Cairo, Misri. Mradi huu wenye barabara yenye urefu wa jumla ya kilomita 112.3 umefikia kwa asilimia 17 katika sehemu ya kwanza na sehemu ya pili imefikia asilimia 22. Aidha, ujenzi wa barabara ya mchepuo Maswa (Maswa Bypass) yenye urefu wa kilomita 11.3 kwa kiwango cha lami umefikia asilimia 72.

**Vivuko**

***85.*** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kujenga vivuko vipya na kukarabati vivuko vilivyochakaa nchini ili kuwaondolea kero ya usafiri wananchi wanaotegemea vivuko ili kuharakisha na kurahisisha shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii. Katika mwaka 2022/23, Serikali imeendelea na ujenzi wa vivuko vipya vya Kisorya – Rugezi, Ijinga – Kahangala, Bwiro – Bukondo na Nyakarilo – Kome. Vilevile, ujenzi wa vivuko vya Buyagu – Mbalika na Magogoni – Kigamboni upo kwenye hatua za ununuzi. Aidha, ukarabati wa vivuko vya MV Musoma, MV Kazi, MV TEMESA na MV Tanga umekamilika kwa asilimia 100 na ukarabati wa vivuko vya MV Misungwi, MV Nyerere, MV Kilombero, MV Mara, MV Ujenzi, MV Kitunda, MV Ruhuhu, MV Old Ruvuvu na MV Magogoni unaendelea.

**Viwanja vya Ndege na Usafiri wa Anga**

***86.*** ***Mheshimiwa Spika***, usafiri wa anga ni kiungo muhimu katika kuchangia ukuaji wa pato la mtu binafsi na Taifa kwa ujumla. Usafiri huu umeendelea kutengeneza fursa za ajira zilizo rasmi na zisizokuwa rasmi, kuimarisha upatikanaji wa huduma za usafiri wa uhakika, na hivyo kutoa mchango muhimu katika maendeleo ya kiuchumi. Kwa kutambua umuhimu huo, Serikali

imeendelea kutoa kipaumbele katika uimarishaji na uboreshaji wa huduma za usafiri wa anga nchini.

***87. Mheshimiwa Spika,*** Serikali katika mwaka 2022/2023 imeendelea na awamu ya kwanza ya ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato. Kukamilika kwa ujenzi wa kiwanja hiki kutarahisisha usafirishaji wa watu na bidhaa kutoka na kuingia katika Jiji la Dodoma, kati ya Tanzania na nchi mbalimbali; kukuza utalii na uchumi na kuongeza fursa za ajira. Aidha, ujenzi huo utakapokamilika pamoja na kuimarisha usafiri anga kwa kuruhusu ndege kubwa na za kimataifa kutua, utasaidia kufanya Jiji la Dodoma kuwa jiji la kisasa na kimataifa.

***88. Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha usafiri wa anga, mashirika ya ndege ya *KLM, Eurowing, Edelweiss Airline* na Saudia *Airline* yameanza kutoa huduma za usafiri wa anga kuanzia Tanzania. Hatua hizi zitaendelea kuimarisha sekta ya utalii na hivyo kuongeza mchango wa sekta hiyo kwenye mapato na ukuaji wa uchumi.

**Reli**

***89. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Serikali imefanya ununuzi wa vifaa vya uendeshaji wa Reli ya SGR ambapo utengenezaji wa mabehewa 59 ya abiria umefikia asilimia 92. Kati ya mabehewa hayo, 14 yaliwasili nchini Novemba, 2022 na 45 yaliyobaki yanatarajiwa kuwasili Mei, 2023. Aidha, utengenezaji wa vichwa vya treni 17 vya umeme na seti 10 za treni (Electric Multiple Unit - EMU) kwa ajili ya treni ya abiria umefikia asilimia 31.6 na seti moja ya treni hizo inatarajiwa kuwasili Juni, 2023. Aidha, utengenezaji wa mabehewa 1,430 ya mizigo umefikia asilimia 35. Upatikanaji wa vifaa hivyo utaboresha na kuongeza kiwango cha ubebaji mizigo na kupunguza gharama za usafiri na usafirishaji, na hivyo kupunguza gharama za maisha.

***90. Mheshimiwa Spika*** Aidha, katika mwaka 2022/2023, pamoja na uendelezaji wa ujenzi wa Reli ya SGR, Serikali

imeendelea na ukarabati wa njia ya Reli ya Kati kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza na Kigoma. Mkataba wa ukarabati wa njia ya reli ya Kaliua-Mpanda ulisainiwa Novemba, 2022.

**Usafiri katika Maziwa Makuu**

***91.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha huduma za usafiri na usafirishaji katika maziwa makuu, Februari, 2023, meli ya MV Mwanza Hapa Kazi Tu iliyo katika Ziwa Victoria ilishushwa majini kwa ajili ya ukamilishaji. Meli hiyo inatarajiwa kuanza kutoa huduma katika mwaka 2023/2024. Aidha, ukarabati wa meli ya MV Umoja katika Ziwa Victoria na MT Sangara katika Ziwa Tanganyika unaendelea. Kukamilika kwa meli hizo kutaboresha huduma za usafiri wa abiria na mizigo kwa njia ya meli; kufungua masoko mapya ndani na nje ya nchi; kurahisisha shughuli za kibiashara, uzalishaji wa mazao, uvuvi, madini; na kuchochea utalii katika maeneo ya maziwa makuu.

**Bandari**

***92.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kutekeleza Mradi wa Bandari Kavu ya Kwala ambapo ujenzi wa barabara ya zege yenye urefu wa kilomita 15.5 kutoka Vigwaza umefikia asilimia 98 na ujenzi wa bandari umefikia asilimia 87. Kukamilika kwa bandari hiyo na kuanza kutumika kutapunguza msongamano wa mizigo na magari katika bandari ya Dar es Salaam, kuongezea nafasi ya kuhifadhi mizigo na kupunguza muda wa magari kusafirisha mizigo. Hali hiyo itaiwezesha bandari ya Dar es Salaam kufanya kazi kwa ufanisi zaidi na hivyo kuongeza mapato kwa bandari na wafanyabiashara.

***93.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, sekta ya usafiri na usafirishaji itaendelea kukamilisha ujenzi wa miundombinu na uboreshaji wa huduma za usafiri kwa njia reli, anga, barabara na majini. Aidha, Serikali imeamua kwa dhati kuanza ujenzi wa bandari ya Bagamoyo kwa kuhamisha wananchi waliolipwa fidia, wanaotakiwa kupisha ujenzi wa bandari na kuanza maandalizi ya ujenzi wa miundombinu

wezeshi kwa ajili ya bandari ya Bagamoyo ikiwemo barabara, reli na umeme.

**MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI**

***94.*** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kuimarisha miundombinu ya mawasiliano na teknolojia ya habari nchini kwa lengo la kuongeza chachu ya maendeleo ya jamii, siasa, usalama na uchumi kwa kuzingatia mabadiliko ya teknolojia ulimwenguni.

***95.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Serikali imeendelea kutekeleza Mfumo wa Anwani za Makazi kwa kuzingatia maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyatoa tarehe 08 Februari 2022 wakati wa uzinduzi wa "Operesheni Anwani za Makazi". Utekelezaji wa Mfumo huo umefanyika nchi nzima ambapo hadi Februari, 2023 jumla ya taarifa milioni 12.66 za Anwani za Makazi zikijumuisha majengo na viwanja zimekusanywa. Utekelezaji wa Mfumo wa Anwani za Makazi umewezesha utambuzi wa mtu, kitu au jengo lilipo na hivyo kuimarisha usalama na kurahisisha utoaji wa huduma na ufikishaji wa bidhaa mahali stahiki. Aidha, Serikali inaendelea na uhakiki wa taarifa za anwani za makazi zilizokusanywa ili kuboresha taarifa hizo.

***96.*** ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, Serikali imekamilisha ujenzi wa minara 1,201 katika kata 1,087 zenye vijiji 3,378. Kwa upande wa Zanzibar ujenzi wa minara 42 umekamilika na kufanya eneo lote la Zanzibar kuwa na mawasiliano ya simu. Aidha, Serikali imesaini mikataba ya ujenzi wa minara katika kata 1,242 zenye vijiji 3,654 Tanzania Bara. Kukamilika kwa miradi hiyo kutafanya Taifa kuongeza usikivu katika mawasiliano ya njia ya simu na usafirishaji wa taarifa kwa kasi na kiwango kinachokusudiwa. Nitoe wito kwa Watanzania wote kuendelea kuchangamkia fursa zinazotokana na matumizi ya teknolojia ya mawasiliano katika kujenga uchumi wa kidijitali.

**Uchumi wa Kidijitali**

***97. Mheshimiwa Spika***, ni ukweli usiopingika kuwa fursa za kidijitali na uchumi zimekuwa zikiongezeka ulimwenguni. Fursa hizo zimewezesha ushiriki wa watu wengi na kurahisisha upatikanaji wa huduma za kimtandao. Vilevile, maendeleo ya kidijitali yamerahisisha mawasiliano ya kijamii, kisiasa na kiuchumi kwa kupunguza gharama, kuokoa rasilimali muda na upatikanaji wa taarifa na fursa mbalimbali.

***98. Mheshimiwa Spika,*** kwa kutambua umuhimu huo, Serikali katika mwaka 2023/2024 itaendelea na maandalizi ya Mkakati wa Taifa wa Uchumi wa Kidijitali ili kuhakikisha nchi yetu haibaki nyuma katika ulimwengu wa kidijitali na kuwa wananchi wananufaika na fursa zitokanazo na uchumi huo. Kwa upande mwingine, Serikali itaendelea kujenga misingi ya matumizi ya TEHAMA ikiwa ni pamoja na kuendeleza na kuboresha Mfumo wa Kidijitali wa Mfumo wa Anwani za Makazi.

**HUDUMA ZA JAMII**

**Elimu**

***99. Mheshimiwa Spika,*** tangu awali, Serikali ya awamu ya sita imejipambanua katika kuinua viwango vya elimu kwa kuweka mazingira bora ya kufundishia na kujifunzia. Hii ni pamoja na kuhakikisha kila mtoto wa Tanzania anapata fursa ya kusoma na kumaliza mzunguko wa elimu kama inavyotakiwa. Ili kutekeleza azma hiyo, Serikali imeendelea kujenga, kukarabati na kukamilisha miundombinu ya kutolea elimu katika ngazi mbalimbali.

***100. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Serikali imeendelea na ujenzi wa shule mpya 231 za sekondari, upanuzi wa shule kongwe 18 za sekondari, ujenzi wa shule mpya sita za Msingi, ujenzi wa vyumba vya madarasa 1,072 katika shule kongwe za msingi, na ujenzi wa nyumba za walimu 809 ambapo kati ya nyumba hizo, 298 ni za walimu wa shule za msingi na 511 za walimu shule za sekondari. Aidha, imeendelea

kutekeleza mradi wa ujenzi wa shule za wasichana za bweni kidato cha tano na sita katika mikoa yote Tanzania bara ambapo ujenzi wa shule 10 kati ya 26 umekamilika.

***101. Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea pia kutoa mikopo na kuongeza wigo wa upatikaji wa mikopo ya elimu ya juu sambamba na kuboresha miundombinu ya vyuo vya elimu ya juu nchini. Katika mwaka 2022/2023, kiasi cha shilingi bilioni 654 zilitengwa kwa ajili ya mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu ikilinganishwa na shilingi bilioni 570 zilizotengwa mwaka 2021/2022. Aidha, idadi ya wanufaika imeongezeka kutoka 177,605 mwaka 2021/2022 hadi 202,877 mwaka 2022/2023.

***102. Mheshimiwa Spika,*** Serikali pia imeongeza kiwango cha posho ya kujikimu ya wanafunzi wa elimu ya juu kutoka shilingi 8,500 hadi shilingi 10,000 kwa siku. Mafanikio haya ni kielelezo tosha cha umakini, uzalendo, maono na mapenzi makubwa ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuboresha ustawi wa maisha ya wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu. Kwa upande mwingine, kupitia *Samia Scholarship*, Serikali imetoa ufadhili kwa wanafunzi 244 wa kike wenye ufaulu wa juu ili kusoma katika vyuo vikuu mbalimbali katika fani za utabibu, uhandisi, sayansi, teknolojia na hisabati. **Ama kwa hakika Mama anajali!**

***103. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Serikali itaendelea kuhuisha Mitaala ya Elimu na kuongeza fursa za upatikanaji wa elimu na mafunzo ya ufundi stadi na elimu ya juu.

**Maji**

***104. Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kuimarisha usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji ikiwa ni pamoja na kuhifadhi na kulinda vyanzo vya maji, kujenga mabwawa makubwa, ya kati na madogo katika maeneo mbalimbali nchini kwa lengo la kuongeza uwezo wa nchi kuhifadhi maji na

kuboresha huduma ya upatikanaji wa maji safi na salama katika maeneo ya mijini na vijijini.

***105. Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kutekeleza dhamira yake ya kuhakikisha upatikanaji wa huduma ya maji mijini na vijijini inafikia asilimia 95 na 85 mtawalia mwaka 2025. Hadi kufikia Februari, 2023, hali ya upatikanaji wa huduma ya maji mijini imeongezeka kutoka asilimia 86 mwaka 2022 hadi kufikia asilimia 88 na vijijini imeongezeka kutoka asilimia 72.3 mwaka 2022 hadi kufikia asilimia 77.

***106. Mheshimiwa Spika,*** ongezeko la hali ya upatikanaji wa huduma ya maji mijini na vijijini limetokana na kukamilika kwa miradi 36 ya maji mijini na miradi 382 ya maji vijijini inayonufaisha wananchi zaidi ya milioni mbili. Aidha, miradi mingine 139 mijini na 647 vijijini ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

***107. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Serikali itaendelea kutekeleza miradi ya maji vijijini na mijini ikiwemo miradi ya miji 28; ujenzi wa bwawa la Kidunda; kuanza ujenzi wa Bwawa la Farkwa; kujenga mabwawa ya ukubwa wa kati; kuanza ujenzi wa miradi ya uondoshaji wa majitaka; na kuimarisha usimamizi na uhifadhi wa rasilimali za maji ili kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

**Afya**

***108. Mheshimiwa Spika,*** ni azma ya Serikali ya awamu ya sita kuhakikisha Watanzania wote wanapata huduma bora za afya. Kwa msingi huo, Serikali imeendelea kutoa kipaumbele katika sekta ya afya kwa kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuimarisha utoaji wa huduma hizo. Mikakati hiyo ni pamoja na ujenzi wa vituo vya kutolea huduma za afya pamoja na kuimarisha upatikanaji wa dawa na vifaa tiba.

***109. Mheshimiwa Spika,*** Serikali katika kutekeleza azma yake kusogeza huduma za afya karibu na wananchi, imekamilisha awamu ya kwanza ya ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Kanda

Mtwara; na Hospitali za Rufaa za Mikoa ya Mara, Songwe, Shinyanga, Geita na Katavi. Aidha, imekamilisha ujenzi wa hospitali 59 za halmashauri, ukarabati wa hospitali kongwe 19 za halmashauri na ujenzi wa maboma ya zahanati 300. Tayari vituo hivyo vimeanza kutoa huduma.

***110. Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha utoaji wa huduma za afya za dharura, Serikali imejenga majengo ya huduma za dharura katika hospitali za kanda na kufikisha hospitali 36 zenye huduma hiyo kutoka hospitali saba mwaka 2020. Mafanikio haya yamepatikana kutokana na jitihada za makusudi za Mheshimiwa Rais wetu mpendwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwani kwa mara ya kwanza tangu uhuru, nchi yetu imeweka historia ya kuwa na mfumo wa huduma za dharura kuanzia ngazi ya Wilaya hadi Taifa. Awali huduma hizo zilikuwa zinapatikana katika ngazi ya Kanda na Taifa pekee. Uwepo wa huduma za dharura katika hospitali zetu utapunguza vifo kwa asilimia 40.

***111. Mheshimiwa Spika,*** Serikali inatambua kuwa, ujenzi wa miundombinu ya vituo vya kutolea huduma za afya hauwezi kuwa na tija pasipokuwa na watumishi wenye weledi, vifaa, vifaatiba na vitendanishi. Kutokana na ukweli huo, hadi kufikia Februari, 2023, Serikali imesambaza vifaa vyenye thamani ya shilingi bilioni 44.3 pamoja na kuajiri watumishi wa kutoa huduma katika vituo vya kutolea huduma za afya. Aidha, kupitia Programu ya Mfuko wa Pamoja wa Afya, jumla ya shilingi bilioni 48.35 zimetolewa kwa ajili ya uboreshaji wa huduma za afya.

***112. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Serikali itaendelea kuimarisha miundombinu ya kutolea huduma za afya, kuimarisha upatikanaji wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi, kuimarisha utoaji wa huduma za kibingwa na ubingwa bobezi, kuimarisha huduma za afya ya uzazi na kudhibiti magonjwa ya mlipuko. Vilevile, itaendelea kutoa

mafunzo kwa wataalam wa sekta ya afya katika ngazi za ubingwa na ubingwa bobezi.

## HUDUMA KWA MAKUNDI MAALUM

### Huduma kwa Watu Wenye Ulemavu

***113.*** **Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kuboresha huduma kwa Watu Wenye Ulemavu ambapo mwaka 2022/2023 ilitenga jumla ya shilingi bilioni 3.46 kwa ajili ya kukamilisha ukarabati wa vyuo vya Watu Wenye Ulemavu vya Mtapika (Masasi – Mtwara), Luanzari (Tabora), Sabasaba (Singida) na Yombo (Dar es Salaam). Ukarabati huu umewezesha Chuo cha Luanzari kuanza kutoa mafunzo kwa kudahili wanafunzi 400 baada kufungwa kwa zaidi ya miaka 10.

***114. Mheshimiwa Spika,*** ili kuongeza ufanisi wa upatikanaji, utunzaji, uchakataji na utumiaji wa taarifa za watu wenye ulemavu, Serikali imetengeneza Mfumo wa Kielektroniki wa Watu Wenye Ulemavu. Mfumo huo utawezesha kumsajili na kumtambua mtu mmoja mmoja mwenye ulemavu, mahali alipo, shughuli anayoifanya na mahitaji yake. Vilevile, utawawezesha kuunganishwa na huduma mbalimbali zikiwemo kupata cheti za kuzaliwa, matibabu, kuandikishwa shule ya awali na msingi, mikopo ya asilimia mbili inayotokana na mapato ya ndani ya halmashauri na vifaa saidizi.

***115. Mheshimiwa Spika,*** vilevile Serikali imeandaa Mwongozo wa Utekelezaji, Ujumuishwaji na Uimarishaji wa Huduma kwa Watu Wenye Ulemavu wa Mwaka 2022. Mwongozo huo utasaidia kuhakikisha masuala ya usawa, haki, fursa na huduma kwa watu wenye ulemavu yanaimarishwa katika nyanja zote za maendeleo.

***116. Mheshimiwa Spika,*** Serikali katika mwaka 2023/2024 imepanga kuwawezesha watu wenye ulemavu kujiajiri na kuajiriwa kwa kuongeza fursa za mafunzo ya ufundi stadi na marekebisho kutoka watu 460 hadi 1,400.

**Huduma kwa Wazee**

***117. Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kuwatambua na kutoa huduma za msingi za chakula, malazi, mavazi na matibabu kwa wazee wasiojiweza. Hadi sasa tunao wazee 268 wanaoishi katika makazi 14 ya wazee ya Kibirizi, Njoro, Kolandoto, Bukumbi, Ipuli, Fungafunga, Mwanzange, Misufini, Nunge, Nyabange, Kilima, Sukamahela, Magugu pamoja na Nandanga. Ninatoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu na wananchi kwa ujumla tuendelee kuunga mkono juhudi za Serikali katika kuwahudumia wazee na hii ni namna bora ya kutambua umuhimu na michango waliyotoa katika ujenzi wa Taifa hili.

**ULINZI NA USALAMA**

***118. Mheshimiwa Spika,*** hali ya ulinzi na usalama wa mipaka ya nchi yetu imeendelea kuwa shwari bila uwepo wa matukio hatarishi. Katika kuhakikisha hali ya usalama nchini inaendelea kuimarishwa, vyombo vyetu vya ulinzi na usalama vimeendelea kulinda mipaka ya nchi; kudumisha amani, usalama wa raia, mali zao na kufundisha wananchi ulinzi wa umma.

***119. Mheshimiwa Spika,*** Jeshi letu limeendelea kushirikiana na Umoja wa Mataifa, Umoja wa Afrika na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika katika operesheni mbalimbali za ulinzi wa amani. Katika mwaka 2022/2023, vikosi vyetu vilipeleka waangalizi wa kijeshi, wanadhimu na makamanda kwenye nchi zenye migogoro za Lebanon, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Jamhuri ya Afrika ya Kati na Msumbiji. Ushiriki huo ni muhimu kwa kuwa unalitambulisha Taifa kimataifa, kuwaweka askari wetu tayari kila wakati, kujifunza teknolojia mpya na kushirikisha vijana katika kuleta amani.

***120. Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kutambua, kusajili na kutoa vitambulisho vya Taifa ili kuwezesha upatikanaji wa huduma mbalimbali za kijamii, kiuchumi na kiusalama. Aidha, hivi karibuni Serikali imefanya marekebisho ya Kanuni za

Usajili na Utambuzi wa Watu za Mwaka 2023 ili kuwawezesha Watanzania kuendelea kutumia Vitambulisho vya Taifa bila kuwa na ukomo wa matumizi. Hatua hii inapunguza usumbufu na gharama kwa wananchi na Serikali.

***121. Mheshimiwa Spika***, nitumie fursa hii kutoa wito kwa watoa huduma wote zikiwemo Ofisi za Balozi mbalimbali hapa nchini waendelee kutambua na kutoa huduma stahiki kwa wananchi wenye vitambulisho vya Taifa bila kujali tarehe za ukomo zilizo kwenye vitambulisho hivyo.

***122. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024 Serikali itaendelea kuviimarisha na kuviongezea uwezo vyombo vya ulinzi na usalama kwa kuvipatia vifaa na zana bora za kisasa. Vilevile, Jeshi litaendelea kuwajengea vijana wa Kitanzania ukakamavu, uzalendo na uwezo wa kujitegemea.

**MASUALA YA KAZI NA WAFANYAKAZI**

***123. Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuboresha mazingira ya kazi na wafanyakazi kwa kusimamia viwango vya kazi pamoja na masuala ya afya na usalama mahali pa kazi. Katika mwaka 2022/2023, jumla ya kaguzi 3,327 za viwango vya kazi zilifanyika sawa na asilimia 69.31 ya kaguzi 4,800 zilizopangwa kufanyika. Vilevile, kaguzi 96,693 zinazohusu afya na usalama mahali pa kazi zilifanyika ambapo kumekuwa na ongezeko la upimaji wa afya kutoka wafanyakazi 125,616 mwaka 2021/2022 hadi wafanyakazi 169,735 mwaka 2022/2023. Kufuatia kaguzi hizo, waajiri 173 waliokiuka sheria za kazi walichukuliwa hatua.

***124. Mheshimiwa Spika,*** kwa upande mwingine, Serikali imeimarisha Mfumo wa Kielektroniki wa Kushughulikia Maombi ya Vibali vya Kazi. Uimarishaji wa mfumo huo, pamoja na mambo mengine umechangia kwa kiasi kikubwa kuongeza ufanisi katika utoaji wa vibali vya kazi nchini. Mathalani, hadi kufikia Februari, 2023 jumla ya vibali vya kazi 8,576 vilitolewa

sawa na asilimia 92.14 ya maombi ya vibali 9,307 yaliyopokelewa.

***125. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Serikali itaendelea kuimarisha usimamizi na utekelezaji wa sheria za kazi, uratibu wa ajira za wageni na masuala yote yanayohusu usalama na afya mahali pa kazi. Aidha, Serikali itaendelea, kutoa elimu na ushauri kwa wafanyakazi, waajiri na vyama vyao ili kuwa na rasilimali watu imara na yenye tija kwa maendeleo endelevu ya Taifa letu.

**HIFADHI YA JAMII**

***126. Mheshimiwa Spika,*** sekta ya hifadhi ya jamii imekuwa na mchango mkubwa kwenye uchumi pamoja na ustawi kwa wananchi. Aidha, hadi Februari, 2023 deni la shilingi trilioni 2.17 limelipwa katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa watumishi wa umma (PSSSF). Fedha hizo ni stahili ya mafao kwa wanachama waliorithiwa kutoka uliokuwa Mfuko wa PSPF Mwaka 1999.

***127. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Mfuko wa PSSSF umelipa mafao kwa wastaafu, wategemezi na wanufaika wengine wapatao 41,939 yenye thamani ya shilingi trilioni 1.074 na pensheni ya kila mwezi ya shilingi bilioni 507.28 sawa na wastani wa shilingi bilioni 63.41 kila mwezi kwa wastaafu 158,351. Aidha, Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) umelipa mafao ya shilingi bilioni 438.32 kwa wastaafu, wategemezi na wanufaika wengine wapatao 66,628. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 72.3 zililipwa kama pensheni ya kila mwezi kwa wastaafu 27,570 ikiwa ni wastani wa shilingi bilioni 9.04 kwa kila mwezi.

***128. Mheshimiwa Spika,*** kutokana na mapenzi makubwa aliyonayo kwa wananchi wake, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alielekeza kurejesha michango ya watumishi walioondolewa kazini kwa kughushi vyeti. Utekelezaji wa maelekezo hayo umeanza ambapo hadi sasa jumla ya watumishi 11,896 wamerejeshewa

michango yao yenye thamani ya shilingi bilioni 35.02 kupitia PSSSF na NSSF. Mifuko hiyo inaendelea kuwalipa watumishi hao kadri inavyopokea taarifa kutoka kwa waajiri.

***129.*** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kujenga mazingira wezeshi kwa waajiri, kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara na uwekezaji, na kupunguza gharama za uendeshaji ili kukuza uchumi wa nchi na kulinda rasilimali watu. Hatua hizo ni pamoja na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi kupunguza kiwango cha uchangiaji kwa waajiri wa sekta binafsi kutoka asilimia 0.6 hadi asilimia 0.5.

***130.*** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2023/2024, Serikali itaendelea kuimarisha sekta ya hifadhi ya jamii kwa kuhakikisha wananchi wengi wanajumuishwa katika mpango wa Hifadhi ya Jamii wa uchangiaji. Natoa wito kwa sekta isiyo rasmi ikiwemo mama/baba lishe, machinga, bodaboda, wakulima, wavuvi, wafugaji, na wengineo kujiunga na mifuko hiyo kwa manufaa yao ya baadaye.

**Ukuzaji wa Fursa za Ajira na Ujuzi**

***131.*** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kuratibu masuala ya uzalishaji wa fursa za ajira nchini kupitia utekelezaji wa miradi ya kielelezo, kujenga mazingira wezeshi kwa wawekezaji na kuimarisha ushirikiano baina ya Serikali na sekta binafsi. Katika mwaka 2022/2023, jumla ya fursa za ajira 547,031 zilizalishwa. Kati ya hizo, ajira 321,363 zilizalishwa kupitia Serikali na utekelezaji wa miradi ya maendeleo na 225,668 kupitia sekta binafsi.

***132.*** ***Mheshimiwa Spika*****,** Serikali imeendelea kuchukua hatua ili kuhakikisha wahitimu wa mafunzo ya ujuzi wanaunganishwa na fursa za kujiajiri. Utaratibu huo utamwezesha mhitimu wa mafunzo ya ujuzi kupata sehemu ya uzalishaji yenye viwango vinavyohitajika chini ya usimamizi wa wataalamu wenye uzoefu

katika fani husika kwa kipindi maalumu cha miezi 6 hadi 12 kutegemeana na aina ya fani.

***133. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Serikali itaendelea kuwezesha na kuratibu masuala ya ukuzaji wa fursa za ajira na kazi za staha kwa kuboresha na kutekeleza Sera, Mikakati na Mipango mbalimbali ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa ili kuhakikisha nguvu kazi ya Taifa inapata fursa za kujiajiri au kuajiriwa ili kuchangia katika maendeleo ya Taifa.

**UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI**

***134. Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kutekeleza shughuli mbalimbali zinazolenga kuwawezesha wajasiriamali kukuza mitaji yao na kufikia masoko makubwa kupitia Vituo vya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Katika mwaka 2022/2023, jumla ya shilingi bilioni 326.6 zimetolewa kwa wajasiriamali 903,763. Kati yao wanawake ni 478,994 sawa na asilimia 53 na wanaume 424,769 sawa na asilimia 47. Upatikanaji wa fedha hizo umewawezesha wajasiriamali kuanzisha na kukuza biashara zao. Aidha, kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake (*Women Development Fund - WDF*), mikopo yenye thamani ya shilingi milioni 663.4 ilitolewa kwa wanawake 96 ili kuwawezesha kiuchumi.

***135. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Serikali itaendelea kuimarisha utendaji wa mifuko na programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi na kuwaunganisha wajasiriamali na fursa za kiuchumi. Aidha, Serikali itaendelea kuimarisha vituo vya uwezeshaji ili kuchochea shughuli za kiuchumi kwa wananchi.

**MAENDELEO YA VIJANA**

***136. Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuwawezesha vijana ili kujiari, kushiriki kwenye shughuli za maendeleo na kuchangia katika pato la Taifa. Katika mwaka 2022/2023, Mfuko

wa Maendeleo ya Vijana umetoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 1.88 kwa ajili ya kuwezesha miradi 85 ya vijana katika sekta za kilimo, viwanda na biashara kwenye halmashauri 28. Aidha, Serikali imetoa mafunzo ya ujasiriamali, usimamizi, kurasimisha na kuendeleza biashara kwa vijana 2,497 walio katika mikoa ya Kagera, Dodoma, Katavi, Shinyanga na Lindi.

Vilevile, kazi ya kuboresha Mwongozo wa Utoaji mikopo kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana imekamilika na mfuko unatoa mikopo kwa vijana walio katika vikundi, mtu mmoja mmoja na kampuni.

***137. Mheshimiwa Spika***, kwa upande mwingine, Serikali imeendelea kutekeleza Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili kupitia **Mpango wa Jenga Kesho Iliyo Bora.** Mpango huo unalenga kuongeza ushiriki wa vijana katika sekta ya kilimo kwa kuwapatia mafunzo, mashamba, mitaji na kuwaunganisha na fursa za masoko. Awamu ya kwanza ya utekelezaji wa Mpango huo imeanza mkoani Dodoma katika Shamba la Chinangali II lenye ukubwa wa ekari 400. Aidha, zaidi ya hekta 47,000 zimeshapatikana katika mikoa mbalimbali nchini na upimaji udongo unaendelea.

***138. Mheshimiwa Spika***, kupitia Programu ya Taifa ya Kukuza Ujuzi, Serikali imetoa fursa za mafunzo ya ujuzi wa kujiajiri au kuajiriwa kwa vijana 14,542 katika fani mbalimbali kupitia mafunzo ya uanagenzi, uzoefu wa kazi, ufugaji wa samaki na viumbe maji na kilimo cha kisasa kwa njia ya vizimba.

***139.*** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka 2023/2024, Serikali itaendelea kuimarisha uwezo wa Mfuko wa Maendeleo ya Vijana katika kutoa mikopo na mafunzo ya ujasiriamali kwa vijana wengi ili kuwawezesha kujiajiri na kuchangia uchumi wa Taifa. Vilevile, itaanzisha kampeni ya kuwashawishi vijana kushiriki katika kilimo

## MASUALA MTAMBUKA

### Sensa ya Watu na Makazi 2022

***140. Mheshimiwa Spika***, nchi yetu ilitekeleza zoezi la Sensa ya Watu na Makazi tarehe 23 Agosti, 2022. Zoezi hilo lililojumuisha sensa ya watu na makazi, anwani za makazi na majengo lilifanyika kwa mafanikio makubwa na wananchi kuonesha ushirikiano wa hali ya juu. Matokeo ya awali ya Sensa ya Watu na Makazi yalizinduliwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 30 Oktoba, 2022. Matokeo hayo ya awali yamechangia kwa kiasi kikubwa katika maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali ya mwaka 2023/2024. Aidha, Serikali imekamilisha ripoti nane ambazo zimejikita kwenye mgawanyo wa idadi ya watu kwa umri na jinsi. Ripoti hizi zitasaidia kuongeza wigo wa matumizi ya takwimu.

***141. Mheshimiwa Spika,*** napenda kutoa wito kwa viongozi wenzangu na wananchi kuwa tuendelee kuhamasisha matumizi ya matokeo ya sensa ya watu na makazi, majengo na anwani za makazi katika biashara, shughuli za kijamii na mipango ya maendeleo ya nchi. Aidha, nitumie fursa hii kulishukuru Bunge lako tukufu kwa ushirikiano mkubwa ambao Waheshimiwa Wabunge walionesha wakati wa utekelezaji wa zoezi la sensa. Nawashukuru wenyeviti wa kamati za sensa katika ngazi mbalimbali kwa uongozi wao mahiri, makamisaa wa sensa na wadau mbalimbali kutoka sekta ya umma na binafsi na wananchi wote katika kuunga mkono juhudi za Serikali katika kufanikisha Sensa ya Watu na Makazi, Majengo na Anwani za Makazi.

### Mapambano Dhidi ya Rushwa

***142. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Serikali imeendelea kupambana na vitendo vya rushwa na ufisadi ambapo nguvu kubwa ilielekezwa kwenye uzuiaji wa vitendo hivyo. Hadi kufikia Februari, 2023, kesi za rushwa zipatazo 696 zikiwemo kesi mpya 203 ziliendeshwa mahakamani. Kati ya kesi

hizo, kesi 248 ziliamuliwa mahakamani na watuhumiwa 142 walikutwa na hatia.

***143. Mheshimiwa Spika,*** vilevile, ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo 810 yenye thamani ya shilingi trilioni 6.89 umefanyika. Kutokana na ufuatiliaji huo, miradi 119 yenye thamani ya shilingi billioni 46.04 ilionekana kuwa na kasoro mbalimbali katika utekelezaji na inaendelea kufanyiwa uchunguzi ili hatua stahiki zichukuliwe.

***144. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024 Serikali itaendeleza mapambano dhidi ya rushwa na ufisadi kwa kuweka kipaumbele katika kuzuia vitendo vya rushwa. Serikali pia itatoa elimu kwa umma kuhusu madhara ya vitendo vya rushwa kupitia programu ya TAKUKURU- RAFIKI.

**Mapambano Dhidi ya UKIMWI**

***145. Mheshimiwa Spika,*** sote tunafahamu UKIMWI umeendelea kuwa miongoni mwa majanga makubwa duniani kwa miongo kadhaa sasa. Serikali kwa kutambua ukweli huo, imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za mapambano dhidi ya ugonjwa huo. Jitihada hizo ni pamoja na kuandaa mikakati na kutekeleza afua mbalimbali za kupunguza maambukizi, unyanyapaa pamoja na vifo vitokanavyo na janga hilo.

***146. Mheshimiwa Spika,*** kama mtakumbuka katika maadhimisho ya Siku ya UKIMWI Duniani ya mwaka 2022 yaliyofanyika mkoani Lindi, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alizindua Mkakati wa Tano wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI wa Mwaka 2021/2022 – 2025/2026. Mkakati huo umelenga kuhakikisha kuwa malengo ya sifuri tatu yatafikiwa ifikapo mwaka 2030. Malengo hayo ni kudhibiti maambukizi mapya ya VVU, kukomesha unyanyapaa na kutokomeza vifo vitokanavyo na UKIMWI.

***147. Mheshimiwa Spika,*** kutokana na jitihada zilizofanyika ikiwemo matumizi ya dawa za ARV, afua za kinga zinazotekelezwa na wadau mbalimbali nchini na afua za mabadiliko ya tabia, tohara ya kitabibu kwa wanaume na kuzuia maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto, maambukizi mapya ya VVU kwa watu wazima (miaka 15 na zaidi) yameshuka kutoka 110,000 mwaka 2010 hadi 54,000 mwaka 2022. Wakati huo huo, vifo vinavyotokana na UKIMWI vimepungua kwa asilimia 55 kutoka vifo 65,000 mwaka 2010 hadi 29,000 mwaka 2022. Vilevile, maambukizi mapya kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto yameshuka kutoka asilimia 18 mwaka 2010 hadi asilimia 7 mwaka 2022.

***148. Mheshimiwa Spika***, matumizi ya dawa za kufubaza virusi vya UKIMWI kwa WAVIU wanaojua hali zao za maambukizi yameongezeka kutoka asilimia 95 mwaka 2016 hadi asilimia 98 mwaka 2022. Hadi kufikia Desemba, 2022 WAVIU zaidi ya milioni 1.5 walikuwa kwenye huduma za tiba na matunzo. Aidha, WAVIU wanaofahamu hali zao za maambukizi na wapo kwenye matibabu ni asilimia 99 na WAVIU waliopo kwenye matibabu na wamefubaza VVU ni asilimia 98. Mafanikio haya ni makubwa ikilinganishwa na malengo ya Kimataifa ya kufikia 95-95-95.

***149. Mheshimiwa Spika,*** pamoja na mafanikio makubwa yaliyopatikana, bado kuna mambo mengi yanayohitaji kufanyika ili kufikia azma yetu ya kumaliza kabisa janga la UKIMWI. Kwa kutambua hilo, Serikali itaendelea kutenga rasilimali za kutosha kwa ajili ya Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti UKIMWI, na kutoa elimu kwa umma kuhusu athari za UKIMWI pamoja na afua nyingine mahsusi za kudhibiti janga hilo. Kwa upande mwingine, Serikali itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali katika kutekeleza afua za mapambano dhidi ya UKIMWI. Nitumie fursa hii kushukuru sana asasi za kiraia na wadau wa maendeleo kwa michango yao katika mapambano ya kutokomeza UKIMWI nchini.

**Mapambano Dhidi ya Dawa za Kulevya**

***150. Mheshimiwa Spika***, Serikali kwa kutambua madhara ya dawa za kulevya kwa nguvu kazi hapa nchini, imeendelea kushirikiana na wadau mbalimbali katika mapambano dhidi ya dawa hizo. Katika mwaka 2022/2023, imeendesha oparesheni za kuwakamata wanaojihusisha na biashara hiyo pamoja na kuzuia mianya ya kusafirisha na kusambaza dawa hizo. Katika oparesheni hizo watuhumiwa 7,113 pamoja na kilogramu 20,450.30 za dawa za kulevya zilikamatwa. Dawa hizo ni *heroin* kilogramu 53.01, *cocaine* gramu 843.55, bangi kilogramu 12,869.39, mirungi kilogramu 7,525.53, na aina nyingine ya dawa za kulevya *(Methamphetamine na Mescaline)* gramu 1,024.7. Aidha, iliteketeza ekari 69 za mashamba ya bangi katika maeneo mbalimbali nchini na kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu madhara ya matumizi ya dawa za kulevya.

***151. Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeimarisha huduma za matibabu kwa watumiaji wa dawa za kulevya kwa kuongeza idadi ya kliniki zinazotoa huduma kwa waathirika wa dawa za kulevya kutoka 9 mwaka 2020/2021 hadi kliniki 15 zinazohudumia waathirika zaidi ya 14,500 mwaka 2022/2023. Licha ya hayo, Serikali kupitia Programu ya Kukuza Ujuzi imewezesha waraibu wa dawa za kulevya waliopata nafuu wapatao 245 kupata mafunzo ya ujuzi kupitia vyuo vya VETA, Don Bosco na SIDO.

***152. Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kusimamia na kuratibu uendeshwaji wa nyumba za upataji nafuu 44 nchini, kuzijengea uwezo asasi za kiraia 65 ambazo zinatoa elimu kuhusu madhara ya dawa za kulevya kwa jamii, kuandaa Mwongozo wa Utoaji Elimu kuhusu Tatizo la Dawa za Kulevya nchini ambao umezinduliwa tarehe 02 Julai, 2022 kwa lengo la kuwapatia elimu na mbinu sahihi kulingana na mahitaji ya makundi mbalimbali ya kijamii. Nitoe wito kwa wadau wote mkiwemo Waheshimiwa Wabunge wenzangu, asasi za kiraia, viongozi wa dini, vyombo vya habari na jamii nzima kushirikiana

na Serikali kutoa elimu kuhusu madhara ya dawa za kulevya ili kuokoa kizazi cha sasa na kijacho.

**Uratibu wa Maafa**

***153. Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kuhakikisha nchi inakuwa stahimilivu dhidi ya majanga kwa kuweka utaratibu mzuri wa kushughulikia masuala ya maafa hapa nchini. Ili kuweka utaratibu huo, Serikali imetunga Sheria ya Usimamizi wa Maafa Na. 6 ya Mwaka 2022; Mkakati wa Taifa wa Usimamizi wa Maafa wa Mwaka 2022-2027; Mpango wa Taifa wa Kujiandaa na Kukabiliana na Maafa wa Mwaka 2022; Mkakati wa Taifa wa Afya Moja wa Mwaka 2022-2027; na Mwongozo wa Taifa wa Kupambana na Vitendo vya Kihalifu katika Bahari na Maziwa Makuu wa Mwaka 2022. Kama mtakumbuka, Nyaraka hizo nilizizindua tarehe 09 Februari, 2023 kwa ajili ya utekelezaji.

***154. Mheshimiwa Spika***, nyaraka hizo zimeweka utaratibu wa kuhakikisha Wizara, Idara, Taasisi za Umma na zisizo za Umma, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa zinashiriki kikamilifu katika kutekeleza shughuli za kuzuia na kupunguza madhara ya majanga. Aidha, zimeweka pia utaratibu wa kujiandaa, kukabiliana na kurejesha hali iliyotoweka pindi maafa yanapotokea. Nitoe wito kwa taasisi husika kuandaa mipango kazi na taratibu za usimamizi wa maafa pamoja na ushughulikiaji wa dharura.

***155. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023, jumla ya wajumbe 555 wa Kamati za Usimamizi wa Maafa na Waratibu wa Maafa walipata mafunzo ya kuimarisha uwezo wa utendaji kazi katika mikoa ya Arusha, Morogoro, Kilimanjaro, Lindi, Mtwara na Singida. Aidha, jumla ya wavuvi 344 katika mwambao wa Ziwa Victoria na vijana 40 wa kujitolea katika mikoa ya Dodoma, Iringa, Songwe na Tabora walipata mafunzo ya uokoaji, yaliyowaongezea uwezo wa kukabiliana na maafa kwa wakati.

***156. Mheshimiwa Spika***, katika kuendeleza ushirikiano na nchi nyingine katika kushughulikia masuala ya maafa ikiwemo nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika, Tanzania imekuwa nchi ya kwanza kusaini mkataba wa kuanzisha Kituo cha Huduma za Binadamu na Operesheni za Dharura cha Kanda ya SADC. Lengo la kuanzisha kituo hicho ni kusimamia utoaji wa huduma na misaada ya kibinadamu kwa nchi wanachama. Hii ni kutokana na ukweli kwamba, masuala ya majanga hayana mipaka na hayana muda na yanahitaji jitihada za pamoja katika kuyashughulikia.

***157. Mheshimiwa Spika***, kama mtakumbuka, katika kuendeleza uhusiano na nchi nyingine, hivi karibuni nchi yetu imeungana na mataifa mengine duniani kutoa misaada ya kibinadamu kwa nchi zilizopatwa na maafa makubwa yaliyosababisha vifo na majeruhi, uharibifu wa mali na mazingira. Nchi hizo ni pamoja na Malawi iliyokumbwa na mafuriko yaliyosababishwa na kimbunga *Freddy* kilichotokea tarehe 13 Machi, 2023 na nchi ya Uturuki iliyokumbwa na tetemeko la ardhi mwezi Februari, mwaka huu. Misaada iliyotolewa kwa nchi ya Malawi ni pamoja na mahindi tani 1,000, mablanketi 6,000, mahema 50, fedha taslimu shilingi milioni 705, dawa za binadamu na helkopta 2 kwa ajili ya kusaidia uokoaji. Aidha, fedha taslimu dola za Marekani milioni moja zilitolewa kwa nchi ya Uturuki.

***158. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024, Serikali itaendelea na ujenzi wa Kituo cha Taifa cha Usimamizi wa Maafa Jijini Dodoma, kuimarisha maghala ya vifaa vya misaada ya kibinadamu kwa kuongeza vifaa na kuendelea kutoa misaada kwa waathirika wa maafa. Hata hivyo, kila wizara na taasisi watalazimika kujiandaa kwa vifaa vya kukabiliana na kulingana na mahitaji ya wizara au taasisi husika.

**Uratibu wa Masuala ya Lishe**

***159. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Serikali imeendelea kutekeleza afua mbalimbali za lishe ili kuimarisha

afya na hivyo kuwezesha wananchi kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo. Kutokana na umuhimu wa masuala ya lishe, tarehe 30 Septemba, 2022 Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alisaini mikataba na Wakuu wa Mikoa yote Tanzania Bara kwa lengo la kuhakikisha kipaumbele kinatolewa kwenye masuala ya lishe ikiwa ni pamoja na kuhakikisha halmashauri zinatenga shilingi 1,000 kwa kila mtoto chini ya miaka mitano. Vilevile, alielekeza fedha zinazopangwa kutekeleza afua za lishe kutolewa kwa wakati na kutumika kwa malengo yaliyokusudiwa, ikiwa ni pamoja na kuimarisha uhamasishaji wa utekelezaji wa afua za lishe bora na kuweka mikakati ya kuhakikisha vyakula vinavyohitajika kukamilisha lishe vinapatikana katika ngazi zote.

***160. Mheshimiwa Spika,*** maelekezo hayo ya Mheshimiwa Rais yaliongeza chachu ya utekelezaji wa masuala ya lishe sambamba na malengo yaliyoainishwa kwenye Mpango Jumuishi wa Kitaifa wa Masuala ya Lishe wa Mwaka 2021/2022 - 2025/2026. Aidha, katika Mkutano wa Nane wa Wadau wa Lishe Kitaifa, uliofanyika Disemba, 2022 Mkoani Mara, Mkakati wa Sekta Binafsi unaoainisha mikakati ya sekta hiyo kuiunga mkono Serikali kuimarisha hali ya lishe nchini ulizinduliwa.

***161. Mheshimiwa Spika,*** kutokana na jitihada mbalimbali za Serikali na wadau, yapo baadhi ya mafanikio yaliyopatikana ambayo ni pamoja na kupungua kwa udumavu kutoka asilimia 34.4 mwaka 2015/2016 hadi asilimia 30 mwaka 2022 na kupungua kwa kiwango cha ukondefu kutoka asilimia 4.5 hadi 3.3 katika kipindi hicho.

***162. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Serikali itaendelea kutoa kipaumbele katika utekelezaji wa Mpango Jumuishi wa Pili wa Kitaifa wa Masuala ya Lishe wa Mwaka 2021/2022 - 2025/2026. Nitoe wito kwa wananchi kuzingatia ulaji sahihi wa vyakula mchanganyiko kama tunavyoelekezwa na wataalamu wetu wa masuala ya lishe. Vilevile, niwaombe

wadau wa maendeleo na sekta binafsi waendelee kuunga mkono juhudi za Serikali katika kuimarisha hali ya lishe nchini.

**Mazingira**

***163.*** **Mheshimiwa Spika**, Serikali ya Awamu ya Sita katika kuweka msisitizo wa uhifadhi wa mazingira imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali pamoja na maboresho ya Sera na Sheria ili ziwiane na mahitaji ya sasa ya kitaifa, kikanda na kimataifa. Katika kutelekeza azma hiyo, Serikali imeandaa Mpango Kabambe wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (2022 - 2032) kwa lengo la kutoa mwongozo wa hatua za kuchukua ili kutatua changamoto za mazingira nchini kwa kuzingatia sehemu husika na hatua mahsusi zinazopaswa kuchukuliwa.

***164. Mheshimiwa Spika***, vilevile, Serikali imeandaa Kanuni za Biashara ya Kaboni za Mwaka 2022 na kutangazwa katika Gazeti la Serikali kupitia GN 636 kwa lugha ya Kingereza na GN 637 kwa lugha ya Kiswahili. Aidha, Serikali imeandaa Mwongozo kwa ajili ya kutoa maelekezo mbalimbali kuhusu ushiriki wa wadau katika biashara hiyo.

***165. Mheshimiwa Spika,*** kwa upande mwingine Serikali imeratibu ushiriki wa nchi katika mikutano ya kimataifa. Mikutano hiyo imekuwa na mafanikio na munafaa kwa Taifa letu ambapo kupitia Mkutano wa 27 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi, Tanzania imepata miradi ya nishati jadidifu ambayo itafadhiliwa na Benki ya Dunia, Taasisi ya Afrika 50 na Shirika la Nishati la Afrika kwa kushirikiana na kampuni ya *China Renewable Energies*.

***166. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Serikali itaendelea kusimamia utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira na kuchukua hatua za kupunguza uharibifu wa mazingira. Aidha, itaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu hifadhi na usimamizi wa mazingira, mabadiliko ya tabianchi na fursa ya biashara ya kaboni. Vilevile, itaratibu utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mazingira ya

Mwaka 2021 na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191 pamoja na kutoa elimu kwa umma kuhusu mabadiliko ya Sheria na Sera ya Mazingira.

**UCHUMI WA BULUU**

***167. Mheshimiwa Spika,*** Serikali inaendelea kuhamasisha wananchi juu ya kuibua fursa zilizo kwenye Uchumi wa Buluu kupitia matumizi endelevu ya rasilimali maji kwa kuzingatia uhifadhi wa mazingira na ushirikishwaji wa jamii. Hatua zinazochukuliwa ni pamoja na kuendelea kukamilisha Sera ya Taifa ya Uchumi wa Buluu pamoja na Mkakati wa Utekelezaji. Sera hiyo italenga kukuza uwekezaji katika rasilimali za Uchumi wa Buluu; kuongeza fursa za ajira na kazi za staha kupitia shughuli za uchumi wa buluu; na kuwa na usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za uchumi wa buluu unaozingatia misingi ya utawala bora.

**Utawala Bora**

***168. Mheshimiwa Spika;*** Serikali imeendelea kujenga uelewa wa pamoja kwa wadau wote hususan wananchi kuhusu masuala ya kisheria, upatikanaji wa haki zao, kuongeza uwazi na kupunguza gharama. Vilevile, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ikiwemo kukamilisha rasimu ya Awali ya ufasiri wa Sheria Kuu 219 na Sheria Ndogo 148 kwa lugha ya Kiswahili. Zoezi la ufasiri wa Sheria Kuu na Sheria Ndogo zote kutoka lugha ya Kingereza kwenda lugha ya Kiswahili ili kupanua wigo wa matumizi ya lugha ya Kiswahili kama lugha ya Sheria katika vyombo vya utoaji haki ikiwemo Mahakama, Mabaraza na vyombo vingine vyenye jukumu la kutoa haki linaendelea.

***169. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Serikali itaendelea kutekeleza Kampeni ya msaada wa kisheria ya Mama Samia, kuimarisha mifumo ya utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala na kuendelea kutafsiri sheria kutoka lugha ya Kiingereza kuwa lugha ya Kiswahili ili kuwawezesha wananchi

kuelewa mwenendo wa mashauri yanayowahusu na hivyo kuweza kupata haki zao.

**MFUMO WA SERIKALI WA TEHAMA**

***170. Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuimarisha matumizi ya Mfumo wake wa TEHAMA wa kubadilishana taarifa ambapo hadi sasa jumla ya mifumo 60 ya Taasisi 55 imeunganishwa na inabadilishana taarifa. Utekelezaji huo pia ni maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuwa na mifumo michache inayobadilishana taarifa. Uunganishaji wa mifumo hiyo umeongeza tija na ufanisi katika kuwahudumia wadau hususan wananchi.

***171. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Serikali itaendelea kurahisisha utendaji kazi kwa kutumia mfumo wa TEHAMA, kupunguza gharama za kutoa huduma ili kutoa unafuu kwa wananchi pamoja na kuimarisha mifumo inayobadilishana taarifa.

**UKATILI DHIDI YA WATOTO**

***172. Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kutekeleza afua mbalimbali za kupinga ukatili dhidi ya watoto shuleni na nje ya shule. Katika mwaka 2022/2023, hatua zilizochukuliwa ili kupinga ukatili huo ni pamoja na kuunda madawati 1,393 ya ulinzi na usalama wa mtoto katika shule za msingi na sekondari kwenye mikoa ya Rukwa, Arusha, Tanga, Dar es Saalam, Pwani, Shinyanga, Dodoma na Geita. Vilevile, Mabaraza ya Watoto 560 yameundwa kwa lengo la kutoa fursa kwa watoto kutoa maoni yao kwa uhuru na kuwajengea uwezo wa kujiamini, kujieleza na kujifunza masuala mbalimbali yanayohusu haki na ustawi wa watoto.

***173. Mheshimiwa Spika***, vilevile, Serikali imeendelea kuhamasisha jamii kushiriki katika ulinzi na usalama wa mtoto ili

kutokomeza ukatili dhidi ya watoto. Aidha, kupitia jitihada mbalimbali ikiwemo utekelezaji wa Programu Jumuishi ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto (2021/2022 - 2024/2025), wananchi wameendelea kuhamasishwa kujitolea kwa hiari kupambana na vitendo vya ukatili ikiwa ni pamoja na kutambua wajibu wao juu ya ulinzi wa mtoto kuanzia ngazi ya familia.

***174. Mheshimiwa Spika***, nitoe rai kwa mamlaka zinazohusika chini ya uratibu wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu kuimarisha mfumo wa ushughulikiaji wa matukio ya ukatili dhidi ya watoto ndani na nje ya shule unaowajumuisha wasimamizi wa shule, wazazi, walezi na jamii na kuandaa mfumo jumuishi wa kukusanya taarifa na takwimu za vitendo vya ukatili dhidi ya watoto.

**MUUNGANO**

***175. Mheshimiwa Spika,*** Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zimeendelea kushughulikia changamoto mbalimbali zinazojitokeza kwa lengo la kuulinda, kuuenzi na kuudumisha muungano wetu. Katika mwaka 2022/2023, jumla ya hoja nne kati ya nane zilipatiwa ufumbuzi na kuondolewa katika orodha ya hoja za Muungano. Vilevile, Serikali iliandaa kitabu kinachoitwa **"Muungano wa Tanganyika na Zanzibar: Chimbuko, Misingi na Maendeleo".** Kitabu hiki kimepatiwa ithibati ili kitumike kama kitabu cha ziada kwa shule za sekondari nchini na kuendelea kukuza uelewa kuhusu Muungano.

***176. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar zitaendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kuendelea kutatua changamoto zilizosalia kwa lengo la kuulinda, kuuenzi na kuudumisha muungano wetu.

**USHIRIKIANO WA KIKANDA NA KIMATAIFA**

***177. Mheshimiwa Spika,*** sote tumeshuhudia kuimarika kwa mahusiano yetu na nchi nyingine, jumuiya za kikanda na mashirika ya kimataifa chini ya Rais wetu mpendwa Mheshimiwa *Dkt.* Samia Suluhu Hassan. Kuimarika kwa ushirikiano huo kumetokana na Serikali kuendelea kutekeleza Sera ya Mambo ya Nje inayoweka msisitizo katika kutekeleza diplomasia ya kiuchumi.

***178. Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha mahusiano na mataifa mengine duniani, Viongozi wetu Wakuu wakiongozwa na Rais wetu wameshiriki katika ziara mbalimbali ambazo zimeiletea manufaa makubwa nchi yetu. Mathalan, Novemba 2022, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliitembelea China kufuatia mwaliko uliotolewa na Mheshimiwa Xi Jinping, Rais wa Jamhuri ya Watu wa China. Vilevile, viongozi wetu wakuu wameshiriki katika ziara mbalimbali za kikazi katika nchi za Marekani, Qatar, Ethiopia, Kenya, Misri, Oman, Afrika Kusini, Rwanda, na Burundi.

***179. Mheshimiwa Spika,*** kutokana na ziara hizo, nchi yetu imenufaika katika uboreshaji wa miundombinu, huduma za jamii, biashara, uwekezaji, uchumi wa kidijitali, maendeleo ya kijani, uchumi wa bluu, uvuvi, fedha, utalii, afya na kilimo.

***180. Mheshimiwa Spika***, katika kutekeleza diplomasia ya kiuchumi, Serikali imeratibu majadiliano ya awamu ya pili ya kuanzisha Eneo Huru la Biashara la Bara la Afrika (AfCFTA) kwa upande wa Afrika Mashariki. Ushiriki wa nchi yetu katika eneo huru la biashara utachochea ukuaji wa uchumi na biashara, kukuza ushiriki wetu katika biashara ya Dunia na kujenga uwezo wa kuongeza thamani ya bidhaa kupitia sera bora za kukuza teknolojia, ubunifu na ushindani.

***181. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024, Serikali itaendelea kufungua nchi kiuchumi kwa kuvutia uwekezaji na kutangaza vivutio mbalimbali vya utalii vilivyopo nchini; kuimarisha mahusiano ya kikanda na kimataifa na kutangaza

fursa za utalii na uwekezaji katika sekta mbalimbali za maeneo ya kipaumbele hususan uchumi wa bluu na kidijitali.

**SERIKALI KUHAMIA DODOMA**

***182. Mheshimiwa Spika,*** Serikali ya awamu ya sita imeendelea kutekeleza kwa vitendo zoezi la Serikali kuhamia Dodoma kwa lengo la kurahisisha utoaji wa huduma za Serikali kwa wananchi.

***183. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Serikali imeendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa majengo ya Ofisi za Wizara na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika Mji wa Serikali Mtumba. Ujenzi huo umefikia wastani wa asilimia 60. Aidha, kazi nyingine zinazoendelea ni pamoja na ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato kitakachogharimu shilingi bilioni 165 na ujenzi wa barabara ya mzunguko ya nje yenye urefu wa kilomita 112.3 kwa gharama ya shilingi bilioni 221. Kwa upande wa Balozi na Jumuiya za Kimataifa, balozi za nchi za Ujerumani, Ufaransa, China na Umoja wa Mataifa zimefungua ofisi ndogo jijini Dodoma.

***184. Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2023/2024, Serikali itaendelea kukamilisha awamu ya pili ya ujenzi wa majengo ya Ofisi za Wizara, Ofisi za Taasisi na miundombinu ya kudumu kwenye Mji wa Serikali pamoja na kuendelea kuratibu uhamiaji wa taasisi.

**SANAA, UTAMADUNI NA MICHEZO**

***185. Mheshimiwa Spika,*** Serikali kwa kutambua umuhimu wa kukuza utamaduni, sanaa na michezo imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuimarisha sekta hiyo kwa kuzingatia kuwa sekta hii ni chachu ya kuendeleza utamaduni wa Kitanzania, utambulisho wa Taifa, chanzo kikubwa cha ajira, huimarisha afya pamoja na kuchangia katika pato la Taifa.

***186. Mheshimiwa Spika,*** ili kukuza na kuendeleza lugha ya Kiswahili ndani na nje ya Tanzania Serikali imechukua hatua mbalimbali ikiwemo kusajili vituo 30 vya kufundisha Kiswahili. Kati ya hivyo: vituo 10 vipo katika Balozi za nchi yetu nchini Korea Kusini, Ufaransa, Italia, Mauritius, Nigeria, Sudan, Zimbabwe, Uholanzi, Cuba na Umoja wa Falme za Kiarabu; vituo vinne nje ya Balozi zetu katika nchi za Afrika Kusini, Italia, Ujerumani na Ethiopia na vituo 16 vya kufundisha lugha hiyo vimeanzishwa nchini. Aidha, kwa upande mwingine Tanzania imesaini makubaliano na nchi ya Afrika Kusini kuwezesha nchi hiyo kutumia Kiswahili kuwa lugha ya kujifunza na kufundishia katika elimu ya msingi.

***187. Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Serikali imeendelea kuimarisha Mfuko wa Utamaduni na Sanaa ili kuwawezesha wasanii kuendeleza kazi zao kwa kuwapa mikopo na elimu ya ujasiriamali. Hadi kufikia Februari, 2023 tayari imeshatoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 1.07 kwa wanufaika 45 ambao ni wasanii na wadau wa sanaa. Mikopo hiyo imewawezesha wasanii na wadau wa sanaa kuandaa kazi bora na zenye uwezo wa kuhimili ushindani katika soko la sanaa.

***188. Mheshimiwa Spika,*** kwa nafasi hii, nimpongeze sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa motisha kwa vilabu vya ndani vinavyoshiriki mashindano ya kimataifa kupitia ***Goli la Mama*** ambapo amekuwa akitoa shilingi milioni tano kwa kila goli linalofungwa. Sote tumeshuhudia *Simba Sports Club* almaarufu *Wekundu wa Msimbazi* wakijitwalia kitita cha shilingi milioni 50 wakati huo huo klabu ya *Young Africans Sports Club* almaarufu *Timu ya Wananchi* wakijitwalia shilingi milioni 45.

***189. Mheshimiwa Spika,*** ninavipongeza sana vilabu hivyo kwa kufika hatua ya robo fainali katika michuano ya Klabu Bingwa Afrika na Kombe la Shirikisho Barani Afrika. Ni matumaini yetu sote kuwa vilabu hivyo na vingine vinavyoshiriki mashindano ya

kimataifa vitaendelea kujituma na kupambana ili vikombe vya ushindi vije nyumbani.

***190. Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2023/2024 Serikali itaendelea kuratibu Programu ya Ukarabati wa Viwanja vya Michezo katika shule 56 katika mikoa yote Tanzania Bara; kuratibu Programu ya Sanaa na Michezo ya kuanzia ngazi ya Mtaa kwa Mtaa kuelekea ngazi za juu ikiwemo *"Taifa Cup"*; kutenga maeneo ya michezo kwa lengo la kujenga miundombinu ya mchezo na kuimarisha michezo katika ngazi za mikoa na wilaya; kuhakikisha kazi za sanaa na utamaduni zinazoandaliwa zinazingatia maadili ya jamii na Taifa kwa ujumla; na kuendelea kutambua maeneo ya urithi wa utamaduni na ukombozi katika mikoa na halmashauri za wilaya kwa lengo la kulinda, kuhifadhi na kuendeleza maeneo hayo ili kuinua utalii wa kiutamaduni na kiukombozi nchini.

**HITIMISHO**

***191. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024, Ofisi ya Waziri Mkuu itaendelea kuratibu utekelezaji wa sera na shughuli za Serikali ili kuendelea kutoa huduma bora kwa wananchi; kuratibu shughuli za maafa nchini; kuratibu shughuli za Serikali Bungeni; kushughulikia kero na malalamiko mbalimbali ya wananchi; kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utendaji wa Serikali; na kuratibu masuala yanayohusu kazi, maendeleo ya vijana, ajira, hifadhi ya jamii na huduma za watu wenye ulemavu.

***192. Mheshimiwa Spika,*** nimeeleza kwa muhtasari baadhi ya shughuli ambazo Serikali imetekeleza kwa kipindi kilichopita na mwelekeo wa kazi zitakazofanyika kwa mwaka 2023/2024. Kwa kuhitimisha, ninapenda kusisitiza mambo muhimu yafuatayo:

**Mosi:** Wizara, taasisi za Serikali, Tawala za Mikoa na Halmashauri ziimarishe ukusanyaji wa mapato na usimamizi wa nidhamu ya matumizi ya fedha za umma pamoja na kutekeleza

vipaumbele vilivyoainishwa katika Mpango na Bajeti ya Mwaka 2023/2024 hususan miradi ya kitaifa ya kimkakati;

**Pili:** Wadau wote pamoja na Serikali kwa ujumla waendelee kutumia matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 katika shughuli mbalimbali kama vile uwekezaji, biashara, tafiti na mipango mbalimbali ya maendeleo. Serikali itaendelea kusimamia utekelezaji wa Mpango Kazi wa Mwongozo wa Kitaifa wa Matumizi ya Matokeo ya Sensa ili kuongeza uelewa, uwazi na kupanua wigo wa matumizi ya matokeo ya sensa kwa Serikali, wananchi na wadau wote;

**Tatu:** Viongozi wote wa Serikali, dini, mila na vyama vya siasa wakemee kwa nguvu zote ushiriki wa sehemu yoyote ya jamii katika matendo yasiyoendana na mila, tamaduni na desturi za Watanzania. Hii ni pamoja na wazazi na walezi wote kushiriki kikamilifu katika makuzi na malezi bora ya watoto yatakayosaidia kuwaepusha na vitendo viovu;

**Nne:** Serikali na taasisi ziendelee kuhakikisha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini yanaendelea kuimarishwa ili kuvutia uwekezaji wa ndani na nje ya nchi;

**Tano:** Wizara na taasisi ziendelee kutenga fedha kwa ajili ya shughuli za ufuatiliaji na tathmini katika maeneo yao ikiwa ni pamoja na kuwajengea uwezo wataalamu wanaotekeleza jukumu hilo. Lengo ni kuwezesha utendaji wenye matokeo na kufanikisha utoaji wa huduma bora kwa wananchi; na

**Sita:** Viongozi wa siasa, dini na wadau wengine wahamasishe wananchi kushiriki kikamilifu katika maandalizi na uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa Mwaka 2024.

**MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA ZA OFISI YA WAZIRI MKUU NA OFISI YA BUNGE KWA MWAKA 2023/2024**

***193. Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2023/2024, Ofisi ya Waziri Mkuu na taasisi zilizo chini yake inaliomba Bunge lako tukufu liidhinishe jumla ya **shilingi 173,733,110,000**. Kati ya fedha hizo, **shilingi 121,364,753,320** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi 52,368,356,680** ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

***194. Mheshimiwa Spika,*** vilevile naliomba Bunge lako tukufu liidhinishe jumla ya **shilingi 165,627,897,000** kwa ajili ya Mfuko wa Bunge. Kati ya fedha hizo, **shilingi 160,458,877,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi 5,169,020,000** ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

***195. Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mliokaa niwakumbushe tu bajeti yenu ya Bunge imesomwa hapa. Nawatazama tu ili niwe nawaangalia ni wepi ambao hawaungi mkono Bajeti ya Bunge letu sisi wenyewe nawatazama. *(kicheko)*

Ni Bajeti ya Bunge kwa hivyo ni lazima muiunge mkono maana ni ya kwetu sasa mkiwa mmekaa ninyi mtalipwa kutoka wapi, hebu simameni ni Bajeti ya Bunge ni sehemu ya hii kwa hiyo, simameni kwa heshima kabisa. Mheshimiwa Easter Bulaya simama ndio utaratibu.

Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hotuba imeshasomwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu ambayo pamoja na mambo mengine imeungwa mkono na Bunge zima. Ni muhimu sana kuzingatia tofauti ya bajeti hii na bajeti zingine. Bajeti hii

Mfuko wa Bunge uko kwenye bajeti hii kwa hiyo mwingine akisimama anaona atakuwa ameunga mkono na Waziri Mkuu na yeye ndio anapita humo humo maana mfalme akiwa anakuja kwako njia husafishwa kwa hiyo ndio utaratibu huo. Kwa hiyo, tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kusoma hotuba hiyo lakini utaratibu wetu wa kawaida utaendelea.

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea na utaratibu wetu wa kawaida sasa nimeletewa matangazo ninayo matangazo ya wageni na matangazo mengine. Tutaanza na tangazo la wageni walioko Bungeni siku ya leo.

Kwanza ni wageni walio Jukwaa la Spika na katika wageni walioko Jukwaa la Spika tutaanza na wageni wangu ninao wageni watatu wa kutoka Kampuni ya Sigara Tanzania *(TCC)* ambao ni Ndugu Takashi Araki ambaye ni Mkurugenzi Mkuu, karibu sana; tunaye pia Ndugu Patricia Mhando ambaye ni Mkurugenzi wa Mahusiano, karibu sana; tunaye pia Ndugu Derrick Stanley ambaye ni Meneja Mahusiano, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni wengine ambao nao ni wageni wangu hawa ni walimu 17 kutoka Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Mtakatifu Francis ya Jijini Mbeya, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni saba ambao hawa ni kutoka Umoja wa Wastaafu Tanzania wakiongozwa na Kiongozi wao Ndugu Dauda Bilikesi, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wa Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambao ni viongozi kutoka kwenye Ofisi yake na hapa tutaanza na Dkt. Jim Yonazi ambaye ni Katibu Mkuu wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yupo pia Profesa Jamal Katundu ambaye ni Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, karibu sana. *(Makofi)*

Hawa wameambatana na menejimenti na watumishi wa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa hiyo na wao wanaweza kusimama kama walipata nafasi humu ndani leo, karibuni sana. Hiyo ndio menejimenti na watumishi wa Ofisi ya Waziri Mkuu, karibuni sana. *(Makofi)*

Pia wapo viongozi kutoka taasisi zilizo chini ya Wizara hii ambao ni Ndugu Sisty Nyahoza, Msajili Msaidizi wa Vyama vya Siasa, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Aretas Lyimo ambaye ni Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Dkt. Leonard Maboko ambaye ni Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yupo pia Ndugu Ramadhani Kailima ambaye ni Mkurugenzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Dkt. Godwill Wanga ambaye ni Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Biashara, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Tumaini Nyamhokya ambaye ni Rais wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi (*TUCTA),* karibuni sana. *(Makofi)*

Yupo pia Bi Jayne Taylor ambaye ni Mwenyekiti wa Chama cha Waajiri Tanzania *(ATE),* karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Dkt. Suleiman S. Mohamed ambaye ni Mwenyekiti Bodi ya Mshahara ya Kima cha Chini kwa Sekta Binafsi, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Edrissa Mavura ambaye ni Mwenyekiti Tume ya Usuluhishi na Uamuzi *(CMA),* karibu sana. *(Makofi)*

Pia wapo wageni 11 wa Mheshimiwa Waziri Mkuu ambao ni Wajumbe wa Kamati ya Uongozi ya Baraza la Vyama vya Siasa; kwanza ni Ndugu Juma Ali Khatib ambaye ni Mwenyekiti wa Baraza kutoka Chama cha *ADA-TADEA* karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Doyo Hassan Doyo ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili na Uhusiano na Katibu Mkuu wa *ADC,* karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Mohamed Omar Shaame ambaye ni Makamu Mwenyekiti na Mwenyekiti wa UMD Taifa, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yupo pia Ndugu Ameir Hassan Ameir ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria na Utawala Bora na pia ni Katibu Mkuu wa Demokrasia Makini, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Rashid Mohamed Rai ambaye ni Makamu Mwenyekiti na Katibu Mkuu wa *AAFP,* karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Abdul Juma Mluya ambaye ni Mwenyekiti wa Masuala ya Bunge na Siasa pia ni Katibu Mkuu wa *DP,* karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Mohamed S. Mohamed ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa hili Baraza pia ni Naibu Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi Zanzibar, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Dorothy Semu ambaye Makamu Mwenyekiti na Mwakilishi wa Viongozi Wanawake wa Vyama vya Siasa na huyu pia ni Makamu Mwenyekiti wa ACT-Wazalendo Bara, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wengine wa Wabunge mbalimbalia ambao wako hapa, tunao wageni 150 wa Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Chana ambaye ni Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo hawa ni washereheshaji wa wanaoitwa Kisima cha Mafanikio Tanzania, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nimejulishwa kwamba washereheshaji hawa wanatoka mikoa yote ya Tanzania kwa hiyo ukiwa na shughuli huko mkoani na majimboni unamuona tu Mheshimiwa Pindi Chana atakupa mawasiliano ya mshereheshaji ambaye anatoka kwenye mkoa wako, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa George Mwenisongole ambao ni familia yake wakiongozwa na mke wake, Ndugu Farida Mwenisongole karibuni sana huyo ni Farida na hao ni wazazi wake. Hebu simama kwanza Farida peke yako, ehe haya karibu sana Farida, mume wako yuko salama kabisa humu Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yupo pia mgeni wa Mheshimiwa Justin Nyamonga ambaye ni Mkurugenzi wa Sauti ya Jamii kutoka Mkoa wa Iringa na huyu ni Ndugu Jane Hussein, karibu sana. *(Makofi)*

Wapo pia wageni 13 wa Mheshimiwa Leah Komanya ambao ni wanafunzi na walimu watatu wa Kimali Sekondari kutoka Mkoa wa Simiyu, karibu sana. *(Makofi)*

Pia wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Ally Mlaghila Jumbe ambao ni rafiki zake kutoka Jijini Mbeya, karibu sana. *(Makofi)*

Wapo wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo na hapa tunao wanafunzi 60 na walimu watano kutoka Shule ya Awali na Msingi ya *Trinity Kingdom* ya Jijini Dar es Salaam, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nawakumbusha siku zote mjadala wa mambo muhimu yale ambayo huwa tunajadiliana huwa inabidi yasubiri niwe nimeketi, yale majadiliano ya mambo muhimu huwa inabidi yasubiri niwe nimeketi. Kwa hiyo, nikiwa nimesimama na majadialiano ya mambo muhimu yanasimama.

Waheshimiwa Wabunge, ninayo matangazo mengine tangazo la kwanza linatoka kwa Katibu wetu wa Bunge, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kuwa utaratibu wa kuomba nafasi ya kuchangia hoja za Wizara mbalimbali ni kupitia Mfumo wa Bunge Mtandao. Kwa hivyo mnakumbushwa kuomba kupitia huko kwa hiyo ukishaomba kule sasa ndio tutaweza kuvipanga vipaumbele vyenu vizuri, usipofanya hivyo itatuwia ngumu kidogo kupanga vipaumbele vyenu kwa sababu hapa mbele huwa inabidi Spika awe navyo pamoja na kwamba kanuni zetu zinaweka utaratibu wa vyama vyenu kuleta hapa mbele wachangiaji wa siku husika.

Sasa nisipokuwa navyo vipaumbele hapa mbele halafu ukaniandikia ujumbe kwamba mimi sijawahi kuchangia, chama changu hakijanipa nafasi nitakuwa sikuelewi kwa sababu utakuwa hukuomba. Kwa hiyo, Katibu wa Bunge anawakumbusha kwamba mjaze vipaumbele vyenu kwenye Bunge Mtandao.

Waheshimiwa Wabunge, ninalo tangazo lingine nalo linatoka kwa Katibu wa Bunge; Katibu wa Bunge anawakumbusha kwamba kwa mujibu wa stahili zenu wakati wa safari za kikazi za nje na ndani ya nchi mnastahili kupewa tiketi za daraja la biashara *(business class)* na kwa sababu hiyo mnastahili kupata huduma zinazotolewa katika chumba cha daraja la biashara *(business lounge)* bura bila ulazima wa kutumia *VIP Lounge* ambayo ina gharama za ziada.

Kwa kuzingatia masharti hayo Ofisi imekuwa ikitoa maelekezo mara kwa mara kuhusu matumizi ya *VIP Lounge* na gharama zinazohusiana na matumizi hayo na kuwashauri Wabunge kutumia *business lounge* ambapo wanaweza kupata huduma bila malipo ya ziada. *(Makofi)*

Hivyo kwa kuwa ofisi imeletewa orodha ya Waheshimiwa Wabunge waliotumia *VIP Lounge* kwa safari za nje kinyume na maelekezo hayo Wabunge hao watajulishwa kwa barua ili waweze kulipa gharama zinazohusika kwa muda muafaka. Tangazo hilo Katibu wetu wa Bunge atawaandikia barua kwa hivyo anawakumbusha hilo ili utakapopokea barua usihangaike ameshakwambia itakuwa ni barua inahusu nini. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, lipo tangazo lingine nalo linatoka kwa Katibu wa Bunge; mnatangaziwa Wabunge wote pamoja na watumishi wote wa Bunge kwamba kesho siku ya Alhamisi tarehe 6 Aprili, 2023 kutakuwa na *Iftar* itakayoandaliwa na Mheshimiwa Toufiq Salim Turky, Mbunge wa Mpendae Zanzibar kwa heshima ya Wabunge na watumishi wote, halfa hiyo itafanyika viwanja vya Bunge kuanzia saa kumi na mbili na nusu jioni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge wote pamoja na watumishi wote mnakaribishwa na mnaombwa kuhudhuria kwa wingi kabisa Mheshimiwa Turky amejiandaa kwa ajili ya sisi sote. Na kwa kusema hivyo niwakaribishe Wabunge wengine pia

ambao wanao uwezo wa kufanya hiyo ibada ya *Iftar* tunawapokea kwa mikono miwili. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo nilikuwa najaribu kutazama muda pale, lakini nadhani tumsikilize Mwenyekiti mmoja halafu tutaendelea na ratiba yetu jioni.

Sasa baada ya kuwa Waziri Mkuu ameshasoma hotuba hiyo pamoja na kuungwa mkono na Bunge zima lakini tutasikiliza kamati zetu ambazo zimepata nafasi ya kutazama hotuba hiyo kwa kirefu zitatueleza mawazo yao.

Kwa hiyo tunazo Kamati nne kwa sasa na kwa muda uliobaki tutaisikiliza Kamati moja; na Kamati yetu ambayo tutaisikiliza muda huu ni Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria. Kwa hiyo nimwite Mwenyekiti wetu wa Kamati hii ya Kudumu ya Bunge Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama aje atoe maoni ya Bunge, karibu sana. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba taarifa yetu ya Kamati iingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Kudumu za Bunge kama ilivyowasilishwa mezani.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu kwa Mwaka wa Fedha wa 2022/2023 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 118 (4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge imeweka masharti yanayotaka Taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya Ofisi hii kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa masharti hayo yamezingatiwa.

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi uliofanywa na Kamati. Kamati ilipitia jumla ya mafungu Matano (5) kama ifuatavyo: -

(a)Fungu Na. 25, Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu.

(b)Fungu Na. 37, Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu.

(c)Fungu Na. 27, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa.

(d)Fungu Na. 61, Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

(e)Fungu Na. 91, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Madawa ya Kulevya.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Makusanyo ya Maduhuli.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu ililenga kukusanya maduhuli ya shilingi 6,135,000,000, kati ya fedha hizo Fungu Na. 37 - Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu ililenga kukusanya shilingi 6,000,000,000, Fungu Na. 61 - Tume ya Taifa ya Uchaguzi ililenga kukusanya milioni 100,000,000 na Fungu Na. 27 - Ofisi ya Msajili wa Vyama Vya Siasa ililenga kukusanya milioni 35,000,000.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli unaonyesha yafuatayo: - Fungu Na. 27 Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa hawajafikia lengo la makusanyo kwa kuwa hadi kufikia Februari, 2023, Ofisi hiyo

imekusanya shilingi 2,000,000 tu sawa na asilimia 5.71 ya lengo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa ukusanyaji wa Maduhuli kwenye Fungu hili unategemea vyanzo viwili ambavyo ni Tozo za Uvunjaji wa Sheria ya Gharama za Uchaguzi, Sheria ya Vyama vya Siasa na Usajili wa Vyama vya Siasa vya muda mrefu na muda mfupi. Hadi kufikia Februari, 2023, vyama viwili tu vilijisajili kwa usajili wa muda mfupi na kulipa gharama hiyo ya shilingi 2,000,000.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa hakukuwa na ukiukwaji wa Sheria iliyofanywa na Vyama vya Siasa au wagombea na hivyo hakuna tozo iliyokunywa kwenye chanzo hiki cha maduhuli.

Mheshimiwa Spika, Fungu Na. 37 - Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu imekusanya chini ya lengo hadi kufikia Februari, 2023 makusanyo ni 913,179,502.62 sawa na asilimia 15.2 tu. Fungu hili lililenga kukusanya shilingi 6,000,000,000 kutoka kwenye Idara ya Mpiga chapa wa Nyaraka za Serikali. Kamati ilielezwa kuwa kutokufikiwa kwa lengo ni kutokana na uchakavu na mashine zinazotumika kwa sasa pamoja na kazi zinazotarajiwa kupelekwa na Idara za Serikali kutopelekwa kwa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali, jambo ambalo pia limechangia kuvuja kwa taarifa za Serikali na taarifa hizo kuchapwa katika ubora hafifu. Aidha, Mpango uliopo wa Serikali ni ununuzi wa mashine mpya mbili, matengenezo ya mashine 13 zilizopo na kununua vifaa vingine vitakavyo wezesha utekelezaji mzuri wa shughuli za Idara ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa uchambuzi huo, Jumla ya shilingi 983,179,502.62 sawa na asilimia 16 tu ya makusanyo yote ya Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu zilikusanywa na Ofisi hiyo. Uwiano huo haujafikia lengo la makusanyo ambalo ni asilimia 66.6 hadi kufikia Februari, 2023.

Mheshimiwa Spika, Kamati ina maoni kuwa, makusanyo hafifu ya baadhi ya taasisi chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu yanaweza kutafsiriwa kwamba malengo ya ukusanyaji yaliyowekwa hayakuwa halisi au vyanzo vya Maduhuli vilivyoainishwa havikuwa vya uhakika na si endelevu. Kwa msingi huo, ni vyema Wizara na Taasisi zake zote kuzingatia uhalisia wa makadirio ya makusanyo ya maduhuli.

Aidha, mchanganuo wa maduhuli kwa kila fungu unaonyeshwa katika Jedwali Na. 1.

Mheshimiwa Spika, eneo linalofuata ni Uchambuzi wa Matumizi ya Bajeti; Fungu Na. 61 Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilihidhinishiwa jumla ya shilingi 10,413,014,000 kati ya fedha hizo bilioni 9,473,014,000 ilitengwa kwa matumizi ya kawaida ambapo shilingi 5,502,983,000 ni mishahara na shilingi bilioni 4,970,031,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, shilingi 940,000,000 ilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Februari, 2023 Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilipokea jumla ya shilingi 18,713,490,158.5 sawa na ongezeko la asilimia 79.7 ya fedha iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo shilingi 5,367,950,937.5 zilipokelewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 12,405,585,221 zilipokelewa nje ya ukomo wa bajeti kwa ajili ya uratibu na usimamizi wa uchaguzi mdogo wa ubunge, udiwani na uboreshaji wa Daftari ya Kudumu la Wapiga Kura, na shilingi 939,999,000 sawa na asilimia 100 zilipokelewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa ongezeko la fedha nje ya ukomo wa bajeti ni kufuatia mahitaji yaliyojitokeza ya uratibu na usimamizi wa uchaguzi mdogo

wa ubunge, udiwani na uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilipokea kiasi cha shilingi 12, 405,585,221 nje ya ukomo wa bajeti kwa ajili kuratibu shughuli hizo. Kati ya fedha hizo 3,783,138,131 ilitumika kwa ajili ya kuratibu na kusimamia uchaguzi mdogo wa ubunge katika Jimbo la Amani Zanzibar na udiwani katika kata 12 za Tanzania Bara; na shilingi 3,397, 132,717.83 ilitumika kwa ajili ya maandalizi ya uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Mchanganuo wa fedha hizo kwa Taasisi za Ofisi ya Wazari Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu ni kama ilivyoonyeshwa kwenye Jedwali Na. 2 na Jedwali Na. 3.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla mwenendo wa upatikanaji wa fedha katika Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu ni wa kuridhisha, isipokuwa katika Mradi Na. 4429: Programu ya kuendeleza Kilimo na Uvuvi ambapo Wizara hadi kufikia Februari, 2023 imepokea kiasi cha shilingi 1,216,000,000 sawa na asilimia 29.59 mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwenye mradi huu siyo wakuridhisha.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa fedha za mradi huu zitatolewa na wafadhili. Aidha Wizara inaendelea na jitihada za kufatilia fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, sasa ni tathimini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kamati ilitembelea miradi miwili kati ya minne iliyosimamiwa na Wizara na kuchambua utekelezaji wa miradi hiyo kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Ujenzi ya Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasi, Dodoma. Mradi huu wa ujenzi wa jengo la Ofisi ya Msajili lenye jumla ya ghorofa sita (06) lenye thamani ya shilingi 20,431,828,642.50 ulianza tarehe 05/02/2022 na unatarajiwa kukamilika 25/05/2023. Hadi wakati wa ukaguzi ujenzi ulikuwa umefikia asilimia 61. Kamati ilielezwa kuwa uwezekano wa mradi kukamilika tarehe iliyopangwa ni mdogo kutokana na kuchelewa kwa kibali cha ujenzi na

uhaba wa malighafi za ujenzi. Aidha, Kamati ilielezwa kuwa jengo hilo pamoja na matumizi mengine ya kiofisi litatumika pia kukodisha kumbi kwa shughuli rasmi kwa taasisi mbalimbali za Serikali.

Mheshimiwa Spika, mradi Na. 2 ni Ujenzi wa Kiwanda cha Uchapaji Nyaraka za Serikali, Dodoma. Ujenzi wa kiwanda hiki ulianza tarehe 25 Machi, 2022 na unatarajiwa kukamilika ndani ya miezi 12 kwa gharama ya shilingi 2,292,745,444.82. Utekelezaji wake wa awamu ya kwanza umefikia asilimia 92 na malipo ya shilingi 1,146,679,501.80 sawa na asilimia 75.4 ya awamu ya kwanza tayari umeishalipwa. Aidha, ununuzi wa mitambo ya kisasa ya uchapishaji wa nyaraka itakayotakiwa kufungwa mara tu baada ya kiwanda kukamilika imetengewa shilingi 3,990,000,000. Kujengwa kwa kiwanda hiki kutawezesha nyaraka za Serikali za siri na za wazi kuchapishwa na Idara ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa ubora na kwa wakati. Jambo hili litachochea kuongezeka kwa usiri na ubora wa nyaraka za Serikali. Aidha, pindi kiwanda kitakapoanza kazi kitaongeza maduhuli ya Serikali kupitia Idara ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kutoka 6,000,000,000 kwa mwaka hadi kufikia 20,000,000,000 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati. Wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 Kamati ilitoa maoni, ushauri na mapendekezo mbalimbali ili kuboresha utekelezaji wa Bajeti wa Ofisi hiyo. Naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kwamba kwa sehemu kubwa Serikali imezingatia maoni na ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, yahusu Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024. Sehemu ya kwanza ni Maduhuli.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu inaomba kuidhinishiwa kukusanya jumla ya shilingi 20,186,000,000 ikilinganishwa na shilingi 6,135,000,000 katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 kama ilivyoainishwa katika Jedwali Na. 5. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 229 ukilinganisha na makadirio ya makusanyo ya maduhuli kwa mwaka unaoisha.

Mheshimiwa Spika, Kamati ina maoni kwamba ongezeko la makadirio ya makusanyo ya maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 inaakisi azma ya Serikali kuongeza wigo wa mapato yake. Aidha, Ongezeko hilo linachangiwa na makusanyo yanayotarajiwa kutokana na kazi ya uchapaji wa nyaraka za Serikali zinazotarajiwa kufanywa na Idara ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu matumizi ya kawaida, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu pamoja na taasisi zilizo chini yake inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 85,381,558,000 ikiwa ni fedha za matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo shilingi 15,587,697,000 ni mishahara na shilingi 17,563,000,000 ni ruzuku kwa Vyama vya Siasa na shilingi 52,230,861,000 ni matumizi mengineyo, kama ambavyo ilichanganuliwa katika Jedwali Na. 5.

Mheshimiwa Spika, kuhusu miradi ya maendeleo. Katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 9,188,506,000 kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kati ya fedha hizo shilingi bilioni 5,079,946,000 ni fedha za ndani, na shilingi 4,108,560,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya maendeleo katika mwaka wa fedha 2023/2024 imeongezeka kwa shilingi 1,319,946,000 sawa na asilimia 16.77 ukilinganisha na bajeti ya mwaka wa fedha unaoisha. Sababu ya ongezeko hilo limechangiwa na

ongezeko la bajeti la kukamilisha mradi wa ujenzi wa kiwanda cha uchapaji nyaraka za Serikali Dodoma kwa fedha za ndani, Kama ambavyo imeainishwa katika katika Jedwali Na. 6.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza jitihada za Serikali kuendelea kupanga bajeti ili kutekeleza miradi mingi zaidi kwa kutumia fedha za ndani. Hata hivyo, katika uchambuzi wake Kamati imebaini kwamba, bado kiwango cha fedha ambacho kinatengwa kwa kutumia fedha za nje ni kikubwa ukilinganisha na kile kilichotengwa kwa fedha za ndani.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya nne na ya mwisho inahusu maoni na ushauri wa Kamati. Maoni ya jumla; kwa kuzingatia majadiliano ya kina kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 Kamati inatoa maoni, ushauri na mapendekezo ya jumla kwa mafungu yote kama ifuatavyo: -

(i) Serikali ijiwekee malengo ya kukusanya maduhuli ambayo yanaakisi uwezo wa ukusanyaji, na hali halisi ya vyanzo vya mapato.

(ii) Serikali ihakikishe kwamba inatoa kwa wakati Fedha za Maendeleo na Matumizi mengineyo ili kuwezesha Wizara hii, taasisi na Idara zilizoko chini yake kutekeleza majukumu yake kwa wakati na kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, sehemu inayofuata ni ushauri mahsusi fungu kwa fungu. Fungu Na. 37 Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu

(i)Serikali ihakikishe kwamba, fedha zinapatikana kikamilifu kwenye Mradi Na. 4429: Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi.

(ii)Serikali ihakikishe kwamba Ujenzi wa Kiwanda cha Uchapishaji wa Nyaraka za Serikali unakamilika kwa wakati.

(iii)Serikali itoe Waraka maalum kuelekeza idara zake zote kutumia Ofisi ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kazi zote zinazohusu uchapishaji, hususani Nyaraka za Siri, Nyaraka za Kitaifa kama (Bendera, Sheria mbalimbali, Kanuni n.k)

Mheshimiwa Spika, hitimisho. Napenda kukushukuru wewe binafsi pamoja na Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa uongozi wenu na kutupatia nafasi ya kuwasilisha taarifa hii. Napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi wa hali ya juu na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao yaingizwe kwenye Taarifa Rasmi za Bunge kama zilivyowasilishwa mezani.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) Waziri Mkuu wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Uongozi wake wa Shughuli za Serikali Bungeni na kwa kuwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya ofisi yake kwa ufanisi mkubwa.

Aidha, naomba nichukue fursa hii kumshukuru Waziri wa na Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu ambao wanamsaidia Mheshimiwa Waziri Mkuu kutekeleza majukumu yake katika ofisi hiyo. Kwa umuhimu wao naomba niwatambue kama ifuatavyo: -

(i)Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu.

(ii)Mheshimiwa Ummy Hamisi Nderiananga (Mb), Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu.

Mheshimiwa Spika, naomba pia niwashukuru watendaji wote Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na taasisi zake kwa ushirikiano waliotupatia wakati wa Kamati wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo Dkt. Jim Yonazi, Mheshimiwa Jaji Francis S. Mtungi - Msajili wa Vyama vya Siasa, Mheshimiwa Jaji Jacobs Mwambegele - Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi na Ndg. Aretas James Lyimo - Kamishina Jenerali wa Mamlaka ya kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya.

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa Mwihambi, *ndc,* kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na Bunge kwa mujibu wa Katiba ya Nchi. Aidha, nawashukuru Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Michael Chikokoto, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Gerald Magili na Makatibu wa Kamati hii Ndg. Frank Nkya, Ndg. Praisegod Lukio na Ndg. Ganjatuni Kilemile wakisaidiwa na Bi. Theresia Jacob, kwa kuratibu shughuli za Kamati na kufanikisha kukamilisha kwa taarifa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kuhidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**5 APRILI, 2023**

# TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISIHIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

## SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

### *1.1. Maelezo ya Awali*

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa **Kanuni ya 118 (9)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 pamoja na maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika**, ili kukidhi matakwa yaliokusudiwa na Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Bunge, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu zifuatazo: -

a) Sehemu ya Kwanza inatoa maelezo ya jumla kuonesha msingi na muundo wa taarifa pamoja na namna Kamati ilivyofanya kazi;

b) Sehemu ya Pili inahusu uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti kwa kuangalia makusanyo ya maduhuli, mwenendo wa upatikanaji wa fedha za Bajeti, utekelezaji wa miradi ya maendeleo na uzingatiaji wa ushauri na maoni ya Kamati;

c) Sehemu ya tatu inahusu uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/2024;

d) Sehemu ya Nne inahusu majumuisho ya maoni na ushauri wa Kamati; na

e) Sehemu ya tano ni Hitimisho.

**1.2. *Msingi wa Uchambuzi***

**Mheshimiwa Spika**, Msingi wa Kamati kufanya uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu ni kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023. Kifungu cha 6(2)(c) kikisomwa kwa pamoja na Kifungu cha 7 (1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, zinatambua jukumu la Kamati hii kufanya uchambuzi huo. Aidha, Kanuni ya 118(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge imeweka masharti yanayotaka Taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya Ofisi hii kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni. Naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa masharti hayo yamezingatiwa.

***1.3. Mawanda ya Uchambuzi***

**Mheshimiwa Spika**, Katika uchambuzi huo, Kamati ilipitia jumla ya mafungu matano (5) ambayo ni: -

a) **Fungu 25** - Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu,
b) **Fungu 37** - Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu,
c) **Fungu 27** - Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa,
d) **Fungu 61** - Tume ya Taifa ya Uchaguzi,
e) **Fungu 91** – Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI NA TATHIMINI

**2.1 *Ufafanuzi wa Jumla***

**Mheshimiwa Spika,** matokeo ya uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi

yanaweka msingi wa ushauri wa Kamati kuhusu hoja hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu. Kwa sababu hiyo, ili kuwezesha ufuatiliaji mzuri wa wasilisho hili, naomba kubainisha mambo makuu manne yaliyochambuliwa kama ifuatavyo; -

(a) Makusanyo ya maduhuli;

(b) Mwenendo wa Upatikanaji wa fedha za Bajeti ya Matumizi ya kawaida na Bajeti ya Maendeleo;

(c) Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu; na

(d) Uzingatiaji wa Maazimio ya Bunge.

**2.2 *Uchambuzi wa Makusanyo ya Maduhuli***

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu ililenga kukusanya maduhuli ya jumla ya **Sh. 6,135,000,000**, kati ya fedha hizo **Fungu Na. 37** - Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu ililenga kukusanya **Sh. 6,000,000,000**, **Fungu Na. 61** - Tume ya Taifa ya Uchaguzi ililenga kukusanya **100,000,000** na **Fungu Na. 27** - Ofisi ya Msajili wa vyama vya Siasa ililenga kukusanya **35,000,000**.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli unaonesha yafuatayo: -

(a) **Fungu 61** - Tume ya Taifa ya Uchaguzi hadi kufika Mwezi Februari, 2023 imekusanya kiasi cha Sh. **68,000,000** sawa na **asilimia 68** ya lengo la Makusanyo.

(b) **Fungu 27** - Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa hawajafikia lengo la makusanyo kwa kuwa hadi kufika Februari 2023 Ofisi hiyo imekusanya **Sh. 2,000,000** sawa na **asilimia 5.71** ya lengo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kuwa ukusanyaji wa Maduhuli kwenye Fungu hili unategemea vyanzo viwili ambavyo ni **Tozo** za uvunjaji wa Sheria ya Gharama za Uchaguzi, Sheria ya Vyama vya Siasa na **Usajili** wa vyama vya Siasa vya muda mrefu na muda mfupi. Hadi kufikia Februari, 2023 vyama viwili tu vilijisajili kwa usajili wa muda mfupi na kulipa gharama ya **Sh. 2,000,000**.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kuwa hakukuwa na ukiukwaji wa Sheria uliofanywa na vyama vya siasa au wagombea, hivyo hakuna tozo iliyokusanywa kwenye chanzo hiki cha maduhuli.

(c) **Fungu 37** - Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu imekusanya chini ya lengo, hadi kufika Februari, 2023 makusanyo ni **Sh. 913,179,502.62** sawa na asilimia **15.2** tu.

**Mheshimiwa Spika**, Fungu hili lililenga kukusanya **Sh. 6,000,000,000** kutoka kwenye Idara ya Mpiga chapa wa Nyaraka za Serikali. Kamati ilielezwa kuwa kutokufikiwa kwa lengo ni kutokana na uchakavu wa mashine zinazotumika kwa sasa, pamoja na kazi zilizotarajiwa kupelekwa na Idara za Serikali kutokupeleka kwa Mpiga chapa wa Nyaraka za Serikali, jambo ambalo limechangia kuvuja kwa taarifa za Serikali na taarifa hizo kuchapwa katika ubora hafifu. Aidha, Mpango uliopo wa Serikali ni ununuzi wa mashine mpya mbili, matengenezo ya mashine 13 zilizopo na kununua vifaa vingine vitakavyo wezesha utekelezaji mzuri wa shughuli za Idara ya Mpiga chapa wa Nyaraka za Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa uchambuzi huo, Jumla ya **Sh. 983,179,502.62** sawa na **asilimia 16 tu** ya makusanyo yote ya Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu zilikusanywa na Ofisi hiyo. Uwiano huu haujafikia lengo la makusanyo ambalo ni **asilimia 66.6** hadi kufika Februari, 2023.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ina maoni kuwa, makusanyo hafifu ya baadhi ya taasisi chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu -Sera, Bunge na Uratibu, yanaweza kutafsiriwa kwamba malengo ya ukusanyaji yaliyowekwa hayakuwa halisi, au vyanzo vya maduhuli vilivyoanishwa havikuwa vya uhakika na si endelevu. Kwa msingi huo, ni vyema Wizara na taasisi zake zote kuzingatia uhalisia wa makadirio ya makusanyo ya maduhuli.
Aidha, mchanganuo wa maduhuli kwa kila fungu unaoneshwa katika **Jedwali Na. 1.**

**JEDWALI NA. 1 – Makusanyo ya Maduhuli 2022/2023**

| **FUNGU** | **MAKADIRIO YA MAKUSANYO YA MADUHULI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023** | **MAKUSANYO YA MADUHULI HADI KUFIKIA FEBRUARI, 2023** | **ASILIMIA YA MAKUSANYO** |
|---|---:|---:|---:|
| **Fungu 37** – Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu | 6,000,000,000 | 913,179,502.62 | 15.2 |
| **Fungu 61** – Tume ya Taifa ya Uchaguzi | 100,000,000 | 68,000,000 | 68 |
| **Fungu 27** – Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa | 35,000,000 | 2,000,000 | 5.71 |
| **JUMLA KUU** | **6,135,000,000** | **983,179,502.62** | **16** |

***Chanzo:*** *Randama za Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu na Usanifu wa Kamati*

## 2.3 Uchambuzi wa Matumizi ya Bajeti

### 2.3.1 Fungu Na. 37 - Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2022/2023, fungu hili iliidhinishiwa jumla ya **Sh. 26,213,149,000**, kati ya fedha hizo **Sh. 20,224,589,000** ilitengwa kwa Matumizi ya Kawaida, ambapo **Sh. 4,915,064,000** ni Mishahara na **Sh. 15,309,525,000** ni kwa ajili ya Matumizi mengineyo. Aidha, **Sh. 5,988,560,000** ilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo, kati ya fedha hizo **Sh. 1,880,000,000** ni fedha za ndani kwa ajili ya Ujenzi wa

Kiwanda cha Kupiga Chapa cha Serikali Dodoma na **Sh. 4,108,560,000** ni fedha za nje kwa ajili ya uratibu wa Programu ya kuendeleza Kilimo na Uvuvi.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Februari, 2023 Fungu hili lilipokea jumla ya **Sh. 16,018,022,267.69** Kati ya fedha hizo, **Sh. 13,385,342,765.89** sawa na **asilimia 66** zilipokelewa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Sh. 2,632,679,501.8** sawa na **asilimia 44** zilipokelewa kwa ajili ya miradi ya Maendeleo.

2.3.2 **Fungu Na. 25 - Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu iliidhinishiwa jumla ya **Sh. 15,475,412,000**, kati ya fedha hizo **Sh. 1,475,412,000** ilitengwa kwa ajili ya Mishahara na **Sh. 14,000,000,000** ilitengwa kwa ajili ya Matumizi mengineyo. Hadi kufikia Februari, 2023 Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu ilipokea jumla ya **Sh. 10,277,434,333.30** sawa na **asilimia 66** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, Kati ya fedha hizo, **Sh. 9,333,333,333.30** zilipokelewa kwa ajili ya Matumizi mengineyo na **Sh. 944,101,000** zilipokelewa kwa ajili ya Mishahara.

2.3.3 **Fungu Na. 27 - Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Ofisi ya Msajili wa vyama vya Siasa iliidhinishiwa jumla ya **Sh. 21,973,414,000**, kati ya fedha hizo **Sh. 21,033,414,000** ilitengwa kwa Matumizi ya Kawaida, ambapo **Sh. 953,044,000** ni Mishahara na **Sh. 2,517,370,000** ni kwa ajili ya Matumizi mengineyo na **Sh. 17,563,000,000** ilitengwa kwa ajili ya Ruzuku ya Vyama vya Siasa. Aidha, **Sh. 940,000,000** ilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Februari, 2023 Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ilipokea jumla ya **Sh. 17,729,878,478.11** kati ya fedha hizo, **Sh. 16,789,878,478.11** sawa na **asilimia 79** zilipokelewa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Sh.**

**940,000,000** sawa na **asilimia 100** zilipokelewa kwa ajili ya miradi ya Maendeleo.

2.3.4 **Fungu Na. 91 - Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Mamlaka ya kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya iliidhinishiwa jumla ya **Sh. 11,974,701,000**, kati ya fedha hizo **Sh. 2,127,286,000** ilitengwa kwa ajili ya Mishahara na **Sh. 9,847,415,000** ilitengwa kwa ajili ya Matumizi mengineyo. Hadi kufikia Februari, 2023 Ofisi hiyo ilipokea jumla ya **Sh. 9,111,230,169.25** sawa na **asilimia 76**, Kati ya fedha hizo, **Sh. 7,459,206,184.25** zilipokelewa kwa ajili ya Matumizi mengineyo na **Sh. 1,652,023,985** zilipokelewa kwa ajili ya Mishahara.

2.3.5 **Fungu Na. 61 - Tume ya Taifa ya Uchaguzi**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Tume ya Taifa ya Uchaguzi iliidhinishiwa jumla ya **Sh. 10,413,014,000**, kati ya fedha hizo **Sh. 9,473,014,000** ilitengwa kwa Matumizi ya Kawaida, ambapo **Sh. 4,502,983,000** ni Mishahara na **Sh. 4,970,031,000** ni kwa ajili ya Matumizi mengineyo. Aidha, **Sh. 940,000,000** ilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Februari, 2023 Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilipokea jumla ya **Sh. 18,713,490,158.5** sawa na ongezeko la **asilimia 79.7** ya fedha iliyoidhinishwa, Kati ya fedha hizo, **Sh. 5,367,905,937.5** zilipokelewa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, **Sh. 12,405,585,221** zilipokelewa njee ya ukomo wa bajeti kwa ajili ya uratibu na usimamizi wa uchaguzi mdogo wa Ubunge, Udiwani na uboreshaji wa daftari la kudumu la wapiga kura na **Sh. 939,999,000** sawa na **asilimia 100** zilipokelewa kwa ajili ya miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kuwa ongezeko la fedha nje ya ukomo wa bajeti ni kufuatia mahitaji yaliojitokeza ya uratibu na usimamizi wa uchaguzi mdogo wa Ubunge, Udiwani na uboreshaji wa daftari la kudumu la wapiga kura,

Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilipokea kiasi cha **Sh. 12,405,585,221** nje ya ukomo wa bajeti kwa ajili ya kuratibu shughuli hizo. Kati ya fedha hizo, **Sh. 3,781,138,131** ilitumika kwa ajili ya kuratibu na kusimamia uchaguzi mdogo wa Ubunge katika Jimbo la Amani Zanzibar na Udiwani katika kata 12 Tanzania Bara na **Sh. 3,397,132,717.85** imetumika kwa ajili ya maandalizi ya uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

Mchanganuo wa fedha hizo kwa taasisi za Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu ni kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 2 na Jedwali Na. 3.

**JEDWALI NA. 2 – Mchanganuo wa Matumizi ya Kawaida 2022/2023**

| FUNGU | FEDHA YA MATUMIZI YA KAWAIDA ILIYOTENGWA KWA MWAKA 2022/2023 | FEDHA YA MATUMIZI YA KAWAIDA ILIYOPOKELEWA HADI KUFIKIA FEBRUARI, 2023 | ASILIMIA YA MAPOKEZI |
|---|---|---|---|
| **Fungu 37** – Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu | 20,224,589,000 | 13,385,342,765.89 | 66 |
| **Fungu 25** – Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu | 15,475,412,000 | 10,277,434,333.30 | 66 |
| **Fungu 27** – Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa | 21,033,414,000 | 16,789,878,478.11 | 79 |
| **Fungu 91** – Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya | 11,974,701,000 | 9,111,230,169.25 | 76 |
| **Fungu 61** – Tume ya Taifa ya Uchaguzi | 10,413,014,544 | 18,713,490,158.50 | 79.7 |
| **JUMLA KUU** | **79,121,130,544** | **67,337,376,905.05** | **85** |

***Chanzo**: Randama za Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu na Usanifu wa Kamati*

**JEDWALI NA. 3 – Mchanganuo wa Bajeti ya Maendeleo 2022/2023**

| FUNGU | FEDHA YA MAENDELEO ILIYOTENGWA KWA MWAKA 2022/2023 | FEDHA YA MAENDELEO ILIYOPOKELEWA HADI KUFIKIA FEBRUARI, 2023 | ASILIMIA YA MAPOKEZI |
|---|---|---|---|
| **Fungu 37** – Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu | 5,988,560,000 | 2,632,679,501.8 | 44 |
| **Fungu 27** – Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa | 940,000,000 | 940,000,000 | 100 |
| **Fungu 61** – Tume ya Taifa ya Uchaguzi | 940,000,000 | 939,999,000 | 100 |
| **JUMLA KUU** | **7,868,560,000** | **4,512,678,501.8** | **57** |

***Chanzo**: Randama za Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, Kwa ujumla, mwenendo wa upatikanaji wa fedha katika Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu ni wa kuridhisha, isipokuwa katika **Mradi Na. 4429: Programu ya kuendeleza Kilimo na Uvuvi** Wizara hadi kufikia Februari, 2023 imepokea kiasi cha **Sh. 1,216,000,000** sawa na **asilimia 29.59** mwendendo wa upatikanaji wa fedha kwenye mradi huu sio wa kuridhisha.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kuwa fedha za mradi huu zinatolewa na wafadhili, aidha Wizara inaendelea na jitihada za ufuatiliaji wa fedha hizo.

## 2.4 Tathmini ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, wakati Waziri Mkuu alipowasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi yake kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 aliidhinishiwa jumla ya **Sh 7,868,560,000** kwa Miradi ya Maendeleo katika Sekta zinazosimamiwa na Kamati. Mchanganuo wa fedha hizo unaonekana katika Jedwali Na. 4

**JEDWALI NA. 4 – Miradi ya Maendeleo Iliyotengewa Fedha 2022/2023**

| FUNGU | NAMBA NA JINA LA MRADI | FEDHA YA MAENDELEO ILIYOTENGWA KWA MWAKA 2022/2023 |
|---|---|---|
| **Fungu 37** – Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu | **NA. 4429** Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi | 4,108,560,000 |
| **Fungu 37** – Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu | **NA. 4937** Ujenzi wa Kiwanda cha Uchapaji Nyaraka za Serikali | 1,880,000,000 |
| **Fungu 27** – Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa | **NA. 6389** Ujenzi wa jengo la Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa Dodoma | 940,000,000 |
| **Fungu 61** – Tume ya Taifa ya Uchaguzi | Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura | 940,000,000 |
| **JUMLA KUU** | | **7,868,560,000** |

***Chanzo****: Randama za Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitembelea miradi miwili kati ya minne inayosimamiwa na Wizara na kuchambua utekelezaji wa miradi hiyo kama ifuatavyo:-

2.4.1 **Mradi Na. 6389: Ujenzi wa Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, Dodoma.**

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu wa ujenzi wa jengo la Ofisi ya Msajili lenye jumla ya ghorofa sita (06) wenye thamani ya **shilingi 20,431,828,643.50** ulianza tarehe 05/02/2022 na unaotarajiwa kukamilika tarehe 25/05/2023. Hadi wakati wa ukaguzi ujenzi ulikuwa umefikia asilimia 61. Kamati ilielezwa

kuwa uwezekano wa mradi kukamilika tarehe iliyopangwa ni mdogo kutokana na kuchelewa kwa kibali cha ujenzi na uhaba wa malighafi za ujenzi uliosababishwa na utekelezaji wa miradi mingi ya ujenzi ya Serikali. Aidha, Kamati ilielezwa kuwa jengo hilo pamoja na matumizi mengine ya kiofisi litatumika pia kukodisha kumbi kwa shughuli rasmi kwa taasisi mbalimbali.

2.4.2 **Mradi Na. 4937: Ujenzi wa Kiwanda cha Uchapaji Nyaraka za Serikali, Dodoma**.

**Mheshimiwa Spika,** Ujenzi wa kiwanda hiki ulianza tarehe 25 Machi, 2022 na unatarajiwa kukamilika ndani ya miezi kumi na mbili (12) kwa gharama ya **shilingi 2,292,745,444.82**. Utekelezaji wake wa awamu ya kwanza umefikia **asilimia 92** na malipo ya **Sh. 1,146,679,501.80** sawa na **asilimia 75.4** ya awamu ya kwanza tayari yameshalipwa. Aidha, ununuzi wa mitambo ya kisasa ya uchapishaji wa nyaraka inayotakiwa kufungwa mara tu baada ya kiwanda kukamilika umetengewa **Sh. 3,990,000,000**. Kujengwa kwa kiwanda hiki kutawezesha nyaraka za Serikali za siri na za wazi kuchapishwa na Idara ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa ubora na kwa wakati. Jambo hili litachochea kuongezeka kwa usiri na ubora wa nyaraka za Serikali. Aidha, pindi kiwanda kitakapoanza kazi, kitaongeza maduhuli ya Serikali kupitia Idara ya Mpiga chapa Mkuu wa Serikali kutoka **Sh. 6,000,000,000** kwa mwaka hadi kufikia **Sh. 20,000,000,000** kwa mwaka.

## 2.5 Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Kamati ilitoa maoni, ushauri na mapendekezo mbalimbali ili kuboresha utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi hiyo. Naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kwamba

kwa sehemu kubwa Serikali imezingatia maoni na ushauri wa Kamati.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

### *3.1 Maduhuli*

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu inaomba kuidhinishiwa kukusanya jumla ya **Sh. 20,186,000,000** ikilinganishwa na **Sh. 6,135,000,000** katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 kama ambavyo imeainishwa katika Jedwali Na. 5. Hii ni na sawa na ongezeko la **asilimia 229** ukilinganisha na makadirio ya makusanyo ya maduhuli kwa mwaka unaoisha.

**JEDWALI Na.5 – Maduhuli kwa Mwaka 2023/2024**

| FUNGU | MAKADIRIO YA MAKUSANYO YA MADUHULI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 | MAKADIRIO YA MAKUSANYO YA MADUHULI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 |
|---|---|---|
| **Fungu 37** – Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu | 6,000,000,000 | 20,000,000,000 |
| **Fungu 27** – Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa | 35,000,000 | 36,000,000 |
| **Fungu 61** – Tume ya Taifa ya Uchaguzi | 100,000,000 | 150,000,000 |
| **JUMLA KUU** | **6,135,000,000** | **20,186,000,000** |

***Chanzo:*** *Randama za Ofisi ya Waziri Mkuu na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ina maoni kwamba, ongezeko la makadirio ya makusanyo ya maduhuli kwa Mwaka wa Fedha

2023/2024 inaakisi azma ya Serikali kuongeza wigo wa mapato yake. Aidha, Ongezeko hilo linachangiwa na makusanyo yanayotarajiwa kutokana na kazi za uchapaji wa nyaraka za Serikali zinazotarajiwa kufanya na Idara ya Kupiga Chapa ya Serikali.

### 3.2 Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge, Uratibu pamoja na taasisi zilizo chini yake inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Sh. 85,381,558,000** Ikiwa ni Fedha za Matumizi ya Kawaida, kati ya fedha hizo **Sh. 15,587,697,000** ni mishahara, **Sh. 17,563,000,000** ni ruzuku kwa vyama vya Siasa na **Sh. 52,230,861,000** ni matumizi mengineyo, kama ambavyo imechanganuliwa katika Jedwali Na. 5

**JEDWALI NA. 5 – Mchanganuo wa Matumizi ya Kawaida 2023/2024**

| FUNGU | MISHAHARA | MATUMIZI MENGINEYO | RUZUKU | JUMLA YA MATUMIZI YA KAWAIDA |
|---|---|---|---|---|
| **Fungu 37** – Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu | 5,543,197,000 | 18,392,026,000 | 0 | 23,935,223,000 |
| **Fungu 25** – Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu | 1,475,412,000 | 14,000,000,000 | 0 | 15,475,412,000 |
| **Fungu 27** – Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa | 1,136,662,000 | 5,021,389,000 | 17,563,000,000 | 23,721,051,000 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Fungu 91** – Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya | 2,661,060,000 | 9,847,415,000 | 0 | 12,508,475,000 |
| **Fungu 61** – Tume ya Taifa ya Uchaguzi | 4,771,366,000 | 4,970,031,000 | 0 | 9,741,397,000 |
| **JUMLA KUU** | **15,587,697,000** | **52,230,861,000** | **17,563,000,000** | **85,381,558,000** |

***Chanzo**: Randama za Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, Bajeti ya Matumizi ya Kawaida katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 imeongezeka kwa **asilimia 9.2** ukilinganisha na Mwaka wa Fedha unaoisha ambapo bajeti ya Matumizi ya kawaida ndani ya ukomo bajeti ilikuwa **Sh. 78,181,130,000**. Kamati imebaini kwamba, moja kati ya sababu ya ongezeko hili ni maoni ya Kamati kwamba Serikali ipange bajeti kulingana na mahitaji halisi. Aidha, ongezeko hilo linaakisi mahitaji ya kifedha kulingana na sababu mbalimbali za kiuchumi ikiwemo kupanda kwa bei ya bidhaa na huduma.

Hata hivyo, Kamati inashauri Serikali kuhakikisha kwamba fedha zinazoombwa zinatumika vizuri. Na ili kuhakikisha hili linatekelezwa ipasavyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba inawasilisha mbele ya kamati taarifa mbalimbali za utekelezaji wa bajeti kwa mujibu wa Sheria.

### 3.3 Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Sh. 9,188,506,000** kwa ajili ya

Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Sh. 5,079,946,000** ni fedha za ndani, na **Sh. 4,108,560,000** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika**, bajeti ya maendeleo katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 imeongezeka kwa **Sh. 1,319,946,000** sawa na **asilimia 16.77** ukilinganisha na bajeti ya Mwaka wa Fedha unaoisha, sababu ya ongezeko hilo imechangiwa na ongezeko la bajeti ya kukamilisha mradi wa ujenzi wa kiwanda cha uchapaji nyaraka za Serikali Dodoma kwa fedha za ndani, Kama ambavyo imechanganuliwa katika **Jedwali Na. 6.**

**JEDWALI NA. 6 – Mchanganuo wa Bajeti ya Maendeleo 2023/2024**

| **FUNGU** | **NAMBA NA JINA LA MRADI** | **BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024** | |
|---|---|---|---|
| | | **FEDHA ZA NDANI** | **FEDHA ZA NJE** |
| **Fungu 37** – Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu | **NA. 4937** Ujenzi wa Kiwanda cha uchapaji nyaraka za Serikali Dodoma | 3,200,000,000 | 0 |
| **Fungu 37** – Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu | **NA. 4429** Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi | 0 | 4,108,560,000 |
| **Fungu 27** – Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa | **NA. 6389** Ujenzi wa jingo la Ofisi ya Msajili wa vyama vya Siasa Zanzibar | 940,000,000 | 0 |
| **Fungu 61** – Tume ya Taifa ya Uchaguzi | Uboreshaji wa daftari la kudumu la wapiga kura | 940,000,0000 | 0 |
| **Jumla Ndogo** | | **5,079,946,000** | **4,108,560,000** |
| **JUMLA KUU** | | **9,188,506,000** | |

***Chanzo**: Randama za Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza jitihada za Serikali kuendelea kupanga bajeti ili kutekeleza miradi mingi zaidi kwa kutumia fedha za ndani. Hata hivyo, katika uchambuzi wake, Kamati imebaini kwamba, bado kiwango cha fedha ambacho kinatengwa kwa kutumia fedha za nje ni kikubwa ukilinganisha na kile kilichotengwa kwa fedha za ndani.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### *4.1 Maoni ya Jumla*

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia majadiliano ya kina kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 Kamati inatoa maoni, ushauri na mapendekezo ya jumla kwa mafungu yote kama ifuatavyo: -

i) Serikali ijiwekee malengo ya ukusanyaji maduhuli ambao yanaakisi uwezo wa ukusanyaji, na hali halisi ya vyanzo vya mapato.

ii) Serikali ihakikishe kwamba inatoa kwa wakati Fedha za Maendeleo na Matumizi Mengineyo ili kuwezesha Wizara hii, taasisi na idara zilizoko chini yake kutekeleza majukumu yake kwa wakati na kwa ufanisi.

### *4.2 Ushauri Mahususi Fungu kwa Fungu*

#### 4.2.1 Fungu 37 – Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu

i) Serikali ihakikishe kwamba, fedha zinapatikana kikamilifu kwenye Mradi Na. 4429 Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi.

ii) Serikali ihakikishe kwamba Ujenzi wa Kiwanda cha Uchapishaji wa Nyaraka za Serikali unakamilika kwa wakati.

iii) Serikali itoe Waraka maalum kuelekeza idara zake zote kutumia Ofisi ya Mpiga chapa Mkuu wa Serikali kwa kazi zote zinazohusu uchapishaji, hususan nyaraka za Siri, Nyaraka za Kitaifa kama (Bendera, Sheria mbalimbali, Kanuni n.k)

**4.3 Fungu 27 - Ofisi ya Msajili wa vyama vya Siasa**

Ofisi ya Msajili wa vyama vya Siasa iweke mpango endelevu na mahsusi wa matumizi ya jengo la Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa.

## 5.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa Uongozi wenu na kutupatia nafasi ya kuwasilisha taarifa hii. Napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi wa hali ya juu na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao yaingizwe kwenye taarifa rasmi za Bunge kama yalivyowasilishwa.

1. Mhe. Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mb. – **Mwenyekiti**
2. Mhe. Florent Laurent Kyombo, Mb. – **M/Mwenyekiti**
3. Mhe. Abdullah Ali Mwinyi, Mb.
4. Mhe. Rashid Abdallah Shangazi, Mb.
5. Mhe. Wanu Hafidh Ameir, Mb.
6. Mhe. Edward Olelekaita Kisau, Mb.
7. Mhe. Boniphace Nyangindu Butondo, Mb.
8. Mhe. Dkt. Alice Karungi Kaijage, Mb.
9. Mhe. Khadija Shaaban Taya, Mb.
10. Mhe. Jonas Van Zeeland, Mb.
11. Mhe. Selemani Jumanne Zedi, Mb.
12. Mhe. Tumaini Bryceson Magessa, Mb.
13. Mhe. Salum Mohammed Shaafi, Mb.
14. Mhe. Yahya Omary Massare, Mb.

15. Mhe. Agnesta Lambert Kaiza, Mb.
16. Mhe. Abeid Ighondo Ramadhani, Mb.
17. Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Mb.
18. Mhe. Hussein Nassor Amar, Mb.
19. Mhe. Ahmed Juma Ngwali, Mb.
20. Mhe. Omar Issa Kombo, Mb.

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake wa Shughuli za Serikali bungeni na kuwa kuwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi yake kwa ufanisi Mkubwa. Aidha, naomba nichukue fursa hii kumshukuru Waziri na Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu ambao wanamsaidia Mheshimiwa Waziri Mkuu kutekeleza majumu yake katika ofisi hiyo. Kwa umuhimu wao, naomba niwatambue kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Jenista Joakim Mhagama, Mb. – Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu

2. Mhe. Ummy Hamisi Nderiananga, Mb. – Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu

**Mheshimiwa Spika**, naomba pia niwashukuru watendaji wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na taasisi zake kwa ushirikiano walioupatia Kamati wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo Dkt. Jim Yonazi, Mhe. Jaji Francis S. Mutungi - Msajili wa vyama vya Siasa, Mhe. Jaji Jacobs Mwambegele – Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi na Ndg. Aretas James Lyimo – Kamishina Jenerali wa Mamlaka ya kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini sio kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa Mwihambi, ndc kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na Bunge kwa mujibu

wa Katiba ya Nchi. Aidha, nawashukuru Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya kamati za Bunge Ndg. Michael Chikokoto, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Gerald Magili na Makatibu wa Kamati hii Ndg. Frank Nkya, Ndg. Praisegod Lukio na Ndg. Ganjatuni Kilemile wakisaidiwa na Bi. Theresia Jacob, kwa kuratibu shughuli za Kamati na kufanikisha kukamilika kwa taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako tukufu likubali kujadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mb
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE**
**YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA**
05 Aprili, 2023

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa wasilisho hilo. Waheshimiwa Wabunge tumemsikiliza Mwenyekiti mmoja wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ambapo kwa ujumla wake ofisi hii iko chini ya Kamati hii, tunamshukuru sana, pamoja na Wabunge wote ambao ni wajumbe wa Kamati hii Wenyeviti wengine tutawasikiliza mchana maoni yao yanasemaje kuhusu mafungu kadhaa ambayo yako chini ya maeneo yao.

Waheshimiwa Wabunge, jambo moja dogo, swali la Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga, Mbunge wa Kilombero wakati akitoa maelezo, pale ameniandikia hapa kwa kirefu sana kuashiria kwamba swali lake lilikuwa na mambo mengi mapana lakini sasa kunakufupisha maswali,

na nadhani hakupata nafasi sasa yakuonana na Serikali kujua kwamba muktadha wa swali lake linamaanisha nini; kwahivyo yeye anapata hisia kwamba swali lake halikuwa limeeleweka vizuri. Si kwamba halijajibiwa vizuri vile lilivyoletwa Serikalini ndivyo lilivyojibiwa sawasawa, ila anapata hisia kwamba swali lake halikuwa limeulizwa vile alivyokuwa anataka hasa ule muktadha.

Sasa muktadha wake kwa upande wa serikali yeye anataka muelewe kwamba alimanisha hawa wake za viongozi wakubwa. Sasa bahati mbaya wakati anauliza swali akataja humo na wasiohusika; lakini nia yake nikwamba wake wa viongozi hawa wanapokuwa madarakani wale wenza wao ama wenzi wao wanapata nafasi ya kutoa huduma mbalimbali kwenye jamii. Sasa wengine wanaanzisha sawa taasisi, wengine awaanzishi taasisi lakini wanakuwa na huduma fulani ambayo ni jambo ambalo yeye pengine anapenda kulihudumia kundi fulani.

Waheshimiwa Wabunge, sasa inapotokea kwamba ile huduma inakoma baada ya uongozi wa yule mwenza ama mwenzi wake basi inakuwa kidogo changamoto, hasa pale ambapo huduma zile zinakuwa bado zinahitajika na jamii na wakati mwingine wale waliyohudumiwa wanaziulizia hizo huduma. Kwamba Mheshimiwa Mbunge uliwahi kumleta fulani hapa akatusaidia mbona sasa hatumuoni. Kwa hiyo wananchi wao wanapo hudumiwa hawawezi sasa kuanza kusema unajua ni kipindi hiki, mumewe kaishatoka madarakani na sasa tunaye Mheshimiwa Rais mwanamke kwahiyo na yeye mumewe pengine anaweza akaanzisha pengine taasisi kwahiyo tutakuwa, na siyo wake tu za viongozi nawaume za viongozi. *(Makofi)*

Sasa mazingira kama hayo ndiyo muktadha wake ulikuwa huo kwamba wanapokuwa wameanzisha huduma kama hizo ama wameanzisha taasisi zinazotoa huduma Je, Serikali haioni pengine ingetafuta namna yakuweka

muendelezo wa zile huduma ambazo walikuwa wanazifanya kwa kuwasaidia hawa wake za viongozi ambao sasa viongozi wanakuwa wamestaafu ama waume za viongozi ambao sasa wanakuwa wamestaafu, huo ndiyo muktadha wake. Kwa hiyo nadhani sasa atakuwa na amani nimeelezea muktadha wa swali lake.

Waheshimiwa Wabunge, kwahiyo majibu yaliyotolewa na Serikali yalikuwa ni majibu sahihi kwa mujibu wa swali lililokuwa limepelekwa, lakini yeye alitaka nimsaidie kueleza huo muktadha ili lieleweke vizuri. Kwahiyo hiyo ndiyo ilikuwa nia yake. Kwa hivyo Serikali pamoja na kwamba kwasasa majibu yametolewa kwamba mpango huo haupo lakini ni jambo ambalo sasa limekuja kwenu kwa hiyo mnaweza kuendelea kutazama namna hapa na pale, pengine si kwa kiasi kile ambacho mtu akiwa madarakani anawezakufikia taasisi mbalimbali lakini kujaribu kuona kama wanaweza kusaidiwa kwa njia hiyo. Kwahiyo huo ndiyo ulikuwa muktadha.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema haya nasitisha Shughuli za Bunge mpaka saa kumi kamili Alasiri leo.

*(Saa 7.05 mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 10.00 jioni)*

*(Saa 10.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tukae. Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti. Mwenyekiti, una dakika 20.

**MHE. DANIEL S. BARAN – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bajeti, kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Bunge (Fungu 42) kwa mwaka wa fedha 2022/2023 na

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania limeundwa kwa mujibu wa Ibara ya 62 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Aidha, Ofisi ya Bunge ina jukumu la kutoa huduma kwa Wabunge ili kuliwezesha Bunge kutekeleza majukumu yake kama yalivyoainishwa kwenye Ibara ya 63(3) ya Katiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilikutana na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa George Boniface Simbachawene aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge), Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na Katibu wa Bunge Ndugu Nenelwa Mwihambi, *(ndc)* ili kupitia utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 pamoja na kufanya mashauriano kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hii inatoa mrejesho kwa Bunge lako Tukufu kuhusu utekelezaji wa Bajeti na majukumu ya Mfuko wa Bunge hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2023, pamoja na vipaumbele na masuala muhimu yanayopendekezwa katika Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa fedha 2023/2024. Naomba Taarifa hii yote ya Kamati iingizwe katika kumbukumbu rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapitio ya utekelezaji wa bajeti na majukumu ya Mfuko wa Bunge kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Katika kuwezesha Ofisi ya Bunge kutekeleza majukumu yake, Kifungu cha 32 cha Sheria ya Uendeshaji wa Bunge kama kilivyofanyiwa rejea mwaka 2015 kilianzisha Mfuko wa Bunge. Hivyo, Mfuko wa Bunge hutengewa fedha kwa ajili ya kugharamia mahitaji mbalimbali, ambapo asilimia

88 ya mahitaji hayo ya fedha hutumika kugharamia Mikutano ya Bunge, Kamati za Bunge, Posho ya Jimbo, Usafiri kwa Wabunge, Matibabu kwa Wabunge, Michezo ya Mabunge ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na sehemu iliyobaki ya asilimia 12 hutumika kutekeleza shughuli za Utawala na Uendeshaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Bunge inatekeleza Bajeti yake kwa kuzingatia Sheria ya Bajeti Sura 439, Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Sheria ya Manunuzi ya Umma, Sura 410 pamoja na Mpango Mkakati na Mpango wa Muda wa Kati 2022/2023 – 2024/2025. Utekelezaji wa Bajeti umezingatia malengo yaliyotarajiwa kufikiwa katika vipindi husika na makisio ya Bajeti yamezingatia kuboresha na kutoa huduma mbalimbali kulingana na mahitaji halisi ili kuliwezesha Bunge na Wabunge kutimiza wajibu wao kwa jamii kwa kutekeleza malengo yafuatayo:-

(a) Kuboresha ufanisi wa Wabunge katika kuchambua Bajeti ya Serikali na kuisimamia Serikali;
(b) Kuboresha utoaji huduma kwa Wabunge kupitia Sekretarieti ya Bunge;
(c) Kuboresha ufanisi wa Ofisi ya Bunge katika kusimamia rasilimali watu na fedha;
(d) Kuimarisha utendaji wa Bunge kwa kutumia Mfumo wa Bunge Mtandao hivyo kuongeza ufanisi wa Bunge;

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mengine yaliyotokea ni kama yalivyoonekana kwenye Taarifa yetu ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti ya Mfuko wa Bunge iliyoidhinishwa kwa mwaka 2022/2023. Katika mwaka wa fedha 2022/2023 Mfuko wa Bunge – Fungu 42 uliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 132.7. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 23.6 ni kwa ajili ya Mishahara, shilingi bilioni 103.6 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo, na shilingi 5.4 kwa ajili fedha za Miradi

ya Maendeleo. Kati ya fedha za Miradi ya Maendeleo shilingi bilioni 4.7 ni fedha za ndani na shilingi milioni 700 ni fedha za nje. Vilevile Mfuko wa Bunge uliidhinishiwa kukusanya maduhuli ya kiasi cha shilingi milioni 131.7.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha zilizopokelewa hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2023; Mfuko wa Bunge umepokea kiasi cha shilingi bilioni 15.4 ambazo ni sawa na asilimia 65 ya fedha zote za Mishahara zilizoidhinishwa na Bunge kwa mwaka wa fedha 2022/23.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi mengineyo; fedha za Matumizi Mengineyo zilizopokelewa hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2023, zinafikia jumla ya shilingi 76.5 ambazo ni sawa na asilimia 73 ya fedha zote za Matumizi Mengineyo zilizoidhinishwa na Bunge kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za miradi ya maendeleo. Hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2023 kiasi cha shilingi bilioni 2.2 kimepokelewa ikiwa ni fedha za ndani kwa ajili ya kugharamia shughuli za Maendeleo, kiasi hiki ni sawa na asilimia 47 ya fedha za ndani zilizotengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Fedha hizi ni kwa ajili ya kugharamia ujenzi wa nyumba za Viongozi pamoja na Ukarabati wa Majengo ya Bunge. Aidha hakuna fedha za nje zilizopokelewa kwa kipindi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, maduhuli; katika mwaka wa fedha 2022/23 Mfuko wa Bunge uliidhinishiwa kukusanya kiasi cha maduhuli cha shilingi bilioni 131.7. Hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2023, kiasi cha shilingi bilioni 103.4 kimekusanywa sawa na asilimia 79.

Mheshimiwa Naibu Spika, shughuli zilizotekelezwa katika bajeti ya mwaka 2022/2023; katika kipindi cha Julai, 2022 hadi tarehe 15 Machi, 2023, Mfuko wa Bunge (Fungu – 42) umefanikisha kutekeleza shughuli mbalimbali zikiwemo za

uratibu wa shughuli za Bunge kwa kuzingatia Mpango Mkakati wa Ofisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, uratibu shughuli za Mikutano ya Bunge pamoja na Kamati za Bunge; Mfuko wa Bunge umeweza kufanikisha uratibu na usimamizi wa uendeshaji wa Mikutano ya Bunge na Mikutano ya Kamati za Bunge ambapo Mfuko wa Bunge umetekeleza masuala yafuatayo:-

(a) Kusimamia na kuratibu shughuli za Mikutano Mitatu (3) ya Bunge ya mwezi Septemba, 2022, Novemba, 2022 na Februari, 2023;

(b) Kuratibu Mikutano mitatu (3) ya Kamati za Bunge ambapo Kamati zilifanya uchambuzi wa Miswada ya Sheria, Sheria Ndogo, Taarifa za Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali;

(c) Kuratibu uwasilishwaji wa Ukomo wa Bajeti ya Serikali, Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2023/2024 pamoja na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2023/24; na

(d) Kuratibu ziara za ukaguzi wa Miradi mbalimbali ya Maendeleo kwa Kamati kumi na tatu (13) za Kudumu za Bunge kama inavyoelekezwa na Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge ili kupata thamani ya fedha ya miradi inayotengewa fedha na Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala mengine yaliyotekelezwa ni kama yanavyoorodheshwa katika Taarifa yetu ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa mfumo wa Bunge Mtandao *(e-Parliament);* Mfuko wa Bunge umeendelea kusimamia uendeshaji wa shughuli za Bunge kwa kutumia TEHAMA ambapo kwa sasa kupitia Mfumo wa Bunge Mtandao *(e-parliament)* unamuwezesha Mbunge akiwa nje ya maeneo ya Bunge kutuma maswali katika Ofisi ya Bunge, kuomba nafasi ya kuchangia, kuuliza swali, kuomba kuhusu utaratibu, mwongozo wa Spika au taarifa; na Mbunge kujulishwa kwenye kishikwambi chake punde nyaraka inapotumwa. Aidha, Ofisi ya Bunge inaendelea na maboresho ya mfumo huu kulingana na mahitaji yanavyoongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwezesha ushiriki wa Bunge katika Mikutano ya Kimataifa; katika medani za Kimataifa Mfuko wa Bunge umetekeleza masuala yafuatayo: -

(a) Kuratibu ushiriki wa Bunge katika Mkutano wa 145 wa Umoja wa Mabunge Duniani *(IPU);*

(b) Kuratibu Mkutano wa 52 wa *SADC Parliamentary Forum;*

(c) Kuratibu Mkutano wa Umoja wa Mabunge ya Maziwa Makuu;

(d) Kuratibu Mkutano wa 42 wa *African Carribean Pacific-EU;*

(e) Kuratibu Mkutano wa 64 wa Umoja wa Mabunge ya Jumuiya ya Madola;

(f) Kuratibu Bunge la Afrika *(PAP);* pamoja na

(g) Kuratibu Mkutano wa Wabunge wenye mahitaji maalum wa *CPA* Kanda ya Afrika uliofanyika Jijini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, uratibu wa Ofisi za Viongozi; Mfuko wa Bunge umewezesha utekelezaji wa majukumu

mbalimbali ya Ofisi ya Spika; Ofisi ya Naibu Spika na Ofisi ya Katibu wa Bunge na kuwezesha kusimamia uendeshaji wa shughuli zinazohusu Ofisi ya Bunge kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutolewa kwa huduma za matibabu; Mfuko umewezesha Waheshimiwa Wabunge na familia zao kupatiwa huduma ya matibabu kwa utaratibu wa Bima ya Afya. Aidha, Mfuko wa Bunge umeendelea kuimarisha Kituo cha Afya cha Bunge kwa kununua vifaa tiba pamoja na madawa mbalimbali kwa ajili ya kuwahudumia Waheshimiwa Wabunge pamoja na watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutoa Elimu kwa Umma; Mfuko umeweza kufanikisha utoaji wa elimu kwa umma kwa wadau na wageni mbalimbali waliotembelea Bunge. Aidha, Watumishi wameweza kushiriki katika Maonesho ya Kimataifa ya Saba Saba, ya Nane Nane ambapo wananchi waliotembelea Banda la Ofisi ya Bunge walipata ufafanuzi wa kina kuhusu shughuli zinazotekelezwa na Ofisi ya Bunge. Aidha, Ofisi ya Bunge iliweza kuendesha na kutoa elimu kwa umma kwa shule mbalimbali za msingi na sekondari hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa majukumu mengine; hadi kufikia tarehe 15 Machi 2023, Mfuko umeweza kufanikisha utekelezaji wa majukumu mbalimbali ikiwa ni pamoja na:-

(i) Kuratibu shughuli za Ulinzi na Usalama kwa Waheshimiwa Wabunge, Watumishi pamoja na Wageni mbalimbali wanaoingia maeneo ya Bunge au kushiriki safari za kibunge;

(ii) Kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Ununuzi wa Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2022/2023 pamoja na kuandaa Taarifa za ununuzi na kuwasilishwa kwenye Menejimenti

ya Mamlaka ya Udhibiti na Ununuzi wa Umma, Bodi ya Zabuni na Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini;

(iii) Kuratibu Shughuli za Muungano zinazohusiana na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na kutoa huduma za kiofisi kwenye Ofisi Ndogo ya Bunge Zanzibar;

(iv) Kuratibu maandalizi ya Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa kipindi cha Robo na Nusu mwaka 2022/2023 na kuwasilishwa Hazina;

(v) Usimamizi wa matumizi ya fedha zilizokasimiwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ulifanyika kwa kuzingatia Sheria za Fedha na Manunuzi ya Umma; na

(vi) Kuwezesha Wabunge na Watumishi kushiriki katika Michezo ya Mabunge ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa mwaka 2022 yaliyofanyikia Juba, nchini Sudan ya Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo ya makadirio ya bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Katika mwaka wa fedha 2023/2024 Mfuko wa Bunge unaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 165.6. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 23.6 zimetengwa kwa ajili ya Mishahara ya Wabunge na Watumishi, shilingi bilioni 136.8 zimetengwa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na Shilingi bilioni 5.2 zimetengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambapo shilingi bilioni 4.7 ni fedha za ndani na shilingi milioni 469 ni fedha za nje. Aidha, kwa upande wa maduhuli, Ofisi imepanga kukusanya maduhuli yenye jumla ya shilingi milioni 131.7.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maandalizi ya Bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/2024 yamezingatia mahitaji ya msingi yakiwemo mahitaji ya shughuli za Bunge (Mikutano ya Bunge na Kamati za Bunge) na uendeshaji wa Ofisi. Hivyo, fedha zimegawanywa katika Mafungu makubwa matatu (3) ambayo ni Programu 10 (Utawala na Uendeshaji), Programu

20 (Shughuli za Bunge) na Programu 30 (Ofisi ya Katibu wa Bunge). Mchanganuo wa mafungu madogo madogo katika programu hizo ni kama yanavyoonekana kwenye jedwali namba moja kwenye Taarifa ya Kamati yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, shughuli zinazotarajiwa kufanyika kwa mwaka wa fedha 2023/2024; katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Mfuko wa Bunge unatarajia kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(a) Kugharamia shughuli za Mikutano minne (4) ya Bunge;

(b) Kugharamia shughuli za Mikutano minne (4) ya Kamati za Bunge;

(c) Kugharamia posho ya Jimbo na usafiri wa Wabunge;

(d) Kugharamia matibabu ya Wabunge na familia zao ndani na nje ya nchi;

(e) Kugharamia ushiriki wa Wabunge katika Mikutano ya Kimataifa kama *SADC-PF, EALA*, Maziwa Makuu, Umoja wa Mabunge - *IPU*, Mabunge ya Jumuiya ya Madola na kadhalika;

(f) Kuwezesha Bunge kushiriki katika michezo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Watumishi kushiriki katika michezo ya SHIMIWI;

(g) Kuratibu na kuchapisha Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)* pamoja na nyaraka mbalimbali za Bunge;

(h) Kuratibu na kusimamia kazi na majukumu ya Tume ya Utumishi wa Bunge;

(i) Kugharamia ununuzi na usimikaji wa mitambo ya ulinzi na usalama katika maeneo ya Bunge;

(j) Kuwajengea Wabunge uwezo ili waweze kutekeleza majukumu yao kikatiba;

(k) Kugharamia uendeshaji wa Ofisi kama vile Umeme, Maji, Shajala na kadhalika;

(l) Kuwezesha Watumishi kushiriki mafunzo ya muda mfupi, mrefu ndani na nje ya nchi;

(m) Kusimamia uendeshaji wa Ukumbi wa Bunge, mitambo na mashine;

(n) Kuratibu kazi ya kukarabati Jengo la Ukumbi wa Bunge na majengo ya Ofisi ya Bunge;

(o) Kuandaa vipindi vya televisheni na kurusha matangazo ya Bunge;

(p) Kuratibu utoaji wa habari kwa wananchi kuhusu shughuli za Bunge na Kamati;

(q) Kufuatilia utekelezaji wa hoja za ukaguzi zilizotolewa kabla ya Mwaka wa Fedha 2023/2024;

(r) Kufanya ukaguzi wa matumizi ya kawaida na maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na kutoa taarifa; na

(s) Kuandaa taarifa za mwaka za utekelezaji, fedha na ukaguzi *(Annual Budget Performance, Financial Statements and Audit Reports)* kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho. Naomba nihitimishe kwa kumshukuru Mheshimiwa Spika, na wewe Mheshimiwa Naibu Spika Spika kwa kuongoza vema mashauriano kati ya Kamati ya Bajeti na Serikali. Pia naomba kumshukuru

Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, Waziri wa Fedha na Mipango na Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao kwa Kamati. Aidha, kipekee nimshukuru Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) kwa kushirikiana na Kamati wakati wa majadiliano kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Omari Kigua, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati hii kwa umakini wao katika kujadili na kutoa maoni na mapendekezo mbalimbali kuhusu Bajeti ya Mfuko wa Bunge. Naomba majina ya Waheshimiwa Wabunge ni kama yanavyoonekana kwenye Taarifa yetu ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii, kumshukuru Ndugu Nenelwa Mwihambi, *(ndc)*, Katibu wa Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Aidha, napenda kuipongeza na kuishukuru Sekretarieti ya Kamati ikiongozwa na Mkurugenzi wa Idara ya Bajeti Ndugu Michael Kadebe kwa kuratibu na kutoa ushauri wa kitaalam ambao umesaidia Kamati katika kukamilisha taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, naliomba Bunge lako tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko wa Bunge – Fungu 42, kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kama yalivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu yenye jumla ya shilingi 165,627,897,000 ambapo kiasi cha shilingi 23,605,226,000 ni kwa ajili ya Mishahara, shilingi 136,853,651,000 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na shilingi 5,169,020,000 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**5 APRILI, 2023**

## TAARIFA YA KAMATI YA BAJETI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MFUKO WA BUNGE KWA MWAKA WA FEDHA 2022/23 PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

---

### 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bajeti, kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Bunge (Fungu 42) kwa Mwaka wa Fedha 2022/23 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2023/24.

**Mheshimiwa Spika**, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania limeundwa kwa mujibu wa Ibara ya 62 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Aidha, Ofisi ya Bunge ina jukumu la kutoa huduma kwa Wabunge ili kuliwezesha Bunge kutekeleza majukumu yake kama yalivyoainishwa kwenye Ibara ya 63(3) ya Katiba.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilikutana na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba (Mb), Waziri wa Fedha na Mipango, Mhe. George Boniface Simbachawene (Mb), aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge), Mheshimiwa Hamad Hassan Chande Naibu Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa Mwihambi, *ndc* ili kupitia utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2022/23 pamoja na kufanya mashauriano kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2023/24.

**Mheshimiwa Spika,** taarifa hii inatoa mrejesho kwa Bunge lako Tukufu kuhusu utekelezaji wa Bajeti na majukumu ya Mfuko wa Bunge hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2023, pamoja

na vipaumbele na masuala muhimu yanayopendekezwa katika Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa fedha 2023/24.

## 2.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI NA MAJUKUMU YA MFUKO WA BUNGE KWA MWAKA WA FEDHA 2022/23

**Mheshimiwa Spika,** Katika kuwezesha Ofisi ya Bunge kutekeleza majukumu yake, Kifungu cha 32 cha Sheria ya Uendeshaji wa Bunge kama ilivyofanyiwa rejea mwaka 2015 kilianzisha Mfuko wa Bunge. Hivyo, Mfuko wa Bunge hutengewa fedha kwa ajili ya kugharamia mahitaji mbalimbali, ambapo **asilimia 88** ya mahitaji hayo ya fedha hutumika kugharamia Mikutano ya Bunge, Kamati za Bunge, Posho ya Jimbo, Usafiri kwa Wabunge, Matibabu kwa Wabunge, Michezo ya Mabunge ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na sehemu iliyobaki ya **asilimia 12** hutumika kutekeleza shughuli za Utawala na Uendeshaji.

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Bunge inatekeleza Bajeti yake kwa kuzingatia Sheria ya Bajeti Sura 439, Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Sheria ya Manunuzi ya Umma Sura 410 pamoja na Mpango Mkakati (*Strategic Plan 2021/22-2025/26*) na Mpango wa Muda wa Kati (*Medium Term Expenditure Framework – MTEF; 2022/23 – 2024/25)*. Utekelezaji wa Bajeti umezingatia malengo yaliyotarajiwa kufikiwa katika vipindi husika na makisio ya Bajeti yamezingatia kuboresha na kutoa huduma mbalimbali kulingana na mahitaji halisi ili kuliwezesha Bunge na Wabunge kutimiza wajibu wao kwa jamii kwa kutekeleza malengo (*objectives)* yafuatayo; -

a) Kuboresha ufanisi wa Wabunge katika kuchambua Bajeti ya Serikali na kuisimamia Serikali;

b) Kuboresha utoaji huduma kwa Wabunge kupitia Sekretarieti ya Bunge;

c) Kuboresha ufanisi wa Ofisi ya Bunge katika kusimamia rasilimali watu na fedha;

d) Kuimarisha Utendaji wa Bunge kwa kutumia Mfumo wa Bunge Mtandao (e-parliament) na hivyo kuongeza ufanisi wa Bunge;

e) Kuboresha huduma na kutekeleza afua za kupunguza maambukizi ya UKIMWI kwa Wabunge na Watumishi kama ilivyoainishwa katika Mkakati wa Nne wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI Tanzania (2018/19-2022/23);

f) Kuimarisha na kuongeza ujuzi wa Wabunge katika kutunga Sheria kwa kutoa mafunzo mbalimbali chini ya Mradi wa Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma Awamu ya Sita (PFMRP VI) na Mradi wa LSP;

g) Kuimarisha miundombinu ya Bunge ili kuwawezesha Waheshimiwa Wabunge na Watumishi kufanya kazi katika mazingira bora na wezeshi;

h) Kununua na kuboresha vitendea kazi kwa Waheshimiwa Wabunge na Watumishi wa Ofisi ya Bunge;

i) Kuimarisha Mifumo ya Ufuatiliaji na Tathmini katika Ofisi ya Bunge;

j) Kuhakikisha kuwa vyama vya Kibunge vinatoa mchango katika utendaji wa Bunge hususan katika kutunga Sheria; na

k) Kuimarisha mahusiano kati ya Bunge na wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na Wadau wa Maendeleo, Taasisi zisizo za Kiserikali na Wananchi kwa ujumla.

### *2.1 Bajeti ya Mfuko wa Bunge iliyoidhinishwa kwa mwaka 2022/23.*

**Mheshimiwa Spika,** Katika Mwaka wa Fedha 2022/23 Mfuko wa Bunge – Fungu 42 uliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 132,728,638,000.** Kati ya fedha hizo **Shilingi 23,658,494,000** ni kwa ajili ya Mishahara (PE), **Shilingi 103,670,144,000** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) na **Shilingi 5,400,000,000** kwa ajili fedha za Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha za Miradi ya Maendeleo **Shilingi 4,700,000,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 700,000,000** ni fedha za nje. Vilevile, Mfuko wa Bunge uliidhinishiwa kukusanya Maduhuli ya kiasi cha **Shilingi 131,766,000.**

### *2.2 Fedha zilizopokelewa hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2023*

#### *2.2.1 Mishahara*

Hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2023 Mfuko wa Bunge umepokea kiasi cha **Shilingi 15,452,258,290.00** ambazo ni sawa na **asilimia 65** ya fedha zote za Mishahara zilizoidhinishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2022/23.

#### *2.2.2 Matumizi Mengineyo*

Fedha za Matumizi Mengineyo (OC) zilizopokelewa hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2023 zinafikia jumla ya **Shilingi 76,506,235,867.00** ambazo ni sawa na **asilimia 73** ya fedha zote za Matumizi Mengineyo zilizoidhinishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2022/23.

#### *2.2.3 Fedha za Miradi ya Maendeleo*

Hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2023 kiasi cha **Shilingi 2,191,611,491.71** kimepokelewa ikiwa ni fedha za ndani kwa ajili ya kugharamia shughuli za Maendeleo, kiasi hiki ni sawa na **asilimia 47** ya fedha za ndani zilizotengwa kwa ajili ya

Miradi ya Maendeleo. Fedha hizi ni kwa ajili ya kugharamia ujenzi wa nyumba za Viongozi pamoja na Ukarabati wa Majengo ya Bunge. Aidha hakuna fedha za nje zilizopokelewa kwa kipindi husika.

### *2.2.4 Maduhuli (Revenue)*

Katika Mwaka wa Fedha 2022/23 Mfuko wa Bunge uliidhinishiwa kukusanya kiasi cha Maduhuli ya **Shilingi 131,766,000.00**. Hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2023 kiasi cha **Shilingi 103,438,140.00** kimekusanywa sawa na **asilimia 79**. Makusanyo ya maduhuli haya yametokana na kodi ya pango katika Jengo la Utawala Annex pamoja na kukodisha Kumbi za Mikutano.

### *2.3 Shughuli Zilizotekelezwa Katika Bajeti ya Mwaka 2022/23*

**Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi tarehe 15 Machi, 2023 Mfuko wa Bunge (Fungu – 42) umefanikisha kutekeleza shughuli mbalimbali zikiwemo za uratibu wa shughuli za Bunge kwa kuzingatia Mpango Mkakati wa Ofisi (*Strategic Plan 2021/2022-2025/2026*), kama ifuatavyo:-

### *2.3.1 Uratibu wa shughuli za Mikutano ya Bunge pamoja na Kamati za Bunge*

**Mheshimiwa Spika**, mfuko wa Bunge umeweza kufanikisha uratibu na usimamizi wa uendeshaji wa Mikutano ya Bunge na Mikutano ya Kamati za Bunge ambapo mfuko wa Bunge umetekeleza masuala yafuatayo:-

a) Kusimamia na kuratibu shughuli za Mikutano Mitatu (3) ya Bunge ya mwezi Septemba 2022, Novemba 2022 na Februari 2023;

b) Kuratibu Mikutano mitatu (3) ya Kamati za Bunge ambapo Kamati zilifanya uchambuzi wa Miswada ya

Sheria, Sheria ndogo, Taarifa za Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali;

c) Kuratibu uwasilishwaji wa Ukomo wa Bajeti ya Serikali, Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2023/24 pamoja na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2023/24;

d) Kuratibu ziara za ukaguzi wa Miradi mbalimbali ya Maendeleo kwa Kamati kumi na tatu (13) za Kudumu za Bunge kama inavyoelekezwa na Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge ili kupata thamani ya fedha ya Miradi inayotengewa fedha na Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

e) Kuratibu utolewaji wa huduma ya matibabu ndani na nje ya nchi kwa Wabunge na Watumishi;

f) Miswada saba (7) ya Sheria pamoja na Maazimio mawili (2) ya Kimataifa ilijadiliwa na kupitishwa na Bunge na hatimaye kuwasilishwa Serikalini kwa utekelezaji;

g) Kuratibu na kuchapisha Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard),* pamoja na kufanya matengenezo kwenye mashine za kurekodia Taarifa Rasmi za Bunge;

h) Kuratibu ununuzi wa magari 3 ya Viongozi ambayo tayari yameshalipiwa fedha na taratibu za kuyapokea zinaendelea;

i) Kutoa ushauri wa kisheria kwa Wabunge pamoja na Kamati za Bunge wakati wa uchambuzi wa Miswada;

j) Kutoa habari mbalimbali zinazohusu Bunge kwa Jamii;

k) Kuratibu na kudhibiti maambukizi ya virusi vya UKIMWI kwa kutoa Lishe kwa Watumishi wanaoishi na VVU;

l) Kuratibu maandalizi ya taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa kipindi cha Robo na Nusu Mwaka kwa mwaka wa fedha 2022/23 na kuziwasilisha Hazina;

m) Kuboresha maslahi ya Wabunge na Watumishi wa Bunge hususan maboresho ya vifurushi vya Bima ya Afya;

n) Katika kipindi hiki, Ofisi imeweza kuajiri watumishi wapya 22 ili kuongeza rasilimali watu katika Bunge;

o) Kuratibu kuulizwa kwa jumla ya maswali ya kawaida 388 na ya nyongeza 1,052 Bungeni na kupatiwa majibu na Serikali;

p) Kuratibu jumla ya maswali 30 ya papo kwa papo yaliyoulizwa moja kwa moja kwa Mhe. Waziri Mkuu na kupatiwa majibu;

q) Kupokea, kuhariri na kuwasilisha Serikalini maswali 1,242 ya Wabunge ili yapatiwe majibu;

r) Kuratibu shughuli za Kamati zilizohusu uchambuzi wa Miswada ya Sheria, Sheria Ndogo, uandaaji wa Taarifa za Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Taarifa za Utendaji wa Wizara na Taasisi za Serikali na ufuatiliaji wa utekelezaji wa Afua za UKIMWI;

s) Kuratibu ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo mbalimbali kwa Kamati Kumi na tatu (13) za Kudumu za Bunge kama inavyoelekezwa na Kanuni za Kudumu za Bunge, aidha Mfuko wa Bunge iliwezesha ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyofanyika nje ya nchi katika nchi za DRC (Kinshasa) na Ethiopia;

t) Kufanya Mafunzo maalumu kwa Wenyeviti na Makamu Wenyeviti wa Kamati zote za kudumu za Bunge ndani ya nchi.

u) Kuchambua Mwongozo wa Maandalizi ya Bajeti kwa Mwaka 2023/24 na kuwasilisha Maoni Bungeni;

v) Kuwezesha Bunge kujadili Taarifa ya Hali ya Uchumi kwa Mwaka 2022/23, Mapendekezo ya Mpango na Bajeti ya Taifa ya Mwaka 2023/24 na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2023/24.

### *2.3.2 Utekelezaji wa Mfumo wa Bunge Mtandao (e-Parliament)*

**Mheshimiwa Spika,** Mfuko wa Bunge umeendelea kusimamia uendeshaji wa shughuli za Bunge kwa kutumia TEHAMA ambapo kwa sasa kupitia Mfumo wa Bunge Mtandao (e-parliament) unamuwezesha Mbunge akiwa nje ya maeneo ya Bunge kutuma maswali katika Ofisi ya Bunge, kuomba nafasi ya kuchangia, kuuliza swali, kuomba kuhusu utaratibu, mwongozo wa Spika au taarifa; na Mbunge kujulishwa (notification) kwenye kishikwambi chake punde nyaraka inapotumwa. Aidha, Ofisi ya Bunge inaendelea na maboresho ya mfumo huu kulingana na mahitaji yanavyoongezeka.

### *2.3.3 Kuwezesha ushiriki wa Bunge katika Mikutano ya Kimataifa*

**Mheshimiwa Spika,** katika medani za Kimataifa Mfuko wa Bunge umetekeleza masuala yafuatayo;

(a) Kuratibu ushiriki wa Bunge katika Mkutano wa 145 wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU);

(b) Kuratibu Mkutano wa 52 wa SADC Parliamentary Forum;

(c) Kuratibu Mkutano wa Umoja wa Mabunge ya Maziwa Makuu;

(d) Kuratibu Mkutano wa 42 wa African Carribean Pacific-EU;

(e) Kuratibu Mkutano wa 64 wa Umoja wa Mabunge ya Jumuiya ya Madola (Commonwealth Parliamentary Association); na

(f) Kuratibu Bunge la Afrika (PAP) pamoja na kuratibu Mkutano wa Wabunge wenye mahitaji maalum wa CPA Kanda ya Afrika (CwPD) uliofanyika jijini Dar es Salaam.

***2.3.4 Uratibu wa Ofisi za Viongozi***

**Mheshimiwa Spika,** Mfuko wa Bunge umewezesha utekelezaji wa majukumu mbalimbali ya Ofisi ya Spika; Ofisi ya Naibu Spika na Ofisi ya Katibu wa Bunge na kuwezesha kusimamia uendeshaji wa shughuli zinazohusu Ofisi ya Bunge kwa ujumla.

***2.3.5 Kutolewa kwa huduma za Matibabu***

**Mheshimiwa Spika,** Mfuko umewezesha Waheshimiwa Wabunge na familia zao kupatiwa huduma ya matibabu kwa utaratibu wa Bima ya Afya. Aidha, Mfuko wa Bunge umeendelea kuimarisha Kituo cha Afya cha Bunge kwa kununua vifaa tiba pamoja na madawa mbalimbali kwa ajili ya kuwahudumia Waheshimiwa Wabunge pamoja na Watumishi.

***2.3.6 Kutoa Elimu kwa Umma***

**Mheshimiwa Spika,** Mfuko umeweza kufanikisha utoaji wa Elimu kwa Umma kwa wadau na wageni mbalimbali waliotembelea Bunge. Aidha, Watumishi wameweza kushiriki katika maonesho ya Kimataifa ya Saba Saba na Nane Nane ambapo wananchi waliotembelea Banda la Ofisi ya Bunge

walipata ufafanuzi wa kina kuhusu shughuli zinazotekelezwa na Ofisi ya Bunge. Aidha, Ofisi ya Bunge iliweza kuendesha na kutoa elimu kwa umma kwa shule mbalimbali za msingi na sekondari nchini;

### *2.3.7 Utekelezaji wa Majukumu Mengine*

**Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia tarehe 15 Machi 2023, Mfuko umeweza kufanikisha utekelezaji wa majukumu mbalimbali ikiwa ni pamoja na: -

I. Kuratibu shughuli za Ulinzi na Usalama kwa Waheshimiwa Wabunge, Watumishi pamoja na Wageni mbalimbali wanaoingia maeneo ya Bunge au kushiriki safari za kibunge;

II. Kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Ununuzi wa Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2022/23 pamoja na kuandaa Taarifa za ununuzi na kuwasilishwa kwenye Menejimenti ya Mamlaka ya Udhibiti na Ununuzi wa Umma (PPRA), Bodi ya Zabuni na Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini (GPSA);

III. Kuratibu Shughuli za Muungano zinazohusiana na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na kutoa huduma za kiofisi kwenye Ofisi ndogo ya Bunge Zanzibar;

IV. Kuratibu maandalizi ya Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa kipindi cha Robo na Nusu mwaka 2022/23 na kuwasilishwa Hazina;

V. Usimamizi wa matumizi ya fedha zilizokasimiwa kwa mwaka wa fedha 2022/23 ulifanyika kwa kuzingatia Sheria za Fedha na Manunuzi ya Umma (PFA na PPRA); na

VI. Kuwezesha Wabunge na Watumishi kushiriki katika Michezo ya Mabunge ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa mwaka 2022 yaliyofanyikia Juba, nchini Sudan ya Kusini.

## 3.0 MAELEZO YA MAKADIRIO YA BAJETI YA MFUKO WA BUNGE KWA MWAKA WA FEDHA 2023/24

### *3.1 Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka 2023/24*

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2023/24 Mfuko wa Bunge unaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 165,627,897,000.** Kati ya kiasi hicho, **shilingi 23,605,226,000** zimetengwa kwa ajili ya Mishahara ya Wabunge na Watumishi, **Shilingi 136,853,651,000** zimetengwa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **Shilingi 5,169,020,000** zimetengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambapo **Shilingi 4,700,000,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 469,020,000** ni fedha za nje. Aidha, kwa upande wa maduhuli, Ofisi imepanga kukusanya maduhuli yenye jumla ya **Shilingi 131,766,000.**

**Mheshimiwa Spika,** Maandalizi ya Bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/24 yamezingatia mahitaji ya msingi yakiwemo mahitaji ya shughuli za Bunge (Mikutano ya Bunge na Kamati za Bunge) na uendeshaji wa Ofisi. Hivyo, fedha zimegawanywa katika Mafungu makubwa matatu (3) ambayo ni Programu 10 (Utawala na Uendeshaji), Programu 20 (Shughuli za Bunge) na Programu 30 (Ofisi ya Katibu wa Bunge). Mchanganuo wa mafungu madogo madogo katika programu hizo ni kama ifuatavyo:-

**Jedwali Na. 1: Mchanganuo wa Bajeti ya Mfuko iliyoidhinishwa kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 na Maombi ya Fedha kwa Mwaka 2023/24**

| NA. | MAELEZO | BAJETI ILIYOIDHINISHWA MWAKA 2022/23 | MAKISIO YA BAJETI KWA MWAKA 2023/24 |
|---|---|---|---|
| **1.** | **MISHAHARA (PE)** | **23,658,494,000.00** | **23,605,226,000.00** |
| 1.1 | Programu 10 – Utawala na Uendeshaji | 1,370,155,500.00 | 1,472,402,000.00 |
| 1.2 | Programu 20 – Shughuli za Bunge | 20,953,152,500.00 | 20,765,244,000.00 |
| 1.3 | Programu 30 – Ofisi ya Katibu wa Bunge | 1,335,186,000.00 | 1,367,580,000.00 |
| **2.** | **MATUMIZI MENGINE (OC)** | **103,670,144,000.00** | **36,853,651,000.00** |
| 2.1 | Programu 10 – Utawala na Uendeshaji | 14,495,702,000.00 | 14,101,851,000.00 |
| 2.2 | Programu 20 – Shughuli za Bunge | 80,218,132,000.00 | 112,257,170,000.00 |
| 2.3 | Programu 30 – Ofisi ya Katibu wa Bunge | 8,956,310,000.00 | 10,494,630,000.00 |
| **3** | **MPANGO WA MAENDELEO (DEV)** | **5,400,000,000.00** | **5,169,020,000.00** |
| 3.1 | PT 6318 - Ukarabati wa Majengo ya Bunge | 0.00 | 539,000,000 |
| 3.2 | PT 6360 - Ujenzi wa Miundombinu ya Bunge | 4,700,000,000.00 | 4,161,000,000 |
| 3.3 | PT 6215 - Mradi wa PFMRP | 300,000,000.00 | 469,020,000 |
| 3.4 | PT 6260 - Kulijengea Uwezo Bunge (LSP) | 400,000,000.00 | 0.00 |
| **4** | **MAKUSANYO (REVENUE)** | **131,766,000.00** | **131,766,000** |
| 4.1 | Maduhuli | 131,766,000.00 | 131,766,000 |
| | **JUMLA YA FUNGU (1+2+3)** | **132,728,638,000.00** | **165,627,897,000.00** |

### *3.2 Shughuli zinazotarajiwa kufanyika kwa mwaka wa fedha 2023/2024*

**Mheshimiwa Spika,** Katika Mwaka wa Fedha 2023/24 Mfuko wa Bunge unatarajia kutekeleza shughuli zifuatazo: -

(a) Kugharamia shughuli za mikutano minne (4) ya Bunge;

(b) Kugharamia shughuli za mikutano minne (4) ya Kamati za Bunge;

(c) Kugharamia posho ya Jimbo na usafiri wa Wabunge;

(d) Kugharamia matibabu ya Wabunge na familia zao ndani na nje ya nchi;

(e) Kugharamia ushiriki wa Wabunge katika Mikutano ya Kimataifa kama SADC-PF, EALA, Maziwa Makuu, Umoja wa Mabunge - IPU, Mabunge ya Jumuiya ya Madola n.k;

(f) Kuwezesha Bunge kushiriki katika michezo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Watumishi kushiriki katika michezo ya SHIMIWI;

(g) Kuratibu na kuchapisha Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard) pamoja na nyaraka mbalimbali za Bunge;

(h) Kuratibu na kusimamia kazi na majukumu ya Tume ya Utumishi wa Bunge;

(i) Kugharamia ununuzi na usimikaji wa mitambo ya ulinzi na usalama katika maeneo ya Bunge;

(j) Kuwajengea Wabunge uwezo ili waweze kutekeleza majukumu yao kikatiba;

(k) Kugharamia uendeshaji wa Ofisi kama Umeme, Maji, Shajala nk;

(l) Kuwezesha Watumishi kushiriki mafunzo ya muda mfupi na mrefu ndani na nje ya nchi;

(m) Kusimamia uendeshaji wa Ukumbi wa Bunge, mitambo na mashine;

(n) Kuratibu kazi ya kukarabati Jengo la ukumbi wa Bunge na majengo ya Ofisi ya Bunge;

(o) Kuandaa vipindi vya televisheni na kurusha matangazo ya Bunge;

(p) Kuratibu utoaji wa habari kwa wananchi kuhusu shughuli za Bunge na Kamati;

(q) Kufuatilia utekelezaji wa hoja za ukaguzi zilizotolewa kabla ya Mwaka wa Fedha 2023/24;

(r) Kufanya ukaguzi wa matumizi ya kawaida na maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2023/24 na kutoa taarifa; na

(s) Kuandaa taarifa za mwaka za utekelezaji, fedha na ukaguzi (Annual Budget Performance, Financial Statements and Audit Reports) kwa Mwaka wa Fedha 2022/23.

## 4.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** naomba nihitimishe kwa kukushukuru wewe Mheshimiwa Spika na Naibu Spika kwa kuongoza vema mashauriano kati ya Kamati ya Bajeti na Serikali. Pia naomba kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba (Mb), Waziri wa Fedha na Mipango na Mheshimiwa Hamad Hassan Chande (Mb), Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao kwa Kamati. Aidha, kipekee nimshukuru Mheshimiwa George Boniface Simbachawene (Mb), aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, na Uratibu) kwa kushirikiana na Kamati wakati wa majadiliano kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kumshukuru Mheshimiwa Omari Kigua (Mb) Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati hii kwa umakini wao katika kujadili na kutoa maoni na

mapendekezo mbalimbali kuhusu Bajeti ya Mfuko wa Bunge. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Daniel Baran Sillo, Mb – Mwenyekiti,
2. Mhe. Omari Mohamed Kigua, Mb – M/Mwenyekiti
3. Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, Mb
4. Mhe. Mariam Madalu Nyoka, Mb
5. Mhe. Dkt. Charles Kimei, Mb
6. Mhe. Subira Khamis Mgalu, Mb
7. Mhe. Jonas William Mbunda, Mb
8. Mhe. Juma Hamad Omar, Mb
9. Mhe. Kwagilwa Reuben Nhamanilo, Mb
10. Mhe. Bahati Kenneth Ndingo, Mb
11. Mhe. Stella Ikupa, Mb
12. Mhe. Joseph Zacharius Kamonga, Mb
13. Mhe. Shally Josepha Raymond, Mb
14. Mhe. Josephat Sinkamba Kandege, Mb
15. Mhe. Leah Jeremiah Komanya, Mb
16. Mhe. Rashid Abdalla Rashid, Mb
17. Mhe. Zainab Athumani Katimba, Mb
18. Mhe. Bahati Khamis Kombo, Mb
19. Mhe. Vedastus Manyinyi Mathayo, Mb
20. Mhe. Oran Manase Njeza, Mb
21. Mhe. Omar Ali Omar, Mb
22. Mhe. Zaytun Seif Swai, Mb

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuchukua fursa hii, kumshukuru Ndg. Nenelwa Mwihambi, *ndc*, Katibu wa Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Aidha, napenda kuipongeza na kuishukuru Sekretarieti ya Kamati ikiongozwa na Mkurugenzi wa Idara ya Bajeti Ndg. Michael Kadebe kwa kuratibu na kutoa ushauri wa kitaalamu ambao umesaidia Kamati katika kukamilisha Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo naliomba Bunge lako tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato

na Matumizi ya Mfuko wa Bunge – Fungu 42, kwa Mwaka wa Fedha 2023/24 kama yalivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu yenye jumla ya **Shilingi 165,627,897,000** ambapo kiasi cha **Shilingi 23,605,226,000** ni kwa ajili ya Mishahara, **Shilingi 136,853,651,000** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **Shilingi 5,169,020,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha.

Daniel Baran Sillo, (Mb)
**MWENYEKITI KAMATI YA BUNGE YA BAJETI**
05 Aprili, 2023

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mwenyekiti wa Bajeti na ahsante Mwenyekiti wa Bunge. *(Makofi)*

Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUNGULILE - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA AFYA NA MASUALA YA UKIMWI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba taarifa yote iingizwe kwenye *Hansard* kama kumbukumbu sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu - Tume ya Kudhibiti UKIMWI *(TACAIDS)* – Fungu 92 kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 pamoja na Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Fungu hilo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, baada ya uchambuzi wa kina wa Taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya Fungu 92, naomba

kutoa taarifa ya Kamati inayofafanua mambo makubwa matatu (3) yafuatayo:-

(a) Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania *(TACAIDS)* kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023;

(b) Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania *(TACAIDS)* kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024; na

(c) Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kwa Fungu 92.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2022/2023, matokeo ya uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 yanatokana na Kamati kufanya mapitio ya mambo makuu yafuatayo:-

(a) Uzingatiaji wa maoni na ushauri uliotolewa na Kamati Bungeni wakati wa kujadili Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu: Fungu 92 - Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania *(TACAIDS)* kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022;

(b) Hali ya upatikanaji wa Fedha hadi kufikia mwezi Februari, 2023; na

(c) Utekelezaji wa malengo yaliyokuwa yamewekwa kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi kuhusu uzingatiaji wa maoni na ushauri wa kamati. Maoni na ushauri uliokuwa umetolewa na Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 ulihusu maeneo makuu manane (8), kama inavyoonekana katika taarifa. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa

baadhi ya ushauri umezingatiwa na kutekelezwa na ushauri mwingine unaendelea kutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa yaliyobainika wakati wa ziara ya Kamati. Kwa Mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, Kanuni ya 117(1), Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI ilifanya ziara za ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyopo katika Mikoa ya Iringa, Mbeya na Songwe. Ukaguzi huu ulifanyika kuanzia tarehe 14 hadi 19 Machi 2023. Katika ziara hiyo, Vituo vya Uangalizi na Matunzo *(Care and Treatment Centre (CTC)* vilivyopo katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Iringa, Hospitali ya Rufaa Mkoa wa Mbeya na Hospitali ya Wilaya ya Mbozi- Mkoa wa Songwe vilikaguliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ziara hiyo, Kamati ilibaini kuwa yapo mafanikio na changamoto mbalimbali na hivyo kutoa ushauri wa namna ya kukabiliana na changamoto zilizoripotiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio yaliyotokana na uwepo wa vituo vya uangalizi na matunzo *(CTC)*:-

(i) Kupungua kwa maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto,

(ii) Kupungua kwa wateja wanaotumia huduma. Hii imewezekana kwa kutumia wakili tiba, mama mwambata na watoa huduma ngazi ya jamii ambao husaidia kutafuta wateja waliopotea,

(iii) Kuongeza hamasa kutokana na kuanzisha huduma za kliniki baada ya saa za kazi. Hii imesaidia kuhamasisha wanaume kuwa wafuasi wa dawa na imeboresha mahudhurio pamoja na upimaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto zilizopo katika vituo vya uangalizi wa matunzo *(CTC)*. Bado kumeendelea kuwepo na changamoto mbalimbali katika kuhakikisha kuwa asilimia 95-95-95 zinafikiwa ifikapo 2030. Changamoto hizo ni pamoja na:-

(i) Unyanyapaa kwenye jamii, hali inayosababisha baadhi ya wateja kutohudhuria kliniki na kuacha dawa;

(ii) Wateja wa dawa za kurefusha maisha kuhama sehemu wanazopata huduma bila kutoa taarifa, jambo ambalo linasababisha kupotea katika mfumo wa ufuatiliaji;

(iii) Kiwango kidogo cha upimaji wa VVU kwa wanaume kwani wengi wamekuwa waoga wa kupima na kujua afya zao;

(iv) Muamko mdogo wa kutekeleza afua za tohara kwa wanaume ili kupunguza mambukizi ya VVU.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi kuhusu upatikanaji wa fedha. Kamati ilichambua taarifa ya hali ya upatikanaji wa fedha kwa lengo la kujiridhisha ni kiwango gani cha fedha hizo zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu zimetolewa ili kuwezesha utekelezaji wa malengo na vipaumbele vya Tume.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania iliidhinishiwa bajeti ya jumla ya shilingi 14,981,224,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na fedha za maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi 2,979,018,000 ni matumizi ya kawaida na yenye kujumuisha mshahara; shilingi 1,766,272,000 na shilingi 1,212,746,000 kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, fedha za miradi ya maendeleo ni shilingi 12,002,206,000 ambapo

kati yake fedha za ndani ni shilingi 1,880,000,000 na fedha za nje ni shilingi 10,122,206,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa kamati umebaini kuwa hadi kufikia mwezi Februari tume ilikuwa imepokea kiasi cha shilingi 8,321,152,143.28 sawa na asilimia 55.4 ya bajeti yote. Kati ya fedha hizo zilizopokelewa fedha ya matumizi ya kawaida ni shilingi 1,694,695,528.28 sawa na asilimia 56.9 kwa matumizi ya kawaida iliyotengwa. Kati ya fedha za matumizi ya kawaida zilizotolewa mishahara ni shilingi 1,084,474,722 sawa na asilimia 61.4 na fedha zote za mishahara zilizoidhinishwa na matumizi mengineyo zimetolewa shilingi 610,220,800 sawa na asilimia 50.3 ya fedha zote za matumizi ya kawaida yaliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa fedha za maendeleo uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa hadi kufikia mwezi Februari 2023, kati ya fedha shilingi 12,002,206,000 zilizoidhinishwa zimepokelewa shilingi 6,626,456,221 sawa na asilimia 55.2 ya fedha zote za maendeleo zilizokuwa zimeidhinishwa na Bunge lako tukufu. Fedha hizo za maendeleo zilizotolewa zinajumuisha fedha za ndani shilingi 940,000,000,000 sawa na asilimia 50 ya fedha za ndani zilizoidjinshwa na fedha za nje zilizoidhinishwa ni shilingi 5,686,456,621 sawa na asilimia 51 ya fedha zote za nje na za maendeleo zilizoidhinishwa na Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti Ukimwi *(Aids Trust Fund - ATF)*. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa kipaumbele cha matumizi ya fedha za ndani za maendeleo zilizotolewa asilimia 60 zimekwenda kununua dawa za *Cotrimoxazole* sawa na shilingi 564,000,000. Asilimia 25 sawa na shilingi 235,000,000 zimetumika kutekeleza programu za kinga hasa utoaji wa elimu ya kujikinga na VVU kwa Wanafunzi na Watumishi wa Vyuo vya Elimu ya Juu Mkoa wa Dar es salaam na uraghbishi na elimu ya VVU na UKIMWI

kwa vijana Mkoa wa Tanga kwenye maeneo ambayo mradi wa bomba ghafi unapita.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile asilimia 15 sawasawa na shilingi 141,000,000 zimetumika katika shughuli za kuendesha Mfuko zinazojumuisha vikao vya kisheria vya Mfuko wa Bodi ya Udhamini wa UKIMWI, Kufanya mkutano wa uraghbishi na sekta binafsi kwa ajili ya kujadili namna bora ya kuchangia mwitikio wa VVU na UKIMWI nchini na kuratibu Mbio za Nyika Marathon zilizofanyika siku ya maadhimisho ya UKIMWI Duniani Mkoani Lindi kwa lengo la kutunisha mfuko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla, hali ya upatikanaji wa fedha ni wastani wa asilimia 55.5 ni ya kuridhisha. Kamati inasisitiza fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya masuala ya UKIMWI zitolewe kwa wakati ili kutokwamisha utekelezaji wa shughuli zilizopangwa kwa kipindi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa mpango wa makadirio ya matumizi kwa mwaka wa fedha wa 2023/2024. Kamati ilipokea na kuchambua Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu – Fungu 92, Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania, kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024. Uchambuzi ulilenga pamoja na mambo mengine kuhakiki Mpango wa Makadirio haya unaozingatia Ilani ya Uchaguzi ya CCM, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano na Mwongozo wa Fedha wa Bajeti uliotolewa na Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi unaonesha maeneo ya vipaumbele katika makadirio hayo yamezingatia miongozo iliyopo japokuwa kumekuwa na changamoto ya Serikali kutenga fedha kwa ajili ya uratibu wa masuala ya UKIMWI jambo linaloashiria kuwa na utegemezi mkubwa wa fedha za wafadhili.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha zinazoombwa kwa ajili ya kudhibiti UKIMWI – Fungu 92. Katika mwaka wa fedha wa

2023/24, Tume ya Kudhibiti UKIMWI – Fungu 92 inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 3,670,817,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na fedha shilingi 1,897,434,000 kwa ajili ya Mishahara na shilingi 1,773,383,000 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa fedha za Maendeleo, Tume inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 22,193,149,000 kwa ajili ya utekelezaji wa Maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi 1,880,000,000 ni fedha za ndani na shilingi 20,312,149,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, ulinganifu wa bajeti ya 2022/2023 na 2023/2024 umeonesha ongezeko la bajeti kwa wastani wa asilimia 73. Ongezeko hili limetokana na ongezeko la fedha za matumizi ya kawaida kwa asilimia 57 na ongezeko la fedha nje za miradi kwa asilimia 101.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa fedha za maendeleo za ndani hakuna ongezeko la fedha, hivyo kiasi kilichotengwa cha mwaka 2022/2023 ndio hichohicho kimeendelea kutengwa katika mwaka wa fedha 2023/2024. Fedha za maendeleo za nje zimeongezeka kwa asilimia 101, hali hii ni dhahiri kwamba bado kuna changamoto ya kutegemea fedha za wahisani katika kuratibu masuala ya UKIMWI, jambo ambalo linatishia usalama wa wagonjwa endapo wahisani watasitisha kutoa fedha hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri na maoni ya Kamati. Baada ya uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti ya 2022/2023 na Makadirio ya Matumizi ya fedha ya Mwaka 2023/2024, Tume ya Kudhibiti UKIMWI – Fungu 92, sasa naomba kutoa maoni na ushauri wa Kamati kama ifuatavyo:-

(i) Serikali iipatie Tume ya kudhibiti UKIMWI *(TACAIDS)* fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge ili kuiwezesha Tume kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

(ii) Serikali ione umuhimu wa kutenga fedha zake za ndani kwa ajili ya udhibiti wa UKIMWI na kupunguza kutegemea fedha za wafadhili kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa UKIMWI *(ATF);* pamoja na Serikali kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya *ATF* bado Kamati inaona upo umuhimu wa kutafutiwa vyanzo mapato ili Mfuko uweze kujiendesha wenyewe. Mlipuko wa ugonjwa wa UVIKO-19 na vita vya Urusi na Ukraine pamoja vimetikisa na kuhamisha vipaumbele vya wafadhili kwenye maeneo hayo. Basi ni vyema kama nchi tukatafuta vyanzo mahsusi vya mapato ili kuwezesha *ATF* kuwa na fedha za uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya UKIMWI ya Mwaka 2001. Kwa kuwa imebainika Sera ya UKIMWI ya mwaka 2001 ni ya muda mrefu na imepitwa na wakati, Serikali kwa kushirikiana na Tume ya udhibiti UKIMWI Tanzania *(TACAIDS)* ifanye mapitio ya Sera ili iweze kuendana na mazingira yaliyopo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utekelezaji wa Afua za UKIMWI. Serikali imejiwekea malengo ya kufikia asilimia 95-95-95 ifikapo 2020. Hadi sasa, Serikali imefanikiwa katika 90 ya kwanza kufikia asilimia 88, asilimia 99 kwa 95 ya pili na 95 katika asilimia 95 ya tatu. Kamati imebaini kuwa kuna changamoto katika kufikia malengo ya asilimia 95 ya kwanza ambayo inahusu upimaji na kujitambua. Kamati inashauri yafuatayo:-

(i) Elimu iendelee kutolewa kwa jamii kuhusu virusi vya UKIMWI ili kupunguza unyanyapaa pamoja na maambukizi mapya kwani bado baadhi ya watu wanaishi na virusi vya UKIMWI hawajajitokeza nakujua hali zao hususan wanawake.

(ii) WAVIU wasajiliwe kwenye mfumo wa kidigitali ili kurahisisha utolewaji wa huduma popote na hatimae kuepusha utoro na pia kuwezesha utunzaji wa kumbukumbu za wateja.

(iii) Serikali kupitia Tume ya UKIMWI na Wizara ya Afya zihakikishe kunakuwepo na mashine za kupima wingi wa virusi vya UKIMWI *(viral load)* katika vituo vyote vya uangalizi wa tiba kwa lengo la kusogeza huduma hizi karibu na walengwa.

(iv) Elimu kuhusu unyanyapaa na ukatili wa kijinsia iendelee kutolewa kwa jamii ili kuondoa hofu ya upimaji, pia kupunguza maambukizi kutokana na vitendo vya ukatili wa kijinsia.

(v) Kamati za UKIMWI za Vijiji zinategemewa sana kusaidia katika mapambano dhidi ya UKIMWI. Hata hivyo, imebainika kwamba, Kamati hizi zimekuwa zinalegalega katika maeneo mengi. Kamati inaishauri Wizara ya Afya, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ione namna ya kuziwezesha Kamati hizi, ili ziweze kusaidia katika mapambano na kupunguza maambukizi.

(vi) Elimu kuhusu umuhimu wa kufanya tohara wanaume waliopo chini ya miaka kumi na tano iendelee kutolewa kwa jamii.

(vii) Serikali kwa kushirikiana na Tume ya UKIMWI *(TACAIDS)*, iweke mkakati wa kudhibiti maambukizi katika kundi la Vijana ambalo ndilo linaloongoza kwa maambukizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hitimisho. Naomba kukushukuru wewe binafsi, binafsi na Wenyeviti wa Bunge kwa kuliongoza vyema Bunge letu, natoa shukrani kwa Mheshimiwa Boniphace Simbachawene aliyekuwa Waziri na Mheshimiwa Ummy Nderiananga, Waziri Ummy Mwalimu,

Naibu Waziri Mheshimiwa Godwin Mollel kwa ushirikiano ambao wametupa. Tunampongeza Mheshimiwa Jenista Mhagama kwa kuteuliwa kuwa Waziri katika Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu, Makatibu Wakuu katika Wizara ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Wizara ya Afya. Mtendaji Mkuu Dkt. Leonard Maboko wa *TACAIDS*.

Mheshimiwa Naibu Spika, njia ya kipekee natoa shukrani kwa Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI kwa kazi nzuri waliyoifanya kujadili na kuchambua utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2022/2023 pamoja na makadirio ya fedha yam waka 2022/2023. Vilevile tunamshukuru sana Katibu wa Bunge na Watendaji wote kwa kazi kubwa na nzuri ambayo imesaidia kukamilisha taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo yote sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Matumizi ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania Fungu 92 kiasi cha shilingi 25,862,966,000 ambapo shilingi 3,670,817,000 ni Matumizi ya Kawaida na shilingi 22,192,149,000 kwa ajili ya fedha ya Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**TAARIFA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA WAZIRI MKUU (TUME YA KUDHIBITI UKIMWI TANZANIA –*TACAIDS*) KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 PAMOJA NA MAONI NA USHAURI WA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

*[Imetolewa chini ya Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu Bunge Toleo la Februari, 2023]*

**5 APRILI, 2023**

## SEHEMU YA KWANZA

### 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kutukutanisha kwa mara nyingine katika Mkutano huu wa Kumi na Moja wa Bunge la Kumi na Mbili, kwa lengo la kutekeleza masharti ya Kanuni ya 118 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu-Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania *(TACAIDS)* **– Fungu 92** kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 pamoja na Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Fungu hilo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika,** kama zilivyo Kamati nyingine za kisekta, kifungu cha 7(1) (a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, pamoja na majukumu mengine, Kamati ya Afya na Masuala ya UKIMWI inajukumu la kushughulikia Bajeti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania. Katika kutekeleza jukumu hilo, mnamo tarehe 23 Machi, 2023, Kamati ilichambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 na kufanya ulinganisho kuhusu Makadirio ya Matumizi ya **Fungu 92** – Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania *(TACAIDS)* kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya uchambuzi wa kina wa Taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya **(Fungu 92),** naomba kutoa taarifa ya Kamati inayofafanua mambo makubwa matatu (3) yafuatayo: -

(a) Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania *(TACAIDS)* kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023;

(b) Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania *(TACAIDS)* kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024*;* na

(c) Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kwa Fungu 92.

## SEHEMU YA PILI

### 2.0 UCHAMBUZI WA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 NA MAKADIRIO YA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

### *2.1 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023*

**Mheshimiwa Spika**, ili kuliwezesha Bunge kufuatilia utekelezaji wa bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 na kushauri ipasavyo kuhusu makadirio ya matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Kamati ilifanya uchambuzi wa wasilisho la Serikali kuhusu mambo makuu matatu (3) ambayo ni:

(a) Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati uliotolewa wakati wa bajeti ya Mwaka wa Fedha 2022/2023;

(b) Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022; na

(c) Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**Mheshimiwa Spika**, matokeo ya uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

yanatokana na Kamati kufanya mapitio ya mambo makuu yafuatayo: -

(a) Uzingatiaji wa maoni na ushauri uliotolewa na Kamati Bungeni wakati wa kujadili Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu: **Fungu 92** - Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania *(TACAIDS)* kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022;

(b) Hali ya upatikanaji wa Fedha hadi kufikia mwezi Februari, 2023; na

(c) Utekelezaji wa malengo yaliyokuwa yamewekwa kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi huo ulilenga kuliwezesha Bunge kujiridhisha na utoshelevu wa utekelezaji wa mipango na mwenendo wa matumizi, ikilinganishwa na madhumuni ya Bunge kuidhinisha bajeti husika.

### *2.2 Uchambuzi kuhusu Uzingatiaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, ili kujiridhisha na namna Serikali inavyozingatia ushauri wa Kamati unaotolewa katika Bunge lako Tukufu, Kamati ilichambua taarifa iliyowasilishwa kuhusu utekelezaji wa Maoni na Ushauri uliotolewa wakati wa kujadili Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu; Fungu 92 – Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania. Uchambuzi wa Kamati umebaini yafuatayo: -

**Mheshimiwa Spika,** maoni na ushauri uliokuwa umetolewa na Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 ulihusu maeneo makuu manane (8) ambayo ni: -

i) Upatikanaji wa Fedha za ndani kwa ajili ya afua za UKIMWI;

ii) Kuanzisha vyanzo vya Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti UKIMWI *(AIDS Trust Fund – ATF);*
iii) Upimaji wa VVU na Tohara ya hiari ya kitabibu kwa Wanaume;
iv) Mkazo wa Utekelezaji wa afua za UKIMWI;
v) Kampeni maalum kwenye Mikoa ambayo ina maambukizi zaidi ya kiwango cha kitaifa cha asilimia 4.7;
vi) Ufuatiliaji wa WAVIU ili kuhakikisha hawakatishi matumizi ya dawa;
vii) Kuendelea kutolewa kwa elimu kuhusu unyanyapaa na ukatili wa kijinsia; na
viii) Kuwezesha na kuhamasisha Kamati za UKIMWI za vijiji ili kusaidia mapambano dhidi ya UKIMWI;

**Mheshimiwa Spika**, naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, baadhi ya ushauri umezingatiwa na kutekelezwa na ushauri mwingine unaendelea kutekelezwa.

### *2.3 Uchambuzi wa yaliyobainika wakati wa Ziara ya Kamati*

**Mheshimiwa Spika,** Kwa Mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, Kanuni ya 117 (1), Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI ilifanya ziara za ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyopo katika mkoa wa Iringa, Mbeya na Songwe. Ukaguzi huu ulifanyika kuanzia tarehe 14 hadi 19 Machi 2023. Katika ziara hiyo, Vituo vya Uangalizi na Matunzo *(Care and Treatment Centre (CTC)* vilivyopo katika hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Iringa, Hospitali ya Rufaa Mkoa wa Mbeya na Hospitali ya Wilaya ya Mbozi- Mkoa wa Songwe vilikaguliwa.

**Mheshimiwa Spika,** katika ziara hiyo, Kamati ilibaini kuwa yapo mafanikio na changamoto mbalimbali na hivyo kutoa ushauri wa namna ya kukabiliana na changamoto zilizoripotiwa.

### 2.3.1 Mafanikio yanayopatikana kufuatia uwepo wa vituo vya Uangalizi na Matunzo(CTC)

i) Kupungua kwa maambukizi ya VVU kutoka kwa mama wajawazito kwenda kwa mtoto kwani vituo hivi vinatekeleza mkakati wa utoaji wa huduma za upimaji na utoaji wa tiba za ARV kwa wajawazito na wanaonyonyesha wenye maambukizi ya VVU. Kwa mfano, katika hospitali ya Wilaya ya Mbozi- Mkoa wa Songwe, kati ya watoto 184 waliozaliwa na akina mama wenye maambukizi ya VVU, watoto 2 sawa na asilimia 1.08 waligundulika kuwa na maambukizi ya VVU na kuunganishwa kwenye huduma za matibabu na matunzo;

ii) Kupunguza upotevu wa wateja wanaotumia huduma, hili limewezekana kwa kuwatumia wakili - tiba, mama mwambata na watoa huduma ngazi ya jamii ambao husaidia kutafuta wateja waliopotea; na

iii) Kuongeza hamasa kwa kuanzisha huduma za kliniki baada ya saa za kazi, hii imesaidia kuhamasisha wanaume kuwa wafuasi wa dawa na imeboresha mahudhurio pamoja na upimaji.

### 2.3.2 Changamoto zilizopo katika Vituo vya Uangalizi na Matunzo (CTC)

**Mheshimiwa Spika**, bado kumeendelea kuwepo na changamoto mbalimbali katika kuhakikisha kuwa asilimia 95-95-95 zinafikiwa ifikapo 2030. Changamoto hizo ni pamoja na; -

i) Unyanyapaa kwenye jamii hali inayosababisha baadhi ya wateja kutokuhudhuria kliniki na kuacha dawa. Katika baadhi ya vituo vilivyotembelea na Kamati kama vile kituo cha uangalizi na matunzo kilichopo hospitali ya Wilaya ya Mbozi- Mkoa wa Songwe, Kamati imebaini kuwa elimu ya UKIMWI bado haijafikia jamii ipasavyo na hivyo kusababisha unyanyapaa kwani baadhi yao

huwatenga WAVIU kwa sababu ya kuona ni watu wenye dhambi na wazinifu. Vilevile, unyanyapaa wa mtu mwenyewe kwa kuamini kuwa kujulikana kuwa na VVU ni aibu na fedheha;

ii) Wateja wa dawa za kurefusha maisha kuhama sehemu wanazopata huduma bila kutoa taarifa jambo ambalo linasababisha kupotea katika mfumo wa ufuatiliaji;

iii) Kiwango kidogo cha upimaji wa VVU kwa wanaume kwani wengi wamekuwa waoga wa kupima na kujua afya zao; na

iv) Mwamko mdogo wa kutekeleza afua ya tohara kwa wanaume ili kuzuia maambukizi ya VVU.

### *2.4 Uchambuzi kuhusu Upatikanaji wa Fedha*

### 2.4.1 Upatikanaji wa Fedha za Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (*TACAIDS)* - Fungu 92 kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilichambua taarifa ya hali ya upatikanaji wa fedha kwa lengo la kujiridhisha ni kwa kiwango gani fedha hizo zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu zimetolewa ili kuwezesha utekelezaji wa malengo na vipaumbele vya Tume.

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha wa 2022/23 Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania iliidhinishiwa bajeti ya jumla ya **Shilingi 14,981,224,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Fedha za Maendeleo. Kati ya fedha hizo **Shilingi 2,979,018,000.00** ni Matumizi ya Kawaida yenye kujumuisha Mishahara **1,766,272,000.00** na **Shilingi 1,212,746,000.00** Matumizi Mengineyo**.** Aidha, fedha za Miradi ya Maendeleo ni **12,002,206,000.00** ambapo kati yake fedha za ndani ni **Shilingi 1,880,000,000.00** na fedha za nje ni **Shilingi 10,122,206,000.00**.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, hadi kufika mwezi Februari 2023, Tume ilikuwa imepokea kiasi cha **Shilingi 8,321,152,143.28** sawa na asilimia **55.54** ya Bajeti yake yote. Kati ya fedha hizo zilizopokelewa fedha za Matumizi ya Kawaida jumla ni **Shilingi 1,694,695,522.28** sawa na **asilimia 56.89** ya fedha zote za Matumizi ya Kawaida zilizotengwa. Kati ya fedha za Matumizi ya Kawaida zilizotolewa Mishahara ni **Shilingi 1,084,474,722** sawa na **asilimia 61.40** ya fedha zote za Mishahara zilizoidhinishwa; na Matumizi Mengineyo zimetolewa **Shilingi 610,220,800** sawa na **asilimia 50.32** ya fedha zote za Matumizi ya Kawaida zilizoidhinishwa.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Fedha za Maendeleo, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa hadi kufika mwezi Februari 2023, kati ya **Shilingi 12,002,206,000.00** zilizoidhinishwa, zimepokelewa **Shilingi 6,626,456,621.00** sawa **asilimia 55.21** ya fedha za maendeleo zilizokuwa zimeidhinishwa na Bunge lako Tukufu. Fedha hizi za Maendeleo zilizotolewa zinajumuisha Fedha za Ndani **Shilingi 940,000,000.00** sawa na **asilimia 50** ya Fedha za Ndani zilizoidhinishwa; pamoja na Fedha za Nje **Shilingi 5,686,456,621.00** sawa na **asilimia 51** ya Fedha zote za Nje za Maendeleo zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu.


### 2.4.2 Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti Ukimwi (*Aids Trust Fund - ATF*)

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa kipaumbele cha matumizi ya fedha za ndani za maendeleo zilizotolewa ni **asilimia sitini (60%)** ya fedha zilizopokelewa sawa na **Shilingi 564,000,000.00** zimepelekwa Wizara ya Afya kwa ajili ya kununua dawa aina ya Cotrimoxazole kwa matumizi ya WAVIU. **Asilimia ishirini na tano (25%)** ya fedha zilizopokelewa sawa na **Shilingi 235,000,000.00** zimetumika kutekeleza programu za kinga hasa utoaji wa elimu ya kujikinga na VVU kwa Wanafunzi na Watumishi katika Vyuo vya Elimu ya Juu vya Mkoa wa Dar es salaam na kufanya uraghbishi na elimu ya VVU na UKIMWI kwa vijana katika

mkoa wa Tanga kwenye maeneo ambayo mradi wa bomba la mafuta ghafi unapita.

Vile vile, zimetolewa **asilimia kumi na tano (15%)** ya fedha sawa na **Shilingi 141,000,000.00** kuwezesha shughuli za uendeshaji wa mfuko zikijumuisha vikao viwili vya kisheria vya Bodi ya Mfuko wa Udhamini wa UKIMWI; Kufanya mkutano wa uraghbishi na sekta binafsi kwa ajili ya kujadili namna bora ya kuchangia mwitikio wa VVU na UKIMWI nchini; na kuratibu Mbio za Nyika *(Marathon)* ambazo zilifanyika wakati wa maadhimisho ya Siku ya UKIMWI Duniani Mkoani Lindi kwa ajili ya kutunisha Mfuko. Katika mbio hizo jumla ya **Shilingi 250,000,000.00** zilikusanywa kwa ajili ya kutekeleza afua za kudhibiti UKIMWI kupitia Mfuko wa ATF.

**Kielelezo Namba 1: Mchanganuo wa Fedha zilizoidhinishwa na Fedha zilizopokelewa kwa kipindi cha kuanzia Julai 2022 hadi Februari 2023:**




***Chanzo; Taarifa ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI (TACAIDS) kuhusu Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023***

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla, hali ya upatikanaji wa fedha ambayo ni wastani wa **asilimia 55.54** ni ya kuridhisha. Kamati inasisitiza fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya masuala ya UKIMWI zitolewe kwa wakati ili kutokwamisha utekelezaji wa shughuli zilizopangwa kwa kipindi husika.

## 3.0 UCHAMBUZI WA MPANGO WA MAKADIRIO YA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA WA 2023/2024

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea na kuchambua Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu –Fungu 92 (Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania) kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024. Uchambuzi ulilenga pamoja na mambo mengine kuhakiki kama Mpango na Makadirio haya umezingatia Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 – 2025, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano na Mwongozo wa Mpango wa Bajeti uliotolewa na Wizara ya Fedha na Mipango.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi unaonesha kuwa maeneo ya vipaumbele katika makadirio hayo yamezingatia miongozo iliyopo japokuwa bado kumekuwa na changamoto ya Serikali kutenga fedha kidogo kwa ajili ya uratibu wa masuala ya UKIMWI jambo linaloashiria kuwa na utegemezi mkubwa wa fedha za wafadhili.

### *3.1 Mapitio ya Makadirio ya Fedha kwa Mwaka 2023/2024*

### 3.1.1 Fedha zinazoombwa kwa ajili ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI – Fungu 92

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mwaka wa fedha wa 2023/24, Tume ya kudhibiti UKIMWI Tanzania – Fungu 92 inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 3,670,817,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi**

**1,897,434,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi 1,773,383,000.00** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

Kwa upande wa fedha za Maendeleo, Tume inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 22,192,149,000.00** kwa ajili ya utekelezaji wa Maendeleo. Kati ya Fedha hizo, **Shilingi 1,880,000,000.00** ni Fedha za Ndani na **Shilingi 20,312,149,000.00** ni Fedha za nje.

**Kielelezo Namba 2: Fedha Zinazoombwa Kuidhinishwa kwa Mwaka 2023/2024**




***Chanzo; Randama ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI (TACAIDS) kuhusu Makadirio ya Fedha kwa Mwaka 2023/2024***

**3.1.2 Ulinganisho wa Fedha zilizoidhinishwa Mwaka 2022/2023 na Fedha zinazoombwa Kuidhinishwa 2023/2024**

**Kielelezo Namba 3: Ulinganisho wa Bajeti ya Mwaka 2022/2023 na 2023/2024**

| AINA | 2022/2023 | 2023/2024 | ONGEZEKO/PUNGUFU | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| **OC** | 1,212,746,000.00 | 1,773,383,000.00 | +560,637,000.00 | 46 |
| **MISHAHARA** | 1,766,271,000.00 | 1,897,434,000.00 | +131,163,000.00 | 7 |
| **MAENDELEO NDANI** | 1,880,000,000.00 | 1,880,000,000.00 | - | 0 |
| **MAENDELEO NJE** | 10,122,206,000.00 | 20,312,149,000.00 | +10,189,943,000.00 | 101 |
| **JUMLA** | **14,981,223,000.00** | **25,870,966,000.00** | **+10,889,743,000.00** | **73** |

***Chanzo: Taarifa ya Bajeti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania 2023/2024***

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi umefanyika wa kulinganisha Bajeti ya Tume kwa Mwaka 2022/2023 na 2023/2024 kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 3 na kubaini ongezeko la bajeti kwa **asilimia 73**. Ongezeko hili limetokana na ongezeko kwenye Fedha za Matumizi ya Kawaida kwa **asilimia 57** na ongezeko la Fedha nje za Miradi ya Maendeleo kwa **asilimia 101.**

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa fedha za matumizi ya Kawaida, ongezeko zaidi ni kwenye Matumizi Mengineyo (OC) kwa **asilimia 46.** Baadhi ya vifungu na kasma zilizoongezewa fedha ni pamoja na Kifungu 1002, Kasma 22008 inayohusu Mafunzo ya Ndani ambapo fedha zimeongezeka kutoka **Shilingi 30,700,000.00** mwaka 2022/2023 hadi **Shilingi 64,805,000.00** mwaka 2023/2024 sawa na ongezeko la **asilimia 111.** Ongezeko hili limetokana na mahitaji ya mafunzo kwa watumishi na kuongezeka kwa posho ya kijikimu. Ongezeko linguine ni katika Kasma 22010 ya Usafiri wa Ndani ya Nchi ambapo fedha zimeongezeka kutoka **Shilingi 104,330,000.00** Mwaka 2022/2023 hadi **Shilingi 184,980,000.00** sawa na ongezeko la **asilimia 77**. Vilevile

Kasma 22032 inayohusu gharama nyingine za uendeshaji ambapo fedha zimeongezeka kutoka **Shilingi 17,100,000.00** hadi **Shilingi 42,500,800.00** sawa na ongezeko la **asilimia 148.5** ambalo limetokana na kutengwa fedha kwa ajili ya kulipa madeni ya watoa huduma.

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla katika mafungu yote ya Matumizi ya Kawaida, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa fedha zimeongezeka zaidi katika kasma tano (5) ambazo ni: -

i. Usafiri wa Ndani ya Nchi ambapo ongezeko limetokana na shughuli za kusambaza Mkakati wa Tano wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI wa Mwaka 2021/2022-2025/2026 kwa wadau katika ngazi ya Taifa, Mikoa 26 na Halmashauri 184;

ii. Mishahara kutokana na kuongezeka kwa watumishi, kujaza nafasi zilizowazi na kutenga mishahara ya wakuu wa Idara na Vitengo ambavyo havikuwa na wakurugenzi kamili;

iii. Kuongezeka kwa viwango vya gharama ya posho ya kujikimu kwa watumishi wawapo safarini pamoja na posho za watumishi kwa mujibu wa sheria;

iv. Mafunzo ya ndani ya nchi kutokana na mahitaji ya mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu kwa watumishi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024; na

v. Gharama za kumbi za mikutano, mafuta, vilainishi pamoja na gharama nyingine za uendeshaji.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Fedha za Maendeleo za Ndani, hakuna ongezeko la fedha; hivyo kiasi kilichotengwa mwaka wa fedha 2022/2023, ndicho kimeendela kutengwa 2023/2024. Hivyo, zimetengwa fedha kwa ajili ya Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti UKIMWI (ATF) **Shilingi 1,880,000,000.00**

zitakazotumika katika maeneo makuu matatu ambapo asilimia sitini (60%) ni kwa ajili ya ununuzi wa dawa kama vile ARV, vitendanishi na bidhaa nyingine za maabara; asilimia ishirini na tano (25%) zimeelekezwa kwenye programu za kinga; na asilimia kumi na tano (15%) ni kwa ajili ya kuwezesha shughuli za uendeshaji wa mfuko.

**Mheshimiwa Spika**, Fedha za Maendeleo za Nje zimeongezeka kwa asilimia mia moja na moja (101%). Kwa hali hii ni dhahiri kwamba bado kuna changamoto ya kutegemea fedha za wahisani katika kuratibu masuala UKIMWI jambo ambalo linatishia usalama wa wagojwa pale endapo wahisani watasitisha kutoa fedha hizo.

## SEHEMU YA TATU

## 4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, baada ya uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha wa 2022/2023; na Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2023/2024 kwa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania – **Fungu 92**, sasa naomba kutoa maoni na ushauri wa Kamati kama ifuatavyo: -

### 4.1 *Upatikanaji wa fedha za ndani kwa ajili ya afua za UKIMWI*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaendelea kusisitiza yafuatayo:-

i) Serikali iipatie Tume ya kudhibiti UKIMWI Tanzania *(TACAIDS)* fedha zote kama zilivyoidhinishwa na Bunge ili kuiwezesha Tume kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi;

ii) Serikali ione umuhimu wa kutenga fedha zake za ndani kwa ajili ya udhibiti wa UKIMWI na kupunguza kutegemea fedha za wafadhili kutoka nje ambazo hazina uhakika na zenye masharti magumu kwa ajili ya mwitikio endelevu wa mapambano dhidi ya UKIMWI hasa tukizingatia

kwamba baadhi ya wafadhili wameanza kupunguza kiwango cha ufadhili wa fedha za UKIMWI; na

iii) Serikali iweke mipango madhubuti ya kupata vyanzo vingine vya mapato vitakavyosaidia kupata fedha zaidi kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Ni muhimu bajeti ya UKIMWI kwa kiasi kikubwa itokane na fedha zetu za ndani.

**4.2 *Mfuko wa Taifa wa UKIMWI* (AIDS Trust Fund - ATF*)***

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na Serikali kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya *ATF* bado Kamati inaona upo umuhimu wa kutafutiwa vyanzo mapato ili Mfuko uweze kujiendesha wenyewe. Mlipuko wa ugonjwa wa UVIKO 19 na vita vya Urusi na Ukraine kwa pamoja vimetikisa uchumi na kuhamisha vipaumbele vya wafadhili kwenye maeneo hayo. Hivyo basi, ni vema kama nchi tukatafuta vyanzo mahsusi vya mapato ili kuwezesha *ATF* kuwa na fedha za uhakika;

**4.3 *Sera ya UKIMWI ya Mwaka 2001***

Kwa kuwa imebainika kwamba Sera ya UKIMWI ya mwaka 2001 ni ya muda mrefu na imepitwa na wakati, Serikali kwa kushirikiana na Tume ya kudhibiti UKIMWI Tanzania *(TACAIDS)* ifanye mapitio ya Sera hii ili iweze kuendana na mazingira yaliyopo sasa;

**4.4 *Utekelezaji wa Afua za UKIMWI***

Serikali imejiwekea malengo ya kufikia asilimia 95-95-95 ifikapo 2030. Hadi sasa, Serikali imefanikiwa katika 95 ya kwanza kufikia asilimia 88, 95 ya pili kufikia asilimia 99 na 95 ya tatu kufikia asilimia 98. Kamati imebaini kuwa kuna changamoto katika kufikia malengo ya asilimia 95 ya kwanza ambayo inahusu kupima na kujitambua. Kamati inashauri yafuatayo: -

i) Elimu iendelee kutolewa kwa jamii kuhusu virusi vya UKIMWI ili kupunguza unyanyapaa pamoja na maambukizi mapya kwani bado baadhi ya watu

wanaoishi na virusi vya UKIMWI hawajajitokeza nakujua hali zao hususan wanaume;

ii) WAVIU wasajiliwe kwenye mfumo wa kidigitali *(finger print)* ili kurahisisha utolewaji wa huduma popote na hatimae kuepusha utoro na pia kuwezesha utunzaji wa kumbukumbu za wateja;

iii) Serikali kupitia Tume ya Kudhibiti UKIMWI na Wizara ya Afya zihakikishe kunakuwepo na mashine za kupimia wingi wa virusi vya UKIMWI *(viral load)* katika vituo vyote vya uangalizi na tiba ili kurahisisha na kuokoa muda pale kipimo hicho kinapohitajika;

iv) Elimu kuhusu unyanyapaa na ukatili wa kijinsia iendelee kutolewa kwa jamii ili kuondoa hofu ya upimaji lakini pia kupunguza maambukizi kutokana na vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa wanawake;

v) Kamati za UKIMWI za Vijiji zinategemewa sana katika kusaidia katika mapambano dhidi ya UKIMWI. Hata hivyo, imebainika kuwa, Kamati hizi katika maeneo mengi zinalegalega katika utendaji kazi wake. Kamati inashauri Wizara ya Afya, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ione namna ya kuziwezesha Kamati hizi ili ziweze kusaidia katika mapambano na hivyo kupunguza maambukizi;

vi) Elimu kuhusu umuhimu wa kufanya Tohara kwa wanaume walio chini ya miaka kumi na tano (15) iendelee kutolewa kwa jamii;

vii) Serikali kwa kushirikiana na Tume ya kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS), iweke mkakati wa kudhibiti maambukizi kwenye kundi la Vijana ambalo ndilo kundi linaloongoza kwa maambukizi mapya;

## 5.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati mbele ya Bunge lako Tukufu. Napenda kukupongeza kwa namna unavyoliongoza Bunge letu kwa umahiri mkubwa. Vilevile, nawashukuru na kuwapongeza Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa utekelezaji mzuri wa majukumu yao.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kutoa shukrani za pekee kwa Mheshimiwa Boniphace Simbachawene (Mb) – aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu, pamoja na Naibu Waziri; Mheshimiwa Ummy Hamis Nderiananga (Mb). Vilevile, nampongeza Mheshimiwa Jenista Joackim Mhagama (Mb) kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu.

**Mheshimiwa Spika**, vilevile, namshukuru Waziri wa Afya Mheshimiwa Ummy Mwalimu na Naibu Waziri Mheshimiwa Godwin Mollel kwa ushirikiano wao mkubwa walioipatia Kamati wakati wote walipohitajika katika kutekeleza majukumu ya Kamati. Napenda pia kumshukuru Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu Dkt. Jim James Yonazi pamoja na Maafisa wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa ushirikiano wanaoipatia Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kumshukuru Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania Dkt. Leonard Maboko na Watendaji wote wa Mfuko wa Kudhibiti UKIMWI Tanzania kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati wakati Kamati ilipokuwa ikitekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika,** kipekee naomba niwashukuru wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kujadili na kuchambua Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Afya kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Tume ya

Kudhibiti UKIMWI Tanzania kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023. Kwa heshima kubwa, naomba kuwatambua kwa majina Waheshimiwa Wabunge ambao ni wajumbe wa Kamati hii kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Stanslaus Haroon Nyongo, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile, Mb - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Aysharose Ndaholi Matembe, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Bernadetha Kasabango Mushashu, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Cecil David Mwambe, Mb- ‘’
6. Mhe. Christopher Olenyokie Ole Sendeka, Mb - ‘’
7. Mhe. Dkt. Christine Christopher Mnzava, Mb - ‘’
8. Mhe. Dkt. Hamis Andrea Kigwangala, Mb - ‘’
9. Mhe. Elibariki Emmanuel Kingu, Mb - ‘’
10. Mhe. George Ranwell Mwenisongole, Mb - ‘’
11. Mhe. Hassan Haji Kassim, Mb - ‘’
12. Mhe. Hassan Seleman Mtenga, Mb - ‘’
13. Mhe. Josephine Johnson Genzabuke, Mb - ‘’
14. Mhe. Juliana Daniel Shonza, Mb - ‘’
15. Mhe. Khalifa Mohamed Issa, Mb - ‘’
16. Mhe. Mohamed Lujuo Monni, Mb - ‘’
17. Mhe. Mrisho Mashaka Gambo, Mb - ‘’
18. Mhe. Mussa Omar Salim, Mb - ‘’
19. Mhe. Seif Salum Seif, Mb - ‘’
20. Mhe. Shamsia Azizi Mtamba, Mb - ‘’
21. Mhe. Zubeida Khamis Shaib, Mb - ‘’

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuwashukuru Watumishi wa Ofisi ya Bunge wakiongozwa na Katibu wa Bunge Ndugu Nenelwa Joyce Mwihambi, Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Michael Chikokoto na Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Gerald Magili kwa kuiwezesha Kamati hii kutekeleza majukumu yake wakati wote. Kipekee, nawashukuru Makatibu wa Kamati Ndugu Hosiana John na Ndugu Victoria Mrema pamoja na Msaidizi wa Kamati Ndugu Grace Gwivaha kwa kuratibu vyema kazi za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kusema hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Matumizi ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania **Fungu 92** kiasi cha **Shilingi 25,862,966,000.00** ambapo **Shilingi 3,670,817,000.00** ni Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 22,192,149,000.00** kwa ajili ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Mhe. Stanslaus H. Nyongo, (Mb)
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA AFYA**
**NA MASUALA YA UKIMWI**
5 Aprili, 2023

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mwenyekiti, Dkt. Ndugulile. Sasa namuita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge, Ustawi, Maendeleo na Jamii.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ – MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Taarifa hii iingizwe kwenye Taarifa rasmi za Bunge *(Hansard)* kama ilivyowasilishwa hapa Mezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, kwa mwaka wa fedha 2022/2023, pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023,

naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii, Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, kwa mwaka wa fedha 2022/2023, pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa bajeti na makadirio ya mapato na matumizi yanaweka msingi wa ushauri wa Kamati kuhusu Hoja hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu. Uchambuzi wa Kamati ulijielekeza katika mambo makuu manne yafuatayo:-

(i) Makusanyo ya maduhuli,

(ii) Mwenendo wa Upatikanaji wa fedha za Bajeti ya kawaida,

(iii) Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo,

(iv) Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Uchambuzi wa Makusanyo ya Maduhuli katika mwaka wa Fedha 2022/2023, Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu ililenga kukusanya maduhuli ya jumla ya shilingi 43,000,000,000. Hadi kufikia Mwezi Februari, 2023 Fungu 65 lilikuwa limekusanya shilingi bilioni 20.4 sawa na asilimia 45.21 ya malengo yaliyokusudiwa. Mchanganuo wa makusanyo hayo unaonekana katika Jedwali Namba 1.

Mhesimiwa Naibu Spika, kutokana na uchambuzi uliofanyika, Kamati ina maoni kuwa mwenendo wa makusanyo kwa Mwaka huu siyo wa kuridhisha kwani kiujumla wameweza kukusanya asilimia 45.44 tu hivyo, kuathiri utekelezaji wa malengo yaliyowekwa. Ni rai ya Kamati kuwa,

Serikali ipange makadirio ya makusanyo kwa kuzingatia uhalisia kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Ofisi ya Waziri Mkuu, Fungu 65, iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 15.9 kwa matumizi ya kawaida. Kati ya Fedha hizo shilingi bilioni 7 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi bilioni 5.8 kwa ajili ya mishahara, ambapo shilingi 2.9 kwa ajili ya ruzuku ya mishahara kwa Wakala wa Afya na Usalama Mahala pa Kazi *(OSHA)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Februari, 2023 Ofisi ya Waziri Mkuu, Fungu 65, ilipokea jumla ya shilingi bilioni 9.5 sawa na asilimia 79.73 ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Mchanganuo wa fedha hizo kama inavyoonekana katika Jedwali Namba 02.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande mwingine Fungu 15 liliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 4.2 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo kiasi cha shilingi bilioni 2.3 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 1.9 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Hadi kufikia Februari 2023, Tume ilikuwa imepokea kiasi cha shilingi bilioni 1.4 sawa na asilimia 33.9. Mchanganuo wa Fedha zilizopokelewa hadi Februari, 2023 ni kama unavyoonekana katika Jedwali Namba 03. Ni maoni ya Kamati kuwa mapokezi ya fedha za matumizi ya kawaida yanapaswa kuwa na uwiano katika mafungu haya mawili kwa sababu katika fedha hizo kuna fedha za mishahara ya watumishi na fedha za matumizi mengineyo ambazo hutumika kwa ajili ya uendeshaji wa kila siku wa taasisi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kuhusu tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Ofisi wa Waziri Mkuu, Fungu 65 ilitengewa jumla ya shilingi bilioni 26.6 kwa ajii ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 13 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 13.6 ni fedha za nje.

Mheshiniwa Naibu Spika, hadi kufikia Februari 2023 Ofisi imepokea kiasi cha shilingi bilioni 5.9 sawa na asilimia 22.45 ya fedha zote. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni nne ni fedha za ndani na shilingi bilioni 1.4 ni fedha za nje. Mgawanyo wa fedha hizo umeainishwa katika Jedwali Namba 04.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa mwingine Fungu 15 linatekeleza mradi mmoja wa Mfumo wa Usimamizi wa Uendeshaji Mashauri *(ECMS)*. Mradi huu uliidhinishiwa shilingi bilioni moja. Hadi kufikia Februari 2023, Tume ilikuwa imepokea shilingi milioni 300 sawa na asilimia 30 ya fedha iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilitaka kujua sababu za kutolewa kidogo kwa fedha za nje za miradi ya maendeleo ambapo ilijulishwa ni kutokana na ucheleweshaji kutoka kwa wadau wanaohusika. Kamati ilishauri mawasiliano yaendelee kufanyika ili fedha hizo zitolewe kabla ya kumalizika kwa mwaka wa fedha Juni, 2023 ili Miradi iliyopangwa kutekelezwa itekelezwe na kuwapatia wananchi huduma zilizokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya miradi Mitano ilitekelezwa na Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu. Kamati ilifuatilia na kuchambua utekelezaji wa miradi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi Na. 6205, Programu ya Kukuza Kazi za Staha *(Decent Work Country Program)*. Mradi huu unahusu kukuza na kujenga stadi za maisha kwa vijana kupitia programu ya kazi za staha. Jumla ya Shilingi Bilioni 13.6 zilitengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu ambapo bajeti yake ni fedha za nje. Kamati ilijulishwa kuwa hadi kufikia Machi, 2023 mradi huu ulipokea shilingi bilioni 1.4. Shughuli zilizofanyika katika mradi huu ni kama inavyoonekana kwenye taarifa yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaona kuwa tija ya mradi huu bado haijaonekana kwa kuwa, bado upo katika hatua za awali, haujafikia idadi kubwa ya walengwa. Kamati ina maoni kuwa taasisi za umma, zinapaswa kuzingatia thamani halisi ya pesa inayopatikana kwa ajili ya utekelezaji wa miradi kwa hatua zinazofikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi Na. 6581 Programu ya Taifa ya Kukuza Ujuzi Nchini, kwa mwaka wa fedha 2022/2023 mradi huu ulitengewa jumla ya shilingi bilioni tisa fedha za ndani kwa ajili ya mafunzo ya ujuzi wa kujiajiri na stadi za kazi kwa vijana 9,775. Hadi kufikia Februari, 2023 programu hii ilikuwa imepokea shilingi bilioni 4.5 na ilitekeleza majukumu mbalimbali yakiwemo kama yanavyoonekana katika taarifa yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipata fursa ya kutembelea Kitalu Nyumba katika Halmashauri ya Wilaya ya Meru, unaotekelezwa chini ya mradi huu. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuwawezesha vijana kupata ujuzi wa kilimo na hatimaye kuweza kujiajiri, kujiingizia kipato na kuongeza uzalishaji wa chakula. Hata hivyo Kamati ilibaini kuwa upatikanaji wa vijana katika mradi huu haujazingatia makundi maalumu kama vile walemavu wenye uwezo wa kufanya kazi. Ni maoni ya Kamati kuwa Serikali ipeleke miradi hii kwenye kila Halmashauri ili kuwawezesha vijana wengi kupata fursa ya kupata ujuzi huo. Aidha, katika kuanzisha miradi hiyo ni vyema miradi hii ikaanzishwa sehemu ambazo ni oevu au kuchimba visima ili kupunguza gharama za uendeshaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile udadisi wa Kamati ulidhihirisha kuwa vijana wanaonufaika na mafunzo hayo hupata ujuzi wenye manufaa, lakini inakuwa vigumu kwa ujuzi huo kuwasaidia katika maisha halisi. Sababu ya ugumu ni ukosefu wa maeneo ya kuanzisha miradi hiyo na ukosefu wa mitaji kwa kuwa gharama ya kujenga vitalu nyumba ni

kubwa. Kwa maoni ya Kamati, hali hiyo isipofanyiwa kazi, programu ya kukuza ujuzi nchini halitakuwa na tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika marekebisho na ujenzi wa vyuo vya watu wenye ulemavu, kwa mwaka wa fedha 2022/2023 mradi huu ulitengewa jumla ya shilingi bilioni tatu kwa ajili ya ujenzi wa vyuo vitatu vya watu wenye ulemavu katika Mikoa ya Mwanza, Kigoma na Songwe. Hata hivyo hadi kufikia Februari, 2023 Ofisi ya Waziri Mkuu, (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye ulemavu) ilikuwa haijapokea fedha yoyote ya utekelezaji wa mradi huu. Kamati inaishauri Serikali kutoa fedha za mradi huu kwa wakati ili kuwawezesha kuanza ujenzi wa vituo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi Na. 5441 ambao ni wa Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO-19, umewezesha kufanya ukarabati wa vyuo vinne vya Ufundi Stadi na umegharimu kiasi cha shilingi bilioni 3.46. Ukarabati huu umewezesha vyuo vilivyokuwa vimefungwa kufunguliwa na kutoa mafunzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 15 Machi, 2023 Kamati ilipata fursa ya kutembelea Chuo cha Ufundi Stadi cha Watu wenye Ulemavu na Marekebisho Masiwani Tanga. Kamati ilielezwa kuwa Chuo hiki kilifanyiwa ukarabati ambao uliwezesha kufunguliwa tena kwa chuo baada ya kuwa kimefungwa kwa takribani miaka 12 kutokana na uchakavu wa miundombinu na ukosefu wa fedha za uendeshaji. Ni rai ya Kamati kuwa Serikali itenge fedha za kutosha ili kuendesha chuo hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi Na. 4952 Mfuko wa Maendeleo ya Vijana kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 mradi huu ulitengewa jumla ya shilingi bilioni moja, fedha za ndani kwa ajili ya kutoa mikopo kwa vijana. Hadi kufikia Februari, 2023, hakuna fedha ya maendeleo iliyopokelewa katika mradi huu. Uchambuzi wa Kamati unaonesha kuwa

katika kipindi cha miaka kuanzia 2015/2016 hadi 2020/2021 Ofisi ya Waziri Mkuu, (Kazi, Ajira na Watu wenye Ulemavu) lilitengewa jumla ya shilingi bilioni tano lakini katika kipindi hicho imepokea shilingi bilioni moja tu sawa na asilimia 20 tu ya fedha zilizotengwa kwa kipindi hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni rai ya Kamati kuwa Serikali ione umuhimu wa kutoa fedha katika mradi huu ili kuwawezesha vijana wengi kufanya shughuli za uzalishaji hivyo kupunguza ombwe la vijana wasio na ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utekelezaji wa maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati, naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba kwa sehemu kubwa utekelezaji wa maoni ya Kamati unaridhisha na kwamba baadhi ya maeneo Ofisi inaendelea na utekelezaji wa ushauri huo wa Kamati kwa kuwa utekelezaji wake ni endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niende kwenye uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa maduhuli, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Ofisi ya Waziri Mkuu - Fungu 65 inaomba kuidhinishiwa kukusanya jumla ya shilingi bilioni 46.5 ikilinganishwa na shilingi bilioni 45 katika mwaka wa fedha 2022/2023. Makadirio yameongezeka kwa Shilingi bilioni 1.5 sawa na asilimia 3.34 ukilinganisha na makadirio ya makusanyo ya maduhuli kwa mwaka unaoisha. Mchanganuo wa lengo la kukusanya kwa Fungu 65 unaonekana katika Jedwali Na. 5.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ina maoni kuwa, pamoja na nia njema ya kuongeza makusanyo ya Wizara ni vema Serikali izingatie na kufanyia kazi changamoto zilizosababisha makusanyo kuwa chini ya lengo na kuzingatia uhalisia katika kupanga makisio.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uchambuzi wa matumizi ya kawaida, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Ofisi ya Waziri Mkuu - Fungu 65 inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 19.9 ikiwa ni fedha za matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 7.1 ni mishahara, shilingi bilioni tatu ni ruzuku na shilingi bilioni 9.1 ni matumizi mengineyo (OC). Kiasi hicho ni ongezeko la asilimia 25 ikilinganishwa na bajeti kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ambapo iliidhinishiwa shilingi bilioni 15.9 kama vile ilivyochanganuliwa katika jedwali Na. 6.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Usuluhishi na Uamuzi Fungu 15 imekadiriwa kutumia kiasi cha shilingi bilioni 5.8 sawa na ongezeko la asilimia 11 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2022/2023. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 2.6 ni kwa ajili ya mishahara sawa na asilimia 12.2 na shilingi bilioni 2.5 kwa matumizi mengineyo sawa na asilimia 31. Mgawanyo wa fedha za matumizi kwa mwaka 2022/2023 ni kama inavyoonekana katika jedwali Na. 7.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza fedha za matumizi ya kawaida hususan katika matumizi mengineyo ambayo itawezesha utekelezaji wa majukumu na vipaumbele walivyojiwekea.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa makadirio ya matumizi kwa ajili ya miradi ya maendeleo katika mwaka wa fedha 2023/2024, Ofisi ya Waziri Mkuu – Fungu 65 imetengewa jumla ya shilingi bilioni 14.7 kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 13 ni fedha za ndani, na shilingi bilioni 1.7 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya maendeleo katika mwaka wa fedha 2023/2024 imepungua kwa takribani shilingi bilioni 11.9 zikiwa ni fedha za nje sawa na asilimia 44.6 ukilinganisha na bajeti ya mwaka wa fedha unaoishia. Mchanganuo ni kama vile unavyooneshwa Jedwali Na. 8.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na uchambuzi huo, Kamati ilibaini kuwa bajeti ya fedha za nje za maendeleo katika mwaka wa fedha 2023/2024 zimepungua kwa asilimia 44.6 ikilinganishwa na mwaka wa fedha unaoisha. Kamati ilihoji sababu ya kupungua kwa bajeti hiyo ambapo ilielezwa kuwa imetokana na mwenendo wa upatikanaji wa fedha hizi toka kwa wadau umekuwa ni wa kusuasua ambapo katika mwaka wa fedha 2022/2023 ilitolewa kwa asilimia 11 tu ya fedha zilizokadiriwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuzingatia ushauri wa Kamati uliotolewa ambapo ulieleza kuwa utegemezi wa fedha za nje katika miradi ya maendeleo unapaswa kupungua na ikiwezekana kuondokana na utegemezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inatoa maoni, ushauri na mapendekezo ya jumla kwa mafungu yote kama ifuatavyo:-

(i) Kutopatikana kwa wakati kwa fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo kunasababisha utekelezaji wa miradi hiyo kusuasua. Hivyo, Serikali ione umuhimu wa kutoa fedha za miradi ya maendeleo kwa wakati na kwa kiwango kilichokusudiwa ili kukidhi matarajio. Aidha, Serikali ijielekeze zaidi kwenye kutumia vyanzo vya ndani vya mapato katika kutekeleza miradi ya maendeleo kutokana na uzoefu kuwa upatikananaji wa fedha za nje ni wa kusuasua.

(ii) Mwenendo wa makusanyo ya maduhuli usioridhisha unaathiri lengo la makusanyo hayo na kupunguza ufanisi. Hivyo, Serikali iweke mikakati madhubuti ya kuhakikisha kuwa lengo la makusanyo ya maduhuli linafikiwa na makadirio ya makusanyo hayo yanaakisi uhalisia.

(iii) Katika kipindi cha miaka kuanzia 2015/2016 hadi 2020/2021 Ofisi ya Waziri Mkuu - Fungu 65 lilitengewa jumla ya shilingi bilioni tano lakini katika kipindi hicho imepokea shilingi bilioni moja tu sawa na asilimia 20 ya fedha zilizotengwa kwa kipindi husika. Aidha, katika mwaka wa fedha 2022/2023 kiasi kilichotengwa ni Shilingi bilioni moja. Mpaka kufikia Februari, 2023 hakuna kiasi cha fedha kilichokuwa kimetolewa. Kamati inashauri kuwa Serikali itoe fedha kwa mwaka na kwa wakati na kuongeza kiasi cha mtaji cha mfuko huu ili kuongeza idadi ya vijana wanaopata mkopo kupitia mfuko huu ili waweze kupata mtaji wa kuanzisha shughuli za uchumi.

(iv) Kutorejeshwa kwa mikopo inayotolewa kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Vijana kunapelekea kutofikiwa lengo la kuendelea kukopesha vijana wengine. Serikali iweke mikakati madhubiti ya kuhakikisha kuwa fedha zinazokopeshwa zinarejeshwa kwa wakati ili kuhakikisha kwamba lengo la kukopesha vijana wengine linafanikiwa. Aidha, Serikali ihakikishe kuwa Mfuko huu unatangazwa ili kutoa fursa kwa vijana wengi zaidi kuwezeshwa kupitia mfuko huu.

(v) Serikali ihakikishe kwamba inaongeza bajeti ya kutosha ya Wakala wa Usalama na Afya Mahala pa Kazi *(OSHA)* ili waweze kuajiri watumishi wa kutosha kuweza kufanya kazi ya kuisaidia nchi katika maeneo la usalama wa wafanyakazi. Aidha, Serikali iangalie utaratibu bora wa kupunguza tozo kila wakati ili kuepuka uwezekano wa kupunguza uwezo wa taasisi wa kuboresha huduma hizo.

(vi) Kupelekwa kwa asilimia 33.9 tu ya fedha za matumizi ya kawaida katika Tume ya Usuluhishi na Uamuzi - Fungu 15, kumeathiri utekelezaji wa majukumu yake. Kamati inashauri kwamba Serikali ihakikishe inatoa

kwa wakati fedha za matumizi mengineyo ili kuziwezesha taasisi na idara za Serikali kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, mapokezi ya fedha za matumizi ya kawaida yanapaswa kuwa na uwiano katika mafungu haya mawili kwa sababu katika fedha hizo kuna mishahara ya watumishi na fedha za matumizi mengineyo ambazo hutumika kwa ajili ya uendeshaji wa kila siku wa taasisi husika.

(vii) Fedha zinazotengwa kwa ajili ya mafunzo ya watumishi zinaweza kusaidia kukuza weledi, kuongeza ufanisi na motisha kwa watumishi iwapo fedha hizo zitatolewa na kutumika inavyostahili. Serikali itumie fedha za mafunzo na matumizi mengineyo kuwapatia watumishi mafunzo ya ndani na nje ya nchi ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi.

(viii) Kamati ilibaini kuwa mwenendo wa fedha za bajeti ya utekelezaji wa programu ya kukuza ujuzi nchini umekuwa ukishuka kutoka shilingi bilioni 18 mwaka 2019/2020 hadi kufikia shilingi bilioni 9 mwaka 2023/2024 na kusababisha kushuka kwa vijana wanufaika kutoka wastani wa vijana 42,000 hadi 12,000. Kamati inashauri kuwa Serikali iongeze bajeti ya programu hii ili kufikia malengo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa kwa jumla ya vijana 681,000 wanaotakiwa kupatiwa mafunzo ya ujuzi katika kipindi cha miaka mitano.

(ix) Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, ihakikishe kwamba inachangamkia fursa za ajira zinazopatikana katika nchi nyingine. Aidha, Serikali iweke mifumo thabiti ya kuhakikisha kwamba Watanzania wanaopata fursa ya ajira hizo, haki zao za msingi na kisheria zinalindwa ikiwemo uhifadhi wa

utu wao. Vilevile Serikali ifanye tafiti za kujua madhara yanayoweza kuambatana na ajira hizo ili kupima iwapo kuna ulazima kwa wananchi wake kwenda kufanya kazi nje ya nchi. Halikadhalika, Serikali iandae Kanzi Data *(Data Base)* ili kujua idadi ya Watanzania wanaofanya kazi nje ya Nchi.

(x) Kamati ilibaini kuwa fedha zilizotengwa kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa Vyuo vya Ufundi Stadi na Marekebisho kwa Watu wenye Ulemavu hazikutolewa hadi kufikia mwezi Februari, 2023 hivyo kukwamisha utekelezaji wa mradi huu. Kamati inashauri kuwa fedha zinazotengwa kwa ajili ya ukarabati wa vyuo hivi zitolewe kwa ukamilifu na…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa malizia, muda wako umekwisha. Nenda kwenye hitimisho.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha taarifa hii. Aidha, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao yaingie kwenye kumbukumbu za kudumu za Bunge kama yalivyowasilishwa katika taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Prof. Joyce Ndalichako, Mbunge na Waziri wa Ofisi ya Waziri Mkuu, (Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu); na Naibu Waziri, Mheshimiwa Paschal Katambi, Mbunge kwa

kuwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya ofisi yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niwashukuru watendaji wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu, (Kazi, Vijana na Watu wenye Ulemavu) pamoja na taasisi zake kwa ushirikiano walioipatia Kamati wakiongozwa na Katibu Mkuu Prof. Jamal Adam Katundu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Nenelwa Mwihambi, *ndc* kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na Bunge kwa mujibu wa Katiba ya Nchi. Aidha, nawashukuru Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Michael Chikokoto, Mkurugenzi Msaidizi; Ndugu Gerald Magili na Makatibu wa Kamati, Bi. Aziza Waziri Kheir, Bi. Rehema Lazarus pamoja na Bi. Jane Ndulesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu) kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

**5 APRILI, 2023**

# TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA WAZIRI MKUU KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 – KAMA IILIVYOWASILISHWA MEZANI

## SEHEMU YA KWANZA

### 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Awali

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa **Kanuni ya 118 (9)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu Tano kama ifuatavyo: -

a) Sehemu ya Kwanza inatoa maelezo ya jumla kuonesha msingi na Muundo wa Taarifa pamoja na namna Kamati ilivyofanya kazi;

b) Sehemu ya Pili ni uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti wa Ofisi hii kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023;

c) Sehemu ya Tatu ni uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/2024;

d) Sehemu ya Nne inahusu maoni na ushauri wa Kamati; na

e) Sehemu ya Tano ni hitimisho.

### 1.2 Msingi wa Uchambuzi wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, Msingi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu ni Masharti ya Kanuni za Bunge. Kanuni ya 6 (5)(a) ikisomwa kwa pamoja na Kanuni ya 7 (1)(a) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, zinaipa Kamati jukumu la kufanya uchambuzi wa Bajeti na Makadirio ya ofisi hii.

Aidha, Kanuni ya 117 (4) ya Kanuni za Bunge imeweka masharti yanayotaka Taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya Ofisi hii kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni. Naomba Bunge lako tukufu liijadili hoja ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu pamoja na Taarifa hii.

### 1.3 Mawanda ya Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika,** Katika kusimamia masuala ya kibajeti, Kamati imechambua **Fungu 65** ambalo ni Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu na **Fungu 15** ambalo ni Tume ya Usuluhishi na Uamuzi. Uchambuzi huu ulifanyika baada ya Kamati kufanya ziara za kujiridhisha na hali halisi ilivyo katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo chini ya mafungu yaliyotajwa hapo juu.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI NA TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

### 2.1 Ufafanuzi wa Jumla

**Mheshimiwa Spika,** matokeo ya uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi

yanaweka msingi wa ushauri wa Kamati kuhusu Hoja hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu. Uchambuzi wa Kamati ulijielekeza katika mambo makuu manne yafuatayo;-

(a) Makusanyo ya maduhuli;
(b) Mwenendo wa Upatikanaji wa fedha za Bajeti ya kawaida;
(c) Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo; na
(d) Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati Bungeni.

## 2.2 Uchambuzi wa Makusanyo ya Maduhuli

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa Fedha 2022/2023**,** Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu ililenga kukusanya maduhuli ya jumla ya **Shilingi 45,000,000,000**.

Hadi kufikia Mwezi Februari, 2023 Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Wenye Ulemavu ilikuwa imekusanya **Shilingi 20,446,311,268.40** sawa na **Asilimia 45.21** ya malengo yaliyokusudiwa. Vyanzo vya makusanyo hayo ni Ada za Vibali vya Ajira za Wageni **Shilingi 20,373,631,268,** Ada za Wakala Binafsi wa Huduma za Ajira **Shilingi 37,000,000,** Pango la Mnara wa Simu Shilingi **17,930,000** na Ada za maombi ya kufanya kazi Nje ya Nchi Shilingi **4,600,000.** Mchanganuo wa makusanyo hayo unaonekena katika Jedwali Na. 1.

**Jedwali Na.1**
**Fungu 65- Makadirio na Makusanyo ya Maduhuli kwa mwaka wa Fedha 2022/2023**

| **MAKADIRIO NA MAKUSANYO 2022/2023** | | | |
|---|---|---|---|
| **Chanzo** | **Makadirio (tsh.)** | **Makusanyo (tsh.)** | **Asilimia** |
| Ada za Vibali vya ajira za Wageni | 42,550,630,595 | 20,428,561,268 | 47.88 |
| Ada za Wakala Binafsi | 174,000,000 | 37,000,000 | 21.26 |

| **MAKADIRIO NA MAKUSANYO 2022/2023** | | | |
|---|---|---|---|
| **Chanzo** | **Makadirio (tsh.)** | **Makusanyo (tsh.)** | **Asilimia** |
| wa Huduma za Ajira | | | |
| Uuzaji wa Nyaraka za Zabuni | 4,875,005 | 0 | 0 |
| Pango la Mnara wa Simu | 12,000,000 | 17,930,000 | 149.42 |
| Ada za Pango | 8,492,400 | 4,600,000 | 0 |
| Ada za Maombi ya kufanya kazi Nje ya Nchi | 1,725,000,000 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **45,000,000,000.** | **20,433,161,268.40** | **45.41** |

*Chanzo: Randama ya Bajeti ya 2022/2023 fungu 65*

**Mheshimiwa Spika,** katika mchanganuo huo, Kamati imebaini mambo yafuatayo;-

(a) Uchambuzi wa mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli unaonesha kuwa jumla ya **Shilingi 20,446,311,268.40** sawa na **asilimia 45.44** ya makusanyo yote ya Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu yalikusanywa katika kipindi hicho.

(b) Hadi kufikia Mwezi Februari,2023 Ofisi hii ilikuwa imekusanya asilimia 45.44 ya lengo; ingawa kwa kipindi hicho ilitarajiwa angalau wawe wamefikia **asilimia 65** ya lengo.

**Mhesimiwa Spika**, kutokana na uchambuzi uliofanyika, Kamati ina maoni kuwa mwenendo wa makusanyo kwa Mwaka huu si wa kuridhisha kwani kiujumla wameweza kukusanya **asilimia 45.44** tu. Kamati ilihoji sababu za makusanyo kuwa madogo kwenye baadhi ya vyanzo vya

mapato ambapo ilielezwa kuwa makusanyo madogo toka kwenye Ada za kufanya Kazi Nje ya Nchi ni kutokana na kutokuwepo kwa mfumo maalumu wa kukusanya fedha za kigeni kutoka kwa waajiri nje ya nchi na kutokamilika kwa mikataba na Waajiri wa Nje ya Nchi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwenendo huu si rahisi kufikia lengo la makusanyo katika kipindi kilichobaki kumaliza mwaka wa fedha 2022/2023 hivyo kuathiri utekelezaji wa malengo yaliyowekwa. Ni rai ya Kamati kuwa Serikali ipange makadirio ya makusanyo kwa kuzingatia uhalisia katika Mwaka wa Fedha 2023/2024. Aidha, uwekwe mfumo madhubuti wa kukusanya fedha za kigeni kutoka kwa waajiri nje ya nchi ili kuhakikisha usimamizi na ukusanyaji wa maduhuli hayo unafanyika kwa ukamilifu.

## 2.3 Uchambuzi wa Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana Ajira na Wenye Ulemavu iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 15,911,037,000** kwa matumizi ya kawaida. Kati ya Fedha hizo **Shilingi 7,084,636,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, **Shilingi 5,880,648,761** kwa ajili ya mishahara na **Shilingi 2,945,752,239** kwa ajili ya ruzuku ya mshahara kwa Wakala wa Afya na Usalama mahala pa kazi (OSHA).

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Februari, 2023 Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu ilipokea jumla **Shilingi 9,503,975,865.53** sawa na **asilimia 59.73** ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo **Shilingi 3,629,417,630.13** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, **Shilingi 4,025,264,907.40** kwa ajili ya mishahara na **Shilingi 1,849,293,328.00** kwa ajili ya ruzuku ya mshahara kwa Wakala wa Afya na Usalama mahala pa kazi (OSHA). Mchanganuo wa fedha hizo ni kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 2.

**Jedwali Na.2**
**Fungu 65- Mapokezi ya Fedha za Matumizi ya Kawaida 2022/2023**

| MAPOKEZI YA FEDHA ZA MATUMIZI YA KAWAIDA 2022/2023 | | | |
|---|---|---|---|
| **Matumizi** | **Fedha iliyotengwa 2022/2023** | **Fedha ziliyopokelewa** | **Asilimia ya mapokezi** |
| Mishahara | 5,880,648,761 | 4,025,264,907.40 | 68.44 |
| Oc | 7,084,636,000 | 3,629,417,630.13 | 51.22 |
| Ruzuku ya mshahara (OSHA) | 2,945,752,239 | 1,849,293,328.00 | 62.77 |
| **Jumla** | **15,911,037,000** | | **59.73** |

***Chanzo:*** *Randama ya Bajeti 2022/2023 Fungu 65*

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa upatikanaji wa fedha hizo unaonesha kwamba kwa ujumla, Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu (**Fungu 65)** imepokea jumla ya **Shilingi 9,503,975,865.53** sawa na **asilimia 59.73** ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi ya kwaida.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande **Fungu 15** wa Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA) iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 4,294,213,000.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo kiasi cha **Shilingi 2,374,063,000** ni kwa ajili ya mishahara na **Shilingi 1,920,150,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Februari 2023, Tume ilikuwa imepokea kiasi cha **Shilingi 1,459,637,347.56** sawa na **asilimia 33.9** Mchanganuo wa Fedha zilizopokelewa hadi Februari, 2023 ni kama unavyoonekana katika **Jedwali Na.3**

**Jedwali 3**
**Fungu 15- Mapokezi ya Fedha za Matumizi ya Kawaida 2022/2023**

| MAPOKEZI YA FEDHA ZA MATUMIZI YA KAWAIDA 2022/2023 | | | |
|---|---|---|---|
| **Matumizi** | **Fedha iliyotengwa 2022/2023** | **Fedha ziliyopokelewa** | **Asilimia ya mapokezi** |
| Mishahara | 2,374,063,000 | 864,237,400.00 | 36.4 |
| Oc | 1,920,150,000 | 595,399,947.56 | 31 |
| Jumla | 4,294,213,000.00 | 1,459,637,347.56 | 33.9 |

***Chanzo:*** *Randama ya Bajeti 2022/2023 Fungu 15*

**Mheshimiwa Spika,** katika uchambuzi kuhusu mwenendo wa bajeti ya matumizi ya kawaida kwa Fungu 65 na 15 Kamati imebaini masuala yafuatayo;

(a) Mapokezi ya fedha za Matumizi ya kawaida kwa **Fungu 65** ni **asilimia 59.75** ya makadirio. Kiwango hiki kimepungua ikilinganishwa na mapokezi katika kipindi kama hicho katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 ambapo mapokezi yalikuwa **asilimia 69**. Mwenendo huu wa upatikananji wa fedha si wa kuridhisha hivyo kuathiri utekelezaji wa malengo yaliyokusudiwa.

(b) **Fungu 15** lililo chini ya Ofisi hii limepokea fedha pungufu za matumizi ya kawaida ukilinganisha na **Fungu 65** ambalo limepokea **asilimia 33.9** ya makadirio. Katika fedha hizo, fedha za mshahara ni **asilimia 36.4.** Kamati ilihoji ili kujua sababu ya fedha za mshahara kutolewa kwa kiwango kidogo ambapo Kamati ilielezwa kuwa imetokana na Watumishi wengi kuhamia kwenye Taasisi zingine.

**Mheshimiwa Spika,** ni maoni ya Kamati kuwa mapokezi ya fedha za matumizi ya kawaida yanapaswa kuwa na uwiano katika mafungu haya mawili kwa sababu katika fedha hizo kuna fedha za mishahara ya watumishi na fedha za matumizi

mengineyo ambazo hutumika kwa ajili ya uendeshaji wa kila siku wa taasisi husika. Mwenendo huu unaweza pia kuwa chanzo cha kuhama kwa watumishi jambo ambalo linaweza kuathiri utendaji kazi wa Ofisi.

## 2.4 Tathmini ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 Ofisi wa Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu ilitengewa jumla ya **Shilingi 26,656,389,000** kwa ajii ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 13,000,000,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 13,656,389,000** ni fedha za nje.

**Mheshiniwa Spika,** hadi kufikia Februari 2023 Ofisi imepokea kiasi cha **Shilingi 5,986,445,504.67**, sawa na **asilimia 22.45** ya fedha zote. Kati ya Fedha hizo **Shilingi 4,500,000,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 1,486,445,506.67** ni fedha za Nje. Mgawanyo wa fedha hizo umeainishwa katika **Jedwali Na. 4.**

**Jedwali Na.4 Fungu 65-Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha 2022/2023**

| MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA 2022/2023 | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Namba na jina la mradi | Bajeti iliyotengwa 2022/2023 | | Mapokezi ya fedha hadi kufikia marchi 2023 | | Asilimia ya mapokezi |
| | Fedha za ndani | Fedha za nje | fedha za ndani | fedha za nje | |
| Na. 6205: Programu ya Kukuza Kazi za Staha Nchini | 0.00 | 13,656,389,000 | | 1,486,445,506.65 | 11 |
| Na. 6581: Programu ya Kukuza Ujuzi Nchini | 9,000,000,000 | 0.00 | 4,500,000,000.00 | | 50 |
| NA.4954 ujenzi wa vituo vya Ufundi na | 3,000,000,000 | | 0.0 | | 0 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Ukarabati wa watu wenye ulemavu | | | | | |
| Na. 4952: Mfuko wa Maendeleo ya Vijana | 1,000,000,000 | 0.00 | 0.0 | | 0 |
| **Jumla Kuu** | **13,000,000,000** | **13,656,389,000** | **4,500,000,000** | **1,486,445,506.67** | |

***Chanzo.*** *Randama ya Bajeti 2022/2023 Fungu 65*

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa **Fungu 25,** Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA) unatekeleza mradi mmoja wa mfumo wa Usimamizi wa Uendeshaji Mashauri (ECMS). Mradi huu uliidhinishiwa Shilingi 1,000,000,000. Hadi kufikia Februari 2023, Tume ilikuwa imepokea **Shilingi 300,000,000** sawa na **asilimia 30** ya fedha zilizoidhinishwa**.**

**Mheshimiwa Spika,** katika uchambuzi uliofanywa na Kamati umebaini mambo mbalimbali kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Maendeleo kama ifuatavyo;

(a) Kwa ujumla mapokezi ya fedha za nje yapo chini ya kiwango kilichotarajiwa kwa Fungu 65 ambapo ilipokea **asilimia 11** ya makadirio. Hali hii imeathiri utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyopangwa;

(b) Kamati imebaini kuwa mapokezi ya fedha za ndani katika **fungu 65** na **15** si wa kuridhisha ambapo imepokea **asilimia 40** na **30** mtawalia ya makadirio. Hali hii imekwamisha baadhI ya miradi kutekelezwa;

(c) Kamati pia imebaini kwamba, **Fungu 65** ilitengewa **Shilingi 3,000,000,000** kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa vituo vya ufundi vya watu wenye ulemavu na **Shilingi 1,000,000,000** kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Vijana (fedha za ndani). Hata hivyo hadi kufikia Februari 2023 hakuna fedha yoyote iliyopokelewa na Ofisi hiyo kutekeleza miradi husika. Ni maoni ya Kamati kuwa mwenendo huu

wa mapokezi ya fedha hauleti tija na unaweza kuathiri utekelezaji wa vipaumbele vya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kwamba, kati ya fedha zilizotengwa na kutolewa ili kutekeleza miradi hiyo, fedha za nje zilitolewa kwa **asilimia 11** ya makisio wakati fedha za ndani zilitolewa kwa **asilimia 40** ya fedha iliyotengwa. Ni maoni ya Kamati kwamba, mwenendo wa mapokezi wa fedha za nje na fedha za ndani uko chini. Kamati inaendelea kusisitiza Serikali kutoa kwa wakati fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kutumia fedha za ndani kwa kuwa mwenendo wa upatikanaji wa fedha za nje ni wa kusuasua.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitaka kujua sababu za kutolewa kidogo kwa fedha za Nje za Miradi ya Maendeleo ambapo ilijulishwa ni kutokana na ucheleweshaji kutoka kwa wadau wanaohusika. Kamati inashauri mawasiliano yaendelee kufanyika ili fedha hizo zitolewe kabla ya kumalizika kwa mwaka wa fedha hapo Juni, 2023 ili Miradi iliyopangwa kutekelezwa itekelezwe na kuwapatia wananchi huduma zilizokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,** jumla ya miradi Mitano ilitekelezwa na Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu. Kamati ilifuatilia na kuchambua utekelezaji wa miradi hiyo kama ifuatavyo: -

2.4.1 **Mradi Na. 6205 Programu ya Kukuza Kazi za Staha *(Decent Work Country Program)***

**Mheshimiwa Spika,** Mradi huu unahusu kukuza na kujenga stadi za Maisha kwa vijana kupitia programu ya kazi za staha. Jumla ya **Shilingi 13,656,389,000** zilitengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu ambapo bajeti yake ni fedha za nje. Kamati ilijulishwa kuwa, hadi kufikia Machi 2023, mradi ulipokea **Shilingi 1,486,445,506.67.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilijulishwa kuwa miongoni mwa kazi zilizofanyika ni kufanya tathmini na mapitio ya sera ya vijana ya 2007 na Sera ya Taifa ya Hifadhi ya Jamii. Kutoa mafunzo ya ufundi stadi katika fani mbalimbali kwa vijana 6,101, kutoa mafunzo ya afya za Uzazi, stadi za maisha, kilimo, biashara, ushirika na uundwaji wa vikundi na makampuni ya vijana, Utafiti na maboresho ya muongozo wa stadi za Maisha kwa vijana; na Mapitio ya programu ya kazi za staha.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaona kuwa tija ya mradi huu bado haijaonekana kwa kuwa bado upo katika hatua za awali na haujafikia idadi kubwa ya walengwa. Kamati ina maoni kuwa taasisi za umma, zinapaswa kuzingatia thamani halisi ya pesa inayopatikana kwa ajili ya utekelezaji wa miradi kwa hatua zinazofikiwa.

2.4.2 **Mradi Na. 6581 Programu ya Taifa ya Kukuza Ujuzi Nchini**

**Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 mradi huu ulitengewa jumla ya **Shilingi 9,000,000,000** (Fedha za Ndani) kwa ajili ya Mafunzo ya ujuzi wa kujiajiri na stadi za kazi kwa vijana 9,775. Hadi kufikia Februari, 2023 programu hii ilikuwa imepokea **Shilingi 4,500,000,000** na ilitekeleza majukumu mbalimbali yakiwemo yafuatayo: -

a) Kuwezesha vijana 11,973 kupata mafunzo ya kukuza ujuzi katika fani mbalimbali.

b) Kuwezesha Wahitimu 1,704 kupata mafunzo ya uzoefu wa kazi,

c) Kufadhili vijana 200 kupata mafunzo ya ufugaji samaki,

d) Kufadhili vijana 234 kupata mafunzo ya kunenepesha mifugo; na

e) Kufadhili vijana 74 kupata mafunzo ya kuweza kushiriki kilimo cha vizimba.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipata fursa ya kutembelea Kitalu Nyumba katika Halmashauri ya Wilaya ya Meru, unaotekelezwa chini ya mradi huu. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuwawezesha vijana kupata ujuzi wa kilimo na hatimaye kuweza kujiajiri, kujiingizia kipato na kuongeza uzalishaji wa chakula. Hata hivyo Kamati ilibaini kuwa upatikanaji wa vijana katika mradi huu haujazingatia makundi maalumu kama vile walemavu wenye uwezo wa kufanya kazi. Ni maoni ya kamati kuwa Serikali ipeleke miradi hii kwenye kila Halmashauri ili kuwawezesha vijana wengi kupata fursa ya kupata ujuzi huo. Aidha, katika kuanzisha miradi hiyo ni vyema miradi hii ikaanzishwa sehemu ambazo ni oevu au kuchimba visima ili kupunguza gharama za uendeshaji.

Vilevile udadisi wa Kamati ulidhihirisha kuwa vijana wanaonufaika na mafunzo haya hupata ujuzi wenye manufaa, lakini inakuwa vigumu kwa ujuzi huo kuwasaidia katika Maisha halisi. Sababu ya ugumu ni ukosefu wa maeneo ya kuanzisha miradi hiyo na ukosefu wa mitaji kwa kuwa gharama ya kujenga vitalu nyumba ni kubwa. Kwa maoni ya Kamati, hali hiyo isipofanyiwa kazi, programu ya kukuza ujuzi nchini halitakuwa na tija.

### 2.4.3 Marekebisho na Ujenzi wa Vyuo vya Watu Wenye Ulemavu.

**Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 mradi huu ulitengewa jumla ya **Shilingi 3,000,000,000** kwa ajili ya ujenzi wa vyuo Vitatu vya watu wenye ulemavu katika Mikoa ya Mwanza, Kigoma na Songwe. Hata hivyo hadi kufikia Februari 2023 Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye ulemavu ilikuwa haijapokea fedha yoyote ya utekelezaji wa mradi huu. Kamati inaishauri Serikali kutoa

fedha za mradi huu kwa wakati ili kuwezesha kuanza ujenzi wa vituo hivyo.

### 2.4.4 Mradi Na.5441 Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO-19

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu umewezesha kufanya ukarabati wa vyuo vinne vya Ufundi Stadi na Marekebisho ambavyo ni Luanzari- Tabora, Sabasaba- Singida, Mtapika Masasi -Mtwara na Yombo- Dar Es Salaam na umegharimu kiasi cha **Shilingi Bilioni 3.46** Ukarabati huu umewezesha vyuo vilivyokuwa vimefungwa kufunguliwa na kuanza kutoa mafunzo.

**Mheshimiwa Spika**, Tarehe 15 Machi 2023 kamati ilipata fursa ya kutembelea Chuo cha Ufundi Stadi cha Watu wenye Ulemavu na Marekebisho Masiwani Tanga. Kamati ilielezwa kuwa Chuo hiki kilifanyiwa ukarabati ambapo ukarabati huo ulihusisha ukarabti wa majengo ya ofisi, madarasa (2), vyoo (7), mabafu (3), mabweni (4), nyumba ya mtumishi (1) na kibanda cha mlinzi.

Awamu ya Pili ya ukarabati ilihusisha jengo la karakana lenye jiko na bwalo la chakula pamoja na uzio. Ukarabati huo uliwezesha kufunguliwa tena kwa chuo baada ya kuwa kimefungwa takribani miaka kumi na mbili kutokana na uchakavu wa miundombinu na ukosefu wa fedha za uendeshaji. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kukarabati chuo hiki ambapo kinatoa ujuzi wa kuwawezesha watu wenye ulemavu kupata kipato. Ni rai ya Kamati kuwa Serikali itenge fedha za kutosha ili kuendesha chuo hiki.

### 2.4.5 Mradi Na. 4952 Mfuko wa Maendeleo ya Vijana

**Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 mradi huu ulitengewa jumla ya **Shilingi 1,000,000,000 (fedha za**

**ndani)** kwa ajili ya kutoa mikopo kwa vijana, Kuratibu mafunzo ya ujasiriamali na usimamizi wa biashara kwa vikundi vya vijana vya uzalishaji mali na Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya miradi iliyowezeshwa kupitia mfuko wa maendeleo ya vijana.

**Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Februari 2023, hakuna fedha ya maendeleo iliyopokelewa katika mradi huu. Uchambuzi wa kamati unaonesha kuwa katika kipindi cha miaka kuanzia Mwaka 2015/2016 hadi 2020/2021 Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Wenye Ulemavu lilitengewa jumla ya **Shilingi 5,000,000,000;** lakini katika kipindi hicho imepokea **Shilingi 1,000,000,000** sawa na **asilimia 20** tu ya fedha zilizotengwa kwa kipindi husika. Aidha Kamati ilijulishwa kuwa katika kipindi cha Julai hadi Februari 2023 mikopo yenye thamani ya Shilingi 1,879,931,992 ambazo ni fedha za mradi wa mfuko (Revolving Fund) ilitolewa kwa ajili ya kuwezesha miradi 85 inayomilikiwa na vijana 406 katika Sekta ya kilimo, viwanda, biashara na makampuni katika Halmashauri 28 ili kuwezesha kufanya shughuli za uzalishaji mali.

**Mheshimiwa Spika**, ni rai ya Kamati kuwa Serikali ione umuhimu wa kutoa fedha katika mradi huu ili kuwawezesha vijana wengi kufanya shughuli za uzalishaji hivyo kupunguza ombwe la vijana wasio na ajira. Aidha Kamati ilibaini kuwa kwa kiasi kikubwa mfuko huu haufahamiki kwa wengi hivyo ni vyema Serikali ikautangaza mfuko huu ili uwafikie wanufaika wengi zaidi.

### 2.5 Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Kamati ilitoa maoni, ushauri na mapendekezo mbalimbali ili kuboresha utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi hii. Naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kwamba

kwa sehemu kubwa utekelezaji unaridhisha na kwa baadhi ya maeneo Ofisi inaendelea na utekelezaji wa ushauri huo wa Kamati kwa kuwa utekelezaji wake ni endelevu. Masuala ambayo utekelezaji wake unaendelea kwa upande mwingine ushauri ambao haujazingatiwa ni wa Serikali kuona umuhimu wa kuongeza Bajeti ya Mfuko wa Maendeleo ya Vijana katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 ili mfuko uweze kuwafikia vijana wengi. Bajeti hii haikuongezwa na hata katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 bado mapendekezo ya Bajeti ni Shilingi 1,000,000,000. Kutokana na changamoto ya ajira kwa Vijana ni vema Serikali ikaongeza fedha hizi mpka kufikia Shilingi 3,000,000,000

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

### 3.1 Maduhuli

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu, inaomba kuidhinishiwa kukusanya jumla ya Shilingi **46,505,749,995** ikilinganishwa na **Shilingi. 45,000,000,000** katika Mwaka wa Fedha 2022/2023. Makadirio yameongezeka kwa **Shilingi 1,505,749,995** sawa na **asilimia 3.34** ukilinganisha na makadirio ya makusanyo ya maduhuli kwa mwaka unaoisha.
Fedha hizi zinatarajiwa kukusanywa kutoka katika ada za maombi ya Vibali vya Kazi kwa Wageni, Malipo ya Usajili wa Wakala Binafsi wa Huduma za Ajira nchini, Ada za maombi ya kufanya Kazi nje ya Nchi na kodi ya mnara wa mawasiliano. Mchanganuo wa lengo la kukusanya kwa Fungu 65 unaonekana katika **Jedwali Na.5** hapa chini.

**Jedwali Na 5**
**Fungu 65-Ulinganisho wa Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 na 2023/2024**

| MAKADIRIO NA MAKUSANYO KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 NA 2023/2024 | | | |
|---|---|---|---|
| **Maelezo** | **2022/2023 (Tsh.)** | **2023/2024 (Tsh.)** | **Asilimia/Pungufu au ongezeko** |
| Ada za Vibali vya ajira za Wageni | 42,550,630,595 | 43,975,630,595 | 3.34 |
| Ada za Wakala Binafsi wa Huduma za Ajira | 174,000,000 | 175,000,000 | 0.57 |
| Uuzaji wa Nyaraka za Zabuni | 4,875,005 | 4,625,000 | 0.9 |
| Pango la Mnara wa Simu | 12,000,000 | 12,000,000 | 0 |
| Ada za Pango | 8,492,400 | 8,492,400 | 0 |
| Ada za Maombi ya kufanya kazi Nje ya Nchi. | 2,250,000,000 | 2,330,000,000 | 3.35 |
| **Jumla** | **45,000,000,000.** | **46,505,749,995** | **3.34** |

*Chanzo: Randama ya Bajeti ya 2022/2023 Fungu 65.*

Mheshimiwa Spika, kutokana na uchambuzi huo, Kamati imebaini mambo yafuatayo;

(a) Makadirio ya makusanyo kwa mwaka wa fedha 2022/2023 yameongezeka kwa shilingi 1,505,749,995 sawa na ongezeko la asilimia 3.34;

(b) Ongezeko kubwa la maduhuli linatarajiwa kutoka makusanyo ya ada za Vibali vya Ajira kwa Wageni kwa **shilingi 1,425,000,000** sawa na **asilimia 3.34.**

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Kamati unaonyesha kuwa kutokana na mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 kufikia **asilimia 40** tu hadi kufikia kipindi cha robo tatu ya muda wa lengo. Kamati haioni uwezekano wa kufikia lengo la makusanyo ililowekwa kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, kwa kuzingatia uzoefu wa makusanyo ya Mwaka uliotangulia.

**Mheshimiwa Spika,** kwa uchambuzi huo, Kamati ina maoni kuwa, pamoja na nia njema ya kuongeza makusanyo ya Wizara ni vema Serikali izingatie na kufanyia kazi changamoto zilizosababisha makusanyo kuwa chini ya lengo na kuzingatia uhalisia katika kupanga makisio hayo.

### 3.2 Uchambuzi wa Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu **Fungu 65** inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 19,920,510,000** ikiwa ni Fedha za Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shlingi 7,180,664,682.06** ni mishahara, **Shilingi 3,600,977,317.94** ni ruzuku na **Shlingi 9,138,868,000** ni matumizi mengineyo (OC). Kiasi hicho ni ongezeko la **asilimia 25** ikilinganishwa na bajeti kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ambapo iliidhinishiwa **Shilingi 15,911,036,999.58** kati ya Fedha hizo **Shilingi 7,084,636,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, **Shilingi 5,880,648,761** kwa ajili ya mishahara na **Shilingi 2,945,752,239** kwa ajili ya ruzuku ya mshahara kwa Wakala wa Afya na Usalama mahali pa kazi (OSHA) kama ilivyochanganuliwa katika Jedwali Na. 6

**Jedwali Na.6**
**Fungu 65- Ulinganisho wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 na 2023/2024**

| ULINGANISHO WA BAJETI FUNGU 65 KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 NA 2023/2024 | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **MATUMIZI** | **2022/2023 (Tsh.)** | **2023/2024 (Tsh.)** | **Ongezeko/ pungufu (tsh.)** | **Ongezeko/ pungufu (tsh.)** |
| Mishahara | 5,880,648,761 | 7,180,664,682 | 1,300,015,921.06 | 22.1 |
| OC | 7,084,636,000 | 9,138,868,000 | 2,054,232,000 | 28 |
| Ruzuku | 2,945,752,239 | 3,600,977,317 | 655,225,078.94 | 22 |
| **Jumla** | **15,911,037,000** | **19,920,510,000** | **4,009,473,000** | **25** |

*Chanzo: Randama ya Bajeti 2023/2024 Fungu 65*

**Mheshimiwa Spika,** Tume ya Usuluhishi na Uamuzi **Fungu 15** imekadiriwa kutumia kiasi cha **Shilingi 5,881,056,000** sawa na ongezeko la **asilimia 11** Ikilinganishwa na Bajeti ya Mwaka 2022/2023. Kati ya Fedha hizo **Shilingi 2,664,898,000** ni kwa ajili ya Mishahara sawa na **asilimia 12.2** na **Shilingi 2,516,158,000** kwa matumizi mengineyo sawa na **asilimia 31.** Mgawanyo wa fedha za matumizi kwa Mwaka 2022/2023 ni kama inavyoonekana kwenye jedwali Na.7

**Jedwali Na.7**
**Fungu 15- Ulinganisho wa Makadirio ya Matumizi ya Kawaida**

| ULINGANISHO WA BAJETI FUNGU 15 KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 NA 2023/2024 | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **MATUMIZI** | **2022/2023 (Tsh.)** | **2023/2024 (Tsh.)** | **Ongezeko/ pungufu (tsh.)** | **Ongezeko/ pungufu (tsh.)** |
| Mishahara | 2,374,063,000 | 2,664,898,000 | 290,835,000 | 12.2 |
| OC | 1,920,150,000 | 2,516,158,000 | 596,008,000 | 31 |
| **Jumla** | **5,294,213,000** | **5,881,056,000** | **586,843,000** | 11 |

***Chanzo.*** *Randama ya Bajeti 2023/2024 Fungu 15*

**Mheshimiwa Spika**, Katika Uchambuzi huo, Kamati imebaini masuala yafuatayo;

(a) **Fungu 65** Bajeti ya Matumizi ya Kawaida katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 imeongezeka kwa **asilimia 25** ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha unaoisha ambapo bajeti ya Matumizi ya kawaida ilikuwa **Sh. 15,911,037,000**. Kamati imebaini kwamba, moja kati ya sababu ya ongezeko ni kutokana na kuongezeka kwa Watumishi waliohamishiwa na kuajiriwa katika Ofisi hii. Aidha, ongezeko hilo linaakisi mahitaji ya kifedha kulingana na ongezeko la viwango vya posho ya kujikimu na posho ya masaa ya ziada na pia sababu mbalimbali za kiuchumi ikiwemo kupanda bei kwa bidhaa na huduma.

(b) **Fungu 15** Bajeti ya Matumizi ya Kawaida katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 imeongezeka kwa **asilimia 11** ukilinganisha na Mwaka wa Fedha unaoisha, ambapo bajeti ya matumizi ya Kawaida ilikuwa **Shilingi 5,294,213,000.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza fedha za Matumizi ya Kawaida hususani katika Matumizi Mengineyo ambayo itawezesha utekelezaji wa majukumu na vipaumbele walivyojiwekea.

### 3.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, imetengewa jumla ya **Shilingi 14,749,713,680** kwa ajili ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 13,000,000,000.** ni fedha za ndani, na **Shilingi 1,749,713,680** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika**, bajeti ya maendeleo katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 imepungua kwa takriban **shilingi 11,906,675,320** zikiwa ni Fedha za Nje sawa na **asilimia 44.66**

ukilinganisha na bajeti ya Mwaka wa Fedha unaoisha. Mchanganuo ni kama unavyoonekana katika Jedwali Na. 8.

**Jedwali Na.8**
**Fungu 65- Ulinganisho wa Bajeti ya Fedha za Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 na 2023/2024**

| ULINGANISHO WA FEDHA ZA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA 2022/2023/ 2023/2024 | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NAMBA NA JINA LA MRADI** | **MAKADIRIO KWA MWAKA 2022/2023** | | **MAKADIRIO KWA MWAKA 2023/2024** | |
| | **Fedha za ndani** | **Fedha za nje** | **Fedha za ndani** | **Fedha za nje** |
| Na. 6205: Programu ya Kukuza Kazi za Staha Nchini | 0.00 | 13,656,389,000 | | 1,334,936,275 |
| Na. 6581: Programu ya Kukuza Ujuzi Nchini | 9,000,000,000 | 0.00 | 9,000,000,0000 | |
| Na.4954 ujenzi wa vituo vya Watu wenye Ulemavu | 3,000,000,000 | | 3,000,000,000 | |
| Na. 4952: Mfuko wa Maendeleo ya Vijana | 1,000,000,000 | 0.00 | 1,000,000,000 | |
| **Jumla Kuu** | **13,000,000,000** | **13,656,389,000** | | |

***Chanzo.*** *Randama ya Bajeti 2023/2024 Fungu 65*

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na uchambuzi huo Kamati ilibaini kuwa Bajeti ya fedha za Nje za Maendeleo katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 zimepungua kwa **asilimia 44.66**

ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha unaoisha. Kamati ilihoji sababu ya kupungua kwa bajeti hiyo ambapo ilielezwa kuwa imetokana na mwenendo wa upatikanaji wa fedha hizi toka kwa wadau umekuwa ni wa kusuasua ambapo katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 ilitolewa kwa **asilimia 11** tu ya fedha zilizokadiriwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuzingatia ushauri wa Kamati uliotolewa ambapo ulieleza kuwa utegemezi wa Fedha za Nje katika Miradi ya Maendeleo unapaswa kupungua na ikiwezekana kuondokana na utegemezi huo.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 4.1 Maoni na Ushauri wa Jumla

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia majadiliano ya kina kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana Ajira na Wenye Ulemavu kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 Kamati inatoa maoni, ushauri na mapendekezo ya jumla kwa mafungu yote kama ifuatavyo: -

i) Kutopatikana kwa wakati kwa fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo kuna sababisha utekelezaji wa miradi hiyo kusuasua. Hivyo, serikali ione umuhimu wa kutoa fedha za miradi ya maendeleo kwa wakati na kwa kiwango kilichokusudiwa ili kukidhi matarajio. Aidha Serikali ijielekeze zaidi kwenye kutumia vyanzo vya ndani vya mapato katika kutekeleza miradi ya maendeleo kutokana na uzoefu kuwa upatikananaji wa fedha za nje ni wa kusuasua;

ii) Kamati ilibaini kuwa, makusanyo ya maduhuli katika mwaka unaoisha upo chini ya lengo ambapo hadi kufikia Februari 2022 Wizara ilikusanya kwa **asilimia 45.44** tu

pamoja na hali hiyo wizara imepanga kukusanya maduhuli kwa ongezeko la **asilimia 3.4** ukilinganisha na mwaka unaoisha. Mwenendo wa makusanyo ya maduhuli usioridhisha unaathiri lengo la makusanyo hayo na kupunguza ufanisi. Hivyo, Serikali iweke mikakati madhubuti ya kuhakikisha kuwa lengo la makusanyo ya maduhuli linafikiwa na makadirio ya makusanyo hayo yanaakisi uhalisia.

iii) Kamati ilibaini kuwa katika kipindi cha miaka kuanzia Mwaka 2015/2016 hadi 2020/2021 Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Wenye Ulemavu lilitengewa jumla ya **Shilingi 5,000,000,000;** lakini katika kipindi hicho imepokea **Shilingi 1,000,000,000** sawa na **asilimia 20** tu ya fedha zilizotengwa kwa kipindi husika. Aidha katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 kiasi kilichotengwa ni **Shilingi 1,000,000,000**, mpaka kufikia Februari 2023 hakuna kiasi cha fedha kilichokuwa kimetolewa. Kamati inashauri kuwa Serikali itoe fedha hizi kila mwaka na kwa wakati na kuongeza kiasi cha mtaji wa mfuko huu ili kuongeza idadi ya vijana wanaopata mkopo kupitia mfuko huu ili waweze kupata mtaji wa kuanzisha shughuli za uchumi.

iv) Kutorejeshwa kwa mikopo inayotolewa kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Vijana kunapelekea kutofikiwa lengo la kuendelea kukopesha vijana wengine. Serikali iweke mikakati madhubiti ya kuhakikisha kuwa fedha zinazokopeshwa zinarejeshwa kwa wakati ili kuhakikisha kwamba lengo la kukopesha vijana wengi linafikiwa. Aidha Serikali ihakikishe kuwa Mfuko huu unatangazwa ili kutoa fursa kwa vijana wengi zaidi kuwezeshwa kupitia mfuko huu.

v) Serikali ihakikishe kwamba inaongeza Bajeti ya kutosha ya Wakala wa Usalama na afya mahala pa kazi (OSHA) ili waweze kuajiri watumishi wa kutosha kuweza kufanya kazi ya kuisaidia nchi katika eneo la usalama wa

wafanyakazi. Aidha serikali iangalie utaratibu bora wa kupunguza tozo kila wakati ili kuepuka uwezekano wa kupunguza uwezo wa Taasisi wa kuboresha huduma zake.

vi) Kupelekwa kwa **asilimia 33.9** tu ya fedha za matumizi ya kawaida katika Tume ya Usuluhishi na Uamuzi **Fungu 15** kumeathiri utekelezaji wa majukumu yake. Kamati inashauri kwamba Serikali ihakikishe kwamba inatoa kwa wakati Fedha za Matumizi Mengineyo ili kuziwezesha taasisi na idara za Serikali kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, mapokezi ya fedha za matumizi ya kawaida yanapaswa kuwa na uwiano katika mafungu haya mawili kwa sababu katika fedha hizo kuna fedha za mishahara ya watumishi na fedha za matumizi mengineyo ambazo hutumika kwa ajili ya uendeshaji wa kila siku wa taasisi husika.

vii) Fedha zinazotengwa kwa ajili ya mafunzo ya watumishi zinaweza kusaidia kukuza weledi, kuongeza ufanisi na motisha kwa watumishi iwapo fedha hizo zitatolewa na kutumika inavyostahili. Serikali itumie fedha za mafunzo na matumizi mengineyo kuwapatia watumishi mafunzo ya ndani na nje ya nchi ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi.

viii) Kamati ilibaini kuwa mwenendo wa fedha za bajeti ya utekelezaji wa programu ya Kukuza Ujuzi Nchini umekuwa ukishuka kutoka **Shilingi 18,000,000,000** Mwaka 2019/2020 hadi kufikia **Shilingi 9,000,000,000** Mwaka 2023/2024 na kusababisha kushuka kwa vijana wanufaika kutoka wastani wa vijana 42,000 hadi 12,000. Kamati inashauri kuwa Serikali iongeze bajeti ya programu hii ili kufikia malengo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa jumla ya vijana 681,000 wanaotakiwa kupata mafunzo ya ujuzi katika kipindi cha miaka mitano.

ix) Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, ihakikishe kwamba inachangamkia fursa za ajira zinazopatikana katika nchi nyingine. Aidha, Serikali iweke mifumo thabiti ya kuhakikisha kwamba, watanzania watakaopata fursa ya ajira hizo, haki zao za msingi na kisheria zinalindwa ikiwemo uhifadhi wa utu wao. Vilevile Serikali ifanye tafiti za kujua madhara yanayoweza kuambatana na ajira hizo ili kupima iwapo kuna ulazima kwa wananchi wake kwenda kufanya kazi hizo nje ya nchi. Halikadhalika Serikali iandae Kanzi Data (Data Base) ili kujua idadi ya Watanzania wanaofanya kazi Nje ya Nchi.

x) Kamati ilibaini kuwa fedha zilizotengwa kwaajili ya ujenzi na ukarabati wa Vyuo vya Ufundi Stadi na Marekebisho kwa Watu wenye Ulemavu hazikutolewa hadi kufikia mwezi Februari 2023 hivyo kukwamisha utekelezaji wa mradi huu. Kamati inashauri kuwa fedha zinazotengwa kwaajili ya ukarabati wa vyuo hivi zitolewe kwa ukamilifu na kwa wakati ili kuboresha huduma za mafunzo stadi na marekebisho nchini.

xi) Watu wenye ulemavu wamekuwa hawajumuishwi vya kutosha kwenye programu mbalimbali nchini. Kamati inashauri kuwa Serikali iweke mkakati maalumu wa kuwajumuisha watu wenye ulemavu kwenye Programu ya Taifa ya kukuza ujuzi nchini na programu zingine ili kuhakikisha kuwa fursa kwa watu wenye ulemavu zinaimarishwa.

xii) Vijana wengi wanaopata mafunzo kupitia miradi ya vitalu nyumba na uanangezi (apprenticeship) wamekuwa wakishindwa kuendeleza ujuzi wao kutokana na kukosa mitaji. Kamati inashauri kuwa Serikali ihakikishe kwamba ujuzi unaopatikana katika vitalu nyumba *(greenhouses)* na uanagenzi *(apprenticeship)* haupotei. Aidha, Serikali

ione umuhimu wa kutoa mikopo kwa vijana wanaoshiriki katika programu hii ili vijana hao waweze kumudu gharama muhimu kama vile kujenga vitalu nyumba.

xiii) Moja ya sababu zilizosababisha kutokupata mapato kwenye chanzo cha mapato ya Ada za kufanya kazi nje ya nchi ni kutokuwepo kwa mfumo maalumu wa kukusanya fedha za kigeni kutoka kwa waajiri nje ya nchi.

## 5.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha taarifa hii. Aidha, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao yaingie kwenye kumbukumbu za kudumu za Bunge kama yalivyo wasilishwa katika taarifa hii; nayo ni kama ifuatavyo: -

1. Mhe.Fatma Hassan Toufiq, Mb. – Mwenyekiti
2. Mhe.Riziki Said Lulida, Mb. – Makamu Mwenyekiti
3. Mhe.Tamima Haji Abbas, Mb.
4. Mhe.Neema Gerald Mwandabila, Mb.
5. Mhe.Tecla Mohamedi Ungele, Mb.
6. Mhe.Kabula Enock Shitobela, Mb.
7. Mhe.Maimuna Salum Mtanda, Mb.
8. Mhe.Mohamed Abdulrahman Mwinyi, Mb.
9. Mhe. Katani Ahmadi Katani, Mb.
10. Mhe. Ahmed Ally Salum, Mb.
11. Mhe. Furaha Ntengo Matondo, Mb.
12. Mhe. Janeth Elias Mahawanga, Mb.
13. Mhe. Mariam Nassoro Kisangi, Mb.
14. Mhe. Athuman Almas Maige, Mb.
15. Mhe. Ali Hassan Omar King, Mb.
16. Mhe. Boniphace Mwita Getere, Mb.

17. Mhe. Sanya Juma Jafar, Mb.
18. Mhe. Shanif Mansoor Jamal, Mb.
19. Mhe. Toufiq Salim Hassan Turky, Mb.
20. Mhe. Michael Mwita Kembaki, Mb.
21. Mhe. Sophia Hebron Mwakagenda, Mb.

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Prof. Joyce Lazaro Ndalichako, (Mb) Waziri wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu na Naibu Waziri Mhe. Paschal Patrobass Katambi, Mb kwa kuwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi yake kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika**, naomba pia niwashukuru watendaji wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana na Wenye Ulemavu pamoja na taasisi zake kwa ushirikiano walioupatia Kamati wakiongozwa na Katibu Mkuu Prof. Jamal Adam Katundu.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini sio kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa Mwihambi, *ndc* kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na Bunge kwa mujibu wa Katiba ya Nchi. Aidha, nawashukuru Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya kamati za Bunge Ndg. Michael Chikokoto, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Gerald Magili na Makatibu wa Kamati hii Ndg.Aziza Waziri Kheir na Ndg. Rehema Lazarus Kipera wakisaidiwa na Bi Jane Ndulesi kwa kuratibu shughuli za Kamati na kufanikisha kukamilika kwa taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Mhe. Fatma H. Toufiq, (Mb)
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII**
05 Aprili, 2023

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mwenyekiti, Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq.

Waheshimiwa sasa tunaanza kuchangia, na tunaanza na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela halafu wajiandae Mheshimiwa Abdul-Hafar Idrissa Juma, Mheshimiwa Deo Sanga na Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu. Nakushukuru sana kwa kunifanya mchangiaji wa kwanza kwa hotuba hii muhimu sana ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kimaumbile nilivyoumbwa, siwezi kunyamaza. Nikitendewa jambo jema, nitasema, tena nitasema kwa sauti kali; lakini likitendwa jambo baya, nasema tena nasema kwa ukali zaidi. Sasa naomba nizungumze kwa sauti nzuri, sauti ya unyenyekevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kama Mbunge wa Jimbo la Same Mashariki, namshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Sita, Mama Samia Suluhu Hassan. Nasema hivyo kwa sababu nimetumwa na wananchi walionichagua. Jimbo langu lilikuwa limejifunga, walioko milimani hawafiki tambarare, na walioko tambarare hawafiki mjini kwa sababu nilikuwa sina barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeanza kuongoza jimbo hili mwaka 2005. Miaka yote nilikuwa napewa pesa Shilingi milioni 350 na majedwali yote ninayo ya kuanzia mwaka 2005, Shilingi milioni 350 za kutengeneza barabara za *TARURA*. Tangu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameingia madarakani tarehe 19 mwezi wa Tatu mwaka 2021 mpaka leo, Jimbo la Same Mashariki limepewa fedha za kutengeneza barabara za *TARURA* Shilingi 5,200,000,000/=. Hili jambo siyo la kawaida. Wananchi wa Same Mashariki wanamshukuru sana Rais aliyeko madarakani, mpaka wananiuliza, hivi hizi pesa zilikuwa wapi miaka yote? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wangu asilimia 100 ni wakulima, na mkulima anahitaji barabara apeleke mazao yake kwenye masoko makubwa. Jimbo lilijifunga, walanguzi ndio wanaoweza kufika milimani kuchukua tangawizi kwa bei wanayoitaka wao; lakini sasa hivi wananchi wangu wanapeleka kwa magari, hawana wasiwasi, njaa jimboni kwangu imepungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi tarehe 01/03/2023 walifanya sherehe kubwa kwangu ya kumshukuru Rais. Leo hii wamenituma kwa Waziri Mkuu, wameniambia tunakutuma kwa Waziri Mkuu na yeye ukamtume akamwambie Rais tunampenda sana, tunamshukuru sana, Mungu ambariki. Hapo nimesema kwa sababu nimefurahi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naingia jambo la pili. Serikali ya Chama cha Mapinduzi nawashukuru. Mimi natokea Mkoa wa Kilimanjaro. Mkoa wa Kilimanjaro elimu ilianza siku nyingi sana, shule zimeanza siku nyingi sana kwa sababu kuna waeneza dini, wamisionari walianza kuingia kwetu mwaka elfu moja mia nane themanini na kitu hivi. Walipoeneza dini wakajenga Shule. Baadae Serikali ikataifisha zile shule, ikajenga pamoja na wananchi. Hata hivyo, Shule zile zimechakaa sana, shule zile za msingi zimechoka sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu kuna waeneza dini, wamisionari walianza kuingia kwetu mwaka elfu moja mia nane themanini na hivi. Walipoeneza dini wakajenga Shule baadae Serikali ikataifisha zile Shule ikajenga pamoja na Wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, shule zile zimechakaa sana, Shule zile za msingi zimechoka sana, naipongeza Serikali ya Awamu ya Sita. Nimeona na nimeletewa ripoti hapa ya pesa za *boost* za kwenda kuboresha na kujenga Shule za Msingi za Mkoa wa Kilimanjaro, nimepokea za kwangu, Charles angalia utaona za kwako huko. Kila Halmashauri ya Mkoa wa Kilimanjaro tunamshukuru Mungu tumepokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali naomba niwambie kitu kimoja Serikali ya Chama cha Mapinduzi, hizi Shule zitajengwa, hizi Shule zitaboreshwa, nitoe mfano; huu mwaka uliokwisha 2022 Serikali ilinipendelea iliniletea Milioni 100 za kujenga upya Shule ya Msingi inayoitwa Kihurio Kata ya Kihurio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ile Shule ilijengwa, aliisimamia Mkurugenzi Vizuri sana na shule ile ikawa mpya. Madarasa tisa yalipokwisha sasa nakwenda kuona shule, Madawati! Ile shule iliyokuwa imechoka Madawati yalikuwa ni Magogo, yalikuwa ni madawati yaliyochoka, nimeshindwa kuingiza hayo magogo kwenye shule mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwenyewe kama Mbunge nimetengeneza madawati ya madarasa tisa kwa sababu nimeona niisaidie Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi, imenipa Milioni 100 na mimi Mbunge niliyechaguliwa na wananchi nikafanya kidogo, nikafanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niiambie TAMISEMI, tumewashukuru mlivyotuletea hii pesa, tunaomba mpange vizuri mlete pesa za Madawati. Nina uhakika sio kwangu tu

kwa sababu ninaangalia mitandao ninaona ni sehemu nyingi sana. Sasa hilo limekwisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge mnisikilize kidogo, sasa naomba niongee na watanzania, naomba niongee kwa unyenyekevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, huko nje watanzania wamekasirika sana lakini naomba niwambie watanzania kitu kimoja, Rais amechukizwa sana. Vilevile watanzania naomba niwambie jambo la tatu, Waheshimiwa Wabunge wote hapa ndani wamechukizwa waliposikia Rais akikabidhiwa ile ripoti ya CAG tarehe 29/3/2023 kila mtu alichukizwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwambie Watanzania kitu kimoja, hizi shughuli kubwa kama hizi sisi Wabunge tunazifanya kwa utaratibu. Wananchi nje wanaona kama wabunge mbona hawasemi? Tunakwenda kwa utaratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba uniruhusu suala la CAG liko hapa kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Suala la CAG sisi Wabunge tunakwenda nalo kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 Ibara ya 143(4) naomba uniruhusu kunukuu; "Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu atawasilisha kwa Rais kila taarifa atakayotoa kwa  kwa mujibu wa masharti ya ibara ndogo ya (2) ya ibara hii. Baada ya kupokea taarifa hiyo, Rais atawaagiza watu wanaohusika wawasilishe taarifa hiyo kwenye kikao cha kwanza cha Bunge kitakachofanyika baada ya Rais kupokea taarifa hiyo na itabidi iwasilishwe katika kikao hicho kabla ya kupita siku 7 tangu siku ile kilipoanza kikao hicho kuketi. Iwapo Rais hatachukua hatua za kuwasilisha taarifa hiyo kwenye Bunge basi Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu atawasilisha taarifa hiyo kwa Spika wa Bunge au Naibu Spika ikiwa kiti cha Spika ki wazi wakati huo au ikiwa kwa sababu yoyote Spika hawezi kutekeleza

shughuli za kazi yake ambaye atawasilisha taarifa hiyo kwenye Bunge" mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Spika wa Bunge anapokea taarifa ya *CAG* kesho, ikiwa na maana nataka kuwambia Watanzania taarifa hiyo haijaingia hapa Bungeni. Watanzania wajue kitu kimoja ambacho na sisi Wabunge tunakijua, Rais Samia Suluhu Hassan anahangaika mno kutafuta pesa kwa ajili ya maendeleo ya watanzania. Hawezi kukubali watu…

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni taarifa? Haya nakaa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**T A A R I F A**

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpa taarifa mzungumzaji kwamba si tu kwamba hayajafika Bungeni lakini kwa mujibu wa Sheria ya Taifa ya Ukaguzi Kifungu cha 39(1) baada ya kuja Bungeni taarifa ya *CAG* ndiyo itakuwa *public document* na hata sisi Waheshimiwa Wabunge ndiyo tutaweza kuisoma *in details* taarifa yote na kila kitu kilichosemwa na *CAG*.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimeipokea na kijana ameidadavua  ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ni lazima watanzania labda hawaelewi. Wakilalamika kwamba Wabunge hawasemi ni vema tuwambie kwamba tunafuata taratibu. Taratibu zitakpofika watanzania wawe na uhakika hakuna atakayepona. Rais hatakubali, Wabunge hatutakubali, sisi

hatutakubali ambaye kweli tutakuwa tumehakikisha amechezea pesa za watanzania akaendelea kuzunguka kwenye nchi hii hapana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaomba na ninawaomba Watanzania kwa unyenyekevu waturuhusu sisi tunaowawakilisha tufuate utaratibu tusifanye kazi kinyume na utaratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo naomba kuunga mkono hoja ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Sasa namuita Mheshimiwa Abdul-Hafar Idrisa Juma, jiandae Mheshimiwa Deo Sanga

**MHE. ABDUL-HAFAR IDRISSA JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia na mimi katika hotuba hii ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuipongeza Serikali hasa Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa yale ambayo amekuwa akiyatenda na haya ambayo yameelezwa katika bajeti ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, dhahiri kama ambavyo mara nyingi nimekuwa nikizungumza humu ndani. Mwaka 2025 Chama changu cha Mapinduzi hakitakuwa na kazi ya kumrejesha Mheshimiwa Dkt. Samia madarakani Wabunge wote wa Chama cha Mapinduzi kwa kazi kubwa ambayo inaendelea kufanywa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba nichangie katika masuala yafuatayo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, katika sekta ya Miundombinu, napongeza kwa jitihada ambazo zinaendelea kufanyika. Ningeomba sasa Ofisi ya Waziri Mkuu katika bajeti

yake hii ione umuhimu wa kuleta mabadiliko ya Sheria ya Manunuzi ili kuruhusu Sekta ya Miundombinu iwe kama Sekta nyingine za kibiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sifurahishwi sana kuona mpaka leo bado tunajenga barabara mfano za Mwendokasi kupitia fedha ambazo zinatafutwa na Rais Samia na Serikali yetu. Kama tumetoa fursa kwa wafanyabiashara wakaweza kuja kujenga viwanda, tukawapa vivutio mbalimbali vya kodi, wakajenga viwanda wakazalisha ndani ya Tanzania, watanzania wakaajiriwa, Serikali ikapata kodi, kwa nini tunashindwa kutoa fursa kama hizo kwa wawekezaji wakajenga miundombinu hasa ile ya mwendokasi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu barabara ya mwendokasi inapojengwa sio watanzania wote na magari yao wanaruhusiwa kutumia ni magari maalumu. Kwa hiyo, ni magari maalumu ambayo yanapita na kufanya biashara katika barabara hiyo. Sasa kwa nini Serikali isitangaze kwa wenye fedha duniani wakaja wakajenga barabara za mwendokasi ili fedha ambazo zingekwenda kujenga barabara zikatumika kwa shughuli nyingine kama vile kuhudumia hospitali zetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo jambo sio geni na huko duniani lipo. Serikali yetu ilitupa nafasi sisi tulikwenda kujifunza nje. Huko duniani ziko bandari zimejengwa na watu kwa asilimia 100 na Serikali inakusanya kodi tu. Sasa kwa nini katika sekta ya miundombinu tusiende huko katika kuleta vivutio kama tulivyoleta vivutio katika sekta ya viwanda? Ningetamani kuona katika suala la bandari ya Bagamoyo linakwisha na kuanza kujengwa kupitia wawekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli inawezekana tumekosea sasa je, tumekosea ndio tuache ibaki hivyo hivyo? Tuache tusiwe na bandari kubwa Zaidi? Makosa yaondoshwe Sheria iletwe katika Bunge hili tuone namna inavyoweza

kubadilishwa basi Bandari ya Bagamoyo na Bandari nyingine ziweze kujengwa kupitia sekta binafsi kwa maslahi ya taifa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba sasa pia nizungumzie suala katika Manispaa hasa zile asilimia 10 zinazohusu vijana wenzangu akina Mama pamoja na Watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwanza nikupe taarifa nina miaka 32 hivi karibuni nitatimiza miaka 33, kwa hiyo bado ni kijana na nina maslahi makubwa sana na vijana katika Taifa hili pamoja na Wananchi wangu wa jimbo la Mtoni. Fedha zile ambazo zinakopeshwa asilimia 10 mara nyingi ukopeshwaji wake hauleti matokeo mazuri. Nafasi hii niitumie kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuelekeza fedha hizi zianze kutolewa kupitia Mfumo wa Kibenki. Hata hivyo, Mheshimiwa Rais amesema suala hilo litafanyika katika bajeti ya Serikali ijayo bajeti ya mwaka 2024/2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, fedha hizi katika bajeti hii ambayo tunaendelea nayo zimetengwa kuendelea kusimamiwa na Halmashauri. Nimuombe Mheshimiwa Waziri Mkuu kama Msimamizi Mkuu wa Serikali basi fedha hizi katika mwaka 2023/2024 zisije zikatumika kama kiinua mgongo kwa wale watu ambao wamekuwa wakigawana na vikundi vyao kwa sababu wanajua baada ya hapo zitaanza kutumika kupitia Benki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka 2020/2021 ilionesha kwamba takribani Shilingi bilioni 47 katika halmashauri 155 katika hizi fedha za asilimia 10 zimeshindwa kukusanywa kurejeshwa. Maana yake nini? Bilioni 47 zingekusanywa wangekopeshwa vijana kila mmoja mwenye uwezo wa kufanya Biashara Milioni 100 maana yake tungetengeneza Mamilionea 470 wakasimamiwa na halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, halmashauri zote zina maafisa biashara. Laiti Maafisa biashara wangeweza kusimamia kuwasaidia wafanyabiashara sio tu kuwakimbiza pale wanapokuwa hawajakata leseni labda tungekuwa na wafanyabiashara wakubwa wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa fedha hizi katika bajeti hii ya mwaka 2023/2024 kwa sababu ndio itakuwa ya mwisho kusimamiwa moja kwa moja na halmashauri kufuatia maelekezo ya Mheshimiwa Rais, basi Ofisi ya Waziri Mkuu ikazisimamie lasivyo nitakapokuja hesabu ya Maguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka huu 2023/2024 ambao tunapitisha bajeti yake itakuja na matatizo yale yale. Ningetamani kuona Ofisi ya Waziri Mkuu inakwenda kuzisimamia ili nione Mamilionea vijana kutokana na fedha ambazo zinatengwa na halmashauri yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa suala la vyama vya siasa. Nitumie nafasi hii kuomba bajeti ya Waziri Mkuu wale ambao wanasimamia masuala ya vyama vya siasa watenge muda zaidi kuvipa Elimu na kuvikumbusha vyama vya siasa umuhimu wa Demokrasia. Mheshimiwa Rais ametuonyesha njia umuhimu wa ustahimilivu, umuhimu wa kusikiliza sasa na wao wawe wastahimilivu na wawe wenye kusikiliza. Hata hivyo, hivi vyombo ambavyo vinasimamia vyama vya siasa vitimize wajibu huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda tukumbushane humu ndani, mwaka 2015 watanzania waliamua Kumchagua Dkt. John Pombe Magufuli na Rais Samia ambaye yuko sasa madarakani kama Makamu wake wa Rais. Watanzania hao hao waliamua kuchagua Wabunge wengi wa upinzani pia na waliamua kuchagua Wabunge wengi zaidi wa CCM lakini mwaka 2020 Watanzania waliamua Kuchagua Wabunge wa CCM wengi zaidi kwa sababu ya yale yaliyotendwa na Serikali iliyokuwa madarakani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa vyama vya siasa kama ambavyo vilifurahia na hasa vya upinzani vilivyopata Wabunge wengi mwaka 2015 vijifunze kustahimili Watanzania wakiendelea kuiamini CCM.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyotangulia kusema awali, kwa mwendo wa Rais Samia hakuna pahala katika Taifa hili ambapo hajaweka mkono. Dhahili, Wabunge wa Chama cha Mapinduzi mwaka 2025 watatawala katika viti vyote vya Bunge hili kwa sababu watanzania watawaamini.

Mheshimiwa Naibu Spika, wale wenye kusimamia vyama vya siasa wakae watukumbushe viongozi wa Chama Tawala na vyama vingine kwamba kushindwa katika uchaguzi Mkuu ni matokeo na baada ya kushindwa wasije wakatumia nafasi hiyo kuwafitinisha watanzania maana baada ya uchaguzi watahitajika kuendelea kulijenga taifa lao. Hata hivyo, wakati wa kuwakumbusha pia wawasomee basi katiba ya Chama cha Mapinduzi Ibara ya 5 ili mioyo yao iwe na amani pale mambo yoyote yatakapotokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hivyo nakushukuru sana naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Deo Sanga jiandae Mheshimiwa Ali Mohamed Kasinge, jiandae Mheshimiwa Neema Gerald Mwandabila.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kuniruhusu na mimi niweze kuchangia. Kwanza nianze sana kwa Kumshukuru Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya ndani ya nchi hii. Vilevile nimpongeze pia Waziri Mkuu na msaidizi wake Makamu wa Rais kwa namna ambavyo wamekuwa wakifanya kazi nzuri ya kuunga mkono jitihada za Rais Mama Samia Suluhu Hassan. Vilevile niwapongeze Mawaziri wote kwa namna

ambavyo wanavyojituma kuunga mkono jitihada za Rais za kutuletea maendeleo katika nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, wamesema wenzangu na mimi niungane. Ukweli utabaki kuwa kweli, kuna methali inasema Mnyonge mnyongeni haki yake mpe. Hapa hakuna mnyonge mnyongeni habari ya mnyonge mnyongeni haipo. Mama Dkt. Samia anafanya kazi kubwa, kazi nzuri ya maendeleo katika Halmashauri zetu na nchi hii haijapata kutokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Miradi iliyoko huko kwenye Halmashauri zetu Mabi, na  Mabii, na Mabii ni nyingi kwa hiyo tunampongeza sana. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu, fedha zinazokwenda huko ni nyingi na wanaosimamia pia katika Shughuli hizi ni pamoja na Waheshimiwa Madiwani wetu. Naomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu ni lazima tuhakikishe ili wakasimamie vizuri na wenyewe waongezewe posho ili wakasimamie vizuri shughuli za maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukulie kwenye jimbo langu la Makambako, ukienda upande wa Maji, miradi iliyofanyika katika jimbo langu ni mingi ya hela nyingi za mabii na Mabii. Vilevile tuna miradi ile ya miji 28 hivi sasa mkandarasi yuko *site* anaendelea na shughuli za miradi ya maji vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaimani atakapomaliza hivi 2025 Mkandarasi huyu tatizo la maji katika Mji wetu wa Makambako litakuwa limeisha kabisa kwa asilimia zaidi ya100. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kwenye Afya, shughuli nyingi nzuri zimefanyika sana katika jimbo letu la Makambako lakini katika nchi nzima. Vilevile ukienda katika upande wa barabara; barabara nyingi zinatengenezwa vizuri hususani

pale mjini tuna barabara zinatengenezwa za lami, kuna barabara za Changarawe na Vumbi zinaendelea kutengenezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu *TARURA* waongenzewe bajeti ili waweze kufanya kazi nzuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukinda kwenye elimu, vilevile kwa miaka nenda inapofika Januari, wananchi wetu huwa wanapata tabu kwa namna ambavyo tunakuwa tunawachangisha ili madarasa yaweze kujengwa. Kwenye Halmashauri yetu na nchi nzima tumepata fedha nyingi madarasa yamejengwa na Shughuli zinaendelea vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi upande wa elimu, kuna Shule kongwe za msingi ikiwepo Shule ya Mwembe Togwa, Shule ya Mashujaa, shule hizi sasa zinahitaji zipate hela kwa ajili ya ukarabati na kujenga madarasa mengine mapya.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto; pamoja na kazi nzuri mbalimbali ambazo zimefanywa tuna changamoto. Tuna tatizo la fidia eneo la Polisi ambalo Mheshimiwa Rais alipokuja Mwezi Agosti, 2022 wananchi wale wanapata tabu fidia ya Shilingi Milioni 235, wanashindwa sasa waende wapi kwa sababu hawaruhusiwi kuongeza kitu chochote. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali ihakikishe fedha hizi zinatolewa kama alivyoagiza Mheshimiwa Rais ili wananchi hawa waweze kulipwa fidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kwenye fidia kuna eneo ambalo walipewa fidia zaidi ya shilingi bilioni 3 kwa ajili ya kujenga Soko la Kimataifa, kuna wananchi 18 walibaki hawakulipwa. Tunaiomba Serikali ihakikishe wananchi hawa wanalipwa fidia zao, stahiki zao ili kero hii iweze kuondoka. Hata hivyo, Mheshimiwa Rais alipokuja aliagiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kwenye fidia kuna tatizo la umeme wa upepo Watu wa muogemo wa upepo walikuja wawekezaji pale na walikuwa tayari kulipa fidia tatizo lipo kwenye wizara ya nishati. Niombe sana Mheshimiwa Naibu Waziri tuhakikishe kwamba hii fidia inalipwa ili wananchi waweze kuishi kwa amani. Nimekuwa nikilizungumza mara nyingi sana jambo hili, na naomba sasa lipate baraka za wananchi hawa kwa kulipwa fidia zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile kuna suala la vifaa tiba. Kwenye halmashauri zetu au kwenye wilaya zetu kwenye hospitali za wilaya tumepata vifaa tiba ambavyo hatujawahi kupata. Tumepata mpaka vifaa ambavyo vinashitua moyo, ambavyo vilikuwa vinapatikana *KCMC* au Muhimbili. Leo sasa makambako vimekuwepo vifaa hivyo. Kwa hiyo tunampongeza sana Mheshimiwa Rais. Vifaa ambavyo vilikuwa vinapatikana Ulaya tu leo viko Makambako, vinapatikana; kwa hiyo tunaipongeza sana Serikali kwa kazi nzuri ambayo tumekuwa tukiifanya *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu lingine, kuna barabara ya kutoka Kigoma kwenda Lupembe. Barabara hii tanga 2015 iko kwenye ilani, 2020 iko kwenye ilani. Ombi langu barabara sasa itengewe fedha kwa ajilli ya kutengeneza na wananchi wa lupembe wana imani kubwa kwa sababu rais wetu akiwa Makamu wa Rais aliwaahidi, na sasa tunaomba barabara hii iweze kutengenezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, si kwa umuhimu, ameteuliwa kijana anayeshughulikia mambo ya dawa za kulevya; tunampongeza sana mama kwa kumteua kijana huyo. Ni imani yetu kwamba vijana wetu watapona; akasimamie vizuri suala la madawa ya kulevya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, la mwisho, na Waheshimiwa Wabunge wenzangu hili la mwisho kabisa. Rais

Mama Samia yaani hata unapotembea kwenye jimbo lako unatembea unaringa, unajidai kwa sababu mabilioni na mabilioni yamekwenda huko. Na imani yangu, kutokana na mabilioni yaliyokwenda huko Wabunge wote mtarudi na Mama Samia atapata kura nyingi haijapata kutokea kwa sababu ya kazi anazozifanya ni nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na wewe kwenye jimbo lako yamefanyika kule. Yaani ukipita huku mara upande juu mara ushuke chini na kadhalika na kadhalika, kazi iliyofanyika Dar es salaam ni nzuri, kwa hiyo na wewe tunakuombea, utarudi. vievile Mbeya kwa Spika haijawahi kutokea, ule msongamano wa Mbeya sasa wamepata *by-pass* ya kupunguza msongamano. Kwa hiyo tunakuombea na wewe Spika na utarudi tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya nichukue nafasi kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia; lakini kwa kweli mama tunampongeza sana kwa kazi nzuri ambayo amekuwa akiifanya. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Au unahitaji dakika tano za ziada? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Ally Kassinge jiandae Mheshimiwa Neema.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ili na mimi jioni hii niweze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nikiungana na Wabunge wenzangu waliopata fursa ya kuanza kuchangia na mimi kwa dhati kabisa nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo anajitoa kuwatumikia Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu katika hotuba yake ukurasa wa kumi na mbili

ametukumbusha Watanzania kwamba mradi wa kufua umeme wa Bwawa la Mwalimu Nyerere megawatt 2115 serikali imetoa bilioni 869.93 na mradi umefikia 83%; hizi ndizo kazi za Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kwamba haitoshi mradi mkubwa wa kusafirisha mafuta kutoka Uganda Hoima mpaka Tanga, kilomita 1443 Serikali imeshatoa bilioni 30.39 kwa ajili ya kulipa fidia waathirika wa maeneo ambayo bomba itapita, hizi ndizo kazi ambazo Watanzania wanafanyiwa na Mheshimiwa Rais Wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upekee wake sisi wana-Kilwa na hususani wana-Kilwa Kusini Rais Samia amefanya ambayo hayajawahi kufanyika, na kwa kweli ameacha alama ambayo kwa kweli hatutoisahau. Kulikuwa na mradi ambao umesuasua kwa muda mrefu wa maji kwenye miji 28 umeanza kutekelezwa katika kipindi hiki cha Dkt. Samia. Pia kulikuwa na ujenzi wa bandari ambao mipango yake ilikuwa ni ya muda mrefu, tulipitisha katika mpango wa miaka mitano ya maendeleo hapa Bungeni. Nitumie fursa hii kuwataarifu Watanzania kwamba mradi huu tayari umeanza pale Kilwa Masoko na unathamani ya shilingi bilioni 266.7; Kilwa hatujawahi kupata mradi mkubwa kama huu tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais Samia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama kwamba haitoshi Mheshimiwa rais ameendalea kutusaidia wanakilwa katika sekta za barabara. Tumeongezewa fedha kwenye *TARURA* kutoka milioni 800 ambayo ilikuwa ni kwa ajili ya Wilaya nzima ya Kilwa kwa wakati ule mpaka kufikia karibu bilioni tatu kwa majimbo yote mawili kwa mwaka, Kilwa Kaskazini na Kilwa Kusini. tunamshukuru na kumpongeza sana Rais Samia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo sasa nije katika baaadhi ya maeneo ambayo nilidhani Serikali

ikitekeleza basi tutakuwa tumemsaidia na kumfanya Rais Samia apendeze zaidi kwa Watanzania na wana Kilwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianza katika eneo la ujenzi wa bandari, nitoe rai kabisa kwamba wakati Serikali inatekeleza ujenzi huu wa bandari basi ifikirie kuweka miundombinu mingine rafiki itakayoendana na uwepo wa Bandari hii ya Uvuvi pale Kilwa Masoko. Kwa mfano barabara iliyopo kutoka pale bandarini kuelekea Nangurukuru kilometa takribani 30 haiko katika viwango ambavyo vitaendana na bandari hiyo. Nitoe rai katika bajeti hii barabara hii ipanuliwe na ijengwe katika viwango. Lakini pili mundombinu rafiki na taasisi rafiki ambazo zitaendana na uwepo huu wa bandari ikiwemo viwanda vya kuchakata mazao ya Bahari na chuo cha uvuvi pale KilwaMasoko ni vitu ambavyo pia vinatakiwa vifikiriwe katika bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo nieleze kwa masikitiko kidogo, kwamba pamoja na utekelezaji wa bandari ambao unaendelea pale Kilwa Masoko lakini wananchi wangu wapatao 54 bado hawajalipwa fidia kupisha upanuzi na ujenzi huu wa bandari. Nitoe rai kabisa, katika kipindi hiki kifupi ndani ya mwaka huu muda si mrefu Serikali ifikirie kuwalipa fidia wananchi wangu wapatao 54 ili masuala ya ujenzi wa bandari yasiingie migogoro ya wananchi kudai fidia *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija katika uboreshaji na upanuzi wa viwanja vya ndege, tulipitisha katika mpango wa miaka mitano, na Kiwanja cha Ndege cha Kilwa Masoko ni miongoni mwa viwanja ambavyo vitapanuliwa na kufanyiwa maboresho. Lakini kwa masikitiko niseme tu kwamba bajeti iliyotengwa kwa mwaka uliopita ilikuwa ni ndogo sana kiasi cha kukarabati *runway* ile kilometa 800 tu kwa kiwango cha changarawe. nitoe rai kwamba kiwanja hiki cha ndege sasa kijengwe katika viwango vinavyotakiwa, kwa maana kuongeza mita 900 zingine za *runway,* kuweka uzio wa

kiwanja cha ndege na pia kuboresha lile eneo la kupumzikia abiria.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo nieleze tu kwamba dhana ya upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kilwa Masoko ni wa miaka takribani miaka 10 iliyopita, na wananchi wangu walifanyiwa tathmini mwaka 2011/2012, na ikarudiwa tena tathmini ili walipwe fidia mwaka 2011/2012 na tathmini hii ilirudiwa tena mwaka jana mwezi wa nne. Kiasi cha wananchi wangu zaidi ya 412 wamefanyiwa tathmini hii lakini bado hawajalipwa fidia hii. Nitoe rai kabisa, Serikali ifanye hima kuwalipa fidia wananchi wangu hawa ili ujenzi utakapokuwa umeanza wa kuboresha na kupanua Kiwanja cha Ndege pale Kilwa Masoko kusiwe tena na malalamiko ya wananchi wetu kudai fidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija katika eneo la maji, pamoja na kushukuru kupatiwa mradi ule wa maji kutoka Mto Mavuji kwa ajili ya Miji ya Nangurukulu Masoko na Kivinje niseme tu kwamba bado tunahitaji kupanua wigo wa upatikanaji wa maji vijijini pamoja na mijni. Hapa kwa upekee wake nizungumzie kata moja ambayo kwa kweli haijawahi kupata kunufaika na mradi wa maji wa aina yoyote ile; na hii si kata nyingine isipokuwa ni Kata ya Lihimalyao iliyopo katika Jimbo langu la Kilwa Kusini. Nitoe rai kwa kata ya Lihimalyao kwa upekee wake, hebu Serikali ione uwezekano wa kujenga mabwawa kwa ajili ya kuvuna maji ya mvua.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia Kata jirani ya Pande kuna maji ya kutosha. Serikali ione uwezekano wa kutoa maji kwa utaratibu wa mtiririko kupeleka katika Kata hii ya Lihimalyao ndani ya kipindi cha mwaka huu wa bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nitoe rai tu kwa Serikali; kwamba ili kupunguza kama si kuondoa kabisa tatizo la maji, si tu Kilwa lakini mikoa yote ya Kusini, kwa nini tusiwe sasa na

mpango wa kupanua wigo matumizi ya maji ya Mto Rufiji? Badala ya kupeleka maji ukanda wa Dar es salaam peke yake tawi lingine lije Ukanda wa Kusini ili Mikoa ya Pwani, Lindi, Mtwara pamoja Ruvuma inufaike. Mradi huu wa Mto Rufiji kama utatekelezwa kuanzia kipindi hiki nakuhakikishia kwamba wananchi wa mikoa yote ya kusini niliyoitaja tatizo la maji au changamoto ya maji litakuwa ni baibai na hapo itakuwa kwamba kweli tumewatendea haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, nije katika miradi ya kimkakati. Sisi pale Kilwa tuna miradi mingi ya kimkakati lakini kwa muktadha wa mchango wangu leo niuzungumzie mradi mmoja tu ambao ni mradi wa kimkakati wa ujenzi wa Stendi ya Nangurukuru. Tunaomba kupitia halmashauri miaka mitatu katika bajeti yetu kama maombi maalum; lakini niombe mwaka huu maombi yetu yale maalum ya bajeti ya kupanua ujenzi wa stendi ya nangurukuru kama mradi wetu mkakati uweze kuidhinishwa na Bunge hili na hatimaye wana-Kilwa waweze kunufaika na stendi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikumbushe pia Bunge lako kwamba katika mpango wa miaka mitano wa maendeleo tulioupitisha hapa bungeni tulipitisha ujenzi wa kiwango cha lami Barabara ya Kiranjeranje Nanjirinji mpaka Ruangwa, lakini pia Barabara ya kutoka Nangurukuru mpaka Liwale. Ninayo furaha kusema kwamba kazi za upembuzi yakinifu na usanifu zimekamilika. Ni wakati muafaka sasa barabara hizi zianze kujengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, nipendekeze barabara ya Nangurukuru mpaka Liwale ambayo kimsingi inahudumia majimbo matatu, Jimbo la Kilwa Kusini, Kilwa Kaskazini pamoja na Jimbo la mtani wangu Kuchauka kule, Liwale ianze kutekelezwa ndani ya mwaka huu angalau kilometa 50 kutoka pale Nangurukuru. Tukifanya hivyo tutakuwa tumeyatendea haki majimbo hayo matatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho niseme tu kwamba tunaendelea kupongeza na kushukuru juhudi za Mheshimiwa Rais Samia katika kuboresha miundombinu katika sekta za huduma ikiwemo afya na elimu. Katika elimu tumepata madarasa ya kutosha. Hata hivyo, nitoe rai, bado tuna tatizo kubwa la nyumba za walimu lakini pia bado tuna tatizo kubwa la madawati katika maeneo yetu ya halmashauri zetu. Niombe katika bajeti hii kwamba tatizo la nyumba za walimu pamoja na madawati liwekewe kipaumbele ili tatizo la ujumla la miundombinula shule zetu za msingi na za sekondari tuweze kulipunguza kwa kiwango kikubwa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzungumza haya naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Neema Gerald jiandae Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu Mollel.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia; na niseme tu ninayofuraha kubwa sana kuanza kuchangia kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuwa *champion* namba moja wa masuala ya lishe katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbukwe tu ni wiki mbili zimepita tumeona Mheshimiwa Rais ameenda kuzindua jukwaa la mfumo wa chakula Barani Afrika, Dar es salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu leo utajikita sana kwenye suala la lishe kwa sababu ni kitu ambacho kama taifa tunapitia changamoto kubwa sana. Na kama tunavyoona, hali ya udumavu kwa nchi yetu tuna asilimia 30, kitu ambacho kama taifa tunatakiwa kujitathmini na kuangalia ni jitihada gani za msingi tunazoziweka ili kuhakikisha hali ya lishe nchini inaimarika.

Mheshimiwa Naibu Spika, na nimeongelea suala tu la udumavu kwamba ni asilimia 30, lakini tuna kitu kinaitwa magonjwa yasiyo ya kuambukiza ambayo hayo yanaenda kwa asilimia 45. Kwa hiyo unaweza ukajumlisha asilimia 30 na asilimia 45 unaweza ukaona kwamba ni kwa kiwango gani nchi yetu ina hali mbaya ya lishe. Kwa hiyo naomba tu niweke msisitizo kwamba kama Taifa ipo jitihada ya kufanya kuhakikisha suala la lishe linapewa kipaumbele *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapoongelea suala la lishe tunaona mikoa inayozalisha chakula ndiyo mikoa ambayo inateseka na hali ya lishe duni. Ukiangalia Mikoa kama ya Iringa, Njombe, Rukwa na mikoa mingine kama Songwe, Morogoro, Mbeya unaona bado hali hali duni ya lishe iko juu. Tunapoongelea udumavu kwenye mikoa yote hii iko juu ya ile *cut-off point* ya hali ya udumavu kwa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ninazidi kusisitiza tu kwamba kama taifa tuone umuhimu wa kupambana na suala la lishe ili tuweze kuondoa hizo changamoto za utapiamlo. Tunapoongela lishe ndicho kitu kinachogusa kuanzia wakati wa mimba mpaka mtu anakuja anazeeka. Katika suala la lishe tunaangalia kuanzia chakula kinapozalishwa, kinapovunwa shambani, kinavyochakatwa mpaka kinavyokuja kwenye utumiaji ule wa mwisho; lakini pia bila kusahau zile hatua za uchakataji wa hiki chakula ili kiweze kuhifadhika kwa matumizi ya baadaye. Kwa hiyo kuna mambo mengi ambayo kama taifa tunatakiwa tuzingatie kwenye suala la lishe ili tuweze kuwa na Taifa ambalo litakuwa na afya nzuri na litakuwa na tija kwenye mchakato mzima wa maendeleo ya kiuchumi wa taifa hili *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo langu kubwa katika kuongea haya yote ninayoyaongea ni kwamba mpaka saa hizi Sera ya Lishe ya Taifa inayotumika ni ya mwaka 1992. Ni miaka 30 nyuma tangu hiyo sera ianzishwe mpaka leo sioni jitihada ya Ofisi ya Waziri Mkuu kuja na Sera ya Taifa ya Lishe

ambayo itaenda kusaidia kupunguza changamoto zote za masuala ya lishe yanayoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona taifa limekuwa linapitia hatua mbalimbali za masuala ya lishe, tunaona kwamba kama Taifa wameweza kuajiri maafisa lishe, walau angalau sasa kila halmashauri ina afisa lishe mmoja, ambao nao si toshelevu. Lakini tunaona kumekuwa na uanzishwaji wa kamati za lishe kwenye halmashauri zetu, na ni kuanzia ngazi ya taifa tumekuwa na *nutritiol steering committee* pamoja na ngazi ya mkoa na wilaya, na wamekuwa na harakati za kuhakikisha zinaenda mpaka kwenye ngazi ya kata.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaona kabisa kumekuwa na utengenezaji wa mikakati ya lishe. Tumeona mkakati wa *MNAP1*, *MNAP2* lakini mambo hayo yote yanafanyika kindi ambacho hatuna sera ambayo inaweza ikasimamia haya mambo yote; yaani sera inayoenda na wakati ya kuweza kuyasimamia haya mambo yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tumeona kabisa Mheshimiwa Rais aliweza kusaini mikataba ya lishe na wakuu wa mikoa; na hii mikataba ya lishe imeenda mpaka ngazi ya chini kabisa kwenye kata, watu wamesaini mikataba ya lishe; lakini inasainiwa kutoka kwenye msimamo upi wa kisera?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapokuwa nayaona hayo ninazidi kuona umuhimu wa Ofisi ya Waziri Mkuu kuona umuhimu wa kufanya uwepo wa sera ambayo inaenda na wakati ya masuala ya lishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchakato wa sera ya lishe ulikuwepo na umeanza tangu 2017 ni miaka mitano zaidi saizi mpaka saizi hatuoni matokeo ya sera ya lishe. Ninapokuwa nayajadili haya natamani kuona Waziri Mkuu atapokuwa ana-*wind-up* mwishoni atuambie ni wapi ambapo hii sera ya

masuala ya lishe imeweza kukwama? Kwa sababu tumeona kumekuwa na uzalishaji wa vyakula saizi tuna vitu vinaitwa *GMO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vitu ambavyo vina-*impact* kwenye chakula na afya za Watanzania, lakini tunaona kabisa kumekuwa na kemikali mbalimbali ambazo zinaingizwa nchini kwa ajili ya *processing* za vyakula mbalimbali. Kuna udhibiti gani, lakini tumeona athari ambazo zimetokea pale ambapo *TFDA* iliweza kuvunjwa ikapelekwa ikapelekwa *TBS*. Tumeona ni wapi ambapo tumekuwa tukifeli kama Taifa. Kwa hiyo kuna mambo mengi katika masuala ya chakula ambayo yamekuwa yakiendelea ambayo yanahatarisha usalama wa chakula chetu, kitu ambacho kingekuwa na sera nzuri inayoenda na wakati ingekuwa rahisi kwa wasimamizi au waratibu wetu wa masuala ya lishe kuweza kuzingatia vigezo ambavyo viko kwenye hiyo sera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapoongelea suala la chakula ni suala la Kitaifa, lakini ni la Kimataifa na ndio maana utakuta wakati mwingine hata bidhaa zetu zinazuiliwa kwenda Mataifa mengine. Mfano mzuri ni lile suala la mahindi yale yalikuwa yanaenda Kenya, masuala ya sumu kuvu, unaona kabisa usimamizi wa namna ya utunzaji wa vyakula vyetu ina maana hauko *smart* mpaka mahindi yanazuiliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kama tutakuja na sera nzuri, sera ambayo inaenda na wakati, ina maana hata wajasiriamali wetu, wakulima wetu wataweza kuzalisha vyakula vitakavyokuwa na ubora na mwisho wa siku sisi kama Taifa tutakuwa tuna uhakika wa chakula kilichobora, lakini pia sisi kama Taifa tutakuwa na uwezo wa ku-*supply* vyakula vyenye viwango vya Kimataifa. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ya kwanza ililia)*

**MBUNGE FULANI:** Endelea ni kengele ya kwanza.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilifikiri muda umekwisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo niseme tu, Ofisi ya Waziri Mkuu ije na kauli ya kusema ni wapi mchakato wa masuala ya Sera ya Lishe umekwamia. Kwa sababu haiwezekani jambo moja miaka mitano linaendelea kutokutekelezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine ambacho ningependa kukiongelea, na-*declare interest* kwamba mimi ni mkazi wa Mji wa Tunduma na Mji wa Tunduma kama Taifa huwa siku zote naendelea kusisitiza kwamba ni mji wenye tija na ni mji ambao kama Taifa kweli litaamua kuwekeza ni kitu ambacho wanaweza wakapata fedha nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na mipango mingi ambayo inatekelezwa upande wa Dar es Salaam bila kuzingatia *destination* ya ile mizigo au shughuli zile zinazofanyika Dar es Salaam kwamba zina *impact* ipi kwa Mji wa Tunduma. Natamani kuona kwamba mipango yao Ofisi ya Waziri Mkuu, sera zao wanazoziunda katika kuhakikisha wanakuza uchumi wa nchi hii, wawe wanafanya kwa kuzingatia na Mji wa Tunduma au Mkoa wa Songwe kwa ujumla; la si hivyo tutakuwa tunawekeza sehemu moja, tunaboresha eneo la Dar es Salaam pekee yake, lakini eneo ambalo mizigo hii inaenda kama Tunduma unakuta halipewi kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo niseme tu hali ya Tunduma kwa maana kwamba kwa kuweza kusaidia mchakato mzima wa ukuaji wa maendeleo ya nchi hii kwa kulinganisha na Dar es Salaam, haina mazingira mazuri. Naamini kabisa kama kweli asilimia 70, kwa sababu takwimu

zilizopo ni asilimia 70 ya mizigo inayotoka Dar es Salaam inapita *custom* ya Tunduma. Waone jitihada ya kuwekeza kule, nakumbuka ni juzi tu hapa Mheshimiwa Stella alikuwa anauliza suala la *dry port,* yakajibiwa majibu kirahisirahisi tu. Majibu ambayo hayakuonesha kwamba Serikali inayo dhamira ya kuhakikisha kwamba kwanza inalinda barabara zetu ambazo zinajengwa kwa gharama kubwa, lakini pia kuona umuhimu wa kuongeza soko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kukiwa na *dry port* Tunduma, wafanyabiashara wa nchi zingine za *SADC* wanaweza kuona wepesi wa kuja kuchukua mizigo yao pale au kuagiza kupitia bandari yetu kwa sababu huduma inakuwa imesogezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo niseme tu na niombe kwamba Wizara hii ya masuala ya mipango izingatie pia Mji wa Tunduma katika mipango yake, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Noah, jiandae Mheshimiwa Samweli. Mheshimiwa Noah hayupo, Mheshimiwa Samweli Xaday Hhayuma.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Hotuba au Bajeti ya Waziri Mkuu. Nianze kama wenzangu kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, lakini Makamu wa Rais Dkt. Philip Isidor Mpango na Waziri Mkuu kwa kazi nzuri ambayo inafanyika katika kutekeleza maendeleo ya nchi yetu na ushahidi unaonekana kwamba kazi kubwa inafanyika katika utekelezaji wa miradi mikubwa; hasa mradi wa reli ambako maeneo mbalimbali kazi kubwa tunaiona ikifanyika, lakini Mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere ambako umeshafikia asilimia 83 na ni mategemeo kwamba baada ya mradi huo kukamilika Watanzania wataisahau shida ya umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu pia inapiga hatua kubwa chini ya usimamizi mahiri wa Daktari Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ni kazi kubwa inafanyika kwenye eneo la elimu, kwenye umeme usiseme lakini miundombinu tunaenda nayo vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kwa niaba ya Wananchi wa Hanang' kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, kwa miradi mingi ya maendeleo ambayo imeelekezwa ndani ya Jimbo la Hanang'. Kwenye upande wa barabara tulikuwa na changamoto kubwa hasa upande wa *TARURA*, bajeti yetu ilikuwa milioni 800 na hamsini na kitu tu, lakini mpaka sasa tuna barabara nyingi ambazo tumefungua. Nitaje barabara chache tu ambazo wananchi sasa hivi wanafurahia matunda ya Daktari Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa na barabara yetu mbovu kabisa ambayo iliyokuwa inatusumbua barabara ya Masqaroda - Lambo – Masakta kwa sasa wananchi wanateleza maendeleo yanaenda sawa sawa. Tulikuwa na barabara mpya nayo imefunguliwa kuunganisha Kata za Bassodesh na Mulbadaw tumefungua barabara mpya kuunganisha Hilbadaw na Mwanga hicho ni kijiji ambako kilikuwa na changamoto kubwa na tuliwaahidi wakati wa uchaguzi, utekelezaji unaenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa maji, kazi kubwa pia imefanyika, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais. Tulikuwa na changamoto kubwa ya maji, nilivyoanza kuja tu hapa Bungeni nilianza kulia kwa Mji wa Katesh, mji mkubwa, maji tunateka kwa mikokoteni ya punda, lakini kwa sasa Wanakatesh wanapata maji ya kutosheleza. Naamini kuna maeneo ya kuboresha ambako tutaendelea kuboresha lakini Mradi mkubwa wa Maji kutoka Mogitu, Gehandu, mradi wa zaidi ya bilioni sita karibu umefika asilimia 80 ya utekelezaji wake ambako utaenda kutekelezwa ndani ya bajeti hii inayokuja. Ni kazi kubwa ambayo imefanyika, tunamshukuru

sana Mheshimiwa Rais. Tumechimbiwa visima zaidi ya 40 ndani ya Jimbo langu la Hanang'

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa na miradi mbalimbali ambayo ilikuwa kwenye hatua mbalimbali za utekelezaji nayo imeendelea kukamilika. Tunashukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kweli ametuwezesha na changamoto ya maji inaendelea kupungua ndani ya Jimbo la Hanang'. Tunalo ombi kwenye visima ambavyo tumechimbiwa visima 24 lakini tunaenda kuchimbiwa visima 16, vile visima ambavyo tayari vimeshachimbwa tunaomba maji yale yasambazwe kwa wananchi. Bajeti tunayotengewa kwa sasa kwa visima hivyo hatuwezi kusambaza kwa wakati, tunaomba tuongezewe fedha ili tuweze kusambaza kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru kwamba kwenye bajeti hizi zinazokuja tutapeleka maji Gawal, tutapeleka maji Gehandu, tutapeleka maji Mureru lakini Gijetamuhog ambako hawajawahi kupata maji nao wataenda kupata maji, lakini Mureru nao wataenda kupata maji. Tunaomba kasi hio iongezeke ili maeneo yote yaweze kupata maji, changamoto ya maji iweze kuondoka. Kwa visima vile 16 naomba maeneo ya Dajameda na Wandela yapewe kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, tulitarajia wakati fulani Waziri Mkuu kututembelea kwenye Jimbo letu la Hanang' akiwa Mgeni Rasmi akamtuma Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Daktari Mwigulu Nchemba. Alipofika pale mbele ya Wanahanang' nilimwomba kwa sababu amebeba pochi ya Mama aifungue aiangalie barabara yetu ya Mogitu – Haydom na yeye kwa kuwa ni mtoto wetu, jirani yetu, aliahidi kwamba pochi ya Mama ataifungua, mpaka sasa sioni dalili ya hiyo barabara kuanza. Naomba hiyo pochi ifunguke barabara ya Mogitu – Haydom ianze kujengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ile barabara inategemewa na wananchi wa Hanang'. Ukanda ule wa juu ndio unakolimwa ngano nyingi na nchi yetu ina changamoto kubwa ya upatikanaji wa ngano, lakini ukanda ule ndiko kunapolimwa shahiri na mazao mbalimbali, ni ardhi ya kilimo, vitunguu tunalima mpaka tunasafirisha katika nchi mbalimbali. Tunaomba tusaidiwe hii barabara ni barabara ya kimkakati. Barabara ambayo itasaidia wananchi wetu pia kupata huduma za afya. Kwa maana ya kurahisisha kuunganisha usafiri kutoka maeneo mbalimbali ya Wilaya ya Hanang' na Wilaya ya Mbulu hasa Hospitali ya Haydom.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba hii barabara kwenye bajeti hii isikose fedha. Jana niliuliza swali la nyongeza hapa kwamba barabara hii itaanza lini, nikaambiwa upembuzi na nini kwamba swali hilo lilishajibiwa, tunachotaka sisi Wanahanang' na Wanambulu tuone barabara inajengwa na hatimaye barabara inapitika ili kurahisha usafiri kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilishawahi kuongelea suala la ugonjwa wa malaria kwenye Bunge hili. Ni ugonjwa ambao unaongoza katika kupoteza maisha ya watu wetu lakini tuna kiwanda kimejengwa cha viua wadudu ambacho kitatokomeza viluwiluwi vya mbu. Mbu ni kero katika makazi yetu katika maeneo yetu, tuna kiwanda ambacho kina uwezo wa kuzalisha lita milioni sita kwa mwaka. Kiwanda hiki kimejengwa toka mwaka 2016. Kiko nchini mwetu mpaka sasa sisi tunahangaika na malaria, tunapoteza watu wetu kwa sababu ya malaria, lakini kiwanda tunacho, hakina soko, ilivyofanyika *feasibility study* wateja wakubwa walikuwa ni Wizara ya Afya kwa sababu ya kudhibiti malaria, lakini TAMISEMI kwa sababu nao wanashughulika na suala la afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa hivi ninavyoongea kiwanda hicho kimeweza tu kuzalisha lita 916,747 kwa miaka yote ambayo imefanya kazi toka mwaka

2016, lakini tunaendelea kupoteza watu. Kiwanda hicho kinaendelea kufanya kazi kwa hasara, kiwanda cha kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri kuna sababu ya sisi akili zetu kuanza kufanya kazi. Kiwanda ni cha kwetu tumekitengeneza, kinapata hasara hakina soko, lakini sisi tunaugua, tunakufa kwa ajili ya malaria. Hii haikubaliki, kila Ripoti ya Wizara ya Afya utaambiwa tu kwamba ugonjwa unaongoza kuua watu Tanzania ni malaria. Tunao mfano Zanzibar, wenzetu malaria wamepunguza kwa asilimia kubwa sana, lakini Tanzania Bara mpaka sasa malaria bado ni changamoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwanda kinaendeshwa kwa hasara, tuchukue hatua sasa, Mheshimwa Waziri Mkuu tunaomba awasimamie hawa watu wake. Wizara ya Afya, Wizara ya Viwanda na Biashara kwa sababu, Viwanda na Biashara wanayo dawa, Wizara ya Afya wanapaswa kununua dawa ili kudhibiti malaria, lakini hilo halifanyiki. Tunaomba eneo hilo lisimamiwe vizuri. TAMISEMI kwenye halmashauri zetu wasimamie kuhakikisha kwamba tunadhibiti mbu wanaoambukiza malaria kwa sababu dawa tunayo hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ingekuwa ni teknolojia tunayotafuta kwa mbali tungekuwa tunahangaika kila siku tunarudia jambo hilo hilo hatusogei, tuchukue hatua sasa tusogee kwenye eneo hilo. Niseme tu, kama changamoto yetu ni kwamba tukiwa na taasisi ikawa ya umma umma hivi watu hawaoni hizi fursa na kuunganisha mazingira yaliyopo ili kuhakikisha kwamba tunachukua hatua na tufanye kazi kwa ufanisi. Tuangalie watu tunaowaweka kwenye maeneo hayo. Taasisi zetu zimekuwa zinajisahau kufanya kazi Kiserikaliserikali, wakati kuna taasisi kama zenyewe zinafanya kazi za binafsi, zinafanya kazi vizuri. Tuchukue hatua tuweke watu ambao tutawawekea vigezo hasa tuangalie *performance base* za wale ambao tunawapa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani una kiwanda kimesimama, wateja wapo, hakuna kinachoendelea na hii imekuwa kila sehemu kwenye nchi yetu. Ukiangalia *TTCL* wenzao kina *Vodacom* kina *Tigo* na wengineo wanaenda vizuri na unawasikia matangazo kila sehemu, *TTCL* anza kutafuta vocha utazunguka mji mzima, kupata vocha ni shida. Tuangalie kama kweli bado tunahitaji kuwa na taasisi zinazofanya biashara kwenye nchi yetu ambazo zinamilikiwa na Serikali. Tukishafanya tathmini hiyo, kama kweli tunahitaji, tuweke watu ambao wanaweza kufanya kazi ya uzalishaji wakashindana sokoni, wakaleta tija. Kama hilo haliwezekani tuwezeshe sekta binafsi iendeshe hivi vitu, sisi tuvisimane. Vile ambavyo vina maslahi ya umma tuweke usimamizi uwe imara zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nayasema haya kwa sababu udhaifu umekuwa mwingi katika maeneo mengi. Nikirudi kwenye *NDC*…

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, wamekopesha matrekta kwa wakulima…

**NAIBU SPIKA**: Taarifa.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nataka nimpe taarifa mzungumzaji Mheshimiwa Hhayuma kwamba ukitaka kutafuta vocha ya *TTCL* ukiwa kule kijijini ni mpaka utafute namna ya kuweka *M-pesa* vinginevyo vocha hakuna. Minara ipo kila kitu lakini vocha ni tatizo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Samweli, endelea.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo taarifa naipokea na naomba nisisitize tu kama Serikali kwenye taasisi zile ambazo zinafanya biashara inamaanisha biashara basi waweke watu ambao kweli watasimamia biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa najaribu kuongelea suala la *NDC* wamekopesha matrekta ya *URSUS* kwa wakulima. Kilichofanyika tu matrekta yale yamekabidhiwa kwa wakulima, walitakiwa wawe na kipindi cha *warrant*, walitakiwa watembelee na kufanya *services,* lakini toka wamekabidhi wameyatupa huko. Wanachofanya kwa juhudi kwa sasa hivi, mara ya wapite kupitia TAKUKURU, kupitia kwa nani kuwakamata wakulima hawa. Wenyewe hawajatekeleza wajibu wao wa kibiashara, lakini wanataka haki, haki yeyote inapaswa kwenda na wajibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa mchango wako. Waheshimiwa kwanza nashukuru kwa michango, wachangiaji wetu wamekwisha na muda wetu umekwisha. Naahirisha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 11.55 Jioni Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi,*
*Tarehe 6 Aprili, 2023 Saa Tatu Asubuhi)*